# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Pili – Tarehe 28 Agosti, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya leo mengi ni marefu na majibu ni marefu kwa hiyo tuvumiliane Maswali ya Nyongeza yatakuwa ni machache. Swali la kwanza ni la Mheshiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

Na. 14

### Kuigawa Kata ya Kipiri

**MHE. SAIDI J. NKUMBA** aliuliza-

Kata ya Kipiri ni kubwa kwa eneo na idadi ya watu:-

Je, Serikali iko tayari kuigawa Kata ili kusogeza huduma za Kiutawala na Kijamii kwa wananchi wa Kata hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naivbu Spika, vigezo vinavyozingatiwa kwa kuanzisha Kata ni idadi ya vijiji vilivyosajiliwa visivyopungua vitano (5), ukubwa wa eneo usiopungua kilometa za mraba mia tano (500), idadi ya watu wasiopungua elfu kumi (10,000) na uwezo wa Halmashauri kumudu gharama za ongezeko la maeneo ya Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI haijapokea maombi hayo kupitia taratibu za uwasilishaji wa maombi ya aina hii. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wananchi wa Kata ya Kipiri pamoja na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kuangalia kama ombi hilo linakidhi vigezo vilivyoainishwa hapo juu na kukamilisha mchakacho wa kuwasilisha maombi haya ili yaweze kushughulikiwa.

**MHE. SAIDI J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninaomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa

vigezo vyote vilivyotajwa vinatimizwa katika Kata hiyo ya Kipiri.

Je, kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge wote unaweza kuzisema hizo taratibu za uwasilishaji wa maombi?

La pili, tutakapokamilisha zoezi hili ofisi yako itakuwa tayari kushughulikia suala hili kabla ya mwaka 2015?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali la nyongeza ya Mheshimiwa Said Juma Nkumba, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoelezea taratibu zikifuatwa na vigezo vikikamilika ofisi yangu itaanza kushughulikia maombi hayo, ingawa kama tunavyofahamu kwa kawaida tutashughulikia au kutoa majibu mwaka 2014 au mwaka 2015 na siyo 2013.

Na.15

## Kodi ya Maegesho ya Magari

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikikusanya kodi ya maegesho ya magari katika Miji mikubwa mingi nchini kwa kutumia kampuni binafsi:-

Je, Serikali imekusanya mapato kiasi gani kwa mchanganuo wa kila mwaka katika Jiji la Dar es salaam kuanzia Julai 1, 2008 hadi Juni, 2013?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis, Mbunge wa Jimbo la Chonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinagana na idadi ya maonyesho yaliyopo kwa sasa na mkataba wa ukusanyaji mapato; kiasi cha jumla ya Tshs 3,334,028,868 kimekuwa kikikusanywa kuanzia mwezi Julai, 2008 hadi Juni 2013 kwa mchanganuo ufuatao:-

| **MWAKA** | **MAPATO KWA MWEZI** | **MAPATO KWA MWAKA** |
|---|---|---|
| 2008/2009 | 50,500,000.00 | 606,000,000.00 |
| 2009/2010 | 50,500,000.00 | 606,000,000.00 |
| 2010/2011 | 50,000,000.00 | 606,000,000.00 |
| 2011/2012 | 50,000,000.00 | 606,000,000.00 |
| 2012/2013 | 75,835,739.00 | 910,028,868.00 |
| **JUMLA** | | **3,334,028,868.00** |

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato haya hugawanywa hugawanywa kwenye Halmashauri zote za Jiji la Dar es Salaam.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika takwimu alizotoa Mheshimia Waziri hapa katika jibu lake inaonyesha kuwa kwa miezi 48 mapato yalikuwa ni sawa sawa shilingi milioni hamsini na laki tano kwa mwezi, kitu ambacho kitakwimu hakikubaliki, haiingii katika akili ni nini kimesababisha kwa miezi 48 mapato yawe ni hayo hayo ina maana magari yaliyokuwa yanapaki ni sawa sawa idadi yake kwa masaa sawa?

Swali la pili ni kwamba. Je, Serikali kwa sasa ina utaratibu gani wa kuondoa makampuni binafsi katika maegesho ya magari Dar es salaam na Miji mingine mikubwa ili kudhibiti mapato ya Serikali ambayo inaonekana kwa takwimu hizi yanavuja na kuna mchezo mchafu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Makusanyo haya yanatokana kwa mujibu wa mkataba Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam iliingia mkataba na kampuni inayokusanya mapato hayo kuwa kila mwezi kuanzia mwaka 2004 - 2008 kuwa kwa mwezi ni lazima apeleke shilingi milioni hamsini na laki tano. Ilipofika mwaka 2008 wakatangaza zabuni na akapatikana

mkandarasi mwingine na makubaliana sasa yakapanda kwenda kwenda milioni sabini na tano. Awe amefikisha makusanyo hayo au amepata zaidi makubaliano yao kwa mujibu wa mkataba wao yalikuwa ni shilingi milioni hamsini na laki tano kwa mwezi na sasa hivi ni milioni sabini na tano na zile pesa nilizozitaja kila mwezi kwa hiyo ni kwa mujibu wa mkataba.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Ninakushukuru Naibu Spika kwa kunipa fursa hii, kwa kuwa yapo maeneo maalum ya maegesho ambayo yanajulikana lakini pia hivi sasa katika Jiji la Dar es salaam mbele ya maduka au sehemu nyingi za biashara zimefanywa maegesho na Serikali wanakusanya kodi.

Je, huoni kuwa hii ni kero na Serikali ina mpango gani wa kuyafanya maeneo haya ambayo ni mbele ya maduka isiwe ni sehemu ya kukusanya kodi yakatengwa maeneo maalum na kuongeza sehemu zingine ambazo yanahitajika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yamepangwa kwa ajili ya makusanyo na kwa mujibu wa mkataba ambayo nimeelezea ni maeneo ya kati ya Mji ambayo ni ya kibiashara na maeneo ya Kariakoo, ambapo maeneo ya kati ya Dar es salaam gari moja inapakiwa kwa shilingi 300/= na maeneo ya Karikoo gari moja unapaki kwa shilingi 100/= kwa masaa ambayo utakaa.

Lakini kwa sasa hivi watu wote ambao wanajenga majengo Serikali imewaagiza kuhakikisha kuwa katika majengo yao wanahakikisha kuwa wanaweka eneo la kupaki magari kwa sababu kadri siku zinavyozidi kwenda maeneo ya kupaki magari yamekuwa yakipungua.

Na.16

## Kuwanyang'anya Leseni Viongozi wa Kisiasa Kutokana na Kukiuka Maadili ya Kazi

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Ni utaratibu wa nchi zote Duniani kuwa wanataaluma kama vile Madaktari, Wahandisi, Wahasibu, Wakandarasi na kadhalika wanapofanya kazi zao wakifanya makosa makubwa kwa kukiuka maadili ya kazi zao hufutiwa leseni zao za kufanyia kazi kazi hizo za kitaaluma.

Vilevile viongozi wa kisiasa au Wanasiasa kwa ujumla wao wanayo maadili yanayowaongoza kutekeleza wajibu wao na pale wanasiasa kwa ujumla wao wanayo Maadili yanayowaongoza kutekeleza wajibu wao. Pale wanapokiuka maadili ya kazi zao na wao walipaswa kuchukuliwa hatua kama ilivyo kwa makundi hayo mengine.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muhimu kuwanyang'anya viongozi wa kisiasa na wanasiasa nafasi ya kazi ya sasa wale wanaokiuka maadili ya kazi ya siasa, kama wale wanaoleta uchochezi unaosababisha

kumwaga damu za Watanzania na kufanya vitendo vyote vinavyotishia amani ya Watanzania?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo utaratibu ambao nchi nyingi Duniani zinafuata ambapo wanataaluma kama vile madaktari, wanasheria, wakandarasi, wahasibu n.k wanapofanya kazi wakifanya makosa makubwa kwa kukiuka maadili ya kazi zao hufutiwa leseni au adhabu nyingine kulingana na na aina ya kosa lililofanyika.

Vilevile ni kweli kuwa viongozi wa kisiasa au wanasiasa kwa ujumla nao wanayo maadili yanayowaongoza katika utekelezaji wa wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini mfumo wa Sheria tulio nao umeweka taratibu mbalimbali za kuwashughulikia viongozi wanasiasa wanaokiuka maadili. Sheria ya Viongozi wa Umma Na.13 ya 1995 chini ya kifungu cha 8, inaainisha adhabu ambazo kiongozi wa Umma anastahili kupatiwa.

Endapo atabainika kukiuka maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kwa makosa ya jinai ambayo kiongozi atafanya yanashughulikiwa na Kanuni ya Adhabu *(Penal Code)* Sura 16 na Sheria nyingine zinazounda makosa ya jinai, na utekelezaji wake kama ushahidi upo umo mikononi mwa Mahakama kama chombo pekee cha utoaji haki nchini. Aidha, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 chini ya Ibara

ya 46A, 50(3),57(2)(B) na 71(a), (d) na (g) inaanisha taratibu za jinsi ya kuwatoa viongozi wa kisiasa kwenye nyadhifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya utawala Bora na Utawala wa Sheria inataka kabla kumnyang'anya kiongozi anayetuhumiwa nafasi ya uongozi kuhakikisha kwamba upo ushahidi unaothibitisha makosa makubwa ya kukiuka maadili. Aidha, Ibara ya 13(6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafafanua kuhusu matakwa ya dhana ya utakato *(presumption of Innocence)* kama miongoni mwa Kanuni za Haki ya Asili *(Natural Justice)* kuwa mtu yoyote kutotendewa haki kama mkosaji mpaka pale itakapothibitika vinginevyo.

Kwa sababu hiyo kiongozi wa Kisiasa hatachukuliwa hatua za kumnyang'anywa nafasi yake isipokuwa hatua au adhabu sitahiki zitachukuliwa dhidi ya kiongozi huyo pale tu chombo/ taasisi yenye mamlaka ya kutoa haki itapothibitisha kuwa kiongozi huyo ni mkosaji wa kosa alilokuwa akituhumiwa kulitenda kwa mujibu wa Sheria za nchi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza swali moja tu la nyongeza, kwa kuwa majibu ya Serikali yana angalia zaidi Sheria ya mwaka 1995, Sheria ya mwaka 1995 ilikuwa inakwenda sambamba na siasa za mwaka 1995 siasa za sasa hivi zimebadilika sana na kupelekea kuwa viongozi wa kisiasa hata sisi Wabunge tunatumia majukwaa kuleta uchochezi, kumwaga damu za Watanzania na kuvunja amani ya nchi yetu Je, Serikali

haioni kuna umuhimu sasa wa kubadilisha Sheria hii ili tupate adhabu kulingana na siasa tunazozipeleka kwa sasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa jinsi alivyomwelewa kuwa katika nchi yetu hii bila amani hakuna siasa, wala biashara wala shule. Ninaomba nijibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Sheria hii ilitungwa mwaka 1995, pengine mazingira tuliyo nayo sasa hayakuwemo ninataka nilithibitishie Bunge hili kuwa Wizara yangu imekwishafanya mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria hii, imekwishapita katika Baraza la Mawaziri na tutaileta hapa wakati wa Bunge la mwezi Novemba, 2013.

Kwa hiyo, wakati wa mjadala tutawaomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuiboresha iwe na meno ili iweze kuwashughulikia vizuri watu wanaoharibu usalama wa nchi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ah! Watu wengi kweli wamesimama maswali madogo ya nyongeza Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika ninashukuru sana. Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia taaluma mbalimbali na ili uwe Daktari, Muhandisi na Muhasibu kama linavyoeleza swali la msingi ni lazima uwe

umepitia kozi mbalimbali yaani uwe umepata mafunzo mbalimbali.

Na kwa kuwa taaluma hii ya siasa ambapo inabidi kuelewa na kujitambua namna ya kushughulikia Umma wa Watanzania katika utumishi zaidi. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwa na Chuo Cha Kitaifa ambacho kitaandaa viongozi kama Wabunge wakisha chaguliwa wanapigwa msasa kwanza ili kuweza kujitambua?

Kama ni Wakuu wa Wilaya au ni Wakuu wa Mikoa ili kuandaa viongozi ambao watatambua kuweka mbele maslahi ya Taifa kwanza kuliko maslahi binafsi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbatia, Mbunge wa kuteuliwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, siasa siyo taaluma ndiyo maana hakuna mtihani unaouandika wa siasa, mtihani wa siasa ninaomba nifahamike vizuri kuwa somo la siasa kwa maana ya *political science* hiyo ni taaluma. Lakini uana siasa siyo taaluma na ndiyo maana unapimwa kwa kura na vidole na kadhalika.

Sasa kuhusu suala la chuo, vyuo vya siasa viko vingi lakini kila chuo kina muhtasari wake wa mafunzo yaani silabasi kwa hiyo, inawezekana chuo cha mafunzo kinachoendeshwa na chama fulani au kinachokubalika na chama fulani kisikubalike na chuo kingine.

Lakini niseme kuwa vipo vyuo hapa nchini ambavyo havizingatii mwelekeo wa upande wa siasa wa chama chochote Chuo cha Uongozi wa Taifa na Vyuo vinginevyo kikiwepo Chuo cha Diplomasia. Kwa hiyo, ningependa kutoa wito kwa wale ambao wangependa kujiendeleza kupata fahamu nzuri kwa upande wa masuala ya kisiasa wakafanya jitihada ya kujiunga katika vyuo hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Swali fupi Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri amesema ikithibitika viongozi wa kisiasa wamesababisha matatizo yaliyoandikwa hapa ndipo watachukuliwa hatua, katika kipindi cha miaka miwili tangia uchaguzi viongozi wa kisiasa walisababisha vifo vya wananchi pale Arusha, viongozi wa kisiasa walisababisha kifo cha kijana pale Ndago, viongozi wa kisiasa walisababisha kifo cha kijana pale Morogoro na viongozi wa kisiasa walisababisha kifo kwa ubabe tu na kwa ubishi pale Iringa.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua kwa wale viongozi wanaosababisha badala ya wale wanaokwenda kwenye matukio?

Maana kama Serikali ingechukua hatua watu kama akina Mbowe na Dkt. Slaa walitakiwa wawe jela siku nyingi kabisa kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora.

**MBUNGE FULANI:** Taratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaimba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nchemba, kama ifuatavyo:-

Katika jibu langu la msingi nilisema kuwa katika nchi inayozingatia Utawala Bora kuna mgawanyo wa kazi, kuna mgawanyo wa majukumu kati ya Serikali yaani *Executive,* Bunge na Mahakama.

Peke yake chombo kinacho ruhusiwa kufanya maamuzi kuamua kuwa huyu ana kosa au hana kosa ni chombo cha Mahakama ndiyo kwasababu nchi yetu inazingatia Utawala Bora hayo matukio uliyoyaeleza uchunguzi umefanyika. Watu wako Mahakamani na ikibainika kuwa walifanya makosa, awe mkubwa,awe mdogo ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuwaomba wanasiasa wenzangu ile nembo ya Tume ya Uchaguzi inasema tushindane bila kupigana, naomba Watanzania wenzangu tuendeshe siasa katika nchi yetu kwa amani na utulivu kwa sababu bila amani Tanzania patakuwa si mahali pazuri pa kuishi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana swali linalofuata linaenda Wizara ya Nishati na Madini, litaulizwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji Mbunge wa Konde.

Na. 17

**Udhibiti wa Biashara Haramu ya Mafuta**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Mapato ya Serikali yamekuwa yakipotea kutokana na wafanyabiashara wasio waaminifu ambao badala ya kupeleka bidhaa zao nje ya nchi bidhaa hizo huishia hapa nchini:-

(a) Je, Serikali imefanikiwa kwa kiasi gani kudhibiti mianya hiyo hasa kwa bidhaa za mafuta?

(b) Je, ni kampuni ngapi zimekamatwa mwaka 2010 hadi 2012 zikishusha mafuta ya *transit* hapa nchini na hatua gani zilichukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA NSHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kwenye biashara

ya mafuta kwa kiasi kikubwa, baada ya kuanza kutumia njia ya kuweka vina saba na ving'amuzi kwenye mafuta na kuongeza ushuru kwenye mafuta ya taa kutoka shilingi 52 kwa lita mpaka shilingi 400 kwa lita. Mafanikio ya mradi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Tatizo la uchakachuaji limepungua kutoka takribani asilimia 78 mwaka 2007 hadi chini ya asilimia 10 kwa sasa.

(ii) Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2011 kiasi cha mafuta yaliyolipiwa kodi kiliongezeka kwa wastani wa lita 9,749,986.74 sawa na ongezeko la asilimia 28.2 kwa mafuta ya *petrol*i na kiasi cha lita 18,511,039.27 sawa na asilimia 26 kwa *diesel* kwa mwezi, ambazo kwa pamoja ni sawa na ongezeko la lita 28,261,026.01;

(iii) Tangu kuongezeka kwa ushuru katika mafuta ya taa mwezi Juni, 2011, kiasi cha mafuta ya taa yaliyokuwa yakiingizwa hapa nchini kilipungua kwa wastani wa lita 11,394,431.11 sawa na asilimia 37.9 kwa mwezi. Kuanzia tarehe Moja Julai, 2011 hadi 31 Desemba 2011, kiasi hiki kilipungua zaidi kwa wastani wa lita 19,757,027.11 sawa na asilimia 65.8 kwa mwezi; na

(iv) Serikali imeongeza makusanyo ya kodi hadi kufikia takribani shilingi bilioni 14.8 kwa mwezi, hii ni sawa na shilingi bilioni 148 kwa miezi 10 ya mwanzo kuanzia mwezi Septemba 2010 hadi Juni 2011. Kuanzia mwezi Julai 2011, kiasi cha makusanyo ya kodi kilizidi kuongezeka hadi kufikia wastani wa shilingi bilioni 25.1 kwa mwezi.

(b) Mheshimiwa Spika, vituo 78 vya mafuta na magari manne (4) ya kubeba mafuta yalikamatwa mwaka 2010 hadi mwaka 2012 yakishusha hapa nchini mafuta yaliyopaswa kwenda kuuzwa nje ya nchi *(transit product)*. Hatua zifuatazo zilichukuliwa dhidi ya vituo na magari hayo:-

(i) Vituo hivyo na magari hayo ya mafuta yalifungiwa kwa muda kufanya biashara ya mafuta pamoja na kutozwa faini kwa mujibu wa *Petroleum marking and quality control rules ,* 2010, *GN* Na. 210; na

(ii) Matokeo ya ukaguzi wa vina saba kwenye mafuta ya vituo na magari yalipelekwa mamlaka ya mapato *TRA* ili kuweza kubaini kiasi cha kodi kilichokwepwa na wahusika. Wamiliki wa vituo na magari hayo ya mafuta walilipa kodi husika.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tumeelezwa hapa kwamba vituo 78 vilihusika katika ushushaji wa mafuta ambayo yalitakiwa kwenda nje ya nchi na hatimaye yakaishia katika nchi yetu.

Hivi karibuni Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweka utaratibu mpya wa kufunga vifaa ambavyo vinadhibiti bidhaa hizi zinazokwenda nje ya nchi kuanzia zinapotoka katika bandari ya Dar es Salaam kufikia mpaka wa nchi jirani zinapokwenda. Vifaa hivi kwa kiasi kikubwa vitasaidia udhibiti ushushwaji wa bidhaa za nje hapa nchini.

Lakini tatizo tunalolishuhudia mara nyingi si shida ya vifaa vinavyowekwa kudhibiti hali ya nyenendo hizi, tumeshuhudia katika uwanja wa Dar es Salaam kuna vifaa vinavyofanya kazi lakini watendaji kwa maksudi wamekuwa wakifanya ubadhilifu, hali kadhalika na sehemu hizi yanaweza kutokea hapa.

Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha watendaji ambao watasimamia mpango huu kuhakikisha hawafanyi ubadhilifu katika maeneo haya?

Swali la pili; Makampuni ya madini ni miongoni mwa wanaonufaika na msamaha wa kodi ya mafuta. Je, ni udhibiti gani ambao umewekwa kuhakikisha mafuta yanayopelekwa kwenye makampuni ya madini yanafikia kwenye migodi hiyo badala ya kushushwa na kuikosesha Serikali mapato?

**NAIBU WAZIRI WA NSHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa Mbunge kukiri kwamba Serikali inafanya jitihada kubwa kudhibiti uchakachuaji na wizi wa mafuta njiani.

Suala aliloliuliza ni suala la kinidhamu, ninachoweza kumhakikishia ni kwamba Serikali itaendela kuwa wakali kwa watendaji wetu ambao wanakiuka taratibu za kiutendaji hasa kwenye masuala ya nidhamu, tutaendelea kuchukua hatua kama ambavyo tunachukua hatua hivi sasa na kuhakikisha kabisa kuwa tunatokomeza tatizo hili.

Swali la pili la misamaha ya mafuta inayotolewa kwenye makampuni ya migodi ni kwamba makampuni ya migodi yanaingia mikataba na *supplies* kwa mfano kampuni ya *GGM* inaingia mkataba na PUMA na PUMA ndiyo ina wajibu sasa wa kusafirisha mafuta yale kuhakikisha inayafikisha kwenye mgodi.

Kwa hiyo, ni PUMA na mgodi wenyewe kuthibitisha kwamba mafuta yaliyolipiwa yamefika kama ambavyo yamelipiwa na sisi Serikali tuna ukaguzi katika maeneo hayo kuhakikisha kwamba lita zilizolipiwa kwenda kwenye mgodi zinafika kama zilivyo na kwenye jibu langu la msingi limeeleza kwamba Serikali imeanzisha utaratibu wa kuweka ving'amuzi katika magari yanayosafirisha mafuta.

Wengi kama mnasafiri njiani ukiona nyuma kwenye matanki kuna mashine inawaka taa maana yake inatuma *signal* kama lile gari litasimama popote kushusha mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa utaratibu huo wa kisayansi tuna uhakika kabisa kwamba tunaweza kusoma na kuona gari inayotoka Dar es Salaam kwenda Kahama ama kwenda Geita limefika bila kufunguliwa na kumwaga mafuta njiani. Ahsante sana.

Na. 18

## Mizani ya Digitali kwa Zao la Korosho

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Tatizo la wanunuzi wa mazao ya kilimo kuwapunja wakulima kupitia mizani ni kubwa si kwa Wakulima wa Pamba tu, bali hata kwa wakulima wa Korosho na mazao mengine:-

Je, kwa nini Serikali haitoi msisitizo wa kutumia mizani ya *digital* kupimia zao la Korosho kama ilivyofanya kwa zao la Pamba.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria Na. 20 ya mwaka 1984 ikisomwa pamoja na tangazo la Serikali Na. 16 la tarehe 8 Februari, 2008, inasisitiza matumizi ya mizani sahihi katika kufanya biashara. Kwa sasa mizani sahihi zinazotambuliwa kisheria ni pamoja na mizani ya *platform, counter, weighbridge, Mechanical Digital.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa, lipo tatizo kubwa la manunuzi ya mazao ya kilimo kuendelea kupunja wakulima kupitia mizani zisizokidhi viwango. Tatizo hili si kwa wakulima wa pamba tu bali hata kwa wakulima wa korosho na mazao mengine.

Kwa mantiki hiyo, wadau wa zao la pamba kupitia *Tanzania Cotton Authority* waliishauri Serikali mizani ya

*digital* itumike kwa lengo la kumlinda mkulima asipunjwe anapouza pamba yake.

Serikali iliridhia ushauri huo kuanzia msimu wa mwaka 2012/2013 na hadi sasa unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kwamba wanunuzi wa mazao ya kilimo waendelee kutumia mizani ambayo inatambuliwa kisheria.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa, Serikali imekiri kuwa imeagiza mamlaka ya zao la Pamba waanze kutumia mizani ya *digit* ili kumlinda mkulima asiendelee kupunjwa na mnunuzi.

Je, Serikali inaona ugumu gani kuagiza Mamlaka zingine za mazao ili ziweze kutumia mizani hii ya *digit* sambamba na wakulima wa pamba ambao imeonekana kwamba wanapunjwa?

Swali la pili; kwa kuwa, wakulima wa korosho wamekuwa wakipata adha nyingi katika maeneo mbalimbali katika uzalishaji wa zao hili la korosho, Serikali kwanini isijikite sasa hivi kuwasaidia katika maeneo haya ambayo yapo ndani ya uwezo wake kuhakikisha kwamba inaanza kutumia mizani ya *digit* ili kuondoa kero kabisa za upunjwaji wa ununuzi wa korosho?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba sheria inasisitiza matumizi ya mizani sahihi katika kufanya biashara. Kwa sasa mizani sahihi inayotambuliwa kisheria ni kama ambavyo nimeitaja.

Kwa hiyo ningeshauri kwamba hata wenzetu wadau wa korosho na mazao mengine waendelee kutumia mizani ambayo inatambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema si *digital* tu. Ipo mizani mingine zaidi ya *digital* ambayo inatumika sasa hivi katika kupima na kusaidia kutokuwapunja wakulima.

Kwa hiyo, nasisitiza zaidi kwamba wadau wa korosho na wengine wa mazao mengine vile vile, waendelee kutumia mizani ambayo inatambuliwa kisheria. Usumbufu ambao unasemwa kwamba wakulima wa korosho wanasumbuliwa muda mrefu.

Nasisitiza kwamba, bado nasema kwamba mizani ambayo inatambuliwa kisheria sasa hizi mizani zitumike, siyo ule mzani wa *digital* tu, ipo mizani mingine zaidi ya digital, ipo mizani mingine minne zaidi ambayo inatambuliwa kisheria na ningeomba kwamba wakulima wa korosho na wengine wazidi kutumia mizani ambayo inadhibitiwa na inakaguliwa na wakala wa vipimo sawasawa na watazidi kusaidiwa. Hivyo na wao wazidi kutumia mizani ambayo inatambulika kisheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Naomba nimwulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, baadhi ya wakulima, wafanyabiashara ambayo siyo waaminifu wanawafuata wakulima katika mashamba na kujaza ujazo wa magunia kwa lumbesa, gunia la kilo mia moja linatoa kilo mia mbili.

Je, wafanyabiashara hawa huoni kama wanawapuma wakulima na utawachukulia hatua gani angalau wale wakulima wanufaike kwa sababu wengine hawana elimu ya ujazo wa magunia.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kusisitiza kwamba wale wafanyabiashara ambao wana tabia ya kuwadhulumu wakulima kwa kutumia vipimo ambavyo haviruhusiwi kama lumbesa waache mara moja na wafuate vipimo ambavyo vinaruhusiwa kisheria sasa hivi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama swali fupi la nyongeza.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa, hoja ya msingi ya swali la Mheshimiwa Mtutura si kwamba matumizi ya mizani ambazo zimekubaliwa kisheria ziwasaidie wakulima, hoja ya msingi ni mizani hiyo ya dharura kuwapunja wakulima wakiwemo wakulima wa mahindi katika Jimbo la Peramiho. Kwa nini Serikali isichukue maamuzi.

Ni lini Serikali itachukua maamuzi mizani ya *digit,* mizani ya saa ndiyo ianze kupima mazao ya wakulima ili kuwapa haki yao wakiwemo wakulima wa mahindi katika Jimbo la Peramiho. Ni lini Serikali itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napokea ushauri wake na vilevile nasisitiza kwamba mizani ya *digital* siyo mizani pekee, kama nilivyosema ni kwamba ipo mizani mingine. Hii mizani ya *digital* inachangamoto zake ambazo zimeshabainika hivi sasa.

Kwa mfano kuna gharama kubwa sana ya mizani hii ya *digital* kwa maana ya kwamba inatumia umeme wakati kuna sehemu zingine hazina umeme. Suala la vumbi nalo linaathiri mizani hii ya *digital*. Vumbi inaleta shida katika mizani hii.

Kwa hiyo, ningesema kwamba mizani ya *digital* si pekee ambayo inaweza kutumika sasa hivi, watumie na mizani mingine ambayo wakala wa vipimo ana haki ya kudhibiti na kukagua mizani ambayo nimeitaja ili kuwasaidia wakulima.

Na. 19

## Kufufua Zao la Michikichi Kigoma

**MHE. DAVID Z. KAFULILA** aliuliza:-

Watu wa Nchi ya Malyasia walikuja Kigoma mwaka 1990 kujifunza kuhusu zao la Michikichi na sasa nchi hiyo ni ya pili kwa uzalishaji wa zao la Michikichi Duniani:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika miaka ishirini (20) kuhakikisha inafufua zao hilo muhimu kwa Uchumi wa Mkoa wa Kigoma na Tanzania kwa ujumla?

(b) Je, Tanzania imeagiza mafuta ya kupikia nje ya nchi kiasi gani na yenye thamani gani tangu mwaka 1990 hadi mwaka 2012?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na mikakati mbalimbali ya kuendeleza mazao nchini ikiwemo zao la michikichi Mkoani Kigoma kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija ya mazao hayo.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuhamasisha uendelezaji wa zao hilo kupitia utekelezaji wa mipango ya kilimo ya Wilaya *DADPS* ambapo wakulima hupatiwa mbinu bora za kilimo na misaada mingine. Kuhamasisha sekta binafsi lakini pia na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kama vile *TACARE, CARITAS* na *TCRS* kuwekeza katika uzalishaji, usindikaji na matumizi ya bidhaa za michikichi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imeingiza Mkoani Kigoma jumla ya miche 605,000 ya *(Pregerminate Hybrid Seeds*) kutoka nchini Costa Rica, Ivory Cost na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni kuzalisha na kusambaza miche bora ya michikichi ili kuongeza eneo linalolimwa michikichi na kuondoa ushuru na kodi kwa uingizaji wa mitambo na mashine za kilimo ikiwa ni pamoja na mashine za kukamilia mafuta ya maweze ili kuyaongezea thamani mazao ya kilimo ikiwemo michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utekelezaji wa mipango hiyo ya Serikali ni kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta ya mawese nchini kufikia tani 32,221 mwaka 2011 kutoka tano 11,360 mwaka 2005/2006. Aidha, uzalishaji wa mafuta ya maweze Mkoani Kigoma pia umeongezeka kutoka tani 10,080 mwaka 2005/2006 hadi kufikia tani 29,686 mwaka 2011/2012.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula kwa mwaka ni wastani wa tani 350,000 ambapo uzalishaji wa ndani asilimia kama 35 na hivyo asilimia 65

inayobaki lazima iagizwe kutoka nchi za nje ikiwemo nchi ya Malyasia. Aidha, wastani wa uagizaji wa mafuta ghafi ya mawese kwa mwaka ni kama tani 300,000 ambapo katika kipindi cha mwaka 2000 hadi mwaka 2012 jumla ya tani kama milioni tatu za mafuta ghafi ya mawese yenye thamani ya shilingi kama bilioni mbili na nusu ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Moja; Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya tatizo kubwa ambalo linasababisha zao la michikichi na hususani uzalishaji wa mawese kushuka ni kutokana na Serikali kuondoa ushuru asilimia kumi kwa waagizaji wa mawese kutoka nje na ndiyo sababu unaona mahitaji ya mafuta yakiwa tani 330,000 tunaagiza mawese tani 300,000.

Ni lini Serikali itafuta huo ushuru wa asilimia kumi ili kuongeza uzalishaji na tija kwa watu ambao ni wa ndani waweze kuzalisha michikichi kwa maana ya uzalishaji wa mawese?

Pili; katika majibu yako umesema kwamba mpaka sasa Tanzania inazalisha tani elfu thelathini mbili wakati mahitaji ya mawese ambayo tunaagiza kutoka nje ni tani laki tatu, naomba kujua tangu mwaka 1990 Malyasia walipokuja kujifunza Mawese na michikichi mpaka leo mpo tani 32,000 badala ya tani laki tatu.

Ni lini sasa utaujengea uwezo Mkoa wa Kigoma uweze kufikisha mahitaji hayo ya tani laki tatu badala ya nchi kuagiza mafuta kutoka nje tuweze kutumia mafuta ya ndani. (M*akofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ule uamuzi wa kuwa na asilimia 10 kwenye ile kodi ulifanyika, ulipita humu Bungeni na ulijadiliwa na Wabunge sisi wote na wakati huo ilikuwa lengo ni kuweka unafuu kwa bidhaa hii ambayo ni muhimu sana sana kwa uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafuta ya kula ndiyo bidhaa inayoagizwa kwa wingi nchini baada ya mafuta ya petroli. Kwa hiyo, ule uamuzi ulikuwa ni uamuzi wa pamoja na misingi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya Kati na unategemea sana *dynamics* za *supply and demand*. Kwa hiyo, kama unavyoona sisi wenyewe tunazalisha mafuta ya mawese tani elfu 30 na wakati mahitaji yetu ni tani laki tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado nakubaliana na Mheshimiwa Kafulila kwamba kuna mkakati wa makusudi ambao Serikali tunataka kutengeneza sasa hivi na tumeanza kuzungumza na wazalishaji pamoja na wasindikaji ili wawekeze kwenye kuzalisha mafuta hapa nchini. Kwa hiyo, hilo bado Mheshimiwa Naibu Spika ni jambo ambalo inabidi tuzungumze lakini pia tuangalie uhalisia wa bidhaa hiyo na matumizi yake nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la kwamba tunazalisha tani 32 elfu na lini tutajifunza kutoka Malaysia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malaysia wamefanya uwekezaji wa makusudi na pale sisi Tanzania uzalishaji wetu wa mawese ni nyumba moja moja nche pale, nche pale. Malaysia wanalima michikichi kwa *plantations.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachofahamu na yeye Mheshimiwa Kafulila anafahamu kwamba kuna wawekezaji wamejitokeza siyo tu kwa Kigoma lakini pia kwa ya Kanda ya Pwani, kwa Tabora kwa maeneo ya Sumbawanga wanataka kuja kuanzisha kilimo cha michikichi kwa hekta elfu kumi, elfu kumi na tano.

Uchimbaji huo utategemea sana wakulima wadogo. Kwa hiyo, jambo hilo Mheshimiwa Naibu Spika tunalifanyia kazi lakini pia uhamasishaji kwanza kupatikana maeneo ya ardhi kwenye maeneo yenu lakini hamasa kwa wakulima wadogo ili wajue kwamba huo ndiyo mfumo wa kisasa wa kulima michikichi.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa katika miaka 2003/2004 ile *CRF* ilifanya utafiti wakishirikiana na *UNIDO* wa kina kabisa wa kusaidia kuainisha ulimaji wa michikichi katika Mkoa wa Kigoma na haswa mashamba makubwa ya magereza yaliyopo pale Kigoma.

Pia walifanya utafiti wa kuhakikisha kwamba viwanda vinaweza vika-*process* au vikaongeza thamani chikichi ambazo zimefanyiwa utafiti.

Je, Serikali imeifanyia kazi kiasi gani hiyo ripoti kwa sababu kama ingeifanyia kazi sasa hivi tungekuwa tuna chikichi za kutosha kutengeneza mafuta nchini na hata kuuza katika nchi za nje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri wakati ripoti hii inatengenezwa Mheshimiwa Rita Mlaki alikuwa ni sehemu ya Serikali kwa hiyo anaifahamu vizuri na walichofanya kwenye ripoti ile ni kuonyesha *technical details* za uwezekano Watanzania kuwa mzalishaji mkubwa wa michikichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichosema hapo awali ni kwamba utaalam ule na uwezo ule tunautambua lakini utekelezaji wake kwa sasa unataka uwekezaji mkubwa sana haswa kupitia Sekta binafsi.

Sasa tunasema tumewahamasisha wawekezaji wa ndani lakini pia wawekezaji wa lakini uwekezaji ule utahitaji sana sana sana ushirikiano na mfumo wa kutumia wakulima wadogo ili uwezekane. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ile ripoti ipo lakini kwa mazingira ya sasa inafanyiwa kazi ili kupatiwa utekelezaji wa wakati huu.

Na. 20

## Serikali Kusaini Mkataba na Kampuni ya Umwagiliaji ya India

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Mnamo mwaka 2012, Serikali ilisaini mkataba na Kampuni ya *Jain Irrigation System* ya India kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji nchini:-

(a) Je, Kampuni hiyo ina uwezo gani wa umwagiliaji zaidi ya kampuni ya Kitanzania?

(b) Je, Serikali inaweza kuthibitisha kwa vielelezo uhalali kwa kampuni hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Serikali ilitiliana saini hati ya makubaliano *Memorandum of Understanding* mwezi Aprili, 2012 na Kampuni *Jain Irrigation Systems* ya India kuhusu ushirikiano katika teknolojia za kilimo cha umwagiliaji kutokana na kampuni hiyo kuwa na uwezo na uzoefu mkubwa katika teknolojia ya kilimo hicho cha umwagiliaji, hususani umwagiliaji wa matone kwa maana ya *drip irrigation* na kwa njia ya kunyunyiza kwa maana ya *sprinkler irrigation systems.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya Jain ni mojawapo ya makampuni yanayoongoza duniani katika teknolojia hiyo ya umwagiliaji wa matone ambapo inashika nafasi ya pili duniani katika teknolojia ya *micro irrigation systems* inayotumia maji kidogo.

Kampuni hiyo pia inajihusisha na shughuli zote za umwagiliaji kuanzia uzalishaji wa vifaa vya umwagiliaji, huduma, *consultation* ushauri elekezi, uchunguzi wa udongo, usanifu na ujenzi wa miradi *Ten Key Projects*, pamoja na kutoa mafunzo ya mbinu za uzalishaji na utunzaji wa mazao shambani na hivyo, kudhihirisha uwezo mkubwa wa kiteknolojia na kifedha wa kampuni hiyo katika kilimo cha umwagiliaji ukilinganisha na makampuni yetu ya Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kusainiwa kwa makubaliano hayo, kulifanyika majadiliano ya kina ambayo yalihusisha pia ziara ya Wataalam wa Wizara ya Kilimo kutembelea kampuni hiyo nchini India kwa lengo la kujifunza na kufanya tathmini ya utendaji wa kampuni hiyo. Aidha kupitia ziara hiyo, watalaam waliridhika kuwa kampuni hiyo ina uwezo na uzoefu mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji na yapo maeneo yanayofaa kuanzishwa ushirikiano ambayo yatasaidia nchi yetu kunufaika na teknolojia bora za kilimo na kuongeza kasi ya kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhalali wa kampuni ya *Jain Irrigation System* napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kampuni hiyo inatambulika duniani kote katika teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone. Aidha, pamoja na masuala mengine makubaliano yaliyosainiwa na hata kampuni hiyo kusajili kampuni tanzu hapa Tanzania kwa kuzingatia Sheria za Tanzania ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa utetezi wake mkubwa kwa *Jain Irrigation System Company,* Taifa letu limekuwa likipoteza pesa nyingi sana kulipa makampuni ya nje badala ya kuwa-*train* Watanzania wakaja wakafanya kazi hiyo hiyo ambayo makampuni haya yanafanya.

Je, Serikali iko tayari sasa kuacha kuingiza makampuni kama hayo badala yake kuwachukuwa Watanzania kwenda kuwa-*train* ili wabobee katika masuala ya *irrigation? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili *irrigation system it is not a big deal,* siyo tatizo kubwa sana na hata wananchi wetu wa Kwimba wanafanya. Kinachotakiwa hapa ni miundombinu. Serikali iko tayari sasa kutuletea miundombinu hasa sisi wananchi wa Kwimba ambao tumekuwa na mabwawa ambayo tunashindwa kuyatumia kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie tu Mheshimiwa Leticia kwamba sikufanya utetezi wa *Jain Irrigation,* nilikuwa naielezea *Jain Irrigation* kama miongoni mwa makampuni makubwa yaliyofanikiwa kufanya teknolojia ya *irrigation* kwa kutumia maji kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa labda tutapata nafasi ya Waheshimiwa Wabunge nawaomba waende

wakaangalie miradi ya umwagiliaji. Sisi tuna miradi ya umwagiliaji ambayo leo tuko kwenye Muswada wa leo Waziri atawasilisha. Tuna matatizo katika *efficiency* ufanisi wa miradi yetu ya umwagiliaji. Mingine inapoteza maji, mingine maji hayafiki kwa *level.* Lakini wenzetu hawa walichofanya ni kubaini mahitaji ya maji kwa mmea. Kwa hiyo, unaweza kukuta kwamba maji unapata matone kwa siku, ukasema mbona maji kidogo.

Lakini kitaalam ndiyo maji yanayotosha. Sasa ili kufikisha idadi ya maji hayo, ni taaluma kubwa sana inayotumika. Si jambo la kufanya tu kienyeji enyeji kama wanavyosema kwa watu wa Kwimba au watu wa Mkuranga ni jambo la kitaalam.

Sasa tulichosema ni kwamba sisi tumekwenda kuangalia namna ya wao kuja utaalam ule kuuleta Tanzania. Lakini nakubaliana na dada yangu hapa kwamba watakapokuwa wanafanya kazi hiyo Watanzania wengi *especially* wataalamu wetu washirikiane nao ili taaluma ile ipate kuwa *assimilated* katika *fabric* ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anasema *kwamba irrigation is not a big deal. Irrigation is the deal.* Kama hatukufanya *irrigation* hatuendi mbele na *irrigation* unayoizungumzia wewe dada yangu siyo *irrigation* ya kienyeji enyeji ni *irrigation* ambayo inatakiwa kuzingatia taaluma. Waziri wangu amesoma digrii yake chungu mzima kwenye *irrigation.*

Kwa hiyo, ni jambo kubwa na ni jambo ambalo ndiyo litatoa katika kilimo hiki cha Tanzania. Naomba ndugu zangu tujue tu kwamba pamoja na miundombinu hiyo na wajibu wa kuweka miundombinu pia tuna wajibu wa kuisimamia hiyo iliyokuwepo ili ifanye kazi kwa ufanisi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tuliache hili swali la mtani wangu Leticia Nyerere. Maana leo amepiga suti na kilemba. Tunaendelea na Wizara ya Fedha Swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kwa niaba yake Mheshimiwa tafadhali.

Na. 21

**Utaratibu gani Unaotumika Kuwapata Wazabuni wa Tenda Katika Miradi ya MCC Hapa Nchini**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE)** aliuliza:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwapata wazabuni hapa nchini na ni kampuni zipi za Kitanzania na zipi za kigeni zilishishinda zabuni hiyo?

(b) Je, fedha zote za miradi ya *MCC* zilikuwa kiasi gani na kati ya fedha hizo, wazabuni wazawa walipata kiasi gani na wazabuni wa kigeni walipata kiasi gani?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa fedha zote za misaada inayotolewa na

wafadhili hapa nchini zinabaki mikononki mwa wazawa kwa kiasi kikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye vipengele vya (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika kuwapata wazabuni wa tenda katika miradi ya *MCC* hapa nchini unafuata mwongozo wa manunuzi wa *program za MCC* zilizoainishwa mwaka 2006 hadi 2009 yaani *MCC Programme Procurement Guide Lines.* Utaratibu huu hautoi kwa makampuni ya nchi iliyotoa fedha au nchi iliyopokea fedha.

Zabuni zote zinakuwa za ushindani wa wazi wa kimataifa. Katika kipindi hiki makampuni ya wazawa 203 yameshinda zabuni za miradi ya *MCC* katika maeneo ya huduma za ushauri na vifaa na makampuni ya kigeni 97 yameshinda zabuni katika maeneo ya wakandarasi na wahandisi washauri.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha za miradi ya *MCC* ni shilingi trilioni 1,119,741 sawa na dola za Kimarekani laki 698,136 elfu katika ya fedha hizo jumla ya shilingi trilioni 1,010,208 zimetumika kuwalipa wazabuni mbalimbali ambako makampuni ya wazawa yalipata kiasi cha shilingi bilioni 24,678 milioni na makampuni ya kigeni yamepata shilingi bilioni 985,530 milioni.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za misaada mara nyingi zinaambatana na masharti. Kwa mfano Sera ya Misaada kwa baadhi ya washirika wetu wa maendeleo ni kuwa ili watoe msaada ni lazima makampuni yao yapewe zabuni ya ukandarasi na ushauri wa kiuhandisi. Aidha, suala la uwezo wa kifedha, utaalam na uzoefu nalo huzingatiwa wakati wa manunuzi. Wakandarasi na wahandisi washauri wazawa wanashauriwa kuungana ili kujenga uwezo wa pamoja na kushindana na makampuni ya nje hususani pale ambako msaada hauna masharti kwenye eneo la manunuzi. *(Makofi)*

Serikali kupitia Taasisi zake kama *Contractors Registration Board* na *Engineers Registration Board* inaendelea na utaratibu wa kutoa mafunzo mbalimbali kwa makampuni ya wazawa ili yaweze kujenga uwezo wa kushindana na makampuni makubwa ya nje.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kwa utafiti wangu miradi mingi ya *MCC* haikupelekwa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, ikiwemo Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga. Nilitaka nijue ni sababu gani hasa ambazo zilipelekea Kanda ya Ziwa wasipate miradi ya *MCC?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu kwamba Serikali iko kwenye mazungumzo ya *MCC* awamu ya pili. Nilitaka nifahamu Serikali imejipanga vipi kupeleka miradi mkubwa *MCC* katika Kanda ya Ziwa hasa Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Karagwe?

**WAZIRI WA FEDHA:** Naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Blandes kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika *MCC* ya kwanza ambayo tulipata jumla dola 698.136 ambayo hiyo sawa na hela ya Kitanzania bilioni 1,119 kama alivyoeleza vizuri Naibu Waziri wangu. Ni kweli katika kuelekeza katika miradi katika awamu hii ya kwanza hatukufanikiwa kwa ajili ya Kanda zote na awamu hiyo inamalizika sasa kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba tunaelekea katika awamu ya pili ya *MCC* namba 2. Tuko katika hatua za mawasiliano nao lakini tumehusisha mikoa yote ili tuweze tukapata mapendekezo yao kwa ajili ya miradi itakayokidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge *MCC* namba 2 itajikita katika kusaidia miradi ya umeme pamoja na kuimarisha mabarabara yetu ya vijijini na kama nilivyosema tunashirikisha uongozi wa mikoa yote pamoja na mikoa ambayo kwa bahati mbaya mara ya kwanza kwa ufinyu wa fedha iliyokuwa imekuja ilikuwa haikubahatika kuwa sehemu ya walionufaika. Asante sana.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongezee tu katika majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika miradi ya *MCC.* Miradi ya *MCC* ilihusisha pia barabara. Ni kweli kabisa kwamba hapakuwa na upendeleo wowote katika miradi ya *MCC* kuhusu barabara. Mheshimiwa Blandes amezungumza kwamba haikuhusisha Ukanda wa Ziwa. Ni kweli katika Ukanda wa Ziwa hapakuwa na mradi wa *MCC* wa

barabara kwa sababu barabara zilikuwa tayari zimeshajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Ndiyo maana mradi wa *MCC* katika upande wa barabara umeenda katika mkoa wa Ruvuma, umetengeneza barabara ya kutoka Tunduma-Sumbawanga kwa sababu haikuwa barabara ya lami. Umetengeneza Tanga hadi Hororo. Sasa ungeweza kwenda Kanda ya Ziwa kutengeneza kutoka kwa Mheshimiwa Blandes kwenda Bukoba kwenda Geita kwenda Musoma ambapo tayari barabara ya lami ilikuwepo.

Kwa hiyo, tusingeweza kupeleka huko kwa sababu fedha za Serikali zilikuwa zimeshatumika huko. Kwa hiyo, nataka kukutoa wasiwasi kwamba mradi wa *MCC* haukuwa na upendeleo wowote katika sehemu yoyote lakini ulikuwa una-*cover* maeneo ambayo hayakuwa *covered* na miradi mingine ya kitaifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ooh Mheshimiwa Waziri Mkuu samahani sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika nimeona nisimame kutoa angalizo kidogo kwenye hii awamu ya pili ya *MCC*. Nimeona baadhi ya maelezo tuliyoyapata kutoka mikoani, barabara ambazo zimependekezwa kwa sehemu kubwa hazitatusaidia sana katika *MCC 2. Proposal* nyingi ni zile zinazungumza ni barabara vile vidogo vidogo, kilomita 8, kilomita 5, kilomita 7, 10 inaonekana waliopewa kazi

walikuwa wanaangalia kujibu pengine hoja, kwa sababu mradi unasema Barabara Vijijini.

Sasa naomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu nyinyi mko hapa mtawasaidia zaidi kule dhana iliyopo kwenye *MCC* tu unaposema barabara vijijini tunazungumza barabara inaweza ikawa ya mkoa, inaweza ikawa kubwa tu iwe ni barabara ambayo itafungua uchumi kwenye eneo hilo la *rural.* *(Makofi)*

Nilipokuwa Manyara juzi nimejaribu kuwaeleza ili kuelewesha jambo hili vizuri. Barabara inaweza ikapita hata Wilaya mbili, hata Mikoa miwili, moja.

Lakini inapopita mchango wake kwenye uchumi kwenye eneo hilo unakuwa kwa haraka zaidi, chonde chonde tusilenge maana inaonekana kama vile walikuwa wanatazama madiwani diwani Kata, kutoka kijiji A kwenda kijiji B. Jamani pesa hizi ni nyingi ni vizuri tulitazame kwa upana.

Leteni barabara zinazounganisha hata Wilaya mbili, tatu lakini unajua barabara ile ukifaulu basi, unajua pale umefungua uchumi kwenye eneo lako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Pauline Philip Gekul?

Na. 22

**Matibabu Bure kwa Kinamama Wajawazito**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Serikali, imekuwa ikitoa kauli Bungeni, kuwa kina mama wajawazito Kisera, hawagharamii matibabu yao na gharama za kujifungua, lakini kiuhalisia kina mama hao hulipia gharama hizo.

Je, ni kwa nini Serikali, inawahadaa wananchi kwa majibu hayo wakati yenyewe (Hazina) ndiyo chanzo cha tatizo kwa kutopeleka fedha hizo katika hospitali za Wilaya na nyinginezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul na wewe ndiyo hali yako au? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philip Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Serikali, imeweka utaratibu wa kutoa huduma ya matibabu bila malipo kwa

mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. Huduma bora kwa wanawake wajawazito, wamepewa kipaumbele katika mikakati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Wizara inatekeleza afua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba, huduma inapatikana kwa kila mwanamke mjamzito kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma zinazotolewa Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imenunua vifaa tiba vinavyotumika wakati wa dharura na kuvisambaza katika Hospitali na Vituo vya Afya Mikoa yote nchini. Vifaa hivi vilinunuliwa na Serikali ikishirikiana na wahisani, hususan Benki ya Dunia, vilivyogharimu Dola za Kimarekani takribani milioni 10. Aidha, Wizara inasambaza vifurushi vyenye vifaa muhimu vinavyotumika wakati wa kujifungua, ambavyo vinagawiwa kwa wanawake wajawazito wanapohudhuria Kliniki, ili wajenavyo wakati wa kujifungua. Hii itawaondolea adha ya kuambiwa wakanunue vifaa hivi na kuwafanya wavutiwe kuja kujifungua kwenye Vituo vya Kutolea Huduma za Afya. Vifurushi hivi, vimekuwa vikitengewa fedha karibu kila mwaka na katika kipindi cha mwaka 2013/2014 vimetengewa shilingi bilioni 3 kwa ununuzi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka 2011/2012 hadi 2012/2013 mafunzo kazini yameendelea kutolewa kwa watoa huduma 1,070 wakiwemo Madaktari na Wauguzi, ili kuboresha huduma wakati wa Kliniki, wakati wa kujifungua, baada ya kujifungua na huduma baada ya mimba kuharibika.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali, haiwahadai wananchi, jitihada zinafanywa kuhakikisha kuwa kila mwanamke mjamzito anapata huduma bora, ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na hatimaye kufikia lengo la Milenia Namba 5. Ili kuonyesha jinsi Serikali, ilivyo na nia ya kuboresha huduma hizo mwaka 2011/2012 zilitengewa shilingi bilioni 11 na milioni 355 kwa ajili ya vifaa vya kujifungulia, dawa za uzazi wa mpango na chanjo na kupokea 100% ya fedha zilizotengwa. Aidha, mwaka 2012/2013 jumla ya shilingi bilioni 15 na milioni 623 zilikuwa zimetengwa na kiasi cha shilingi bilioni 15 na milioni 663 zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa, nia ya Serikali ya kutoa huduma kwa mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka 5 bila malipo, ipo palepale haijabadilika. Aidha, jukumu la kutekeleza Sera hii, linahitaji usimamizi madhubuti katika ngazi zote. Mamlaka za Usimamizi zinawajibika kusimamia utekelezaji wa Sera hii.

Kwa mantiki hii, mtumishi yeyote atakayethibitika kuwatoza akinamama wajawazito, atakuwa amefanya kosa kwa mujibu wa Sera. Hivyo Serikali, haitasita kuchukua hatua za kinidhamu dhidi yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi na Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma. Asante sana.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwanza; kwa kuwa, Watumishi wa Afya, Madaktari na Manesi, wanalazimika kuwatuma wenza wa wale akinamama wanaokwenda kujifungua kununua vifaa hivyo, siyo kwa kuwa wanapenda ni kwa sababu, havipatikani katika vituo hivyo vya afya.

Je, Naibu Waziri, leo uko tayari kuwatangazia wamama wote wajawazito na ambao wanatarajia kwamba, pale watakapotumia fedha zao Serikali, itawa-*refund* haraka sana baada ya kujifungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika Mkutano wa 11 wa Bunge, uliopita, Wizara ya Afya iliwapa Wabunge Semina jinsi gani Mkoa wa Singida umefanikiwa kumaliza tatizo la ukosefu wa dawa katika Hospitali zao na vifaa tiba. Napenda kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali, imetumia uzoefu wa Mkoa wa Singida, ili kuhakikisha Mikoa mingine yote na vituo vingine vyote vya afya nchini, vinamaliza tatizo hili la ukosefu wa madawa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Gekul, ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba, utaratibu wa utoaji huduma nchini kote unaenda katika kutekeleza Sera ya Afya, pamoja na kuhakikisha kwamba, tunatumia rasilimali zote zilizopo kwenye Kituo katika kutoa huduma. Pale rasilimali hizo zinapokuwa zimepungua au

kuna uhaba, basi inakuwa ni jukumu sasa la mgonjwa au jamii inayotuzunguka au Halmashauri, kuchukua hatua ya kuweza kusaidia na kuweza kutatua tatizo linalojitokeza, ikiwemo upungufu wa vifaa au kununua kitu ambacho kimekosekana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kwamba, Serikali, imekuwa ikoongeza uwezo wa kufanya vituo hivi viwepo na viwe na zile *delivery parks,* ambazo tumezifanya sasa ziwepo katika vituo. Itakapokuwa inatokea *delivery parks* hizo zina upungufu basi hatua za dharura zinaweza zikawa zinachukuliwa, lakini hatuna utaratibu wa kufanya *refund.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba, uzoefu wa Mkoa wa Singida katika kudhibiti dawa na vitendea kazi katika Hospitali za Mkoa wote wa Singida ni mzuri. Na kutokana na ukweli kwamba, Mganga Mkuu wa Mkoa ule tulimpa nafasi na fursa, akaweza kutoa maelekezo ya namna ambavyo yeye anafanya kwenye Kikao vya Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya kilichofanyika hapa Dodoma katika kipindi kilichopita, uzoefu ule umejaribu kwenda.

Lakini, naomba nitoe angalizo moja tu, kutokana na ukweli kwamba, jitihada za mtu mmoja katika kufanya, hafanyi vile ambavyo ataweza, itakuwa ni kipindi tu cha mpito ambacho yule mtu atakuwa kwenye uongozi wake. Cha maana na kikubwa ambacho Serikali inafanya ni kuhakikisha kwamba, tunakuwa na mfumo madhubuti kuhakikisha kwamba, tunasimamia uwepo na matumizi

bora ya rasilimali zote ikiwepo dawa pamoja na watumishi na vitendeakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo tuna mkakati tunaouita *E-Health,* ambao upo njiani kukamilika na tunaweza tukafika hatua ya kuutekeleza. Lakini katika kudhibiti dawa tumeshaweka sasa, na dawa zinazoagizwa kuanzia mwaka huu zimeshawekewa na baadhi ya vidonge nimeviona, tayari vina nembo yenyewe kwenye kidonge chenyewe kimeandikwa *GOT;* maana hiyo ni kwamba, dawa hizo zitakapokuwa zimeingia kwenye vituo vya Serikali, tunategemea dawa hizo hazitatoka tena kwenda kwenye maduka ya watu binafsi na tutakuwa tunasimamia. Dawa kama hiyo tukiikuta kwenye duka la mtu binafsi, basi hatua stahili zitachukuliwa dhidi ya huyo mtu.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, tatizo hili la matibabu pia limekuwa kubwa sana hasa kwa wazee wa Jiji la Mbeya, ambao wamekuwa wana kadi za matibabu bure, lakini wakienda Hospitali wanapata usumbufu sana; nini tamko la Serikali, katika hili? Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo mgonjwa anafika kwenye kituo akiwa ana kadi ya bima kwa mfano au yeye yumo katika kundi ambalo kwa mujibu wa Sera ya

Afya wamo katika msamaha, taratibu pale ziko za namna mbili tu; ya kwanza, yule ambaye yumo katika Sera ya Msamaha anatakiwa apate zile huduma kulingana na Sera yetu ya Msamaha. Lakini yule ambaye anatakiwa kuchangia, kutakuwa na namna mbili ambazo zinatakiwa pale kufanyika, kama yumo katika kuchangia katika tafsiri kwamba, anayo bima, basi ataendelea kupata zile huduma.

Mheshimiwa naibu Spika, nirudie kusema tena kwamba, tatizo la kutokuwepo dawa au tatizo la kutopatikana huduma stahili inayotakiwa katika kipindi kile kwa mgonjwa maalum ni tatizo ambalo hatuwezi kulizuia leo. Lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba, tunaweka utaratibu mzuri ili kuhakikisha vifaa vinakuwepo, Waganga wanakuwepo wenye uwezo huo na dawa zile zinadhibitiwa, ili ziweze kutumika kwa muda mrefu na kuweza kuwaokoa na kuwatibia wagonjwa wengi kadiri inavyowezekana.

Na. 23

**Uanzishwaji wa Hospitali za Rufaa za Kanda na Mikoa**

**MHE. AMINA M. MWIDAU K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Hospitali ya Muhimbili, inaonekana kuzidiwa na idadi kubwa ya wagonjwa kutokana na idadi ya ongezeko la watu nchini, hasa katika Jiji la Dar-es-Salaam. Katika

kukabiliana na msongamano wa wagonjwa Muhimbili, Serikali imekuwa na mipango ya kuanzisha hospitali za rufaa Kikanda na Mikoa.

Je, Hospitali ngapi za Kikanda na Mikoa zimeanzishwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imekuwa ikikabiliwa na msongamano wa wagonjwa. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali, ilipandisha daraja Hospitali zote 20 za Mikoa na 3 za Manispaa ya Dar-es-Salaam kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Katika jitihada za kupunguza msongamano huo Serikali, iliongeza idadi ya Hospitali za Kanda kutoka 3 kuwa 5, ambazo ni Mbeya, *KCMC*, Bugando, Hospitali ya Jeshi Lugalo na moja ya Shirika la Kujitolea ya *CCBRT.* Sambamba na hilo, imepandisha daraja Hospitali Teule 10 katika Mikoa 10 na kuzifanya Hospitali za Rufaa ngazi ya Mkoa, ili kusogeza huduma za Kitaalam karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, sambamba na kupandisha Hospitali za Rufaa za Mikoa za

Mkoa wa Temeke, Mwananyamala na Ilala, baadhi ya Vituo vya Afya vimepandishwa daraja na kuwa Hospitali, nazo ni Sinza, Rangitatu na Mnazi mmoja. Serikali kwa kusaidiana na Wahisani, wameziboresha Hospitali hizo kwa kufanya upanuzi wa majengo, kutengeneza vyumba vya upasuaji na maabara na kununua vifaa tiba.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mgonjwa apate matibabu kunahitajika jengo, madaktari, vifaa na madawa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuzipandisha daraja tu Hospitali hizo za Mkoa, bila ya Madaktari Bingwa, bila ya vifaa, bila ya madawa, kweli kutaweza kutatua tatizo la msongamano wa wagonjwa Muhimbili? Ambapo ndio pekee kuna vifaa vya kisasa na Madaktari Bingwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lako la msingi umeonesha kuwa baadhi ya Vituo vya Afya vimepandishwa daraja na kuwa Hospitali, Mnazi Mmoja, Sinza na Rangitatu. Na ni yaleyale, bila ya Madaktari, bila madawa, bila ya vifaa. Je, Mheshimiwa naibu Waziri, huoni kuwa unawadanganya wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na UstaWI WA Jamii, kuna hoja nzito hapo kuwa unawadanganya wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza utoaji wa huduma za afya kote Duniani unaenda sambamba na utekelezaji wa uwepo wa jengo, uwepo wa vifaa, uwepo wa Wataalam, lakini utaalamu uwepo wake unapikwa, unatayarishwa. Ni sawasawa na mtu kwenye kiwanda unazalisha.

Tatizo la kuzalisha Wataalam Tanzania, limetokana na historia tulikotoka mpaka sasa tuliko. Na tumekuwa tukiongeza juhudi hizo, lakini haziendi sambamba na mambo makubwa mawili ya msingi. Kwanza, uzalishaji wenyewe tumeanza kuwa na Vyuo Vikuu baada ya miaka ile ya sabini, ongezeko la Vyuo Vikuu vimeongezeka kwenye miaka ya tisini (1990).

Kwa namna yoyote ile Wataalamu, idadi ya kuwazalisha haikuwa inaenda sambamba na ongezeko la watu kama ambavyo tumekuwa tukienda nalo. Na hii ndio imesababisha nchi zote chini ya Jangwa la Sahara, hata hivi sasa, jumla ya Wataalam wote wa Afya ambao wanatoa huduma chini ya Jangwa la Sahara ni sawasawa na 3% tu ya Watumishi wote Duniani. Lakini Afrika, chini ya Jangwa la Sahara, kwa kuwa na mzigo wa magonjwa ni sawasa na kwamba, tuna mzigo wa magonjwa sawasawa na robo ya mzigo wa magonjwa yote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili ndilo lililotufikisha hapa. Kwamba, tumeongeza juhudi za kuzalisha sio miaka mingi kutoka sasa. Nitoe tu mfano, katika miaka ya 2006/2007, tulikuwa tumepeleka Wataalamu kwenda kusoma katika Vyuo vyetu takribani 3,000 lakini mwaka jana Wataalamu ambao wameingia Vyuoni kwenda kusoma mbalimbali za mambo haya ya kuhudumia wagonjwa wetu wamefikia 7,800 karibu 8,000. Lengo letu ni kufikia Wataalamu 10,000 ambao wanaingia Vyuoni kabla ya mwisho wa mwaka 2015 na ambalo ninaamini tutalifikia. Kwa hiyo, hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa naibu Spika, la pili ni kwamba, Vituo tunavyoviweka pale, ukaviongezea ukazipandisha hadhi, maana yake umetengeneza *demand,* umatengeneza sasa Kituo kile kina ngazi mpya, kinaanza kusema kina upungufu wa Watumishi. Kitaanza kusema kina upungufu wa Jengo kwa ajili ya huduma fulani, kulingana na hadhi yake mpya na hivyo ndivyo ambavyo tutaweza kuboresha na kukifanya Kituo hicho kuwa na hadhi mpya, kuwa na Wataalamu, kuwa na vifaa vinavyolingana na hadhi yake hiyo mpya. Kwa hiyo, maamuzi ya Serikali, kupandisha hadhi hivi vituo sio kuwahadaa wananchi, lakini kuwatayarishia wananchi huduma bora zaidi ambazo watakuwa wanazipata na wanaweza kuzipata. *(Makofi)*

Na. 24

## Mauaji ya Raia Yanayofanywa na Jeshi la Polisi

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Kumekuwepo na wimbi kubwa la mauaji ya raia yanayofanywa na Jeshi la Polisi nchini, hususan Wilaya ya Serengeti na Tarime. Kwa mfano tarehe 29 Machi, 2010 Askari wa Gereza la Tabora *B* la Serengeti alimpiga risasi Bwana Daudi Makabara, ambaye ni mkulima na kumwua. Hata hivyo, askari huyo alikaa Mahabusu miezi kadhaa na kuachiwa huru bila kwenda Gerezani:-

(a) Je, kwa nini Askari huyu hakushtakiwa Mahakamani, kwa kosa la mauaji kama Sheria inavyotaka na kama raia wengine wa kawaida wanavyofanyiwa kwa kosa kama hilo?

(b) Je, nchi yetu ina aina ngapi za mashtaka na uendeshaji wa kesi za jinai?

(c) Je, ni askari wangapi wameshtakiwa kwa kosa la kuua au kulemaza raia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu *(a), (b)* na *(c),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, tukio la mauaji ya Bwana Daudi Makabara, lilitokea tarehe 29 Machi, 2010 katika Gereza la Tabora *B,* lililoko Wilaya ya Serengeti, ambapo Askari Magereza mwenye Namba *B 5000 WDR* Bahati, alivamiwa na kundi la wananchi wakiwa na silaha za jadi yaani mapanga, pinde, mishale, kwa lengo la kutwaa mifugo iliyokuwa imekamatwa ikichungwa katika eneo la Gereza bila kibali. Wananchi hao walimzidi nguvu Askari huyo na mmoja kati yao akiwa katika harakati za kutaka kumnyang'anya Askari silaha, aligusa usalama wa bunduki na kusababisha risasi nne kufyatuka mfululizo, zilizomjeruhi marehemu na hatimaye kusababisha kifo chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tukio hilo mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Upelelezi ulifanyika na jalada kutumwa kwa Mwanasheria Mfawidhi wa Kanda ya Ziwa, ambaye alilipitia na kuelekeza upelelezi zaidi ufanywe. Hata baada ya kukamilisha maelekezo hayo, jalada lilitumwa tena kwake na alibaini kuwa ushahidi uliokusanywa hautoshelezi na hivyo, akafuta Shauri hilo kwa *"Nolle Prosequi"* chini ya Kifungu cha Sheria Namba 91 (i) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985 na iliyorudiwa Mwaka 2002 ya Sheria za nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna aina moja tu ya mokosa ya jinai yanayoendeshwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai na kusimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai *(DPP)* kwa mujibu wa Sheria ya Waendesha Mashtaka, Namba 1 ya Mwaka 2008.

(c) Katika mwaka 2012 jumla ya Askari 6 walishtakiwa kwa makosa ya mauaji hapa nchini. Aidha, kati ya kipindi cha 2010 hadi 2012 jumla ya Askari 29 walishtakiwa Kijeshi na wengine kufikishwa Mahakamani kwa makosa ya kujeruhi, ambayo yalisababisha wahanga kupata ulemavu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, napenda tu kutoa tahadhari kwa Serikali maana tukiuliza maswali kuhusu wananchi kuuwawa na Polisi, wanatumia mwamvuli kwa kusema kwamba wananchi wamevamia kinyume na ukweli. Kwa hiyo, kusema kwamba tukio la tarehe 29/3, wananchi walivamia wakiwa na silaha za jadi, mikuki na nini inatufedhehesha sana Wakurya na hatupendi kwa kweli wananchi wa Mkoa wa Mara, iwe mwisho maana mnateketeza familia, nguvu kazi, vijana wetu kwa kuji-*cover. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali sasa, kwa kuwa marehemu alipigwa risasi mbele ya kijana wake Dickson Daudi baada ya kuamrishwa na Afande mwenzake, Serikali inamjua; na kwa kuwa Mwenyekiti wa kijiji cha Bonchugu ambaye ni wa CCM, Ndugu Samweli Makena, anaujua ukweli na anaweza akasema ukweli wa halali; na kwa kuwa sasa hata aliyekuwa *RPC* wa Mara, Ndugu Robert Boazi analijua hili; na kwa kuwa Naibu Waziri amesema kwamba shauri lilifutwa baada ya ushahidi kutokuwepo, napenda kujua, je, shauri lilifunguliwa katika Mahakama ipi na ni jinai namba ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, swali langu la msingi lilikuwa kwamba, Askari huyu aliweza kukaa kituo cha Polisi Mugumu zaidi ya miezi nane. Nataka kujua, wananchi wa Tanzania wanaokuwa wanatuhumiwa na kesi za mauaji kama Askari huyu, ni wangapi wameweza kukaa Kituo cha Polisi zaidi ya miezi nane wakisubiri ushahidi au maamuzi ya Mwanasheria wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, suala la jumla kwamba pengine kuna visingizio vinavyotolewa katika mauaji, hili naomba kwa niaba ya Serikali nilikanushe. Niseme kwamba Serikali hii inatekeleza *rule of law* na hili sidhani kama linaweza likafanyika. Kama ingekuwa inafanyika hivyo watu hawa hata Mahakamani wasingepelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili kuhusu ushahidi ambao anao Ndugu Jackson Daudi, Ndugu Samweli Makweli na Ndugu Boazi, shauri hili kuondolewa Mahakamani ni kwamba ushahidi zaidi unatafutwa. Kama hawa wanao ushahidi basi na uletwe halafu kesi hii inaweza ikaanza upya na huyo bwana akapata haki kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ni watuhumiwa wangapi wamekaa miezi minane Polisi? Hizi takwimu kwenye hafla hii sinazo lakini naweza nikachukua hatua kuzipata na nikampatia muuliza swali.

Na. 25

**Bunge la Afrika Mashariki Kutumia Kiswahili**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Je, ni kwa nini lugha ya Kiswahili inatumika katika Bunge la Afrika lakini haitumiki kwenye Bunge la Afrika Mashariki *(EALA)*?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 137, inaainisha kuwa lugha rasmi itakayotumika katika shughuli za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Kiingereza. Kwa hiyo, hadi sasa Kiswahili hakitajwa katika mkataba kuwa ni lugha rasmi ya kutumika katika shughuli za Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Umoja wa Afrika, sheria iliyounda Umoja huo, *The Constitutive Act of African Union,* inaainisha katika Ibara ya 25 kuwa lugha zitakazotumika katika shughuli za Umoja huo, ni lugha kuu za nchi wanachama ambazo kwa sasa ni Kingereza, Kifaransa, Kireno, Kiswahili na Kiarabu. Kwa mantiki hiyo,

Umoja wa Afrika unajumuisha lugha nyingi zaidi ikilinganishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni za Bunge la Afrika Mashariki, Kanuni ya 36, inaainisha kuwa shughuli zake zitafanyika kwa lugha ya Kiingereza. Hali hii kimsingi ni ya mpito kutokana na hali halisi kuwa baadhi ya nchi wanachama hawana uelewa mpana na wa kutosha wa lugha ya Kiswahili na pia kuepusha gharama za ziada za uendeshaji kwa kutumia lugha zaidi ya moja. Tunaamini kwamba kutokana na juhudi za Tanzania na Kenya hali hii itabadilika katika siku za usoni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njwayo ameridhika, Mheshimiwa Njwayo swali la nyongeza.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Kiswahili kimeendelea kwa kasi sana Afrika Mashariki na Duniani kote kiasi cha kuchangia ajira nyingi na vilevile kuwepo kwa vyuo Vikuu karibu 100 Duniani vinavyofundisha Kiswahili; na kwa kuwa chimbuko la lugha hii ni Afrika Mashiriki, je, kuna mpango wowote maalum wa kukiendeleza Kiswahili na hatimaye kuwa lugha rasmi ya Jumuiya hii?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za kuendeleza Kiswahili ni kubwa sana na hivi ninavyozungumza tunao Walimu wa Kiswahili takribani 1000 katika nchi mbalimbali za Afrika Mashariki lakini hilo ni suala tofauti. Suala la kukubaliwa lugha iwe lugha rasmi ya kutumika katika shughuli za Umoja

wetu huu wa Afrika Mashariki, linahitaji maridhiano na uzoefu wangu ni kwamba kila ambapo tumekuwa tukiliomba likubalike, wenzetu wa Rwanda na Burundi hasa wamekuwa wakitaka na Kifaransa pia kitumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukiwa na lugha tatu; Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa, uendeshaji unakuwa na gharama kubwa na mkumbuke tu Waheshimiwa Wabunge kwamba kuendesha shughuli za jumuiya ni michango tu ya wanachama na bajeti yake siyo kubwa. Kwa hiyo, hadi sasa jambo hili halijafikia mahali ambapo tumepata maridhiano ya wote na ndiyo maana bado tunasema hii ni hatua ya mpito lakini ipo siku ambayo Kiswahili kitakubalika kuwa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Na. 26

**Kampuni za Simu Kuuza Kazi za Wasanii kama Miito ya Simu *“Ring Back Tones (RBT)”***

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kampuni za simu hufanya biashara ya kuuza kazi za wasanii kupitia miito ya simu *(Ring Back Tones) (RBT):-*

(a) Je, katika mwaka ulioishia Desemba, 2012 kampuni hizo ziliingiza pato ghafi kiasi gani kwa biashara hiyo na kati ya pato hilo ililipa asilimia ngapi kwa kila mmoja wa hawa; msanii husika *content provider* na ni asilimia ngapi ilibaki kwa kampuni ya simu husika?

(b) Mwezi Januari, 2012, wimbo wa ‘KESHO’ wa msanii Diamond ulinunuliwa na watu wangapi kwenye mitandao ya Tigo, Vodacom, *Airtel* na *Zantel* na wimbo uliingiza mapato kiasi gani *(turn over)* kwa kampuni hizo na msanii husika alilipwa kiwango gani kwa kazi yake hiyo?

(c) Je, ni lini Serikali itatunga Kanuni za kuweka wazi mapato ya kazi za sanaa kwa kampuni za simu na kiwango cha chini *(minimum percentage)* cha Mtanzania kulipwa kutokana na pato ghafi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna taarifa mahsusi za pato ghafi lililotokana na biashara ya kuuza milio ya simu kwa kuwa makampuni ya simu kutokana na mauzo ya makampuni ya simu, kutokana na huduma na bidhaa mbalimbali kwa mfano *message,* M-pesa, vifurushi vya *internet,* huchanganywa na kuripotiwa Serikalini kama pato la jumla. Hata hivyo, kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa *Ben,* Mtunzi anapaswa kulipwa si chini ya asilimia kumi ya bei ya rejareja ya ya kila nakala ya kazi inayouzwa sokoni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, kwa kuwa makampuni ya simu yanaporipoti mapato yao kwenye mamlaka husika, huripoti mapato ya jumla, makampuni haya hayajaripoti kwamba kila wimbo kati ya maelfu ya nyimbo umeingiza shilingi ngapi na kila Msanii kati ya mamia ya Wasanii amelipwa shilingi ngapi. Hata hivyo, wasanii wenyewe wapo katika fursa nzuri ya kusema wamelipwa kiasi gani kwa kuwa wameingia katika mikataba na makampuni haya.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukubaliana na changamoto zilizopo kwenye suala la usambazaji wa kazi za Wasanii kupitia simu za mikononi, Wizara yangu iliitisha kikao cha wadau na baadaye kuunda Kamati iliyoshirikisha Wizara ya Viwanda na Biashara, COSOTA, BASATA, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Makampuni ya Simu pamoja na wawakilishi wa wasanii. Pamoja na mambo mengine Kamati hii imedhamiria kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuweka utaratibu wa kufanyia marekebisho Sheria za *COSOTA*, Sheria ya BASATA na Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ili kuondoa mwingiliano wa majukumu na kurahisisha malipo ya haki kwa wasanii.

(ii) Kamati hii iliadhimia kwamba malipo ya msanii yasiwe chini ya kiwango kinachotajwa na Sheria kwa mapato yanayoingia kwa *operator* na wala siyo kwa *content service providers* ili kuondoa utata wa kudhulumiwa kwa wasanii.

(iii) Kamati hii iliadhimia kwamba *COSOTA* izichukulie hatua za kisheria kampuni zinazowalipa wasanii chini ya kiwango kilichowekwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kufuatilia utekelezaji wa maadhimio haya. Serikali vilevile kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara ipo kwenye mchakato wa kuweka utaratibu wa wazi na wa haki zaidi kuwezesha wasanii kunufaika kwa kazi zao zinazopigwa kwenye *radio* na *television* kama Serikali inavyotaka.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, si haki kusema kwamba wasanii ndiyo wanaotakiwa waseme kwamba wanapokea kiasi gani kwa sababu hiyo ni sawasawa na kurudisha mpira kwa wasanii ambao tayari wameshalalamika kwetu sisi Wabunge na ndiyo sisi tumelileta kwenu nyinyi Serikali ili kuwasaidia kwa sababu wao wameshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema, ni udhaifu kusema kwamba Serikali haiwezi kupata *data* kwa sababu haya makampuni yana *data* kama ambavyo wana *data* za *text message,* wana *data* za simu tunazopiga, wanachofanya ni kuficha ukweli na kuendelea kuwanyonya wasanii wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi, kwanza, kwa nini Serikali isiunde sasa Timu Huru siyo Tume, Timu Huru ya wataalamu kwa sababu unasema umeshirikisha wadau lakini unakuta haohao wadau unaosema umewashirikisha, ukirudi ndiyo haohao wasanii wanawalalamikia kwamba

ndiyo vinara wa wizi mara nyingi. Kwa nini Serikali isiunde Tume Huru kama ilivyomtuma Dokta Aikaeli wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye alileta ripoti kwamba mapato ya kazi za sanaa ni *around* shilingi bilioni 91 lakini Serikali inashindwa kuya-*control* au kuya-*fetch. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa sasa swali.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Kwa nini isiundwe Tume Huru ambayo itafanya kazi ya kujua ukweli wa mamilioni ambayo yanaibiwa na makampuni haya ya simu kutoka kwa wasanii? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mimi sioni kama Serikali ina dhamira ya dhati ya kuwasaidia wasanii au la haijui nini cha kufanya katika hili. Madhara yake ndiyo unakuta wasanii sasa wanakuwa wahanga wa madawa ya kulevya. Nitatoa mfano na hili atanijibu Waziri wa Fedha kwa ruhusa yako*...(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa swali moja kwa moja.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Tumefikia hatua gani kuhusiana na stika za *TRA* ambazo kwanza tulisema zingeanza Januari mwaka jana lakini baadaye tukasema zingeanza Januari mosi mwaka huu na mpaka leo nikipita barabarani najaribu kuitisha *CD* za wasani hazina stika za *TRA. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wasanii wamekuwa wanapunjwa na wananyonywa katika kazi zao na ndiyo maana Serikali imechukua hatua madhubuti za kumaliza tatizo hilo. Dokta Aikaeli wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye Mheshimiwa Mbunge amemtaja kama alifanya huo utafiti, napenda tu kumpa taarifa kwamba fedha za ule utafiti alioufanya Dokta Aikaeli, shilingi milioni 19, shilingi milioni 16 alilipa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete toka Ikulu, kwa maana yeye mwenyewe na Serikali kwa ujumla unyonyaji huu unatugusa na siku zote tumekuwa mstari wa mbele katika kutetea kazi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningependa kusema tu ni kwamba Mheshimiwa Mbunge angekuwa anashiriki naye na angekuwa anatufuata Wizarani kujua juhudi tunazofanya na ninamwalika kushiriki katika mchakato wa kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo lake la kuunda Tume Huru, tunalichukua, ni wazo zuri na tunamwomba naye ashiriki kwa sababu naye ni msanii, ashiriki katika kumaliza matatizo haya na tuache tu kulaumu na kupiga kelele wakati fursa za kusaidia kumaliza matatizo haya zipo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pato ghafi ni pamoja na huduma zinazotozwa na kampuni ya simu bila mteja kutaka. Utakuta kwenye simu unaambiwa ombi lako limekubaliwa na gharama ya ombi lako ni Sh.350 bila kutaka ombi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili tuliliuliza Bungeni. Tatizo linakuja, ukitazama wateja wa simu nchini mwetu milioni 28, ukichukua watu milioni tano tu watakaotozwa Sh.350 kwa siku ni takribani makampuni haya ya simu yanapata shilingi bilioni 630 kwa njia ambazo si halali za mteja mwenyewe kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulivyouliza swali hili hapa Bungeni, majibu yaliyotolewa ni kwamba makampuni haya yameomba muda, hivi makampuni haya yanaomba muda kudhulumu watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni wakati gani sasa Serikali itadhibiti, hii ni *program* tu, una i-*program within a second* inatoka na tena mapato haya ambayo Watanzania wanalipa bila wenyewe kutaka ni dhambi kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nataka kujua, lini sasa tatizo hili litazuiwa na mtu akitaka huduma aiombe siyo alazimishwe kukatwa fedha bila yeye mwenyewe kutaka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niweke

taarifa sahihi kwamba watu wanaotumia simu siyo milioni 25 hizo ni *sim card*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba ni kweli lipo tatizo kubwa na Serikali imeanza sasa na kwenye Wizara yetu tumewaagiza *TCRA* wakae na wataalamu wetu tuandike kanuni mpya za kudhibiti mambo anayosema Mheshimiwa Zungu. Siyo tu kudhibiti mambo hayo ya kwamba unalipia huduma ambayo hukuitaka lakini vilevile mambo mengine kwa mfano unapopiga simu inaita hukumpata lakini ukiangalia salio limepungua, tunadhani pia hiyo ni dhuluma. Pia tumebaini kwamba kuna upungufu katika Kanuni za Sheria yetu ya *EPOCA* na hivi tunavyozungumza, wataalamu wanakaa na kuandika Kanuni mpya za kubana makampuni ya simu katika mambo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine tu ni kwamba katika udhibiti, teknolojia ni muhimu na huko nyuma tulikuwa tunapungukiwa na teknolojia ya kudhibiti baadhi ya mambo ambayo tumeyaweka kwenye Kanuni, kwa mfano ubora wa huduma. Zipo Kanuni zinaitwa *Quality of Service Regulations* ambazo zinataka simu yako isikatike katikati mara kadhaa. Sasa hatukuwa na uwezo wa kujua kama zile *Quality of Service Regulations* zinazingatiwa kwa sababu hatukuwa na teknolojia hiyo lakini kuanzia mwezi Oktoba mwaka huu tumefunga mtambo ambao utatusaidia na sisi kujua kama zile Kanuni zetu za ubora wa mawasiliano zinatimizwa kwa teknolojia na kwa uhakika zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Ni matumaini yangu kwamba hili jambo la Kanuni halitakuwa ni sababu ya mabilioni ya shilingi kuendelea kupotea. Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

Na. 27

**Kutoa Siri za Mawasiliano ya Simu za Wateja**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Mawasiliano ya simu ni siri kwa mtumiaji wa simu kwa mujibu wa sheria lakini baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni za Simu hasa *Zantel* wamekuwa wakitoa siri za mawasiliano ya simu za wateja/watumiaji wao kinyume cha sheria:-

(a) Je, Serikali inatoa tamko gani dhidi ya kadhia hii ya kukashifiwa kwa watumiaji wa simu hasa *Zantel*?

(b) Je, ni adhabu gani inayotolewa kwa wale wanaobainika kufanya kosa kama hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa kifungu cha 98 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta *(EPOCA)* ya mwaka

2010 ni kosa kwa mtoa huduma kutoa siri za mteja au mtumiaji bila kibali cha mamlaka husika. Kwa mujibu wa sheria hii, taarifa za matumizi zinaweza kutolewa pale ambapo kuna uchunguzi wa kijinai, kuhusu matumizi ya namba ya simu husika. Iwapo mtu ana malalamiko kuhusu matumizi ya namba yake ya simu, anatakiwa kuwasilisha malalamiko hayo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ambapo kuna kitengo mahususi cha kushughulikia malalamiko ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 6(e) cha Kanuni za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano *(EPOCA)* yaani *Consumer Protection Regulations* za 2011, watoa huduma wana wajibu wa kulinda taarifa za wateja wao ili zisitolewe bila kufuata utaratibu wa kisheria. Kifungu cha 6(f) cha Kanuni hiyo kinamtaka mtoa huduma kutokutoa taarifa za mteja kwa mtu mwingine bila idhini ya mteja isipokuwa pale anapotakiwa kufanya hivyo kwa mamlaka husika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba matakwa haya ya sheria yanatimizwa. Vilevile Serikali inaendelea kuyabana makampuni ya simu kuwadhibiti wafanyakazi wake wanaotoa taarifa za mawasiliano ya wateja bila idhini yao. Kwa sababu hili ni tatizo kubwa sana kwamba kuna rushwa kwa baadhi ya wafanyakazi wa makampuni ya simu ambapo hutoa taarifa kwa wateja kwa watu ambao wanazungumza nao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 inatoa adhabu

kwa makosa haya. Kifungu cha 120, kinasema kwamba mtu yeyote ambaye anaingilia au anajaribu kuingilia au anamtaka mtu mwingine kuingilia mawasiliano ya mtu mwingine au anatoa taarifa za mawasiliano kwa kujua au kwa kuamini kwamba taarifa hizo zimetokana na kuingiliwa kwa mawasiliano, anakiuka matakwa ya sheria. Akipatikana na kosa hilo, atatozwa faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni tano au kifungo cha jela kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina maswali mawili. Je, ni wafanyakazi wangapi wa makampuni ya simu waliowahi kufungwa au kutozwa faini kwa kutoa siri za mawasiliano ya wateja wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, tokea Serikali kuanzisha kodi ya laini za simu, makampuni ya simu yame-*take advantage* na kuwatoza watu gharama kubwa sana kwa matumizi ya simu. Je, Serikali inawalindaje watumiaji wa simu za mkononi na wizi huu mpya uliokithiri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kwa hapa niliposimama, sina taarifa ni wafanyakazi wangapi wa makampuni ya simu wamefungwa kutokana na kutoa

taarifa za wateja bila ridhaa yao au bila kutumia mamlaka husika. Hata hivyo, niko tayari kuwasilisha taarifa hizi kwa Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa mara nitakapokuwa nimezitafuta na kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya swali lake, ni kweli kwamba kumekuwa na dhuluma kubwa, kama nilivyosema awali wakati najibu swali la mwanzo, kwa makampuni ya simu kwa kutoza gharama kwa wateja katika huduma ambazo hawakuzihitaji na kama nilivyosema kuna upungufu mkubwa kwenye Kanuni lakini vilevile kwenye teknolojia ya kujua kwamba hilo linafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile liko tatizo kubwa kuhusu *consumer protection* kwa ujumla. *TCRA* wanalo Baraza la Kulinda Wateja *(TCRA-CC)* ambalo kwa muda mrefu limekuwa halina nguvu wala meno ya kuweza kudhibiti baadhi ya dhuluma zinazofanyika kwa wateja. Kwa hiyo, katika mwaka huu tumekubaliana na *TCRA* wenyewe kuliongezea uwezo Baraza hili na lijitangaze ili walaji walijue na waweze kuwasilisha malalamiko yao kwenye Baraza na kuhakikisha kwamba haki zao zinalindwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakiri kwamba upo udhaifu wa wateja kutojua mahali pa kuripoti mara wanapokuwa na malalamiko. Serikali inaahidi kwamba itaweka wazi utaratibu wa namna ya kuripoti malalamiko kama haya na kufuatilia utekelezaji wa utatuzi wa malalamiko yao dhidi ya makampuni ya simu hasa kuhusiana na dhuluma hizi.

Na. 28

## Mashamba yanayomilikiwa na wageni Wilayani Arumeru

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE (K.n.y. MHE. NAMELOK E. SOKOINE)** aliuliza:-

Asilimia 50% ya ardhi katika Wilaya ya Arumeru ni mashamba makubwa yaliyokuwa yanamilikiwa na wageni ambayo kwa sehemu kubwa yametelekezwa huku wananchi wa kijiji cha Oldonyosambu wakiendelea kuteseka baada ya Serikali kutwaa ardhi yao mwaka 1984 na kuikabidhi JWTZ wakiahidiwa kupewa ardhi mbadala lakini hadi sasa hawajapewa na kuwafanya kukosa mahali pa kulima na pa kuishi.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mustakabali wa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwisha kuanza kutekeleza ahadi ya kuwagawia ardhi wanavijiji wa

Oldonyosambu ambao ardhi yao ilitwali na Serikali kwa ajili ya manufaa.... *(Makofi)*

*(Hapa Naibu Waziri alikuwa akitafuta kitu kwenye iPod yake)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *sorry*. Ni kweli kuwa mwaka 1984, Serikali ilitwaa ardhi ya Kijiji cha Oldonyosambu na kukabidhi Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Wananchi hao waliahidiwa kupewa ardhi mbadala ahadi ambayo Serikali imeendelea kuitimiza kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Mwaka 1997 baadhi ya wananchi waligawiwa ardhi kwenye mashamba Na. 1, 5, 10 na 13 yaliyoko eneo la Oljoro yenye ukubwa wa ekari 6,051 ambayo yalikabidhiwa Halmashauri ya Wilaya Arumeru ili iwagawie wananchi husika.

(ii) Kutokana na udogo wa ardhi iliyotolewa ikilinganishwa na idadi ya wananchi ambao ardhi yao ilitwaliwa Oldonyosambu, Serikali imeendelea na jitihada za kupata ardhi sehemu nyingine ili kuwamilikisha wananchi hao. Kutokana na umuhimu ambao Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeweka katika kutatua kero za wananchi, tarehe 20 Machi, 2012, Mheshimiwa Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha awapatie wananchi hao ardhi kwenye eneo lililokuwa linamilikiwa na Jeshi la Wananchi

katika eneo lililokuwa la *Tanganyika Packers*, Kata za Moshono na Mlangarini.

Hata hivyo, uhakiki wa eneo hilo ulionesha kuwa, ardhi iliyoko ni kidogo ikilinganishwa na idadi ya wananchi wa Kata za Mshono, Mlangarini na Oldonyosambu ambao wote wanahitaji ardhi kwa ajili ya kilimo na makazi. Hivyo, Serikali ilielekeza kuwa, uongozi wa Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Arumeru watafute mashamba yasiyoendelezwa ili Serikali iyatwae na kuwamilikisha wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya uhakiki wa mashamba Wilayani Arumeru na hususan eneo la Oldonyosambu imekamilika na hivi sasa Mkoa unakamilisha maandalizi ya taarifa ambayo itawasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ili kibali cha Mheshimiwa Rais kiombwe kwa ajili ya kuyafutia miliki. Kwa kuwa suala la wananchi hawa limechukua muda mrefu, kupitia Bunge lako Tukufu natoa maelekezo kwa uongozi wa Mkoa wa Arusha, kuhakikisha kuwa taarifa ya uhakiki na mapendekezo ya utoaji mashamba hayo inakamilika ili kibali cha Mheshimiwa Rais kiombwe kabla ya mwisho wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali, nawashukuru sana wananchi wa Oldonyosambu, kwa uvumilivu wao na nawasihi waendelee kuwa na subira hadi taratibu za kuwapatia ardhi zitakapokamilika.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu

Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa uhakiki wa mashamba haya umekamilika, je, Serikali inajipanga vipi katika zoezi la ugawaji wa mashamba haya kuhakikisha yanatolewa bila upendeleo ili walengwa wakuu waweze kupata mashamba haya?

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba wananchi wanaostahili kupatiwa ardhi, wanapata ardhi hiyo kwa utaratibu ufuatao. Kwanza, tumeshafanya uhakiki na kupata idadi halisi ya wananchi ambao wanahitaji ardhi na orodha ya wananchi wale imewasilishwa na mapendekezo ya kutwaa mashamba hayo yatakapopelekwa kwa Mheshimiwa Rais, yatapelekwa pamoja na orodha ya wananchi wale ambao watanufaika.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kabisa kwa siku ya leo, Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wawekezaji wa ndani na nje, kutumia ardhi yetu kwenda kukopa benki na pindi mtikisiko wa uchumi unapokuwa mkubwa, wamekuwa wakishindwa kuwekeza na wakati wananchi wanahitaji ardhi hiyo na mwisho wake kuleta migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa maeneo mawili. Kuna Kampuni ya Bioship ya Kilwa, ilichukua ardhi zaidi ya vijiji vinne kwa ajili ya kulima mibono, baada ya kukosa mikopo wameshindwa kuwekeza na matokeo yake wanafanya biashara haramu ya kuvuna mbao. Pili, kulikuwa na mashamba ya *NAFCO* maeneo ya Kigamboni, wakamuuzia mwekezaji Manji, zaidi ya heka mia mbili na hilo eneo lipo, limeshindwa kuwekezwa. Sasa tunaenda katika mkakati wa kilimo cha *SAGCOT*, nilitaka kujua Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wawekezaji wanaopewa maeneo wana mitaji ya kutosha na kutumia maeneo hayo kwa uwekezaji ambao wamepanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kifupi uwezavyo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumezingatia mifano ambayo Mheshimiwa Mbunge ametupa na napenda tu kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekwishabaini matatizo hayo ambayo wenzetu wanakuja na kutujulisha nia yao ya kuwekeza katika kilimo lakini baada ya kupewa ardhi, kikubwa wanachofanya ni kwenda kutumia ardhi ile kukopa. Wakishakopa, fedha zile haziendi sana kwenye kilimo, huenda kwingine na baadaye hutafuta visingizio vya kutaka kugawa ardhi ile na kuiuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, tumechukua hatua ifuatayo:-

(i) Tumetoa maelekezo kwamba mwekezaji yeyote anapoleta maombi ya kupewa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi, kabla ya kufikiria ombi lile, ni sharti ijiridhishe kwamba mwekezaji huyo ameleta *business plan* pamoja na kuonyesha chanzo cha fedha zitakazotumika kwa ajili ya uwekezaji huo.

(ii) Tumemwelekeza Mkurugenzi wa Mipango Miji na Vijiji kwamba kuanzia sasa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo, haitabadilishwa matumizi. Kwa sababu kumekuwa na tabia hiyo, watu wanachukua ardhi halafu kesho wanagawa viwanja ili wauze, wapate fedha harakaharaka waondoke. Kwa hivyo, kuanzia sasa, ardhi ya kilimo hatabadilishwa matumizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaenda kwenye matangazo mtaona kwamba majibu yalikuwa marefu na maswali yalikuwa marefu, kama ambavyo Mheshimiwa Spika mara kadhaa amesisitiza, naomba pande zote tujitahidi kurudi kwenye *line*.

Tangazo la Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo mchana, ukumbi Pius Msekwa B, saa saba.

Mheshimiwa William Ngeleja, Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo mchana saa saba jengo la utawala, ukumbi 219.

Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wanaombwa kukutana ukumbi wa Pius Msekwa saa saba kwa ajili ya kikao chao cha Chama.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wabunge wa Kamati hiyo kukutana ukumbi 227, jengo la utawala, ghorofa ya pili, leo saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue uwepo wa Spika, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda kwenye Kiti chake, akiwawakilisha wananchi wa Njombe Kusini, karibu sana. *(Makofi)*

Pia nimemwona Mheshimiwa Nassari, muda mrefu sana hakuwepo Bungeni, tunakukaribisha.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na uchangiaji katika sheria zetu hizi tunazojadili safari hii, mtakumbuka kwamba wakati ule wa bajeti tulikuwa tunaomba nafasi kupitia vyama vyetu, sasa mabadiliko yale yalikuwa ni wakati wa bajeti peke yake. Wakati huu wa kutunga sheria, tunaendelea kama kawaida, uchangiaji ni dakika kumi na tano kama kawaida na unaomba kwenye Meza kama ilivyokuwa pale mwanzo. Kwa hiyo, naomba wale ambao

mna nia ya kuchangia muendelee kuwaletea Makatibu wetu Mezani kama kawaida.

Baada ya maelezo hayo, Katibu!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naona watu watatu harakaharaka, tuanze na Esther halafu tutaendelea.

**MHE. ESTHER A. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) lakini nijielekeze kwenye Kanuni ya 46(1), sijui kama nitahitaji kuisoma kwa ajili ya muda niendelee?

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. ESTHER A. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nauliza maswali yangu ya nyongeza, swali langu la kwanza la nyongeza halikuweza kujibiwa ambapo nilitaka kujua, je, shauri limefunguliwa katika Mahakama ipi na ni shauri namba ngapi? Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali langu namba 24, hilo lilikuwa swali la nyongeza, hakunijibu kabisa kuhusu hicho kipengele. Nataka kupata Mwongozo wako, ni kwa nini Naibu Waziri hakuweza kujibu swali langu na nifanye nini kuweza kupata hilo jibu maana ni la msingi sana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba Mwongozo wako chini ya Kanuni 68(7). Jana wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri (Sera, Uratibu na Bunge), alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya swali la msingi la Mheshimiwa Catherine Magige, lililohusiana na biashara ya madawa ya kulevya, kwenye maelezo yake alisema iwapo atawataja wale waliotuhumiwa katika biashara hii ya madawa ya kulevya, ndani ya Bunge lako Tukufu hakuna atakayebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo tu kwamba kauli hii inalidhalilisha tu Bunge lako na kutoa taswira isiyo sahihi bali tutakosa mahali pa kuficha nyuso zetu tukitoka hapa hata sisi ambao hatujawahi kushuhudia au kuona madawa ya kulevya inavyofanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesimama kuomba Mwongozo wako kama Serikali au Waziri anaweza kuwataja Wabunge hao kwa majina au vinginevyo afute kauli yake ili heshima ya Bunge lako iweze kubaki mahali panapostahili. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 64(1)(a)(f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema leo asubuhi katika kipindi cha maswali na majibu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alipokuwa anauliza swali la nyongeza, akatoa maeneo mbalimbali ambayo watu wamewahi kufariki na akatoa mfano wa Morogoro, Polisi walivyompiga risasi mtu

mmoja anayeitwa Juma kwenye mkutano. Akatoa mfano wa Ndago, mtu mmoja alifariki kwenye mkutano wa hadhara, kutokana na watu ambao walienda kufanya fujo. Mwisho akasema kwamba, kama sheria ingekuwa inafutwa, *then* Mheshimiwa Mbowe pamoja na Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa walikuwa wanapaswa wawe gerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa Kanuni ya 64(1)(a)(f) na (g), haya ni maneno ambayo siyo ya kweli, haya ni maneno ya kuchafua watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kama haki inatakiwa itendeke; mnakumbuka kifo cha Msafiri Mbwambo, aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Tawi la *USA River*, aliyechinjwa kwa *chainsaw* na waliomchinja wakabainika ni Wenyeviti wa Matawi ya CCM ambao walitoroka kwenye Mahakama ya Arusha wakiwa wamefungwa pingu na wakatoroka mpaka leo hawajulikani wako wapi kwa sababu wangetaja waliowatuma ambao wanatoka katika chama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa, namwomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba afute kauli yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Umemlaumu mwenzako kwa kutuhumu na wewe umeenda kutuhumu. Mheshimiwa Haroub! *(Kicheko)*

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni ya 68(7) pia nikirejea Kanuni ya 46(1) ambayo inasema, Waziri aliyeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali langu la msingi namba 15, kabla halijajibiwa niliomba lijibiwe kwa usahihi, lakini niliuliza maswali ya nyongeza mawili lakini swali langu la pili la nyongeza halikujibiwa kabisa. Swali hilo nilitaka kujua kama Serikali ina mpango gani wa kukusanya mapato katika Halmashauri zetu hasa za mijini, mapato ambayo yanatokana na kodi za maegesho ya magari na kodi nyingine ambazo sikuzitaja katika swali hilo lakini pia zinakusanywa kama kodi za kukusanya taka ngumu, ambazo zinakusanywa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili kama unavyojua limejidhatiti kusaidia Serikali kukusanya mapato, mapato haya yanakusanywa mengi lakini hayafiki Serikali. Mapato yanavuja na ushahidi unaonekana na hata katika takwimu alizoleta Mheshimiwa Waziri. Swali hili Mheshimiwa Waziri aliliacha, hakulijibu, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Kwa sababu ya muda, nitaruhusu moja tu lipate maelezo ya haraka kwa sasa. Mheshimiwa Waziri ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, jana ni kweli nilijibu swali hilo lakini muuliza swali alikuwa anataka mimi niwataje,

yaani Serikali iwe inawataja watu wote wanaotuhumiwa na wanasema kwamba kuna orodha nyingi zimekabidhiwa kila mahali, kwa nini Serikali tuna kigugumizi cha kutaja orodha hiyo ya majina? Sasa mimi nikasema, kazi ya Serikali siyo kutangaza majina. Kazi ya Serikali ni kukamata, kupeleleza na kupeleka kwenye vyombo vya sheria. Nikatoa mfano, yako magazeti yameanza kutangaza na kama kuna mtu anaona kwamba amehujumiwa atakwenda Mahakamani. Hata hivyo, Serikali hii ambayo inaongozwa kwa misingi ya sheria, hatutakubali kutangaza orodha ambazo ni nyingi, nyingi sana zinaandikwa na watu mbalimbali na nyingi zinaandikwa hazina hata majina ya nani ametunga hiyo orodha, majina mengi yanaorodheshwa kila mara. Ndiyo maana nikatoa mfano; nikasema hizi orodha nyingi sana zinazoandikwa, hata sisi Wabunge humu ndani wanatuandika au wanatuorodhesha, humu ndani hatutapona.

**WABUNGE FULANI:** Wataje.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Kwa msingi huohuo nimesema, hata awe nani ameandika katika orodha hizo zinazosambazwa hovyohovyo kwenye magazeti na sehemu nyingine, Serikali haitatangaza hata siku moja mpaka ifanye uchunguzi, ijiridhishe na ndipo hawa watu wanaweza kwenda kwenye vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awe Mbunge ameandikwa kwenye orodha yoyote, awe kiongozi wa namna gani, awe mwananchi wa kawaida akiandikwa kwenye orodha

yoyote na mtu yeyote, Serikali hatutakurupuka kutangaza. Narudia tena hatutakurupuka kutangaza kwa sababu siyo kazi yetu, kazi yetu sisi tumepewa madaraka na uwezo Kikatiba, kuchunguza na kufikisha kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hayo ndiyo yalikuwa majibu yangu ya jana kwamba, sisi hatutakubali kutangaza orodha yoyote itakayoandikwa. Katika orodha hizo zinazosambazwa, mmesoma hata kwenye gazeti la Jamhuri la juzi, kuna majina ya Wabunge humo na majina ya wafanyabiashara. Kazi hiyo hatufanyi sisi, wafanye watu wengine, Serikali hatufanyi kazi hiyo ya kutangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sikuwa nimekusudia kwamba, Wabunge ni wafanyabiashara wa madawa ya kulevya; ila nimekataa Serikali kujiingiza katika kitendo cha kushabikia mambo yasiyo ya ukweli. Serikali itafanya mambo ya uhakika na yaliyo ya kweli yataishia Mahakamani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru, mengine haya nitayatolea maelezo mbele ya safari, Katibu!

## HOJA ZA BUNGE

### Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kuchaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association-CPA)* Kanda ya Afrika

**NAIBU SPIKA:** Naomba nimwite Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Zungu ni Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* kwa Bunge la Tanzania.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda (MB), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Jumuiya ya Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 17 - 27 Julai, mwaka 2013, ulifanyika mkutano wa 44 wa Chama cha Mabunge ya Nchi ya Wanachama Jumuiya ya Madola Afrika, *Commonwealth Parliamentary Association (CPA)*, uliofanyika Windhoek Namibia na Bunge letu liliwakilishwa na Wabunge wafuatao:-

Mheshimiwa Anne Semamba Makinda - Spika, Mheshimiwa Mussa A. Zungu-Mwenyekiti wa *CPA* Tawi la Tanzania, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo – Makamu Mwenyekiti wa *CPA,* Kanda ya Afrika, Mheshimiwa Kabwe

Z. Zitto, Mwakilishi wa Tawi na Mjumbe wa Kamati ya Mipango ya Fedha wa CPA Kanda ya Afrika, Mheshimiwa Magale J. Shibuda, Mheshimiwa Dkt. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine kataka Mkutano huo, ambao lengo lake kuu lilikuwa ni kujadili na kuona ni namna gani nchi wanachama wanaweza kutumia Umoja wao katika kutatua migogoro pamoja na kustawisha maendeleo ya kiuchumi Barani Afrika *(utilizing our Commonwealth Partnership to promote conflict resolution and economic development in Africa)*. Kulikuwa na jukumu kubwa na zito kumchagua Rais wa Chama hiki atakayekuwa kiongozi wa nchi 19 na matawi 45 ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua uwezo na sifa za viongozi wa Tanzania, Tawi la *CPA* Tanzania lilipendekeza jina la Mheshimiwa Anne S. Makinda – Spika, kuwa mgombea wa nafasi hii kwa kuamini kuwa ni mwadilifu, mwenye uzoefu wa kutosha na mchapa kazi na hivyo kuwa na sifa stahiki za kugombea nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada mbalimbali zilizofanywa siku zote na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, za kutangaza nchi yetu kimataifa, zilisaidia sana katika mchakato wa kumnadi mgombea wetu kwa wajumbe wa mkutano ambao ndio walikuwa wapiga kura katika uchaguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi huo, Mheshimiwa Anne S. Makinda alichaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa *CPA* kanda ya Afrika kwa muda wa mwaka mmoja, jambo ambalo limeiletea nchi yetu heshima na sifa kubwa sana kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua jambo hili, natumia fursa hii kuliomba Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi kuridhia Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa *CPA* Kanda ya Afrika kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Bunge la Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Kibunge Jumuiya ya Madola, *The Commonwealth Parliamentary Association*' kwa muda mrefu sasa na imekuwa ikishiriki kikamilifu shughuli za umoja huo na kutoa fursa sawa za uwakilishi kwa raia wake wote bila kujali jinsia, jambo ambalo limewezesha wanawake wengi kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

NA KWA KUWA Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameonesha jitahada mbalimbali za kuitangaza nchi yetu Kimataifa, jambo ambalo limewezesha fursa nyingi kupatikana. *(Makofi)*

NA KWA KUWA katika mkutano wa 44 wa *CPA* –Afrika uliofanyika Windhoek, Namibia, Mheshimiwa Anne S. Makinda - Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, alichaguliwa kuwa Rais wa *CPA,* Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Spika ana uzoefu wa kutosha katika medani za siasa na uongozi kwa zaidi ya miaka 37 kwa kushika nyazifa mbalimbali kama vile kuwa Naibu Spika, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wa Bunge, Waziri katika Wizara mbalimbali, Makamu Mwenyekiti wa *SADC-PF* na kadhalika, jambo ambalo linaondoa shaka ya aina yoyote juu ya uwezo wake. *(Makofi)*

HIVYO BASI Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili linaazimia kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Wanachama Jumuiya za Madola, *Commonwealth Parliamentary Association,* Kanda ya Afrika na kwamba linamtakia kila kheri Mheshimiwa Spika katika kutekeleza majukumu yake haya mapya na mazito, kwa kuongoza nchi 19 na Matawi 45 katika Bara zima la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu. Hoja imetolewa na imeungwa mkono na Wabunge wote, sijawahi kuona Hoja imeungwa mkono kwa kishindo namna hii, hongereni sana.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walishangilia kwa kupiga makofi na vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa kwa niaba yetu sisi sote, niwaombe Wabunge watatu wazungumze kwa kifupi kwa dakika zisizopungua kumi na tano kila mmoja. Tunaanza na Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Rashid Mohammed na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza na mimi nichangie katika hoja hii aliyoitoa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Azimio la kumpongeza Spika wetu wa Bunge, Mheshimiwa Anne S. Makinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kuunga mkono Azimio hili. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuunga mkono Azimio hili japo kila mtu hatapata nafasi ya kusema na akasikika hapa, lakini tu kwamba wote tumesimama kuliunga mkono, ni jambo la heshima sana kwa Spika wetu na Bunge letu Tukufu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabisa kuunga mkono Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu

wa Bunge, Mheshimiwa Anne S. Makinda kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, Mheshimiwa Makinda ni Mtanzania mwenzetu siyo kwamba hapajatokea kuwa na Wenyeviti wengine wa *CPA* Afrika, wapo lakini kwa leo ni Mtanzania. Kwa hiyo, sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri hii, tunayo kila sababu ya kufurahia na Watanzania wenzetu wana kila sababu ya kufurahia uteuzi huu wa Mheshimiwa Anne S. Makinda. Kubwa ni kwamba, yeye ni Spika wetu. Wakati kinara wa Bunge anapopata heshima ya namna hii katika Afrika basi kwa kweli anabeba heshima ya Watanzania wote na kwa kweli amebeba heshima ya sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme heshima hii amepata yeye lakini ni kwa niaba yetu sisi. Ameipata kwa sababu ya uwezo wake wa kuongoza na kwamba amekuwa kiongozi siyo tu kwa kuchupia humu ndani ya Bunge, la hasha! Amekuwa ndani ya Bunge hili na hiki ni kipindi cha nane. Kwa hiyo, anaelewa mambo ya Bunge yanavyokwenda na ni mtu ambaye anaweza kutabiri mambo kwamba hapa linalokuja ni hili. Kwa hiyo, tunampongeza sana na nina hakika atatumia ujuzi wake huo katika kuongoza *CPA* Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni heshima kwa wanawake wa Tanzania na wanawake wa Afrika nzima. Sisi wanawake tumekuwa siku zote tukieleza na kutabiri na kusisitiza juu ya kumpa fursa sawa mwanamke kama anao uwezo wa kuongoza. Sasa hakuna shaka yoyote kwamba,

mwana mama huyu, Spika wa Bunge letu ni kiongozi mwenye uwezo. Kwa hiyo, sisi wanawake tuna kila sababu ya kufurahia uteuzi huu na kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe zaidi ya hapo. Hata kama atagombea *CPA* ya Kimataifa, tunamshauri akagombee tu, tuna hakika tutashinda. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, kwani hata akigombea Urais wa Jamhuri kutakuwa na tatizo gani? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunampongeza sana, apokee salamu kutoka kwa akina mama wenzake ambao ni asilimia 51% ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Anna Abdallah. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikishukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya pili ya kuunga mkono Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Anne S. Makinda, Spika wetu wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, kwa nafasi hii muhimu, kwake na kwa Taifa. Zaidi nisemi kwamba, tangu nimfahamu Mheshimiwa Makinda, mwaka 1977, tulipokuwa pamoja kwenye *Public Accounts Committee*, kwa umahiri wake na

namna anavyojituma katika kazi, haya ndiyo matokeo ya mtu anayejituma katika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makinda ana rasilimali kubwa sana ya uelewa wa taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi, lakini kubwa alilolifanya katika kipindi chake hiki ni kuhakikisha vilevile hawi mchoyo katika kuwa-*promote* na wengine. Ndiyo maana ukaona katika Bunge letu hili amewajaalia na kuwasaidia Wabunge wengine kupata nafasi mbalimbali katika taasisi mbalimbali za uongozi bila kujali vyama, itikadi, rangi, kabila au udini. Mimi naomba tumpongeze kwa hilo na tunajifunza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumpongeze, kwa Tanzania ni bahati, katika Maspika wote niliokaa nao ni mara ya kwanza kuwa na Spika mwanamke. Alikuwa na *challenge* kubwa kuchukua nafasi ya Uspika, lakini amedhihirisha uwezo wake na ndiyo maana leo *CPA* wamemfanya kuwa *president* wa Afrika *CPA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwangu namwomba kwanza Mwenyezi Mungu amwongezee afya, aendelee kutoa mchango kwa Taifa letu, aendelee kuwashauri na vijana vilevile waige nyayo zake, maana bila ya kuwa na watu ambao wana uzoefu, uzoefu wa uadilifu, uzoefu wa kutenda kazi, vijana hawawezi kupata dira nzuri ya kujifunza. Kwa hiyo, naomba aendelee na awe mvumilivu na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu, taasisi hii ya *CPA,* imekuwa ikionekana kama ni chombo cha wenzetu, Waingereza zaidi, sasa tunapata fursa ya kuonekana kwamba ni taasisi inayomilikiwa na nchi za Jumuiya ya Madola ambazo idadi kubwa ni nchi za Kiafrika na Kiasia. Mimi nafikiri hiyo ni kazi muhimu inatakiwa ifanyike sasa hivi ili ionekane inatoa yale matunda ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mheshimiwa Anne Makinda amepata *challenge* kubwa sana kuwa Spika wetu hapa. Wakati mmoja nilikuwa nasema, inahitaji pande zote mbili ili Jaji aweze kufanya kazi yake vizuri. Ili Jaji afanye kazi vizuri, Mawakili wa upande wa utetezi na washtaki lazima wafanye kazi nzuri vilevile, ili yeye aweze kutoa haki. Tumemsadia na wenzetu nje wameona kazi aliyoifanya hapa na ndiyo maana amepata nafasi hii. Naomba tuendelee kumsaidia kufanya kazi zake hapa ndani ya Bunge, tumsaidie katika kazi hii mpya aliyoipata ili nchi yetu izidi kung'ara na heshima yetu tuliyokuwa nayo Tanzania katika nyanja za Kimataifa irudie kama ilivyokuwa zamani na zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nami niunge mkono Azimio hili alilowasilisha Mheshimiwa Zungu, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Anne na ninamwomba Mwenyezi Mungu amsaidie katika kazi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid, ahsate sana. Sasa namwomba Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya azungumze.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wana sifa nyingi lakini wengine wana sifa zilizozidi, ndivyo Mwenyezi Mungu alivyotuumba na ndivyo ambavyo wengine wanapata uongozi. Sasa kwa maana ya Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, mimi naweza kuziweka hizo sifa katika vigezo kumi na nitavisema harakaharaka.

(i) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mtu anayejiamini. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mtenda haki.

(iii) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mchapa kazi. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mzoefu. *(Makofi)*

(v) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni msikivu. *(Makofi)*

(vi) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mbunifu. *(Makofi)*

(vii) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mwelewa. *(Makofi)*

(viii) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda mvumilivu. *(Makofi)*

(ix) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ni mnyenyekevu. *(Makofi)*

(x) Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ana msimamo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, si wengi na hatutakuwa wengi au hawatakuwa wengi ambao wameanza kuwa Wabunge, wamekuwa Mawaziri, wamekuwa Wakuu wa Mikoa, wamekuwa Naibu Spika mpaka kuwa Spika, haiwezekani, ni wachache sana. Hizi ni sifa ambazo zote ni za Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ambazo amemjalia Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hajajitokeza hivihivi, amejengwa, alilelewa, amepikwa, mpaka amefikia hapo. Nani aliyefanya kazi hiyo, lazima tuwape sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa hiyo ni ya wachache na nitawataja. Kwanza, familia yake, wananchi wa Njombe, Watanzania kwa ujumla wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda uongozi wake umeanzia alipokuwa Shule ya Msingi inayoitwa Wemba. Kaenda sekondari

inayoitwa Kilakala, nadhani alianzia Masasi halafu akaenda Kilakala. Vilevile, kasoma Chuo cha Maendeleo na Uongozi Mzumbe, ndiyo walioweka msingi wa Chuo Kikuu cha sasa cha Mzumbe. Sasa mimi nasema Wemba, Masasi, Kilakala, Mzumbe, tunawashukuru kwa kumjenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda mwaka 2015…

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwenzangu mmoja hapa alikuwa ananong'ona, sitamtaja jina, akamwambia mwenzake akasema, unasikia, ni tishio mwaka 2015. *(Vicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitalizungumzia la mwaka 2015 kutokana na mwongozo na vilevile mfano aliouweka. Unajua unaweza ukatenda mambo Kitaifa yakafanyika Kisheria au Kikatiba lakini mengine ni watu kuiga mfano wa watu. Sasa kwa upande wa Mheshimiwa Anne Makinda, yeye kuwa pale, kuwa mfano, kwa sifa nilizozitaja, ninaamini, wasichana wengi nchi hii watataka kuwa viongozi. Naamini, wanawake wengi nchi hii watataka kuwa Wabunge kwamba bila Katiba mpya, mimi naamini kwamba, mwaka 2015 wanawake watakuwa asilimia 55 na zaidi katika Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ahsante sana kwa maneno yako ya busara sana.

Sasa naomba nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* Tanzania, aje ahitimishe hoja aliyoitoa.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijakamilisha hoja yangu hii, kwanza naomba nimtaje Mheshimiwa Nassir Abdallah, Mbunge wa Korogwe na yeye alihudhuria kikao hiki na alikuwa mpiga debe mkubwa sana wa Mheshimiwa Spika. Nimwombe radhi tu kwa kutolitaja jina lake mwanzo kutokana na hitilafu za uchapishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawashukuru Wabunge wote waliounga mkono hoja hii, kwa ujumla wote, lakini vilevile niwashukuru Wabunge watatu mahiri ambao wamesema maneno ya busara, ya hekima na ya kumpa nguvu. Kazi hii si ndogo, ni kazi kubwa sana na kipindi hiki licha ya kuwa yeye ni Spika wa Bunge letu, bado atakuwa na majukumu ya Afrika, majukumu ya migogoro, ya uchumi, ya jinsia na yeye ni Mheshimiwa Spika, yuko mstari wa mbele sana ku-*balance gender,* nampongeza sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namwombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema, umri mrefu, aweze

kutimiza majukumu yake kwa ujasiri na kwa busara kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Z. Azzan, ahsante sana kwa kuhitimisha hoja yako na kabla sijawahoji Waheshimiwa Wabunge na mimi niseme kidogo tu. Imekuwa si kawaida sana kwa nchi yetu kuwatambua na kuwathamini na kuwaenzi viongozi ambao wamechangia sehemu kubwa sana ya maisha yao katika maendeleo ya watu wetu wa Tanzania. Kwa maoni yangu, hili ni moja ya upungufu mkubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania, kutotambua mchango wa mtu ambacho kimekuwepo Tanzania ni lawama kwa viongozi mazuri yao hakuna anayeyaona hata mmoja. Hata mimi Jimboni kwangu nilikuwa najiuliza, sasa ni Mbunge kipindi cha tatu, ni mambo mengi sana yamefanyika ndani ya Jimbo langu, kwa kusukuma na mimi nikiwa na mchango mkubwa pia, hakuna jengo la darasa, wala zahanati, wala choo cha shule ambacho kimeandikwa kwamba jengo hili limewekwa Jiwe la Msingi wala kufunguliwa na Job Ndugai katika Wilaya ya Kongwa, hakuna. *(Kicheko)*

Wanakuja wenzangu wa kila aina wanaweka majina yao lakini mimi hakuna hata moja. Kwa hiyo, siku nikitoka hakuna kumbukumbu hata moja, natumaini hata Wabunge wenzangu wengi ni hivyohivyo.

Kwa hiyo, tuna tatizo hilo katika nchi yetu kutotambua juhudi na michango ya watu, jambo ambalo ndilo

lingesaidia sana kuwapa moyo katika kufanya mambo makubwa zaidi. Sisi tunachokumbuka ni kuwalaumu tu watu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kipekee jambo hili la Azimio hili lililoletwa mbele yetu limenikumbusha mbali na mimi nikiwa mwanafunzi wa Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, kwa sababu nilipofika tu hapa Bungeni niliingia katika Kamati ya Ardhi na Mazingira kwa miaka mitano, akawa ni Mwenyekiti wangu wa Kamati. Miaka mitano iliyofuata nimekuwa Mwenyekiti wa Bunge, yeye akiwa Naibu Spika alikuwa kiongozi wangu. Miaka mitano hii, yeye amepanda amekuwa Spika, bado niko chini yake kama Naibu wake. Kwa hiyo, nimejifunza mambo mengi sana yanayohusu masuala ya Bunge kupitia kwake na yote yaliyoelezwa hapa ni kweli tupu, yaliyoelezwa na Wabunge wenzetu ambao ni mahiri kabisa, wazoefu na tunaowategemea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa niaba ya Wabunge wote, tukutakie maisha marefu Mheshimiwa Anne Makinda, tukutakie utendaji bora na kwa kweli sisi wenzako tuko na wewe kwa pamoja kuhakikisha kwamba nafasi hii ya Rais wa Chama cha Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za Afrika utaisimamia vizuri na tutakuwa pamoja nawe katika kuandaa mkutano mkubwa utakaofanyika Arusha mwakani hapa Tanzania kwa ajili ya Mabunge yote ya Afrika. (*Makofi*)

Kwa hatua hiyo basi, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge niwahoji kuhusu Azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuchaguliwa kuwa

Rais wa Chama cha Jumuiya ya Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola Afrika.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Spika wa Bunge laJamhuri ya Muungano wa Tanzania, lilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nawashukuruni sana, Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI
## Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka *2013 (The National Irrigation Bill, 2013)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, mwasilishaji wa Muswada wa Umwagiliaji, Mheshimiwa Waziri *Engineer* Chiza, karibu. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

## Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 *(The Irrigation Bill, 2013)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**ISSN 0856-035X**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

***No. 6***
***7th June, 2013***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 23 Vol. 94 dated 7th June, 2013*

Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

# THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section* *Title*

PART I
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title and commencement.
2. Interpretation.

PART II

ADMINISTRATION

3. Establishment of National Irrigation Commission.
4. Investment in the Irrigation development.
5. Functions and powers of the Commission.
6. Committees of the Commission.
7. Seal of the Commission.
8. Appointment of the Director General.
9. Appointment of other Directors.
10. Staff of the Commission.
11. Regional Irrigation offices.
12. Regional Secretariat.
13. District Irrigation Department.
14. Appointment of Irrigation Inspectors.
15. Powers of Irrigation Inspector.
16. Restriction of unqualified Irrigation Inspector.

PART III

DECLARATION OF IRRIGATION AREA AND LAND CLASSIFICATION

17. Declaration of irrigation area.
18. Land acquisition for irrigation development.
19. Classification of Irrigation land.

PART IV

CONSTRUCTION OF IRRIGATION WORKS

20. Undertaking of irrigation works.
21. Application for construction of irrigation works.
22. Construction and commissioning of irrigation works by Commission.

23. Consequences of construction of irrigation works.
24. Compensation for damage suffered due to construction of irrigation works.
25. Entrustment of irrigation works.
26. Construction of minor irrigation works.

PART V
CATEGORIZATION AND APPROVAL OF IRRIGATION

SCHEMES AND IRRIGATORS

27. Categorisation of irrigation schemes.
28. Categorisation and approval of irrigators.

PART VI

MANAGEMENT OF IRRIGATION SCHEMES

29. Management of irrigation schemes.
30. Establishment of irrigators' organizations.
31. Objects of the Irrigators' Organizations.
32. Functions of the Irrigators' Organizations.
33. Sources of funds for the Irrigators' Organizations.
34. Procedure for taking up works.
35. Allocation of irrigation plots.
36. Disputes settlement on irrigation schemes.
37. Withdraw and surrender of irrigation plots.
38. Power to prescribe good agricultural practices and irrigation methods
in the irrigation area.
39. Power to take over irrigation works.
40. Irrigation service fees.
41. Operation and maintenance of irrigation schemes.

42. Clearance of banks.
43. Commission to order provision of proper banks.
44. Procedure on failure to contribute for the cost or labour for work to be done by joint labour.
45. Distribution of water from Irrigation works.
46. Prohibited acts.
47. Obligation of land owners in respect of works affecting safety of the irrigation works.
48. Control of navigation and unplanned canal crossings.
49. Inter-basin water transfer for irrigation.
50. Monitoring and evaluation or performance of irrigation schemes.

PART VII

ENVIRONMENTAL AND HEALTH PROTECTION

51. Compliance with environmental requirement.
52. Commission to coordinate and promote irrigation research

PART VIII

FINANCIAL PROVISIONS

53. Establishment of the Irrigation Development Fund
54. Use of the Fund
55. Advances to the Fund.
56. Management of the Fund.
57. Accounts and Audit of the Irrigation Development Fund.
58. Funds of the Commission.
59. Annual budget of the Commission.
60. Accounting and audit.
61. Powers to borrow and invest.
62. Financial year.

PART IX

OFFENCES AND PENALTIES

63. Offences and penalties.
64. Offence by body corporate or firm.
65. Civil liability not affected.

PART X
GENERAL PROVISIONS

66. Duty of secrecy.
67. Service of notices.
68. Keeping records.
69. Stakeholders' meeting.
70. Commission to call for information.
71. Powers of the Minister to require information.
72. Commission to establish and maintain collaboration.
73. Indemnity and liability.
74. Recovery of cost of repairing damage where an offender is unascertainable.
75. Mode of recovery of money.
76. Powers to make Regulations.
77. Transitional provisions.

**SCHEDULE**

## NOTICE

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information

to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam, **OMBENI Y. SEFUE**

5th June, 2013 *Secretary to the Cabinet*

## A BILL

*for*

**An Act to provide for the establishment of the National Irrigation Commission; to provide for the development, operation and maintenance of irrigation and drainage systems; to provide for effective implementation the National Irrigation Policy, the National Irrigation Development Strategy and to provide for other related matters.**

Enacted by the Parliament of the United Republic of Tanzania.

## PART I

## PRELIMINARY PROVISIONS

Short title and Commencement

**1.** This Act may be cited as the National Irrigation Act, 2013 and shall come into operation on such date as the Minister may by notice in the *Gazette* appoint.

Interpretation

**2**. In this Act unless the context otherwise requires-

"authorized officer" means an officer acting for and on behalf of the Commission, Local Government Authority or the Management Committee of Irrigators' Organisation for the purposes of implementation of this Act;

"canal" means an open channel carrying water including situations passing through tunnel enroute;

"channel" means any ditch, channel, aqueduct, trench, conduit, tunnel, sluice, or fluming;

"Commission" means the National Irrigation Commission a established under section 3;

"conduit" means a pipe or line of pipes of any material or a series of culverts joined together for conveyance of water for irrigation or drainage purposes;

"Director General" means the Chief Executive Officer of the Commission appointed under section 8;

"distribution system" includes-

(a) all main canals or conduits, branch canals or conduits, distribution canals or conduits or minor canals constructed, maintained and operated for the supply and distribution of water for irrigation;

(b) all works, structures and appliances connected with the distribution of water for irrigation; and

(c) all field channels, farm channels and other related channels and structures under a sluice or turn out;

"drainage" means the practice of causing water to be removed from the surface or subsoil of land by natural or artificial means for betterment of agriculture or other purposes;

"drainage system" means a series of structures and other allied infrastructure including the main, secondary, tertiary and field drainage canals or conduits necessary for the removal of excess water and salts from an irrigation scheme in order to allow effective agricultural operations and to prevent water logging;

"drainage water" means water which is removed from land by means of drainage works or by natural drainage means;

"drainage works" includes the construction and maintenance of drainage canals and channels including sub-oil drain pipes, culverts, banks, water gates, sluices and other similar works for

drainage purposes;

"Fund" means Irrigation Development Fund as established under section 53 of this Act;

"field channel" means irrigation system channel used to convey irrigation water from tertiary canal into the fields;

"headworks" means the engineering works constructed at the point of abstraction of irrigation water such as structures on a river stream, pumping system or works at a dam or water reservoir;

"Integrated Water Resources Management" means an approach in water resources management and development which holistically considers all users of the resource upstream and downstream of the system including the ecology;

"irrigable" as applied to land means land of such situation and quality as to be capable of being irrigated from the works or proposed works of an undertaking;

"irrigation" means the application of a specific amount of water at a particular location in order to meet the requirements of a crop growing at that location in amounts that are appropriate to the crop's stage of growth, it can also involve the application of water in amounts necessary to bring soil to the desired moisture level prior to crop planting;

"irrigation activities" means operation and maintenance of the irrigation system in an irrigation scheme for the purpose of crop

production;

"irrigation area" means an area irrigated or capable of being irrigated either by gravitational flow or by lift irrigation or by any other method so declared by the Minister under the provisions of section 17 of this Act;

"irrigation efficiency" means a ratio between the amount of water effectively used for crop growth to the amount diverted from the source;

Cap.366

"irrigation Inspector" means an officer appointed under section 14 of this Act to work as inspector;

"irrigation potential" means a total area which is technically feasible, economically and financially profitable, socially viable and environmentally acceptable that is irrigated or capable of being irrigated on the basis of water availability, land availability and suitability;

"irrigation project" means an undertaking to rehabilitate, upgrade, improve or develop an irrigation and drainage system within a specified time frame;

"irrigation scheme" means an area where crops are grown under irrigation through any method including flood recession; gravity or pump fed canal systems supplying either surface or groundwater; water harvesting and pressurized systems such as drip and sprinkler;

"irrigation season" means that period of time determined by the Irrigators' Management Committee during which irrigation water shall be made available to an irrigation area";

"irrigation service" means all activities aimed at enhancing sustainability of an irrigation scheme including but not limited to studies, planning, research, designing, construction, operation and maintenance of irrigation scheme and capacity building programme;

"irrigation service fees" means fees payable and collected in terms of section 40 of this Act for the purposes of meeting costs of development, operational and maintenance of irrigation works;

"irrigation system" means a series of structures and other allied infrastructure including the headworks, water conveyance and distribution systems, farm infrastructure, machinery and equipment, necessary to provide the supply of water for irrigation to a parcel of land;

"irrigation water" means water which is put on to or retained on land in an irrigation area by means of irrigation works and includes water reaching such land as rainfall;

"irrigation works or irrigation and drainage infrastructure" means physical infrastructure developed or installed in an irrigation system for the purpose of facilitating availability of irrigation water from a water source for crop production covering abstraction structures, conveyance structures, distribution structures, drainage structures and on-farm service roads and include-

(a) all canals, field channels, dam and tanks, tube wells and filter point wells which are intended or which may be used for the supply, collection, storage or retention of water for

agricultural purposes;

(b) all works, embankments, structures, supply and escape channels connected with such canals, channels, dams or tanks and spouts installed to supply water;

(c) all water courses which are supplied with water from such canals, channels, dam, tanks or spouts;

(d) all drainage works associated with irrigation systems, that is to say, canals, channels, escape channels from a canal or channel, dam or tanks, weirs, embankments, sluices, groynes, field channels, and other works for the protection or benefit of agricultural lands or for the reclamation of such other lands;

(e) all works intended for preventing or regulating the entry of salt water into agricultural lands;

(f) all works in an irrigation scheme occupied by irrigators for the purpose of facilitating irrigated agriculture such as canals, channels, reservoirs or tanks and all buildings, machinery, fences, gates and other erections on such lands; and any other work which the Commission may, by notification, declared to be an irrigation work;

"irrigator" means an individual, company, or organization which undertakes irrigation operation in a particular scheme;

"irigators' organization" means group of farmers formed and registered under this Act or any other written law and approved by the Commission pursuant to section 30 of this Act to accommodate the joint interests and activities of all the farmers on an irrigation scheme primarily

for ensuring increased crop production and productivity through optimal management of irrigation water and the operation and maintenance of their scheme;

"land or plot holder" means the owner, or any other person in lawful possession of land in the irrigable area of any irrigation scheme recorded as such in the records of the Commission and includes a lease or tenant and cultivator or other person in actual possession, management or control of any irrigable land;

"large scale irrigation scheme" means an irrigation scheme with a command area greater than two thousand hectares;

"lift irrigation work" means an irrigation work by which water is supplied for agricultural purposes with the aid of a pump set or other mechanical devices;

"local government authority" means a local government authority as defined in the Local Government (District Authorities) Act and term "Local Government Authorities" shall be construed accordingly;

"medium scale irrigation scheme" means irrigation scheme with a command area between five hundred and two thousand hectares;

"member" means a member of the Commission;

"Minister" means the Minister responsible for irrigation;

"minor irrigation work" includes any irrigation work facilitating irrigation or useful for the drainage or protection of an irrigable area of not more than

fifteen hectares but shall not include a lift irrigation work;

"prescribe" means prescribed by Regulations or Rules made under this Act;

Cap. 97

"Regional Secretariat" means the Regional Secretariat established under the Regional Administration Act;

Caps. 113 and 114

"right of occupancy" has the meaning ascribed to it under the Land Act and Village Land Act;

"shared functions" means a joint function undertaken or to be undertaken by all stakeholders as may be agreed upon including research, training, extension services, inputs supply, crop development and promotion, irrigation and drainage infrastructure development;

"smallholder farmer" means a farmer engaged in irrigation farming on a small holding of agricultural land which is up to five hectares and which is worked by only himself or with members of his family;

"small scale irrigation scheme" means an irrigation scheme with a command area up to five hundred hectares;

"stakeholders" means a person or an organisation involved in the irrigation sector including central government, local government authorities, Commission, development partners, cooperative societies, producers, dealers of irrigation equipment, input suppliers, research and extension service providers and all persons with vested interest in irrigation development;

"water course" means a river, stream, springs, channel, lake and includes any tributary or branch of any river, stream, springs or channel;

"water management" means all deliberative human activities designed to optimize the availability and utilization of water for agricultural purposes;

Cap. 331

"water resource" has the meaning ascribed to it under the Water Resources Management Act;

"water user" includes any individual or body corporate or a society or an institution or organization using water for any purpose from an irrigation system;

Cap. 331

"water use permit" shall have the same meaning as ascribed to it under the Water Resources Management Act.

## PART II

## ADMINISTRATION

Establishment of the National Irrigation Commission

**3**.-(1) There is hereby established a Commission to be known as the National Irrigation Commission.

(2) The Commission shall be an independent department of the Government under the Ministry responsible for irrigation.

(3) The Commission shall be a body corporate with perpetual succession and a common seal and shall in its own corporate name, be capable of-

(a) suing and be sued;

(b) acquiring and disposing movable or

immovable property;

(c) borrowing money and entering into contracts or other transactions; and

(d) do all such other things for proper performance of its duties, and discharge its functions under this Act and any other subsidiary legislation made thereunder.

(4) Notwithstanding the preceding provisions of this section -

(a) the Commission shall have a duty of notifying the Attorney General of any impending suit or intention to institute a suit or matter for or against the Commission;

(b) the Attorney General shall have the right to intervene in any suit or matter instituted by or against the Commission.

(5) Where the Attorney General intervenes in any matter in pursuance of subsection (4), the provisions of the Government Proceedings Act, shall apply in relation to the proceedings of that suit or matter as if it had been instituted by or against the Government.

Cap. 5

(6) The Commission shall have a governing Board composed of a Chairman appointed by the President and ten other members appointed by the Minister as follows-

(a) a representative nominated from the Ministry responsible for agriculture;

(b) a representative nominated from the Ministry responsible for land;

(c) a representative nominated from the Ministry responsible for water;

(d) a representative nominated from the Ministry responsible for environmental matters;

(e) a Principal State Attorney nominated by the Attorney General;

(f) a representative nominated from the Ministry responsible for local government;

(g) a representative nominated from the Ministry responsible for livestock and fisheries development;

(h) two representatives from the Irrigators' Organizations;

(i) a person qualified in matters relating to irrigation nominated from a higher learning institution that offers irrigation training programme.

(7) The Director General of the Commission shall be the Secretary.

(8) In nominating a representative, regards shall be had on the need to nominate a person who has adequate knowledge in their respective profession and capacity to make decisions.

(9) The provision of the First Schedule shall have effect as to tenure of office, cessation of membership and other proceedings of the Commission.

(10) The Minister may, by Order published in the *Gazette,* amend, add to, vary, revoke or replace any of the provisions of the First Schedule other than the provisions set out in paragraph 2 of the Schedule.

Investment in the Irrigation development

**4**.-(1) Subject to the provisions of this Act, the Commission may by itself or in collaboration with the private sector, invest in the irrigation development as the Commission may deem fit, and may from time to time vary, withdraw or realize any such investments.

(2) The Commission shall exercise such powers for the carrying out of such activities as are necessary and advantageous in the development and management

of the irrigation sector.

(3) The Commission shall primarily oversee, monitor, regulate and supervise the implementation of functions of the Commission as prescribed under this Act.

Functions and powers of the Commission

**5.**-(1) The Commission shall be responsible for coordination, promotional and regulatory functions in the development of the irrigation sector.

(2) Without prejudice to the generality of subsection (1), the Commission shall-

(a) advise the government on implementation and review of the National Irrigation Policy, Strategy, National Irrigation Master Plan and related legislation;

(b) represent the government in the national and international *fora* and collaborate with both local and international firms or organizations in all matters pertaining to irrigation development and management;

(c) coordinate all interventions in irrigation sector conducted by the development partners and other stakeholders;

(d) promote and maintain cooperation in irrigation and drainage with similar bodies in other countries and with international bodies connected with irrigation and drainage;

(e) advise the Minister on declaration of irrigation areas for the purposes of this Act;

(f) plan, carryout studies, design, construct, supervise and administer implementations of the irrigation projects;

(g) establish and maintain irrigation construction equipment centres and provide hiring services to support private sector in the irrigation investment;

(h) register and maintain a register of all Irrigators;

(i) promote institutional linkages training programmes and support the recruitment of persons for purposes of employment in connection with the irrigation sector;

(j) act as a forum for information sharing pertaining to irrigation and drainage matters;

(k) build capacity of the irrigator for effective participation at all levels in irrigation planning, implementation, operation and management;

(l) undertake and coordinate research, disseminate appropriate technologies emanating from the research findings and provide technical support services on irrigation;

(m) promote development of multipurpose water storage facility for irrigation purposes and other social economic activities;

(n) regulate all matters related to irrigation development and overseeing collaborations among different players in the development of irrigation and drainage;

(o) approve construction of irrigation works, standards and guidelines for the development and management of irrigation and drainage;

(p) promote efficient water use in irrigation systems and ensure compliance with the Integrated Water Resources Management approach in irrigation development;

(q) advise the government in all matters relating to development and management of irrigation sector in the country; and

(r) perform any other functions which are necessary for effectively carrying out the purposes of this Act.

Committees of the Commission

**6**.-(1) The Commission may, for the purpose of facilitation of the performance of its functions under this Act, establish such number of Committees to perform specific functions as may be directed by the Commission.

(2) The size functions and terms and conditions of such committees shall be as may be determined by the Commission.

Seal of the Commission

**7**.-(1) The common seal of the Commission shall not be affixed to any instrument except in the presence of the Chairman or the Director General or some other officer of the Commission and at least one member of the Board.

(2) The Commission may appoint and employ agents or officer to manage, administer, transact any business or do any act or render any services required to be transacted or done in the execution of its functions or for the better carrying into effect the purposes of this Act or any other written law enforced by the Commission.

Appointment of the Director General

**8**.-(1) There shall be the Director General of the Commission who shall be appointed by the President from amongst persons who possess high level of integrity, necessary qualifications, experience and competence to manage efficiently and effectively the

affairs of the Commission.

(2) The Director General shall be the Chief Executive Officer of the Commission and shall be responsible for day to day administration and management of the affairs of the Commission and shall in particular-

(a) be responsible for the management of funds, property and business of the Commission and for the administration, organization and control of the staff of the Commission;
(b) enforce the provisions of this Act and any other subsidiary legislation made thereunder;
(c) keep in custody the seal of the commission;
(d) maintain records of all activities of the Commission;
(e) register and maintain a register of irrigators and irrigation schemes;
(f) monitor and assess activities being carried out in the irrigation schemes in order to ensure that they are advantageous to the national economy;
(g) perform any other functions that are necessary for effective carrying out the provisions of this Act.

(3) For proper discharge of his functions under this Act, the Director General may assign his powers provided herein to any officer by title or name.

(4) In the performance of his function under this Act or any subsidiary legislation made thereunder, the Director General shall comply with the directive of the Commission as may be issued from time to time.

Appointment

**9.** There shall be such number of Directors to be

of other Directors

appointed or employed by the Commission from amongst persons who possess high level of integrity, necessary qualifications, experience and competence to manage efficient and effectively the affairs of the Commission.

Staff of the Commission

**10.-**(1) The Commission shall have powers to establish such numbers of sections or offices as it may deem fit for proper discharge of its functions under this Act.

(2)The Commission may appoint such officers or other staff as necessary for the proper discharge of its functions under this Act or any other written law and upon such terms and conditions of service as the Commission may determine.

(3) Officers and employees of the Commission shall hold office for such period, receive such salaries, allowances and benefits, subject to such terms and conditions of services as may be determined by the Commission.

(4) Where a person is seconded or transferred to the service of the Commission under this Act, his terms and conditions of employment with the Commission shall not be less favourable than those of his previous employment in the public service, and his service with the Commission shall be deemed to be continuous with his previous employment in the public service for the purposes of determining his entitlement to and quantum of pension, gratuity or other superannuation benefit.

Regional

**11**.-(1) For effective discharge of functions of the

irrigation offices

Commission, the Commission shall establish such number of region irrigation offices to be headed by Regional Irrigation Managers as it may deem fit.

(2) A Regional Irrigation Managers shall be responsible for the following functions-

(a) provision of expertise and services to the local government authorities in the development and management of irrigation and drainage infrastructure within respective jurisdictions in collaboration with other relevant authorities;

(b) identification of irrigation potential areas for irrigation development within their respective jurisdictions;

(c) preparation of irrigation projects feasibility studies, detailed designs and tender documents;

(d) provision of technical support to local government authorities and the private sector in the development and management of irrigation schemes in their areas;

(e) preparation of manuals for operation and maintenance of irrigation schemes;

(f) assisting in the formulation of farmers irrigation organizations;

(g) incorporate or mainstream environmental management issues in irrigation and drainage plans and designs;

(h) data collection for irrigation data bank;

(i) preparation of plans for the utilization of groundwater and rain water resources for irrigation purposes;

(j) ensuring quality control of irrigation and drainage infrastructure;

(k) supervision of construction and rehabilitation of irrigation and drainage works;

(l) dissemination of new construction innovations on irrigation and drainage infrastructure;

(m) facilitation on the undertaking of adaptive and applied research on various irrigation and drainage aspects;

(n) promotion of renewable energy for irrigation and drainage purposes;

(o) promotion on the use of locally available construction materials tested with positive results for optimization of costs and water losses; and

(p) collaboration with Basin Water Boards established under the Water Resources Management Act to promote integrated Water Resources Management and issues regarding irrigation water use permits.

(3) A regional irrigation manager shall be appointed from amongst senior public officers with relevant qualifications, experience, skills and competence in irrigation development.

(4) The Regional irrigation Manager shall, in the performance of his functions be accountable to the Director General.

Regional Secretariat

**12**.-(1) There shall be recruited within the Regional Secretariat a Regional Irrigation Officer who shall be responsible for coordination of regional irrigation development and in particular-

(a) be a liaison officer between the Commission and the District authorities on the implementation and enforcement of this Act;

(b) facilitate the promotion, development, fostering and upholding of local government authorities in realisation of the goals and targets of those local government authorities in relation to irrigation development;

(c) advise the designation of the District Irrigation Offices in their areas to foster irrigation development and management.

District Irrigation Departments

**13**.-(1) For the betterment of carrying out the provisions of this Act, the Minister responsible for local government may, in consultation with the Minister establish Irrigation Department in a District Authority as may be advised by the Commission.

(2) The District Irrigation Department shall be headed by the District Irrigation Engineer and equipped with professional qualified staff in relevant field.

(3) Functions of the District Irrigation Department shall be to assist the Commission in execution of its functions as provided for under section 5 of this Act.

(4) Without prejudice to the generality of sub-section (3), the District Irrigation Department shall be responsible for the following-

(a) to identify irrigation schemes, planning and designing, construction and operation and maintenance of irrigation schemes in collaboration with the Regional Irrigation Offices;

(b) to provide linkage between Regional Irrigation Offices and irrigators' organizations;

(c) to collaborate with stakeholders in respective districts as regards to the

development and management of irrigation schemes;

(d) to collect, maintain and disseminate data in relation to the irrigation activities in their respective areas;

(g) atatekeleza majukumu yoyote yatakayosaidia utekelezaji wa Sheria hii;

(3) Kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake katika Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu anaweza kukasimu madaraka yake kwa afisa yeyote.

(4) Katika utelekezaji wa majukumu yake katika Sheria hii au Kanuni, Mkurugenzi Mkuu atatekeleza maelekezo ya Tume yatakayokuwa yakitolewa mara kwa mara.

Uteuzi wa Wakurugenzi

**9.** Kutakuwa na idadi ya wakurugenzi watakaoteuliwa au kuajiriwa na Tume kutoka miongoni mwa watu wenye maadili, sifa, uzoefu na ujuzi wa kusimamia utekelezaji mzuri wa kazi za Tume.

Watumishi wengine wa Tume

**10**.-(1) Tume itakuwa na mamlaka ya kuanzisha sehemu au ofisi kama itaona inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake na kuajiri watumishi mbalimbali katika ofisi hizo.

(2) Kwa madhumuni ya Kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua maafisa au watumishi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria au Sheria nyingine yeyote na kwa kuzingatia masharti ya utumishi kama Tume itakavyoona inafaa.

(3) Maafisa na wajiriwa wa Tume watakuwa madarakani kwa, kipindi, kitakachoainishwa na watapokea mshahara, posho na stahili, kulingana na masharti ya utumishi kama Tume itakavyoona inafaa.

(4) Mtu anapohamishiwa au kupelekwa kwenye

ajira ya Tume kwa muda maalum chini ya Sheria hii, masharti yake ya ajira hayatapunguzwa chini kulinganisha na aliyokuwa nayo katika nafasi yake kwenye utumishi wa umma, na utumishi wake utahesabika kuendelea kama ilivyokuwa kabla ya kuhamia Tume kwa madhumuni ya mafao, kiinua mgongo au stahili nyinginezo.

Ofisi za Mikoa za umwagiliaji

**11**.-(1) Kwa lengo la kuleta ufanisi katika kutekekeleza majukumu yake, Tume itaanzisha Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa zitakazosimamiwa na Mameneja wa Umwagiliaji wa Mikoa kwa kadri itakavyoona inafaa.

(2) Meneja wa Umwagiliaji wa Mkoa atatekeleza majukumu yafuatayo-

(a) kutoa utaalam kwa Serikali za Mitaa katika uendelezaji na uendeshaji wa kilimo cha umwagiliaji na matupio kwa ushirikiano na mamlaka husika;

(b) kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yao;

(c) kuandaa upembuzi yakinifu wa miradi ya umwagiliaji, usanifu wa kina na nyaraka za zabuni;

(d) kutoa huduma za kiufundi kwa Serikali za Mitaa na sekta binafsi kwa maendeleo na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji katika maeneo yao;

(e) uandaaji wa mongozo ya uendeshaji na matunzo ya skimu za umwagiliaji;

(f) kusaidia katika uanzishaji wa Vyama vya Wamwagiliaji;

(g) kuzingatia masuala ya usimamizi wa mazingira katika kilimo cha umwagiliaji na matupio wakati

wa kuandaa mipango na usanifu;

(h) kukusanya takwimu na kuzihifadhi kwenye benki ya takwimu ya kilimo cha umwagiliaji;

(i) kuandaa mipango ya matumizi ya maji yaliyo chini ya ardhi na maji ya mvua kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji;

(j) kuhakikisha udhibiti wa ubora katika miundombinu ya umwagiliaji na matupio;

(k) usimamizi wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na matupio;

(l) kusambaza ubunifu wa teknolojia mpya kuhusu miundombinu ya umwagiliaji na matupio;

(m) kuwezesha kufanyika kwa utafiti katika masuala ya miundombinu na matupio;

(n) kuhamasisha nishati jadidifu kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji na maji ya matupio;

(o) kuhamasisha matumizi ya vifaa vya ujenzi vilivyojaribiwa na vinavyopatikana nchini kwa minajili ya kupunguza gharama na upotevu wa maji;

Sura 331

(p) kushirikiana na Bodi za Mabonde ya maji zilizoanzishwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji kwa madhumuni ya kuhamasisha ushirikishwaji wa usimamizi wa rasilimali za maji na masuala ya hati za haki ya matumizi ya maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

(3) Meneja wa Umwagiliaji wa mkaoa atateuliwa kutoka miongoni mwa watumishi waaandamizi wa umma wenye sifa, uzoefu, ujuzi na uwezo katika maendeleo ya umwagiliaji.

(4) Meneja wa Umwagiliaji wa Mkoa katika utekelezaji wa majukumu yake atawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Sekretarieti za Mikoa

**12**. Kutakuwa na Ofisi Afisa wa Umwagiliaji wa Mkoa ndani ya Sekretarieti ya Mikoa atakayeratibu maendeleo ya Umwagiliaji katika Mkoa na-

(a) atakuwa kiunganishi baina ya Tume na Mamlaka za Wilaya katika utekelezaji wa Sheria hii;

(b) itawezesha uhamasishaji, uendelezaji na kuzijengea uwezo mamlaka za Serikali za Mitaa katika maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji;

(c) itashauri kuhusu kuanisha Ofisi za Umwagiliaji za Wilaya katika maeneo yao kwa madhumuni ya uendelezaji na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji.

Idara za Umwagiliaji za Wilaya

**13**.-(1) Kwa utekelezaji wa vifungu vya sheria hii, Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa anaweza, kwa kushauriana na Waziri, kuanzisha Idara ya Umwagiliaji katika Mamlaka ya Wilaya kama atakavyoshauriwa na Tume.

(2) Idara ya Umwagiliaji ya Wilaya itaongozwa na Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya na itaajiri watumishi wenye sifa katika taaluma husika.

(3) Majukumu ya Idara ya Umwagiliaji ya Wilaya yatakuwa kusaidia Tume katika utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 5 cha sheria hii.

(4) Bila kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (3), Idara ya Umwagiliaji ya Wilaya itawajibika kwa yafuatayo-

(a) kuanisha skimu za umwagiliaji, kupanga na kusanifu, kujenga, uendeshaji na kukarabati skimu

za umwagiliaji kwa kushirikiana na Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa;

(b) kuunganisha Ofisi ya Mkoa ya Umwagiliaji na taasisi za Umwagiliaji;

(c) kushirikiana na wadau katika wilaya husika kuhusu maendeleo na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji;

(d) kukusanya, kuhifadhi na kusambaza taarifa kuhusu shughuli za kilimo cha umwagiliaji katika maeno yao;

(e) kuwezesha uanzishaji wa Vyama vya Wamwagiliaji na kuhakikisha kwamba vina ujuzi kwa ajili ya usimamizi wa kilimo endelevu cha umwagiliaji;

(f) kuhakikisha kwamba wamwagiliaji wanapata mafunzo kwa ajili ya usimamizi wa skimu za umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao;

(g) kusaidia uandaaji na utekelezaji wa masharti ya umwagiliaji ya vyama vya umwagiliaji katika maeneo yao;

(h) kusaidia wamwagiliaji kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji;

(i) kusambaza miongozo kuhusu shughuli za kilimo cha umwagiliaji;

(j) kuhakikisha kwamba uongozi wa kijiji unasaidia shughuli za umwagiliaji katika maeneo yao;

(k) kusaidia wakulima katika skimu za umwagiliaji kwa kuanzisha timu ya wataalam katika uendeshaji wa skimu;

(l) kutekeleza maelekezo yote yatakayotolewa na Tume kuhusu maendeleo na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji;

(m) kutekeleza majukumu mengine yanayohusu maendeleo ya umwagiliaji kama yalivyoainishwa katika Sheria hii.

(5) Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya ataandaa taarifa kila robo ya mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu yake na kuwasilisha katika Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda.

Uteuzi wa Wakaguzi wa Umwagiliaji

**14**.-(1) Tume, kwa kuzingatia mapendekeo ya Mkurugenzi Mkuu na kwa taarifa itakayochapishwa katika *Gazeti* la Serikali, itateua wahandisi wa umwagiliaji au afisa yeyote kutoka Ofisi za Mikoa au kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwa Wakaguzi wa Umwagiliaji ambao watakuwa na mamlaka kuhusu masuala ya umwagiliaji chini ya Sheria hii.

(2) Mtu yeyote atakayeteuliwa kuwa Mkaguzi wa Umwagiliaji kulingana na kifungu kidogo (1), atapewa kitambulisho, kama uthibitisho wa uteuzi wake na ambacho atakitumia katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

(3) Wakaguzi wa Umwagiliaji walioteuliwa chini ya kifungu hiki, watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mamlaka ya Mkaguzi wa Umwagiliaji

**15**.-(1) Mkaguzi wa Umwagiliaji aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 14 (1) anaweza katika muda muafaka na baada ya kutoa notisi-

(a) kuingia katika skimu ya umwagiliaji au sehemu yeyote ambayo shughuli za umwagiliaji zinaendelea, na kukagua miundombinu ya umwagiliaji kwa madhumuni ya kuhakikisha Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii au maelekezo au amri ya Waziri, Mkurugenzi

Mkuu zinafuatwa;

(b) kumtaka mtu yeyote kutoa kwa madhumuni ya ukaguzi nakala au maandishi, nyaraka yoyote inayohusu fedha, michoro, usanifu, kwa madhumuni ya ujenzi au shughuli za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(c) kumwamrisha mmiliki wa ardhi:

(i) kutunza, kukarabati, kubadilisha mtaro, bomba, jengo, maumbo, kifaa, tangi, dimbwi, bwawa au miundombinu mingine ambayo ni sehemu ya mfumo wa umwagiliaji na matupio ya maji;

(ii) kusafisha mtaro, bomba, kifaa, tangi, dimbwi, bwawa au miundombinu mingine ambayo ni sehemu ya mfumo wa umwagiliaji na matupio ya maji;

(iii) kusafisha msitu, magugu au kingo za mfumo wa matupio ya maji au miundombinu ya umwagiliaji ambayo inaweza kuharibu miundombinu au kuhifadhi panya na wadudu wengine;

(d) kukagua, kupima ardhi kwa ajili ya kupanga, kusanifu au kujenga miundombinu ya umwagiliaji na maji ya matupio, au kuongeza au kubadilisha, mfumo wa umwagiliaji na wa maji ya matupio na kwa madhumuni haya Mkaguzi wa umwagiliaji anaweza:

(i) kuweka nguzo au alama nyingine kwenye eneo husika;

(ii) kuchimba mitaro au kuchimba mashimo kwa lengo la kuchukua sampuli;

(iii) kuomba sampuli za udongo kwa ajili ya uchunguzi;

(iv) kufanya jukumu lolote ambalo ni muhimu katika utekelezaji wa Sheria hii.

(2) Mmiliki wa ardhi au mali na mtu yeyote aliyepanga au atakayepatikana ndani ya eneo hilo atampa Mkaguzi wa Umwagiliaji ushirikiano wakati akitekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii.

(3) Mkaguzi wa Umwagiliaji akiwa na sababu za msingi kwamba Sheria hii na Kanuni zake au amri iliyotolewa chini ya Sheria hii imekiukwa, anaweza kuzuia au kutoa amri ya zuio kuhusiana na ukiukwaji huo.

(4) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na amri ya Mkaguzi wa Umwagiliaji chini ya kifungu hiki anaweza, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kutolewa kwa amri hiyo, kukata rufaa kwa waziri.

Zuio dhidi ya wasio na sifa ya kuwa wakaguzi wa umwagiliaji

**16.** Mtu yeyote asiye na sifa za kuwa Mkaguzi wa Umwagiliaji, ambaye atafanya kazi za Mkaguzi wa Umwagiliaji atakuwa anatenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isizozidi millioni kumi au atatumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote faini na kifungo.

## SEHEMU YA TATU

## TANGAZO LA MAENEO YA UMWAGILIAJI NA MGAWANYO WA ARDHI

Tangazo la eneo la umwagiliaji

**17.**-(1) Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi anaweza, kwa kushauriana na Waziri na kwa amri itakayochapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali, kutangaza kwamba eneo lolote lililoainishwa kwenye amri hiyo kuwa

ni eneo la umwagiliaji kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Tangazo lililotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), litaainisha mipaka ya eneo hilo na linaweza kujumuisha miundombinu ya kuchepusha maji na mifumo ya kusafirisha maji ya umwagiliaji.

(3) Iwapo inapendekezwa kutenga eneo la umwagiliaji chini ya kifungu kidogo cha (1), Tume itawasilisha kwa Waziri, taarifa kuhusiana na maeneo yanayopendekezwa ambayo itakuwa na taarifa zifuatazo-

(a) ramani au mchoro unaoonesha mipaka na ukomo wa ardhi inayopendekezwa kujumuishwa kwenye eneo;
(b) maelezo yanayoainisha skimu na dhumuni la miundombinu inayopendekezwa;
(c) ramani iliyoandaliwa na kuthibitishwa na Waziri mwenye dhamana inayoonesha eneo linalopendekezwa kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji;
(d) taarifa ya madhara kijamii na kimazingira katika eneo linalopendekezwa;
(e) makisio ya gharama ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji ikiwa miundombinu hiyo itajengwa na Tume pamoja na gharama za ada za uendeshaji na tozo zitakazotozwa kila mwaka;
(f) makadirio ya mapato kwa mwaka yanayotarajiwa katika eneo lengwa;
(g) makisio ya kiwango cha maji yanayokusudiwa kwa ajili ya umwagiliaji kwenye eneo linalopendekezwa kwa kuzingatia matumizi ya wakati huo na ya baadaye kwa kuzingatia matumizi kwa shughuli nyingine za kijamii na kimazingira pia taarifa itahitajika inayoeleza vyanzo vya maji vinavyopendekezwa na kuweka

bayana pale inapobidi kiwango cha maji na ubora wake pamoja na misimu ambayo inafaa maji hayo kutumika;

(h) taarifa ya vyanzo vya maji vilivyopo ambavyo vipo ndani ama nje ya eneo linalopendekezwa ambavyo Tume itakuwa na mamlaka ya kudhibiti matumizi yake kwa kuzingatia aina au ukomo wa uidhibiti huo;

(i) makadirio ya thamani ya miundombinu ya umwagiliaji iliyopo ndani ya eneo ambalo linapendekezwa kuwa eneo linalomilikiwa na mtu au mamlaka yoyote litwaliwe na Tume;

(j) taarifa ya eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji likiwa na sifa na thamani ya wakati huo ikiambatana na maboresho ambayo yatakuwa yamefanyika kwa wakati huo;

(k) taarifa inayohusu manufaa kwa ujumla yanayoweza kupatikana kwa kuanzisha skimu ya umwagiliaji katika eneo linalopendekezwa; na

(l) taarifa yoyote kwa kadri itakavyokuwa imeainishwa katika Kanuni.

(4) Waziri anaweza kwa wakati wowote na kwa kushauriwa na Tume, kupitia Amri itakayotangazwa katika *Gazeti* la Serikali-

(a) kuunganisha maeneo mawili ya umwagiliaji au zaidi kuwa eneo moja;

(b) kugawa eneo la umwagiliaji katika maeneo mawili au zaidi;

(c) kubadilisha mipaka ya eneo la umwagiliaji kwa kuingiza sehemu ya eneo jingine na pia kutoa sehemu ya eneo la awali;

(d) kufanya marekebisho katika masuala yanayohusu fedha au masuala mengine ambayo kwa maoni yake yatakuwa na manufaa au faida kwa uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji nchini.

(5) Iwapo azimio lolote linalotajwa katika kifungu kidogo (1), litaathiri haki za umilikaji ardhi, mmiliki wa ardhi hiyo atastahili fidia kwa kuzingatia sheria ya ardhi ama kadri makubaliano yatakavyokuwa yamefikiwa.

Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji

Sura 118

**18.** Pale ambapo ni lazima na kwa lengo la kufanikisha madhumuni ya Sheria hii, Waziri anaweza baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi na Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, kumshauri Rais kwa kuzingatia Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, kutwaa ardhi yoyote kwa lengo la kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Madaraja ya ardhi ya kilimo cha umwagiliaji

**19**. Tume inaweza, kwa kushauriwa na Mkurugenzi Mkuu kuweka madaraja ya ubora wa ardhi wa eneo la umwagiliaji kwa kuzingatia aina ya mazao na aina ya umwagiliaji unaofaa.

SEHEMU YA NNE

UJENZI WA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI

Utekelezaji wa Miundombinu ya umwagiliaji

**20**.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, miundombinu ya umwagiliaji inaweza kutekelezwa katika eneo la umwagiliaji na wahusika wafuatao-

(a) Halmashauri za Wilaya;

(b) mkulima binafsi;

(c) vyama vya wamwagiliaji;

(d) kampuni iliyosajiliwa;

(e) asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali; au

(f) mtu mwingine yeyote aliyethibitishwa na Tume kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Bila kujali masharti yaliyopo kwenye kifungu kidogo cha (1), utekelezwaji wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji unaweza kuchangiwa na Tume kwa kushirikiana na wadau wengine waliothibitishwa.

(3) Pale ambapo Halmashauri ya Wilaya au mtu mwingine au kampuni inadhamira ya kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu, utekelezaji, utunzaji na matengenezo, inaweza kuomba huduma ya kitaalamu kutoka kwenye Tume kwa kadri taratibu na makubalino yatakavyofikiwa.

(4) Pale inapolazimu, ujenzi wa skimu za umwagiliaji utazingatia kuweka sehemu za kunyweshea mifugo.

Maombi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

**21**.-(1) Hapatakuwa na miundombinu ya Umwagiliaji itakayojengwa hadi hapo pendekezo la skimu lithibitishwe na Tume na pendekezo hilo liwe limezingatia tathmini ya mazingira kama ilivyoanishwa katika Sheria ya Mazingira.

Sura. 191

(2) Mtu yeyote mwenye dhamira ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo lolote la umwagiliaji isipokuwa Tume, atalazimika kuomba na kupata kibali cha Mkurugenzi Mkuu au afisa yeyote aliyeruhusiwa kwa kuzingatia taratibu kama zitakavyofafanuliwa katika kanuni za Sheria hii.

(3) Maombi yatakayofanywa kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), yataambatana na-

(a) taarifa ya usanifu;

(b) orodha ya michoro;

(c) gharama ya ujenzi;

(d) hati ya haki ya kutumia maji;

(e) hati ya kumiliki ardhi iwapo mmiliki ni sekta binafsi; na

(f) hati ya usajili kwa vyama vya wamwagiliaji;

(4) Endapo Mkurugenzi Mkuu atakuwa ameridhika na maombi hayo, atawasilisha orodha ya maombi hayo kwenye Tume ili yaweze kupewa kibali.

(5) Mkurugenzi Mkuu atatoa Hati ya Kibali kwa kila miundombinu ya umwagiliaji iliyokubaliwa.

Ujenzi na Makabidhiano ya miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa na Tume

**22.** Pale ambapo Tume itaona ipo haja kwa maslahi ya umma kujenga miundo mbinu ya umwagiliaji kwenye eneo la umwagiliaji kwa kushirikiana na mtu au kampuni yoyote, Tume inaweza kwa kupitia taarifa kwenye *Gazeti la Serikali*, kutangaza dhamira hiyo ikitaja eneo linalopendekezwa kuwekwa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na nyaraka nyingine muhimu kwa ajili ya ujenzi huo.

Madhara ya ujenzi wa miundombinu Sura 331

**23.** Kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, pale ambapo Tume au mtu yeyote atakayekuwa anakasimu, kwa kupitia Sheria hii atajenga miundombinu ya umwagiliaji itakayochepusha maji kutoka kwenye chanzo cha maji, Tume au mtu mwingine aliyeteuliwa ataratibu uchepusaji, utumiaji uzuiaji na mgawanyo wa maji kulingana na kiwango kilichoainishwa kwenye hati ya haki ya kutumia maji kwa kile chanzo cha maji ili kukidhi matarajio ya jamii husika.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji au kuzuia mtiririko wa maji katika mfereji wa maji bila ridhaa ya Tume au mamlaka yeyote iliyokasimiwa.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa kutumia hati ya haki ya kutumia maji kutoka kwenye miundombinu ya umwagiliaji kwa matumizi yoyote mbali ya umwagiliaji kwa matumizi yoyote mbali na matumizi ya nyumbani bila kupewa kibali na Tume au afisa yeyote aliyeidhinishwa.

Fidia inayotokana na uharibifu wa ujenzi wa miundo mbinu ya umwagiliaji

**24**. Mtu yeyote, ambaye kutokana na sababu za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji au utekelezaji wa mamlaka na mtu yeyote au kikundi cha watu chini ya Sheria hii atapata hasara ya mali kutokana na kunyimwa au ukiukwaji wa haki ya kutumia chanzo cha maji kwa shughuli za kumwagilia shamba lake au kwa shughuli nyingine yoyote, atastahili kupata fidia kwa hasara hiyo kwa mujibu wa sheria zinazohusu fidia.

Kukasimu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

**25**.-(1) Pale ambapo Tume itaona kuwa inafaa, inaweza kwa kuzingatia taratibu na masharti yaliyowekwa kukasimu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa au vyama vya wamwagiliaji au shirika lolote.

(2) Mamlaka ya Serikali za Mitaa au vyama vya umwagiliaji au shirika lolote ambalo limekasimiwa majukumu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), italazimika kufanya shughuli za uendeshaji na matunzo ya miundombinu baada ya kuingia mkataba ambao utakuwa umeweka bayana taratibu na masharti ya matengenezo na utunzaji.

Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji midogo

**26**. Tume inaweza kuingia mkataba wa huduma na Mamlaka za Serikali za Mitaa, vyama vya wamwagiliaji au mtu yeyote kwa lengo la kuchangia ujenzi au matengenezo ya miundombinu midogo ya umwagiliaji kwa kadri itakavyokubalika.

## SEHEMU YA TANO

## MAKUNDI NA UIDHINISHAJI WA SKIMU ZA UMWAGILIAJI NA WAMWAGILIAJI

Makundi ya skimu za umwagiliaji

**27**.-(1) Yafuatayo yatakuwa ni makundi ya skimu za umwagiliaji kwa madhumuni ya Sheria hii-

(a) skimu ndogo za umwagiliaji;

(b) skimu za umwagiliaji za ukubwa wa kati; na

(c) skimu kubwa za umwagiliaji.

(2) Kazi zote za umwagiliaji katika maeneo ya umwagiliaji zitahitaji kuidhinishwa au kusajiliwa na Tume kulingana na makundi yaliyoidhinishwa katika nagazi za mikoa na wilaya kama itakavyofafanuliwa katika Kanuni.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (2), hayatatumika pale ambapo Serikali itaona kuna masilahi ya kuanzisha skimu za umwagiliaji ambazo zina ukubwa mdogo, wa kati na skimu ambazo ni kubwa.

(4) Ujenzi wowote wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la umwagiliaji sharti upate kibali cha Tume kabla ya kufanya hivyo kwa kuzingatia taratibu kama

itakavyoelezwa katika Kanuni.

Makundi na Kibali cha wamwagiliaji

**28**.-(1) Makundi ya wamwagiliaji yatakuwa kama ifuatavyo kwa madhumuni ya Sheria hii:

(a) mkulima binafsi;

(b) vyama vya wamwagiliaji;

(c) makampuni;

(d) taasisi za umma;

(e) mashirika ya dini;

(f) asasi zisizo za kiserikali; na

(g) kikundi chochote kinachotambulika kisheria.

(2) Mkulima au shirika atatambuliwa na kupewa kibali kama mmwagiliaji kwa mujibu wa Sheria hii kama:

Sura 331

(a) ni mmiliki au mpangaji wa ardhi katika skimu ya umwagiliaji na anayo hati ya haki ya kutumia maji kwa lengo la kilimo cha umwagiliaji kama ilivyotolewa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji;

(b) yumo ndani ya skimu ya umwagiliaji iliyopata kibali; na

(c) anayo hati ya umwagiliaji iliyotolewa chini ya Sheria hii;

## SEHEMU YA SITA

## USIMAMIZI WA SKIMU ZA UMWAGILIAJI

Usimamizi wa skimu za umwagiliaji

**29**.-(1) Skimu ya umwagiliaji itasimamiwa na Serikali za Mitaa, taasisi za Serikali na za binafsi, mkulima binafsi, au vyama vya wamwagiliaji au chombo chochote au shirika.

(2) Ili kuwa na usimamizi wa skimu za umwagiliaji zenye ufanisi, litakuwa jukumu la Tume, Sekretareti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wamwagiliaji husika-

(a) kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya wamwagiliaji kwa ajili ya usimamizi wa skimu za umwagiliaji;
(b) kuhakikisha kuwa wakulima wote wanaomiliki ardhi katika skimu ya umwagiliaji wanakuwa wanachama wa vyama vya wamwagiliaji;
(c) kujenga uwezo wa wamwagiliaji katika suala zima la ufuatiliaji na usimamizi wa skimu za umwagiliaji;
(d) kusaidia vyama vya wamwagiliaji katika kuanzisha na kusimamia sheria ndogo ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa skimu za umwagiliaji;
(e) kuhakikisha uwepo wa utaratibu rasmi na wa wazi wa kuhamisha umiliki wa ardhi katika skimu za umwagiliaji kutoka mkulima mmoja kwenda kwa mwingine na unaozingatia uwajibikaji katika uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji pale inapobidi;
(f) kuhamasisha juu ya usimamizi shirikishi wa rasilimali maji;
(g) kusaidia kuanzishwa kwa jukwaa kilele la vyama vya wamwagiliaji ili kuwa na uwakilishi

kamili wa usimamizi wa skimu katika suala zima la usimamzi wa mabonde madogo ya mito kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Usimamzi wa Rasilimali Maji;

Sura 331

(h) kuanzisha utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafisi kwa lengo la kuwa na uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji wenye ufanisi;

(i) Kuweka utaratibu wa mpito kwa kuweka wataalam wenye sifa ambao wataunda timu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu wakati wakulima kupita vyama vyao, wanapata uzoefu wa kuchukua majukumu hayo;

(j) kuhakikisha taasisi za umma na wawekezaji binafsi kwenye skimu za umwagiliaji za kibiashara zenye ukubwa wa kati na zile ambazo ni kubwa wanazingatia makubaliano ya mikataba na kuhakikisha kuwa wanawapa uzoefu na ujuzi wakulima wadogo wanaowazunguka;

(k) kuhamasisha usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia watoa huduma wa sekta binafsi pale ambapo wakulima wamedhihirisha kwamba wana uwezo mdogo;

(l) kuhamasisha na kuteketeza dhana shirikishi na yenye msukumo unaotokana na mahitaji ya walengwa na uchangiaji na urejeshaji wa gharama za uwekezaji husan kwa skimu zinazotekelezwa kwa kutumia fedha za umma;

(m) kuhimiza uanzishwaji wa miundombinu ya kuongeza thamani ya mazao na masoko ili kuvutia uwekezaji;

(n) kuanzisha na kutunza benki ya takwimu za umwagiliaji katika ngazi ya taifa na Mamlaka za

Serikali za Mitaa ili kuwa na mipango, utekelezaji na usimamizi wa shughuli za umwagiliaji zenye ufanisi; na

(o) kutekeleza majukumu mengine ambayo ni muhimu katika kuboresha usimamizi wa skimu za umwagiliaji;

Uanzishaji wa vyama vya wamwagiliaji

**30**.-(1) Tume, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa itasaidia uanzishwaji wa vyama vya wamwagiliaji kwa kuzingatia mfumo wa umwagiliaji wa skimu husika.

(2) Kuanzia tarehe ya kusajiliwa wakulima wote wanaomiliki ardhi, mashamba katika skimu husika watatakiwa kuwa wanachama wa umoja na watalazimika kutekeleza mashartiya umoja huo.

(3) Kutakuwepo na mtaalam mwenye sifa wa kusaidia suala la usimamizi wa shughuli za vyama vya wamawagiliaji ambaye atateuliwa kutoka katika Idara ya Umwagiliaji ya Halmashauri husika baada ya kuwasiliana na Tume.

(4) Tume au Mamlaka za Serikali za Mitaa inaweza, kwa kadri itakavyolazimu, kutoa mwongozo au mapendekezo ya mabadiliko katika majukumu ya vyama vya wamwagiliaji au Kamati au kukasimisha afisa au timu ya maofisa kwa ajili ya kuanzisha na kufuatilia shughuli za umoja huo.

Madhumuni ya vyama vya umwagiliaji

**31**. Madhumuni ya vyama vya wamwagiliaji yatajumuisha-

(a) kuhamasisha na kuhakikisha usawa katika ugawaji wa maji ya umwagiliaji kwa watumiaji;

(b) kuelimisha juu ya uhifadhi wa maji, utunzaji bora wa mifumo ya umwagiliaji, ufanisi na matumizi bora ya maji kwa ajili ya uzalishaji wa mazao;

(c) kutunza mazingira na kuhakikisha uwiano wa kimazingira kwa kushirikisha wakulima ili wawezeshwe kumiliki mifumo ya umwagiliaji kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji, na sheria nyingine zinazohusika.

Sura 191

Sura 331

Majukumu ya Vyama Wamwagiliaji

**32.** Vyama vya umwagiliaji vitatekeleza majukumu yafuatayo-

(a) kuandaa na kutekeleza mpango wa maji kwa kila msimu wa umwagiliaji, uendelevu wa mpango wa utekelezaji kwa kuzingatia kibali cha matumizi ya maji, eneo, udongo na mpangilio wa upandaji wa mazao kama ulivyoidhinishwa na Tume au Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(b) kuandaa mpango kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya mifumo ya umwagiliaji kila mwisho wa msimu wa upandaji na kutekeleza shughuli za matengenezo ya mfumo wa umwagiliaji chini ya mamlaka yake kwa kutumia fedha za chama cha wamwagiliaji kila baada ya muda;

(c) kusimamia matumizi ya maji na ardhi katika mfumo wa umwagiliaji;

(d) kuhamasisha matumizi ya maji kwa ufanisi na ugawaji wa maji;

(e) kuisaidia Tume au Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kukusanya ada ya huduma ya umwagiliaji na ada ya marejesho vyovyote vile itakavyokuwa;

(f) kutunza daftari la wamiliki wa ardhi na wanachama wa chama cha wamwagiliaji katika skimu ya umwagiliaji;
(g) kuandaa na kutunza taarifa za mifumo ya umwagiliaji ikijumuisha mali na madeni katika skimu za umwagiliaji;
(h) kufuatilia na kutunza taarifa za mtiririko wa maji kwa ajili ya umwagiliaji;
(i) kutatua migogoro baina ya wanachama katika skimu za umwagiliaji;
(j) kusababisha na kutunza vitabu vya hesabu zilizokaguliwa kwa kila mwaka, na taarifa nyingine kwa kadri zitakavyotakiwa;
(k) kufanya mapitio, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mara kwa mara na ugawaji wa maji kwa kadri itakavyotakiwa; na
(l) kutekeleza majukumu yoyote mengine kama itakavyotamkwa katika sheria zake ndogo.

Vyanzo vya fedha vya Vyama vya wamwagiliaji

**33**.-(1) Vyama vya wamwagiliaji vitatunza fedha zao kwa ajili ya kusimamia shughuli zao na fedha hizo zitajumjuisha-

(a) ada zilizokusanywa kutoka kwa wanachama wake kwa mujibu wa sheria ndogo;
(b) fedha nyingine zitakazopokelewa kwa njia ya misaada au ufadhili kutoka Serikalini, watu binafsi au shirika kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya umwagiliaji katika eneo la uendeshaji; na
(c) fedha yoyote itakayopokelewa kutoka vyanzo vingine halali.

Utaratibu wa kutaa shughuli za ujenzi

**34.** Tume au Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatoa mamlaka kwa vyama vya wamwagiliaji kutwaa na kutekeleza majukumu yote ya ukarabati wa mifumo ya

umwagiliaji chini ya uangalizi wa Tume au Mamlaka ya Serikali za Mitaaa vyovyote vile itakavyokuwa.

Ugawaji wa vitalu kwa ajili ya umwagiliaji

**35**.-(1) Kwa skimu zinazomilikiwa na vyama vya umwagiliaji, Kamati za Usimamizi wa Vyama vya wamwagiliaji, kwa kushauriana na baraza la kijiji, zitahakiki umiliki wa vitalu au kugawa vitalu katika skimu za umwagiliaji kama itakavyokuwa, kwa wanachama wake kwa kuzingatia masharti zitakavyoona inafaa kwa ajili ya maendeleo ya umwagiliaji katika eneo lake.

(2) Katika kuhakiki au kugawa vitalu, Kamati ya Usimamizi itazingatia ukaguzi wa mkulima husika na uwezo wake katika kusimamia uhakiki au ardhi aliyotolewa.

(3) Kitalu kitasajiliwa katika jina la mtu ambaye kwa ajili lake kitalu kimehakikiwa au kimegawiwa.

(4) Mmiliki wa kitalu aliyesajiliwa anaweza, kwa kushauriana na Kamati ya Usimamizi, kutoa au kuhamisha haki yake kwa mtu yeyote au shirika kwa kuzingatia sheria husika za ardhi.

(5) Iwapo haki ya kumiliki kitalu imehamishiwa kwa mtu mwingine, mmiliki huyo mpya atawajibika kusimamia ardhi na miundo mbinu husika ya umwagiliaji kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Usuluhishi wa migogoro katika skimu za umwagiliaji

**36.-**(1) Ili kupunguza migogoro katika matumizi ya ardhi na maji katika skimu za umwagilliaji, Tume itaimarisha mahusiano ya karibu na Halmashauri za Wilaya, Bodi za Mabonde za Maji na wamwagiliaji husika wanaotumia chanzo kimoja cha maji na kuhakikisha kuwa utaratibu wa usuluhisi wa migogoro kwa njia ya

makubaliano unaanzishwa katika kila skimu kwa kuhusisha vyombo vya Serikali husika.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki; "Bodi za Mabonde za Maji" maana yake ni bodi zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Sura ya 331

Kutoa na kuachia kitalu cha Umwagiliaji

Sura 113

Sura 114

**37.** Masharti ya Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji yanayotawala utoaji na uachiaji wa ardhi yatatumika kwa mmiliki yeyote wa kitalu anayekiuka masharti ya umiliki au utumiaji wa kitalu katika skimu ya umwagiliaji au anayekusudia kuachia kitalu vyoyote vile itakavyokuwa.

Mamlaka juu ya kilimo bora na njia za umwagiliaji

**38**.-(1) Pale ambapo Tume imeridhika kuwa kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi, umwagiliaji na ufanisi katika matumizi ya maji katika skimu ya umwagiliaji, ni muhimu na haraka kwa maslahi ya umma kusimamia utaratibu tofauti wa kilimo na njia za umwagiliaji katika eneo la umwagiliaji chini ya skimu ya umwagiliaji, Tume kupitia Tangazo la Serikali itatoa tamko kwa ajili hiyo.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Tume, baada ya kushauriana na mamlaka husika ya Serikali za Mitaa, inaweza kuainisha kupitia taarifa iliyochapishwa utaratibu ulioelekezwa, aina ya mfumo wa kilimo na njia za umwagiliaji zitakazotumika katika eneo la umwagiliaji.

(3) Baada ya kuchapisha taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1), hakuna mtu atakayetumia mfumo wa kilimo au kutumia njia za umwagiliaji nyingine zaidi ya zile zilizoainishwa katika taarifa kwa kipindi kilichotamkwa katika taarifa hiyo.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (3), atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shingi milioni kumi au atatumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka miwili au vyote.

Mamlaka ya kutwaa kazi za umwagiliaji kwa ukarabati

**39**.-(1) Ikiwa Tume itaona kuwa skimu yoyote ya umwagiliaji inayomilikiwa na mtu yeyote au kikundi cha watu imetelekezwa au inasimamiwa vibaya, kwa kuzingatia maslahi ya umma, Tume kwa kutoa taarifa kwa mmiliki au mtumiaji itatwaa kwa kipindi kifupi skimu na kuiweka chini ya usimamizi wake au usimamizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa lengo la ukarabati.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha 1, Tume itarudisha usimamizi wa skimu husika kwa mmiliki au mtumiaji baada ya kufanya ukarabati unaostahili na kudai gharama za ukarabati wa skimu hiyo kutoka kwa mmiliki au mtumiaji husika.

Ada za huduma ya umwagiliaji

**40**.-(1) Waziri baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Fedha, na kupitia Amri iliyotangazwa katika *Gazeti,* atatamka viwango vya ada za huduma za umwagiliaji na ada nyinginezo au tozo kwa ajili ya uendeshaji wa umwagiliaji na utunzaji wake katika eneo la umwagiliaji.

(2) Ada za huduma za umwagiliaji zitakusanywa na Tume, Mamlaka za Serikali za Mitaa au vyama vya wamwagiliaji vyovyote itakavyokuwa kwa ajili ya uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji.

Uendeshaji na utunzaji wa skimu

**41**.-(1) Kutegemeana na ukubwa na aina ya skimu

za umwagiliaji

ya umwagiliaji, uwajibikaji kwa ajili ya uendeshaji na utunzaji wa skimu hiyo utakuwa kama ifuatavyo:

(a) kwa skimu ndogo, wamiliki wa ardhi inayonufaika na mfumo wa umwagiliaji watawajibika kwa ajili ya uendeshaji na utunzaji wa skimu isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo;

(b) kwa skimu za kati na kubwa za umwagiliaji, wamwagiliaji wanaonufaika na mfumo wa umwagiliaji watawajibika kuendesha na kutunza mifumo ya mifereji ya kati na midogo hadi kiwango cha usawa wa shamba, na Mamlaka za Serikali za Mitaa au Tume vyovyote itakavyokuwa, itawajibika kuhakikisha usimamizi bora wa miundombinu ya kwenye vyanzo vya maji na mifumo mikubwa ya kusafirisha maji, isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo; na

(c) kwa skimu za umwagiliaji zinazomilikiwa na watu binafsi, itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa skimu kuendesha na kusimamia mfumo wa umwagiliaji isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo.

(2) Pale ambapo wamiliki wa ardhi wameshindwa kuendesha na kutunza skimu yao ya umwagiliaji na Mkaguzi wa Umwagiliaji ameridhika kuwa uendeshaji na utunzaji wa skimu ni lazima kwa ajili ya umwagiliaji bora wa ardhi ya wamiliki hao, atatoa taarifa kimaandishi kuwataka wamililiki wa ardhi husika, kuendesha na kutunza mifumo katika muda na utaratibu kama itakavyobainishwa katika taarifa.

Usafirishaji wa kingo

**42**.-(1) Tume inaweza, kupitia taarifa ya kimaandishi, kumtaka mmiliki au mtumiaji wa ardhi yeyote ndani ya eneo la umwagiliaji au matupio kusafisha kingo za miundombinu ya matupio au

umwagiliaji ambazo zinaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu au kutunza wanyama waharibifu.

(2) Taarifa itamtaka mmiliki au mtumiaji kuchukua hatua za lazima katika muda uliowekwa ambao hautapungua siku kumi na nne kuanzia siku ya kutolewa kwa taarifa, na ikiwa kutakuwa na ukiukwaji wa masharti ya taarifa, hiyo, Mkaguzi wa umwagiliaji anaweza kuingia katika ardhi na kusababisha hatua kuchukuliwa kama ilivyotakiwa katika taarifa na anaweza kurejesha gharama alizotumia kutoka kwa mmiliki au mtumiaji huyo katika Mahakama yenye mamlaka.

(3) Mkaguzi wa umwagiliaji anaweza kwa taarifa ya kimaandishi, kuzuia mmiliki au mtumiaji wa ardhi yoyote katika eneo kupanda mti au mimea kwenye kingo za miundombinu ya umwagiliaji au matupio ambayo inaweza kuharibu miundombinu au kutunza wanyama waharibifu.

(4) Iwapo kutakuwa na ukiukwaji wa masharti ya taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (2), Mkaguzi wa Umwagiliaji au afisa mwenye mamlaka anaweza kuingia katika ardhi hiyo na kusabibisha hatua kuchukuliwa kwa kukata mti, mmea au gugu lolote kutoka kwenye kingo hizo au kung'oa mti, mmea au gugu lolote na anaweza kurejesha gharama za kufanya hivyo, kutoka kwa mmiliki au mtumiaji katika mahakama yenye mamlaka.

(5) Pale ambapo Mkaguzi wa Umwagiliaji ametaka uharibifu ufanyike wa miti au mimea ya thamani, atamfidia mmiliki au mtumiaji fidia inayostahili, isipokuwa kama taarifa ilitolewa chini ya kifungu kidogo cha (2) kuhusu ardhi ambayo miti au mimea hiyo inaendelea kukua.

Tume kuamuru uwekaji wa kingo sahihi

**43**. Tume au Mkaguzi wa Umwagiliaji anaweza, kwa taarifa ya kimaandishi kumtaka mmiliki au mtumiaji wa ardhi yoyote katika eneo husika kuweka au mtu binafsi au kwa umoja na wamiliki au watumiaji wengine, kingo zinazostahili katika kiwango kilichotamkwa na usambazaji au mifereji ya matupio kwa ajili ya ugawaji, matupio, ukingaji au utengaji wa maji.

Isipokuwa kwamba, hakuna mtu atakayetakiwa chini ya kifungu hiki kuweka mifereji ya kingo, tuta au matupio ambayo haitakuwa na manufaa kwa ardhi ambayo mtu huyo ni mmiliki au mtumiaji.

Kuchangia gharama au kazi za pamoja

**44**.-(1) Pale ambapo kwa makubaliano au sababu nyingine yoyote, miundombinu ya umwagiliaji inatakiwa kushughulikiwa na ushirika wa wamwagiliaji katika skimu ya umwagiliaji au kwa gharama za wamiliki wa ardhi yote itakayonufaika na miundombinu hiyo, na pale ambapo wamiliki hao wameshindwa au kughairi kufanya sehemu yake au kuchangia sehemu ya gharama, itakuwa halali kwa Mkaguzi wa Umwagiliaji au Kamati ya Usimamizi au ofisa yoyote aliyeruhusiwa na Tume kuchunguza suala hili na kutoa amri kama atakavyoona inafaa, na inaweza kwa amri hiyo kumwelekeza mmiliki aliyekiuka kutengeneza sehemu ya miundo mbinu au kulipa sehemu ya gharama ya kazi hiyo.

(2) Amri inayoelekeza kuwa mmiliki aliyekiuka kutengeneza sehemu ya kazi, itaainisha sehemu ya kazi itakayotekelezwa, na muda wa utekelezaji, au makadirio ya gharama ya kazi hiyo katika utaratibu utakaowekwa.

(3) Iwapo mmiliki aliyekiuka amekataa au ameshindwa kutekeleza kazi hiyo katika muda ulipangwa

katika amri chini ya kifungu kidogo cha (1), Mkaguzi wa Umwagiliaji, Kamati ya Usimamizi au Ofisa yeyote aliyeruhusiwa na Tume chini ya kifungu kidogo hicho, inaweza ikadhamini kazi hiyo kutekelezwa na watu wengine na gharama husika inaweza kurejeshwa kutoka kwa mmiliki mkiukaji katika utaratibu uliowekwa.

Miongozo ya Usambazaji wa maji kwenye miundombinu ya umwagiliaji

**45**.-(1) Tume, baada ya kushauriana na Mkurugenzi Mkuu, na kwa taarifa itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali na gazeti linguine linalofikiwa na watu wengi, itaainisha na kusambaza kwa vyama vya wamwagiliaji miongozo kuhusu usambazaji wa maji katika miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa au kutunzwa yote au kwa sehemu kwa gharama za Serikali.

(2) Wamiliki wa skimu binafsi wataandaa taarifa za uchepushaji na usambazaji wa maji na kuwasilisha nakala ya taarifa hizo kwa Tume kupitia Ofisi za Umwagiliaji za Mkoa ili kuiwezesha Tume kufuatilia uzingatiaji wa uhitaji wa maji kwa mazao na vibali vya matumizi ya maji.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) na cha (2), atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kutumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Vitendo vinavyokatazwa

**46**.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya yafuatayo-

(a) kutumia au kuingia katika ardhi ya umwagiliaji kwa madhumuni mengine zaidi ya kilimo cha umwagiliaji na umwagiliaji;

(b) kuruhusu sumu za viwandani au uchafu wa nyumbani katika skimu yoyote ya umwagiliaji, bila kutibu maji kikamilifu;

(c) kuzuia ufanisi wa maumbo mbalimbali ya mfumo wa matupio na kuhatarisha usalama wa mifereji ya kusafirisha maji ya umwagiliaji na matupio;

(d) kufungua au kufunga mlango au chombo cha kudhibiti mwenendo wa mafuriko kwenye bwawa, mfereji au mfumo wowote wa kusafirisha maji kwenye miundombinu ya umwagiliaji unaomilikiwa na kuhudumiwa na Serikali au vyama vya wamwagiliaji isipokuwa Mkaguzi wa Umwagiliaji au mtu yeyote aliyepewa mamlaka hayo;

(e) kuvua katika mabwawa yanayomilikiwa, kutunzwa au kusimamiwa na Serikali au vyama vya wamwagiliaji bila kibali cha maandishi kutoka kwa mkaguzi wa umwagiliaji na isipokuwa kwa masharti na vigezo na kwa kulipa ada kama itakavyopangwa;

(f) kutumia milipuko au kitu chochote cha sumu kwa madhumuni ya kuvua katika bwawa;

(g) bila kibali cha maandishi cha Tume kuchimba madini au kufanya shughuli kwa kutumia mlipuko au shughuli yoyote inayoweza kusababisha mtikisiko ndani ya umbali wa kilometa moja kutoka kwenye skimu;

(h) kuruhusu maji kutoka katika miundombinu ya umwagiliaji inayomilikiwa, kusimamiwa au kutunzwa na Serikali na vyama vya wamwagiliaji kwa kukata tuta au kutoboa, kujenga mlango au kwa njia nyingine zinazofanana na hizo;

(i) kuunganisha mifereji au bomba kwenye mifumo ya umwagiliaji au matupio;

(j) kuweka au kusababisha kuweka umbo au kuweka kifaa katika mfereji au bomba iliyounganishwa kwenye mifumo ya umwagiliaji na matupio; na

(k) kutumia njia ya usambazaji wa maji ya umwagiliaji kwenye mimea katika ardhi yake ambayo haijapata kibali cha Tume.

(2) Kila mmiliki wa ardhi atatakiwa-

(a) kuhakikisha maji ya umwagiliaji hayavuji au kupotea kwenye ardhi iliyokaribu na kusababisha usumbufu kwa mwenye ardhi hiyo;

(b) kutunza na pale ambapo ni lazima kufanya matengenezo au kubadilisha mfumo wa umwagiliaji na matupio kama itahitajika kufanya hivyo;

(c) kutokuziba au kuzuia mtiririko wa maji katika sehemu yoyote ya mfumo wa umwagiliaji au matupio isipokuwa kwa maelekezo au kibali cha Tume au ofisa aliyeruhusiwa kufanya hivyo kwa niaba ya Tume;

(d) pale ambapo ni lazima, kusafisha mifereji na mabomba ya mfumo wa umwagiliaji au matupio uliowekwa katika ardhi yake;

(e) kuhakikisha mifereji na mabomba katika ardhi yake ikiwemo yale yanayoweka sehemu ya mifumo ya umwagiliaji na matupio vinalindwa kutokana na uharibifu unaoweza kujitokeza.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano au atatumikia adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Wajibu wa

**47**.-(1) Kila mmiliki wa ardhi ambapo tangi, kisima,

wamiliki wa ardhi kuhusu usalama wa miundo mbinu ya umwagiliaji

dimbwi, au bwawa lolote limejengwa juu ya kiwango cha miundombinu ya umwagiliaji, atatunza au kuweka matuta na utaratibu mwingine wa kuhifadhi tangi, kisima, dimbwi au bwawa ili kuweka mazingira ya usalama.

(2) Pale ambapo Maguzi wa Umwagiliaji ana maoni kuwa matuta au hifadhi iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1), haiko katika mazingira bora na inaweza kuhatarisha miundombinu ya umwagiliaji iliyoko nchini, mmiliki mhusika ataandikiwa taarifa ya kumtaka kuweka matuta hayo au kuweka mpango wa hifadhi katika mazingira bora katika utaratibu na katika muda uliotamkwa katika taarifa.

(3) Iwapo mmiliki anashindwa kukidhi masharti ya taarifa chini ya kifungu kidogo cha (2), au iwapo ukarabati uliofanywa na mmiliki huyo, kwa maoni ya Mkaguzi wa Umwagiliaji, hauridhishi, Mkaguzi wa Umwagiliaji anaweza kufanya ukarabati stahiki ili kuweka vizuizi na mikakati ya kuhifadhi katika namna inayofaa, na gharama zake zitabebwa na mmiliki huyo katika namna itakayoainishwa.

(4) Rufaa yoyote dhidi ya amri ya Mkaguzi wa Umwagiliaji chini ya kifungu kidogo cha (3), itapelekwa kwa Mkurugenzi Mkuu ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokelewa amri hiyo na Mkurugenzi Mkuu atatoa uamuzi kuhusu rufaa ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea rufaa hiyo na uamuzi wake utakuwa ni mwisho.

Udhibiti wa usafiri ndani ya mifereji na vivuko visivyopangwa

**48**.-(1) Tume inaweza, kwa kushauriana na wizara yenye dhamana na masuala ya uchukuzi na mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa kutumia Kanuni, kuzuia au kusimamia usafiri katika muundombinu ya umwagiliaji.

(2) Kila mmwagiliaji au mmiliki wa skimu ya umwagiliaji atahikikisha kwamba hakuna njia za mifereji zisizopangwa au vituo vya kuchotea maji visivyopangwa katika skimu yoyote ya umwagiliaji.

(3) Mtu yeyote anayevuka katika njia ya mfereji isiyopangwa au anayechukua maji au anayepeleka mifugo katika vituo vya kunyweshea maji visivyopangwa, atakuwa ametenda kosa na, baada ya kutiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kutumikia adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote.

Uhamishaji maji kati ya mabonde kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji

Sura 331

**49.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali maji, hakuna maji yoyote ya umwagiliaji, kutoka kwenye chanzo cha maji kilicho katika bonde la eneo la umwagiliaji, yatahamishiwa kwenye bonde jingine lolote isipokuwa kwa mujibu wa makubaliano baina ya Tume, Bodi za Mabonde ya Maji na Mamlaka husika na Serikali za Mitaa.

Ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa skimu za umwagiliaji

**50.**-(1) Mwishoni mwa kila msimu wa mazao, Kamati tendaji ya wamwagiliaji, kwa kushirikiana na Tume na Mamlaka za Serikali za Mitaa itafanya tathmini inayojumuisha ufuatiliaji endelevu wa skimu husika ya umwagiliaji.

(2) Ufuatiliaji na tathimini inayorejewa kwenye kifungu kidogo cha (1), utajumuisha matumizi ya maji dhidi ya mgawanyo wa maji, gharama zilizotumika kukarabati mfumo wa umwagiliaji kwa kurejea fedha zilizopo katika chama cha wamwagiliaji.

(3) Ufuatiliaji na tathminiya utendaji utahusisha-

(a) usawa katika usambazaji maji;

(b) ongezeko la uzalishaji;

(c) ongezeko la tija;

(d) mazao mbadala;

(e) upandaji wa mazao mchanganyiko kwenye eneo moja kwa wakati mmoja;

(f) ufanisi wa matumizi ya maji;

(g) ubora wa maji;

(h) matumizi ya rasilimali katika utendaji kazi;

(i) maboresho katika maeneo yaliyolimwa ya vyama vya wamwagiliaji ikilinganishwa na msimu uliopita;

(j) matumizi ya huduma za utafiti katika kupata aina stahiki mbalimbali za mbegu na viuatilifu;

(k) ubora wa kazi iliyofanywa; na

(l) uboreshaji wa mfumo wa umwagiliaji kwa awamu.

(4) Matokeo yaliyopatikana yatawekwa bayana kwa wadau wa vyama vya wamwagiliaji kwa kutoa orodha yenye manufaa yaliyopatikana kutokana na fedha zilizotumika na orodha hiyo itawekwa kwenye mbao za matangazo za vyama vya wamwagiliaji.

(5) Inapotokea kazi imefanywa na vyama vya wamwagiliaji, makisio ya gharama ya kazi hiyo, kipengele cha kazi kinachopendekezwa kufanywa, na mnyambulisho wa kazi zilizokwisha fanyika zitabandikwa kwenye ubao mahali kazi hiyo ilipofanyika.

(6) Tume inaweza kutoa msaada wowote katika uendeshaji wa zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya utendaji na matokeo yake yatawasilishwa kwa wahusika wote

kama itakavyoelekezwa na Tume.

(7) Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji itatumiwa katika kuboresha utendaji wa skimu.

(8) Nakala ya taarifa ya tathimini inayorejewa katika kifungu kidogo cha (7), itabandikwa kenye ubao wa matangazo wa chama cha wamwagiliaji.

## SEHEMU YA SABA

## UHIFADHI WA MAZINGIRA NA ULINZI WA AFYA

Kukidhi matakwa ya kimazingira

**51**.-(1) Tume itahakikisha kwamba maendeleo yote ya umwagiliaji yanaenda sambamba na shughuli za maendeleo na usimamizi wa mali asili kama vile usimamizi wa vyanzo vya maji kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

(2) Mtu yeyote anayeosha vifaa ndani ya, au nayechafua au anayesababisha kuchafuliwa kwa, miundo mbinu ya umwagiliaji atakuwa amefanya kosa na, endapo atatiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili, faini na kifungo.

(3) Bila kuathiri ujumla wa masharti yaliyotangulia, Tume kwa kushirikiana na mamlaka stahiki zinazohusiana na mazingira na afya-

(a) itafanya shughuli nyingine zozote na kuchukua hatua kuhusiana na umwagiliaji kwa kadri itakavyofaa au kuonekana ni muhimu kwa uhifadhi wa mazingira na afya ya binadamu;

(b) itahakikisha kwamba masharti yanayohusu uhifadhi wa mazingira yanazingatiwa wakati wa kupanga, kutekeleza na kuendesha skimu za

umwagiliaji;

(c) itahakikisha kwamba athari za mazingira zisizokubalika zinaepukwa na kwamba masuala yanayohusu maji yasiyotakiwa kutuama juu ya ardhi, kiwango cha chumvi kwenye maji na mmomonyoko, yanasimamiwa;

(d) itahakikisha kwamba usanifu wa skimu za umwagiliaji unazingatia hatua za kiusalama kuhusu udhibiti wa mafuriko na majanga mengineyo;

(e) itazuia matumizi ya kemikali, viuatilifu na vitu vinginevyo kama vitakavyoainishwa, kwenye ardhi yoyote itumiwayo kwa kilimo cha umwagiliaji;

(f) itadhibiti uchungiaji wa mifugo kwenye maeneo ya umwagiliaji na yale ya matupio na kingo za mito ambayo ni chanzo cha maji katika skimu ya umwagiliaji;

(g) itaainisha viwango vya kimazingira vinavyotakiwa kuzingatiwa na wamwagiliaji katika uendelezaji wa skimu; na

(h) itahakikisha kwamba wamwagiliaji wote wanazingatia sheria za nchi zinazosimamia uhifadhi wa mazingira na mbinu bora za kilimo.

(4) Kwa madhumuni ya uhifadhi mazingira, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine-

(a) watahakikisha kwamba wamwagiliaji wanakidhi maelekezo yanayowataka kuhifadhi mazingira ndani ya eneo la umwagiliaji; na

(b) itahakikisha kwamba wamwagiliaji na wadau wengineo hawafanyi shughuli zinazoweza kupelekea uharibifu wa mazingira katika maeneo ya umwagiliaji.

Tume itafanya,

**52**.-(1) Kwa madhumuni ya kuboresha utendaji wa

itaratibu na kuendeleza utafiti wa umwagiliaji

kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya uzalishaji mazao, tija na faida na kuhakikisha ufanisi wa matumizi ya maji ya umwagiliaji, Tume kwa kushirikiana na taasisi binafsi za umma za ndani ya nchi na za kimataifa, itaendesha, itaratibu utafiti kuhusu umwagiliaji na matupio na kuhamasisha matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa wanufaika kwa mujibu wa Mkakati na Sera ya Taifa ya Umwagiliaji.

(2) Utafiti wa umwagiliaji na matupio utalenga katika kuboresha ufanisi wa miundombinu ya umwagiliaji katika kudhibiti matumizi ya maji na kuendeleza uzalishaji wenye tija wa mazao katika skimu za umwagiliaji Tume-

(a) itahakikisha uendeshaji na utunzaji bora wa skimu za umwagiliaji;
(b) itaongeza matumiziya teknolojia sahihi kwa wakulima kwa ajili ya maendeleo endelevu ya umwagiliaji;
(c) itajenga uwezo wa wataalam wa umwagiliaji, watoa huduma na wakulima katika sekta ya umwagiliaji;
(d) itatambua changamoto za utafiti wa umwagiliaji na matupio ya maji na hatua za kuchukua;
(e) itatafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za utafiti wa umwagiliaji wa matupio;
(f) itahifadhi, kuchapisha na kusambaza matokeo ya tafiti;
(g) itaanzisha wa mfumo wa mahusiano na uratibu aina zote za tafiti za umwagiliaji kwa wadau mbalimbali wa kitaifa na kimataifa;
(h) itafanya utafiti na kusambaza matokeo ya utafiti na teknolojia za umwagiliaji kwa wamwagiliaji nchini;

(i) itahamasisha matumizi sahihi ya teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya umwagiliaji;
(j) itaendeleza mwamko kuhusu mbinu sahihi na boa za umwagiliaji na kuendesha parogramu mahsusi za mafunzo kwa wamwagiliaji;
(k) itaendesha mafunzo katika maeneo mahsusi kwa ajili ya kuwaendeleza waajiriwa wapya kitaaluma mapema iwezekanavyo kwa kuzingatia matokeo ya tafiti kwa lengo la kuimarisha weledi na ujuzi wa watumishi wa umwagiliaji ili kuimarisha na kuboresha maendeleo endelevu kwenye sekta ya umwagiliaji;
(l) itatambua, itahifadhi, na itatumia teknolojia, mbinu na ubunifu uliopo;
(m) itawezesha upatikanaji wa fedha ili kusaidia kilimo cha umwagiliaji katika miji na pembezoni mwa miji ambapo maji yanayovunwa kwenye paa, maji taka yaliyowekwa dawa na teknolojia sahihi zinazoweza kutumiwa;
(n) itaanzisha na kuimarisha ushirikiano na kuwa na mtandao wa taasisi za umwagiliaji za ndani ya nchi na za kimatifa ikiwemo taasisi za elimu ya juu; na
(o) itafanya kazi nyingine yoyote inayofaa.

## SEHEMU YA NANE

## MASHARTI KUHUSU MASUALA YA FEDHA

Uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji

**53**.-(1) Unaanzishswa Mfuko utakaojulijana kama Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji kwa lengo la kuhakikisha maendeleo na uendelevu wa sekta ya umwagiliaji.

(2) Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji utakuwa na-

(a) fedha zitokanazo na uuzwaji au uhamishwaji wa skimu za umwagiliaji zinazomilikiwa na serikali;
(b) fedha zozote zitokanazo na gharama zinazorejeshwa ambazo zitalipwa na wamwagiliaji kwa maendeleo ya umwagiliaji chini ya Sheria hii;
(c) fedha zitakanazo na mauzo ya mitambo chakavu na vifaa vilivyotumika kujengea skimu za umwagiliaji;
(d) fedha zozote zinazoweza kulipwa kwenye Mfuko kutoka kwenye fedha zilizoidhinishwa kwa ajili hiyo na Bunge;
(e) fedha zilizopatikana kwa njia ya ada au tozo kuhusiana na programu, uchapishaji, nyaraka na huduma nyinginezo zinazotolewa na Tume;
(f) fedha zozote ambazo Mfuko utapata, kwa idhini ya Waziri na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, kwa njia ya misaada, mikopo au misaada mingine ya kifedha kutoka ndani au nje ya nchi; na
(g) fedha zozote ambazo zitapatikana kwenye Mfuko kwa kuzingatia masharti ya sheria hii au vinginevyo kama itakavyoidhinishwa na Tume.

Matumizi ya Mfuko

**54**.-(1) Rasilimali za Mfuko zitatumiwa kwa -

(a) kugharamia mipango, upembuzi yakinifu, usanifu, ujenzi, uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji;
(b) kugharamia, kwa njia ya mkopo au msaada, utafiti wa masuala yoyote ya umwagiliaji na matupio yanayofanywa na, au kwa faida ya

watu au vyama vinavyojihusisha na umwagiliaji na matupio;

(c) kutwaa ardhi, vifaa, malighafi na mali nyinginezo na ujenzi wa majengo kwa lengo la kuendeleza madhumuni ya Mfuko;

(d) kugharamia kwa njia ya mkopo au msaada, mafunzo au kozi za kujenga uwezo wa wataalam au wakulima wanaojihusisha katika sekta ya umwagiliaji;

(e) kutoa tuzo kwa watu waliochangia maendeleo ya sekta ya umwagiliaji;

(f) kugharamia matumizi ya Tume na yale yatokanayo na uanzishwaji na uendelezaji wa Mfuko; na

(g) dhumuni lolote ambalo Waziri, kwa ushauri wa Tume, ataona ni kwa maslahi ya malengo ya Mfuko.

Malipo ya awali kwenye Mfuko

**55.** Iwapo katika mwaka wowote wa fedha, mapato ya Mfuko na mapato mengine ya nyongeza yatokanayo na mwaka uliotangulia hayatoshelezi kugharamia mahitaji halisi au makisio ya mahitaji ya Tume, Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha anaweza kutoa malipo ya awali kwa Mfuko ili kukabiliana na upungufu au sehemu ya upungufu, na malipo hayo ya awali yatafanywa kwa kuzingatia vigezo na masharti, ama ya kurejesha fedha au vinginevyo, kama Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha atakavyoamua.

Usimamizi wa Mfuko

**56.**-(1) Kwa kuzingatia maelekezo ya jumla au mahususi ya Waziri, Mfuko utasimamiwa na Tume.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Tume itatunza

fedha zake katika akaunti tofauti za benki ambazo zitatumika kwa kuzingatia maelekezo ambayo Waziri anaweza kuyatoa, isipokuwa kwamba Tume haitafanya malipo yoyote kutoka kwenye Mfuko isipokuwa kwa kuzingatia mpango wa matumizi wa mwaka uliokubaliwa.

(3) Bila kuathiri masharti yaliyotangulia ya kifungu hiki, Tume inaweza, iwapo mazingira yatahitaji hivyo, kutunza na kusimamia akaunti mahsusi yoyote ya benki kwa madhumuni ya mradi au programu inayotekelezwa kwa ushirikiano na taasisi, idara au shirika la kigeni kwa maendeleo ya umwagiliaji katika Jamhuri ya Muungano.

(4) Mtu yeyote anayeidhinisha malipo kutoka kwenye Mfuko kwa kukiuka masharti yoyote ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atawajibika, baada ya kutiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au vyote viwili, faini na kifungo.

Hesabu na ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji

Sura ya 418

**57.-(**1) Tume itaweka na kutunza vitabu sahihi vya mahesabu ya malipo yaliyofanywa kwenye, na kutoka katika Mfuko.

(2) Vitabu vya mahesabu ya Mfuko vitakaguliwa kila mwisho wa mwaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, hesabu za Mfuko zilizokaguliwa zitachapishwa sambamba na hesabu nyingine za Tume zilizokaguliwa.

Fedha za Tume

**58**. Vyanzo vya fedha za Tume vitakuwa ni-

(a) fedha zinazoweza kutengwa na Bunge;

(b) kiasi cha fedha kitakacholipwa kwa Tume kwa njia ya msaada, zawadi, na mkopo;

(c) tozo za huduma ya umwagiliaji; na

(d) vyanzo vingine vyovyote halali vilivyopatikana au vipatakavyopatikana.

Bajeti ya mwaka ya Tume

**59**. Tume itaandaa makisio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka uanofuatia na kuyawasilisha kwa Waziri ili yapitiwe na kisha yawasilishwe Bungeni ili yaidhinishwe.

Hesabu na Ukaguzi wa hesabu

**60**.-(1) Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya hesabu, Tume itatunza na kuhifadhi vitabu sahihi vya hesabu kuhusiana na-

(a) fedha zote zilizopokelewa na kutumiwa;

(b) mali na madeni yote ya Tume; na

(c) taarifa zote za mapato na matumizi ya Tume.

(2) Ndani ya miezi sita ya kufungwa kwa kila mwaka wa fedha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Ukaguzi wa Umma atakagua hesabu ikiwemo mizani ya hesabu ya Tume.

Sura 418

(3) Kila mahesabu ya mapato na matumizi na mizani ya mahesabu iliyokaguliwa itawajibishwa kwenye kikao cha Tume na, iwapo itathibitishwa, itaidhinishwa kwa cheti kwa ajili hiyo.

(4) Mapema baada ya hesabu za Tume kukaguliwa, na kwa hali yoyote ile si zaidi ya miezi sita baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha, Tume itawasilisha kwa Waziri nakala ya taarifa ya hesabu zilizokaguliwa pamoja na taarifa kuhusu taarifa

iliyotolewa na wakaguzi wa hesabu.

(5) Waziri anaweza, iwapo taarifa iliyowasilishwa kwake chini ya kifungu hiki ina makosa yoyote, kuielekeza Tume irekebishe au iwasilishe kwake maelezo ya kina na Tume itatekeleza maelekezo hayo ya Waziri.

(6) Waziri, mapema iwezekanavyo baada ya kupokea taarifa, atawasilisha Bungeni hesabu zilizokaguliwa za Tume pamoja na taarifa ya wakaguzi.

Mamlaka ya kukopa na kuwekeza

**61**.-(1) Kwa kuzingatia idhini ya awali ya Waziri na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, Tume inaweza kukopa fedha kwa madhumuni ya shughuli zake kwa njia ya mkopo au mkopo bila kuwa na fedha baada ya amana na vigezo na masharti yahusianayo na ulipwaji wa kiasi cha fedha cha msingi na malipo ya riba, kwa kuzingatia maelekezo yoyote ya Waziri kama Tume itakavyoona inafaa.

(2) Fedha zinazomilikiwa na Tume chini ya Sheria hii, ambazo hazihitajiki kutumiwa na Tume zitawekezwa kwa namna ambayo Tume itaona kuwa inafaa baada ya kupata kibali cha Waziri wa Fedha.

Mwaka wa fedha

**62.** Mwaka wa Fedha wa Tume utakuwa ni kipindi cha miezi Kumi na mbili kuanzia tarehe 1 ya mwezi Julai na kuishia tarehe 30 ya mwezi Juni ya mwaka unaofuatia.

## SEHEMU YA TISA

## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

**63**.-(1) Mtu yeyote ambaye-

(a) kwa makusudi anaharibu au anashindwa kutunza mfumo wa umwagiliaji au miundo mbinu ya umwagiliaji;

(b) anaingilia sehemu yoyote ya miundo mbinu ya umwagiliaji au mali yoyote inayotumiwa na vyama vya wamwagiliaji kuhusiana na umwagiliaji au matupio au kukausha maji katika ardhi bila ruhusa ya mamlaka husika;

(c) kwa makusudi anasema maneno ambayo ni ya uongo au ambayo hana sababu ya kuyaamini kuwa ni ya ukweli;

(d) kwa kitendo au kwa maandishi, anatishia, anachochea, au anazuia ujenzi wa miundombinu yoyote ya umwagiliaji;

(e) anajihusisha katika vitendo ambayo vinaharibu au vinaweza kuharibu vyanzo vya maji katika mfereji au mikondo ya maji ya umma ambayo inapeleka maji kwenye skimu za umwagiliaji;

(f) analisha au anaruhusu mifugo kulishwa katika maeneo ya umwagiliaji tofauti na ilivyoelekezwa na Waziri;

(g) anawasha au anasababisha moto kuwashwa kwenye mazao yaliyopo kwenye skimu za umwagiliaji au sehemu yoyote ya shamba, bustani au kitalu kinachomwagiliwa;

(h) bila kuwa na sababu ya msingi, anakataa kutoa msaada wa kuzima moto katika Skimu za umwagiliaji au eneo lolote la umwagiliaji ikiwa ni

shamba, bustani au kitalu;

(i) anatumia au anasababisha kutumia katika skimu ya umwagiliaji, shamba, bustani au kitalu ndani ya eneo la umwagiliaji kemikali yoyote au kitu chochote kilichozuiwa chini ya Sheria hii au Amri itakayotolewa na Waziri;

(j) anatoa au atatoa taarifa za uongo au taarifa za kumpotosha Mkurugenzi Mkuu au afisa aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu chini ya Sheria hii;

(k) anakataa au atakataa au anazembea kutoa taarifa ambazo angepaswa kuzitoa chini ya masharti ya Sheria hii au Sheria Ndogo itakayotengenezwa chini ya Sheria hii;

(l) anajenga au anapanua miundombinu ya umwagiliaji kinyume cha masharti ya Sheria hii au anashindwa bila kuwa na sababu ya msingi, kuzingatia masharti yaliyotolewa kwenye Sheria hii au Sheria Ndogo;

(m) kwa makusudi anazuia, anaharibu au anabomoa kazi yoyote ya umwagiliaji au miundombinu ya umwagiliaji;

(n) anamzuia, anamnyanyasa kijinsia au anamkwamisha afisa wa Serikali katika utekelezaji wa mjukumu yake chini ya Sheria hii au Sheria Ndogo zilizotengenewa chini ya Sheria hii;

(o) anaingilia kwa kuongeza au kupunguza maji katika miundo mbinu ya umwagiliaji;

(p) anaingilia kwa kubadili mtiririko wa maji katika miundombinu yoyote ya umwagiliaji kiasi cha kusababisha uharibifu;

(q) ameruhusiwa kutumia maji katika kazi yoyote ya umwagiliaji anasababisha upotevu wa maji katika eneo la umwagiliaji au anaingilia utaratibu uliowekwa wa kutumia maji bila

utaratibu;

(r) kwa makusudi anaachafua maji katika miundombinu ya umwagiliaji na kusababissha yasiweze kutumika kama ilivyokusudiwa;

(s) anaharibu, anaondoa au anabadili kiasi cha maji kilichokusudiwa kutumika katika shughuli za umwagiliaji,

atakuwa ametenda kosa na baada ya kutiwa hatiani:

(i) ikiwa ni mtu binafisi, atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitatu au vyote, faini na kifungo; na

(ii) ikiwa ni kampuni, italipa faini isiyopungua milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni hamsini.

(2) Mahakama inaweza kuamua kuongeza adhabu iliyotolewa chini ya Sheria hii, kwa kuamuru kuwa kifaa kilichotumiwa kutenda kosa kitaifishwe.

(3) Waziri atakuwa na mamlaka ya kutoa utaratibu utakaotumika kutaifisha kifaa kilichotumika kutenda kosa chini ya kifungu kidogo cha (2) ili kiweze kumilikiwa na Serikali.

(4) Ikiwa kosa limetendeka na kwa sababu hiyo, mtu amejeruhiwa au kupoteza mali, mahakama inaweza, katika nyongeza ya adhabu iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), kuamuru mtenda kosa kumfidia mtu aliyeumia au kupoteza mali.

(5) Ikiwa mtu ametiwa hatiani kwa kosa lililotendeka chini ya kifungu hiki, gharama za kuondoa uharibifu uliojitokeza, kukarabati, au kubadilisha mfumo wa umwagiliaji zilizotumiwa na afisa yeyote wa Serikali

anayetekeleza masharti ya Sheria hii zitalipwa na mtu huyo kama itakavyokuwa imeelekezwa.

Makosa kwa chombo hodhi

**64**.-(1) Kitendo chochote ambacho kama kingefanywa na mtu binafsi kingekuwa ni kosa chini ya Sheria hii au Kanuni zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii, kama kitafanywa na chombo hodhi, kitakuwa ni kosa lililotendwa na Mkurugenzi, Katibu au Meneja isipokuwa kama atathibitisha kuwa kosa hilo limetendwa bila idhini yake au kushirikishwa na kwamba alitumia jitihada zake kuzuia kufanyika kwa kosa kama alivyotakiwa kulingana na majukumu yake katika nafasi yake katika mazingira yote.

(2) Ikiwa kosa chini ya Sheria hii, Kanuni au Amri iliyotengenezwa chini yake limetendwa na mbia katika kampuni, itakukwa kosa hilo limetendwa na mtu yeyote ambaye kwa wakati kosa likitendeka alikuwa mbia katika kampuni hiyo au alikuwa anatenda katika wadhifa huo isipokuwa kama atadhibitisha kwamba kosa limendwa bila idhini yake au kushirikishwa na kwamba alitumia jitihada zote kuzuia kutendeka kwa kosa kama alivyopaswa kulingana na majukumu yake katika mazingira yote.

Madai

**65.** Kwa kuzingaia masharti bayana ya Sheria hii, hakuna kitu chini ya Sheria hii, kitakachozuia madai ya mtu yeyote kutokana na uharibifu unaosabishwa na ujenzi, maadiliko au uharibifu wa miundo mbinu ya umwagiliaji au kushindwa kuifanyia matengenezo.

## SEHEMU YA KUMI

## MASHARTI MENGINEYO

Utunzaji wa siri

**66**.-(1) Kila mjumbe wa Kamati ya Tume na kila mtu aliyeajiriwa chini ya Sheria hii hatatoa kwa mtu yeyote, isipokuwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii au pale atakapotakiwa kufanya hivyo chini ya Sheria iliyoandikwa, taarifa yoyote ambayo atatakiwa katika kutekeleza majukumu yake kuhusiana na masuala ya fedha au taarifa za biashara za mtu.

(2) Mtu yeyote ambaye atakiuka mashartiya kifungu kidogo (1), atakuwa ametenda kosa na atawajibika baada ya kutiwa hatiani kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au kiasi cha fedha ambacho ni sawa na faida aliyoipata kutokana na kosa hilo, ikiwa kiasi hicho ni kikubwa, au kifungo cha miaka mitano au vyote, faini na kifungo.

Kutoa taarifa

**67**. Taarifa chini ya Sheria hii itakuwa imetolewa kwa mtu ikiwa-

(a) atapewa mtu huyo binafsi;

(b) itaachwa katika eneo lake la makazi linalojulikana; au

(c) itatumwa kwake kupitia anuani ya posta ya mahali alipokuwa anaishi mwishoni.

Uwekaji kumbukumbu

**68**.-(1) Waziri anaweza, kwa mapendekezo ya Tume, kuanisha vitendo ambavyo kumbukumbu zitahifadhiwa kwa madhumuni ya Sheria hii na anaweza kumtaka mtu yeyote anayemiliki au kutunza kumbukumbu hizo kuziwasilisha kwenye Tume kwa muda

utakaoamuliwa.

(2) Mtu yeyote ambaye-

(a) atashindwa kutunza kumbukumbu zinazotakiwa chini ya Sheria hii; au

(b) kwa makusudi atabadilisha kumbukumbu hizo,

atakuwa ametenda kosa na atawajibika baada ya kutiwa hatiani kulipa faini isiyopungua shilingi million moja au kifungo cha miaka miwili au vyote, faini na kifungo.

Mikutano ya wadau

**69**.-(1) Kwa madhumuni ya kukuza maendeleo katika sekta ya umwagiliaji, kutakuwepo na Jukwaa la wadau ambalo litakuwa linahusika na mambo yafuatayo-

(a) kuweka taratibu za kulipia majukumu yanayowashirikisha wadau katika sekta ya umwagiliaji;

(b) kuweka taratibu za kuendesha mkutano mkuu wa mwaka;

(c) kuweka utaratibu wa namna ya kugharamia shughuli na mikutano;

(d) kuanzisha Sekretariati ya wadau pamoja na vyombo vingine kwa ajili ya kutekeleza majukumu yanayowashirikisha.

(2) Mkutano wa wadau utafanyika angalau mara moja kwa mwaka kwa lengo la kukubaliana ugharamiaji wa shughuli au kazi mbalimbali na kutekeleza majukumu ya pamoja na kufanya jambo lolote linalowahusu.

(3) Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza, kwa kushauriana na Tume, kutengeneza Sheria Ndogo kwa utekelezaji bora wa majukumu yanayowashirikisha

wadau kama watakavyokubaliana.

Tume inaweza kuhitaji taarifa

**70.** Tume inaweza kwa maandishi, kumtaka mtu yeyote au kikundi cha watu wanaojihusisha na masuala ya kukuza maendeleo ya umwagiliaji kuipatia taarifa zinazohusu jukumu hilo kama Tume itakavyoainisha.

Mamlala ya Waziri kupata taarifa

**71.** Tume itawasilisha kwa Waziri mrejesho wa takwimu, akaunti, maandiko au taarifa kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii kama Waziri atakavyoelekeza.

Tume kuanzisha mahusiano

**72.** Kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Tume itaanzisha na kuweka mahusiano, mashauriano na ushirika pamoja na vyombo na watu wengine, ikiwa wamejiunga au sivyo, na ikiwa wapo ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano, kama itakavyoonekana inafaa kwa utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii.

Kinga

**73.** Hakuna mjumbe wa Tume au mtumishi wa Tume atakayewajibishwa kwa kitendo chochote alichofanya au kushindwa kufanya kwa nia njema wakati akiwa anatimiza wajibu wake ndani ya Sheria hii au chini ya Sheria Ndogo itakayotengenezwa chini ya Sheria hii.

Ukusanyaji wa gharama ikiwa mtenda kosa

**74**. Ikiwa mtu aliyesababisha kuharibika, mabadiliko, ongezeko au kuzuia kazi za umwagiliaji bila ruhusa ya mamlaka husika, hawezi kupatikana baada

hajulikani

ya uchunguzi uliofanywa na Mkaguzi wa Umwagiliaji, kadri atakavyoona inatosha kuwa angekuwa ameshajulikana, Mkaguzi wa Umwagiliaji anaweza kwa idhini ya Mkurugenzi Mkuu baada ya kutoa taarifa ya mwezi mmoja kwa wamiliki wa ardhi iliyoathiriwa na uharibifu, baada ya kupokea maoni yao kama yatakuwepo, kurejesha toka kwao kiasi cha fedha ambacho ataona kinatosha kufanya marekebisho ya uharibifu au kuondoa mabadililo au zuio katika kazi za umwagiliaji.

Njia za kurejesha fedha

**75.** Kiasi chochote cha fedha kinachodaiwa kutoka kwa mtu yeyote kulingana na masharti ya Sheria hii au Kanuni zitakazotengenezwa chini yake, kama kiasi hicho ni cha kazi iliyopaswa kuwa imefanywa lakini haikufanywa, kitakusanywa, bila ya kuathiri njia nyingine za urejeshaji, kwa namna ambayo mapato ya Serikali yanakusanywa.

Mamlaka ya kutengeneza Kanuni

**76.**-(1) Baada ya kushauriana na Tume, Waziri anaweza kutunga kanuni kwa lengo la kutelekeza Sheria hii kikamilifu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutunga Kanuni-

(a) kutoa utaratibu wa matengenezo ya mfumo wa umwagiliaji;
(b) kuelekeza namna ambavyo maji ya umwagiliaji yatakavyotumika katika umwagiliaji na utoaji wa maji katika maeneo ya umwagiliaji;
(c) kuelekeza muda ambao maji ya umwagiliaji yanaweza kutumika katika maeneo ya umwagiliaji;

(d) kutoa utaratibu wa matengenezo au uboreshaji wa ubora wa maji ya umwagiliaji katika maeneo ya umwagiliaji na matupio;

(e) kutoa utaratibu wa matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji;

(f) kuelekeza namna ambavyo maji yaliyozidi kwenye umwagiliaji yatakavyokaushwa kutoka kwenye mfumo wa umwagiliaji;

(g) kutoa utaratibu wa namna ya kuunda, majukumu na kuendesha vyama vya umwagiliaji;

(h) kusimamia ugawaji wa maji miongoni mwa wamwagiliaji;

(i) kuelekeza namna ya kutoa taarifa ambazo zinatakiwa kutolewa chini ya "Sheria hii;

(j) kukadiria kiasi cha maji ya umwagiliaji au matumizi mengine ya maji yanayotumiwa na wamiliki wa ardhi katika mfumo wa umwagiliaji na matupio;

(k) kutoa taratibu za ugawaji wa ardhi na usimamizi wa vyama vya umwagiliaji;

(l) kuhusiana na usuluhishi wa migogoro;

(m) kuelekeza viwango vya ada na tozo chini ya Sheria hii na namna ya ulipaji;

(n) kuelekeza fomu zitakazotumika na ada zinazopaswa kulipwa kulinga na masharti yanayoruhusu katika Sheria hii;

(o) kutoa matangazo kuhusu maombi ya kutumia kazi za umwagiliaji;

(p) kutoa taratibu za kukata rufaa ndani ya Sheria hii;

(q) kuelekeza namna ya kuwa na rejista ya kuweka kumbukumbu;

(r) kuelekeza namna ya kujenga, kutengeneza na kujaribu mifumo ya umwagiliaji au huduma

nyingine zinazohusu mifumo ya umwagiliaji na matupio;

(s) kuelekeza namna ya kujenga, kutengeneza na taratibu za kujaribu miundombinu, kutoa fidia chini ya Sheria hii;

(t) kutoa utaratibu wa kuandikisha na kuwafuta wamwagiliaji;

(u) kutoa utaratibu wa kutengeneza Sheria Ndogo, uanzishwaji wa Kamati za vyama vya umwagiliaji na uendeshaji wa vyama hivyo;

(v) kuzuia au kusimamia usafiri wa majini katika maeneo ya umwagiliaji;

(w) kuelekeza usimamizi na uendeshaji wa mfuko;

(x) kueleza kitu chochote ambacho kinaweza au kinachotakiwa kuelezwa ndani ya Sheria hii.

Masharti ya Mpito

**77**.- (1) Ndani ya miezi kumi na mbili baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, chama cha umwagiliaji, chama cha ushirika, au taasisi yoyote au chombo chochote kinachojishughulisha na shughuli za umwagiliaji kama chama cha wamwagiliaji wanapaswa kuwasilisha maombi yao kwa Mkurugenzi Mkuu kwa ajili ya kusajiliwa chini ya Sheria hii**.**

(2) Baada ya Sheria hii kuanza kutumika, Ofisi za Umwagiliaji za Kanda zitaendelea kutekeleza majukumu yake mpaka Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa zitakapoanzishwa kama ilivyoainishwa katika Sheria hii.

## JEDWALI

*(Chini ya Kifungu cha 3(7)*

### VIPENGELE KUHUSU UENDESHAJI WA TUME

Makamu Mwenyekiti

**1**. Katika Kikao cha Kwanza Wajumbe wa Tume watachagua mmoja wao kuwa Makamu Mwenyekiti.

Muda wa uteuzi

**2.** Wajumbe wa Tume watashikilia madaraka yao kwa miaka mitatu, isipokuwa ujumbe wao umetenguliwa au umefutwa kutokana na utovu wa nidhamu au kutohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Tume bila sababu ya msingi, na atastahili kuteuliwa tena kwa kipindi kingine**.**

Mikutano na utaratibu wa kuendesha mikutano

**3**.-(1) Tume itafanya mikutano yake kwa wakati na katika eneo litakaloamuliwa na mwenyekiti baada ya kushauriana na Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mkutano wa kawaida wa Tume utaitishwa na Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti na taarifa inayoainisha mahali,

tarehe na muda wa mkutano itatumwa kwa kila mjumbe kupitia sehemu yake ya kawaida anapofanya shughuli au anapoishi katika kipindi kisichopungua siku kumi na nne kabla ya tarehe ya mkutano huo.

(3) Mwenyekiti, au kama hayupo, Makamu mwenyekiti au mmoja wa wajumbe aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti, ataongoza mkutano maalum wa Tume kwa kusambaza Waraka wa maandishi yaliyosainiwa na wajumbe wasiopungua watatu wa Tume, na pale ambapo mkutano maalum utafanyika dondoo za kikao hicho zitasambazwa kwa kila mjumbe kupitia sehemu yake ya kawaida anapofanyia shughuli katika kipindi kisichopungua siku tatu kabla ya tarehe ya mkutano huo.

(4) Kikao cha Tume kitaongozwa na Mwenyekiti au kama hayupo Makamu Mwenyekiti au Mjumbe mwingine atakayeteuliwa na wajumbe waliopo kuongoza kikao.

Akidi

**4.** Wajumbe watano wataunda akidi ya mikutano ya Tume.

Mjumbe mshirikishwa

**5.** Tume itakuwa na mamlaka ya kumwalika mtu yeyote kuhudhuria vikao vya Tume isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

| | |
|---|---|
| Mgongano wa maslahi | **6.** Mjumbe ambaye atakuwa na mgongano wa maslahi katika hoja yoyote iliyopo mbele ya Tume au Kamati ya Tume anapaswa kutangaza kuwa na maslahi na jambo hilo kwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti, na hataruhusiwa kushiriki katika kutoa maamuzi kuhusu hoja hiyo, isipokuwa kwa idhini ya wajumbe wengi waliopo katika kikao hicho anaweza kuruhusiwa ushiriki katika mjadala. |
| Tume itajiwekea utaratibu | **7**. Kulingana na aya za Jedwali hili, Tume inaweza kujiwekea utaratibu. |
| Taarifa za shughuli za Tume | **8.** Tume itaandaa taarifa ya mwaka itakayoonyesha mpango kazi wa Tume ikianisha malengo ya muda mfupi na muda mrefu. |
| Marupurupu | **9.** Waziri baada ya kushauriana na Waziri wa fedha ataainisha marupurupu ya wajumbe wa Tume. |

## MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kutunga Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka

2013 ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kuondoa changamotozilizojitokeza

kwenye sekta ya kilimo cha umwagiliaji. Changamoto hizo nipamoja na kukosekana

kwa mfumo wa kisheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha

umwagiliaji; kutoendelezwa, kutelekezwa na kuhujumiwa kwa miundombinu ya

umwagiliaji; udhaifu wa mfumo wa kitaasisi usiokidhi kasi ya kuendelea kupanuka kwa

shughuli za umwagiliaji; na uelewa mdogo wawananchi unaopelekea kushindwa

kutambua na kutekeleza kikamilifu wajibu wao katika katika kumiliki na kuchangia

ukarabati wa miundombinu yaumwagiliaji inayojengwa kwa fedha nyingi za Serikali.

Kadhalika,Sheria inayopendekezwa inalenga kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji,

kuendeleza, kuendesha na kusimamia kilimo cha umwagiliaji na mifumo yaUmwagiliaji na kuanisha masuala mengine yanayofanana na hayo.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu kumi.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaaainisha masharti ya utangulizi yakiwemo jina la Sheria pamoja na tafsiri ya manenona virai vilivyotumika katika muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa lengo la kuratibu, kuendeleza na kusimamia sekta ya umwagiliaji. Kadhalika, Sehemu hii pia imeainisha muundo wa Tume, Kamati za

Tume, mamlaka ya Tume, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Tume, na mamlaka ya Tume ya kuajiri au kuteua watumishiw a Kamisheni. Maeneo mengine muhimu

katika sehemu hii yanajuisha Ibara ya 10 ambayoinapendekeza kuundwa kwa Ofisi za umwagiliaji za kanda, idara za umwagiliaji za Wilaya na uteuzi wa wakaguzi

wa umwagiliaji.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kuweka masharti yahusianayo na utangazaji wa maeneo ya umwagiliaji na ugawaji wa makundi ya ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

Katika sehemu hii, Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo amepewa mamlaka ya kutangaza maeneo maalum ya umwagiliaji. Mamlaka hayo yanatekelezwa baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi, Waziri mwenye dhamana na masuala ya maji na Waziri mwenye dhamana na masuala ya mamlaka za Serikali za mitaa. Masharti mengine ya muhimu katika sehemu hii ni pamoja na Ibara ya 17 ambayo inampa Rais mamlaka ya kutwaa ardhi kwa madhumuni ya umwagiliaji, na Ibara ya 18 ambayo inahusu ugawaji wa ardhi kwa madhumuni ya Kilimo cha umwagililiaji.

Sehemu ya Nne, Muswada unapendekeza kuweka masharti yanayohusu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Masuala ya muhimu katika sehemu hii ni pamoja na Ibara ya 19 inayoainisha watu na taasisi zinazoweza kufanya shguhuli hizi za ujenzi pamoja na utaratibu wa kupata kibali cha ujenzi wa miundombinu ya miundombinu ya umwagiliaji; Ibara ya 22 inayohusu fidia kutokana na uharibifu ambao mtu yeyote ameupata kutokana na ujenzi huo wa miundombinu ya umwagiliaji; na Ibara ya 23 inayotoa mamlaka kwa Tume kukabidhi jukumu la ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa mamlaka ya Serikali ya mtaa, vyama vya wamwagiliaji au chombo kingine hodhi.

Sehemu ya Tano, Muswada unapendekeza kuweka masharti yanayohusiana na skimu za umwagiliaji na wamwagiliaji. Kwa misingi hiyo, masharti yahusianayo na mgawanyo

wa skimu za umwagiliaji na makundi ya wamwagiliaji yameainishwa bayana.

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu usimamizi wa skimu za umwagiliaji. Katika sehemu hii inapendekezwa kwamba skimu za umwagiliaji zisimamiwe na Tume, mamlaka za Serikali za mitaa, taasisi za umma na binafsi na wakulima au vyama vya wamwagiliaji. Kadhalika, inapendekezwa katika sehemu hii kuweka masharti yanayohusu uanzishwaji wa vyama vya wamwagiliaji, ugawaji wa maeneo ya umwagiliaji, utunzaji wa ardhi ya umwagiliaji, wajibu wa umiliki wa ardhi kuhusiana na shughuli zinazoweza kuathiri shughuli za umwagiliaji, usimamizi wa mjongeo na mifereji isiyopimwa, uhamishaji wa maji ya umwagiliaji baina ya mabonde na usimamizi na tathmini ya utendaji wa skimu za umwagiliaji.

Sehemu ya Saba inaweka masharti kuhusu uhifadhi wa mazingira na ulinzi wa afya. Kadhalika, inapendekezwa katika sehemu hii kuweka masharti yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira, uendelezaji wa tafiti

za umwagiliaji na uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Utafiti wa Umwagiliaji.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kuweka masharti kuhusu masuala ya fedha.

Maeneo ya muhimu katika sehemu hii ni pamoja na Ibara ya 52 ambayo inapendekeza kuanzishwa kwa mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji kwa lengo la kuendeleza na kuimarisha sekta ya umwagiliaji; Ibara ya 55 inahusu usimamizi wa Mfuko; na Ibara ya 60 inayotoa mamlaka kwa Tume kukopa na kuwekeza fedha za Tume kwa kadri Tume itakavyoona inafaa kwa maendeleo ya sekta ya umwagiliaji.

Sehemu ya Tisa inapendekeza kuweka masharti kuhusu makosa na adhabu mbalimbali kwa watu wanaokiuka sheria inayopendekezwa. Makosa yanayopendekezwa chini ya sehemu hii ni pamoja na kuaharibu mifumo ya umwagiliaji au miundombinu ya umwagiliaji; kuzuia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; kumzuia afisa yeyote wa umma asitekeleze mamlaka yake halali chini ya sheria inayopendekezwa; na kuingilia au kubadilisha mkondo wa maji kwenye muundmbinu wowote wa umwagiliaji.

Sehemu ya Kumi inahusu masharti ya jumla. Sehemu hii inaweka masharti yanayotoa kwa wajumbe na watumishi wa Tume na Kamati, wajibu wa kutunza siri katika utekelezaji wa majukumu yao chini ya Sheria inayopendekezwa. Kadhalika, sehemu hii pia inaweka masharti kuhusiana na mikutano ya wadau, mamlaka ya Waziri kutengeneza Kanuni.

Dar es Salaam, **CHRISTOPHER K. CHIZA**

4 Juni, 2013 *Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada uitwao Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji *(The National Irrigation Bill, 2013)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu liujadili na hatimaye upitishwe kuwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Waheshimiwa Mawaziri, kwa ushirikiano mkubwa mnaoendelea kunipa.

Kwa dhati kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla – Mbunge wa Kilolo, kwa maoni, ushauri na ushirikiano walioutoa na ambao wanaendelea kuutoa wakati wa maandalizi na uwasilishaji wa Muswada huu hapa Bungeni. Maoni yao kwa kiasi kikubwa sana yamesaidia katika kuuboresha Muswada kama inavyoonekana kupitia Jedwali la Marekebisho ambalo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi wa Sheria, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wataalamu wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na pia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa ushirikiano wao mkubwa wa kuwezesha kuandaliwa kwa Muswada huu. Katika hatua hii pia, napenda kuwashukuru sana Wadau wote wa Sekta Ndogo ya Umwagiliaji wakiwemo Wakulima na Wadau wengine wa Maendeleo, kwa jitihada

zao za kuendeleza Sekta ya Kilimo hususan kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunatambua kuwa, uchumi wa Taifa letu unategemea na utaendelea kutegemea zaidi kilimo. Hata hivyo, kilimo chetu bado kinatengemea mvua kwa kiasi kikubwa na hivyo kusababisha Taifa kukumbwa na njaa mara kwa mara hasa katika miaka ya ukame. Tukirejea kumbukumbu, juhudi za Serikali za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji zilianza mara tu baada ya uhuru, ambapo Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ilianzisha Miradi mikubwa ya Umwagiliaji. Katika kipindi hiki, msisitizo uliwekwa kwa sehemu kubwa katika uendelezaji wa Miradi ya Mashamba ya Kitaifa *(State Farms)* na kiasi kidogo katika uboreshaji wa kilimo cha umwagiliaji ya wakulima wadogo *(Smallholder Irrigation Improvement Programme).*

Miradi hiyo ni pamoja na ile ya mashamba ya mpunga ya Mbarali, Kapunga, Ruvu na Dakawa yaliyokuwa chini ya Shirika la Umma la Kilimo na Chakula *(National Agriculture and Food Corporation - NAFCO);* mashamba ya miwa ya Mtibwa, Kilombero na Kagera yaliyokuwa chini ya Shirika la Umma la Sukari *(Sugar Development Corporation - SUDECO).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia matukio ya ukame yaliyoikumba nchi yetu katika miaka ya 1970 na kusababisha janga la upungufu wa chakula; mwaka 1975 Serikali iliipa Wizara ya Kilimo jukumu la kusimamia maendeleo ya umwagiliaji na kuanzisha Idara mpya ya

Umwagiliaji. Hatua mbalimbali zilichukuliwa kati ya mwaka 1975 na 1985, ili kujenga uwezo wa rasilimali watu na kiutendaji katika kusimamia maendeleo ya umwagiliaji nchini kwa kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kuwatafuta wataalam wa muda kutoka nchi nyingine rafiki kwa utaratibu wa makubaliano kati ya nchi na nchi *(Bilateral Agreements),* ambapo Wataalam wa Umwagiliaji walipatikana kutoka iliyokuwa Sudani sasa Sudani ya Kaskazini na Nchi ya India;

(b) Kuanzisha mafunzo ya Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji *(Irrigation Technicians)* katika Chuo cha Kilimo MATI Nyegezi;

(c) Kuajiri wataalam wapya waliomaliza elimu kutoka vyuo vya elimu ya juu hapa nchini;

(d) Kufanya mapitio na tathmini ya malengo ya kuendeleza umwagiliaji na kuweka msisitizo mpya katika kuendeleza na kukarabati skimu za umwagiliaji za vijiji kupitia Mradi wa Kitaifa wa Kuendeleza Umwagiliaji Vijijini *(National Village Irrigation Development Programme - NVIDP)*. Skimu za umwagiliaji zilizolengwa wakati huo ni za ukubwa wa hekta 200 hadi 2,000 ili kufikia hekta 150,000 ifikapo mwaka 1985 kwa wakati huo.

(e) Kuwapeleka wanafunzi na wataalam kupata mafunzo ngazi ya vyuo vikuu katika fani ya umwagiliaji katika nchi za India, Uingereza, Korea, China, Cuba na Marekani;

(f) Kuanzisha vituo sita vya Kanda za Umwagiliaji ili viweze kusimamia kwa karibu uendelezaji wa umwagiliaji katika Mikoa na Wilaya nchini; na

(g) Kuajiri Wataalam Waelekezi wa Kigeni *(International Consultants)* waliofanya kazi na Wataalam wa Kitanzania kwa lengo la kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuhimiza umwagiliaji, Serikali imekuwa ikijenga, ikiboresha na kukarabati miundombinu ya skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo ambazo humilikiwa na wakulima wenyewe. Kwa hivi sasa skimu zilizoendelezwa kwa utaratibu huu ni 1,350 katika nchi nzima.

Ili kutoa dira na mwongozo kwenye usimamizi na kwa kutambua umuhimu wa Sekta Ndogo ya Umwagiliaji, mwaka 2002, Serikali iliandaa Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji *(The National Irrigation Master Plan - NIMP, 2002).* Mpango huu uliainisha eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini kuwa ni hekta milioni 29.4.

Eneo hilo limegawanyika kulingana na uwezekano wa kuendeleza umwagiliaji *(Irrigation Potential),* ambapo kuna eneo la hekta milioni 2.3 lenye uwezekano mkubwa, hekta milioni 4.8 zenye uwezekno wa kati; na hekta milioni 22.3 zenye uwezekano mdogo. Hadi sasa eneo linalomwagiliwa nchini ni jumla ya hekta 450,392, sawa na asilimia 1.5 tu ya eneo lote llinalofaa. Eneo hili linatakiwa kuwekewa

utaratibu wa kitaalamu na uendeshaji ili liweze kutumika kuzalisha mazao zaidi ya mara moja kwa mwaka.

Mheshimwia Naibu Spika, MKUKUTA II, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010, Dira ya Maendeleo ya Taifa pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, vimelenga kuongeza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 450,392 mwezi Juni, 2013 hadi kufikia hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2015/2016.

Malengo ya Serikali ni kufanya umwagiliaji uweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mapinduzi ya kijani na kuliwezesha Taifa kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula ili angalau asilimia 25 ya mahitaji yetu ya chakula itokane na kilimo cha umwagiliaji ifikapo mwaka 2015/2016. Lengo hili linatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Program - ASDP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inatekeleza Mpango wa Kuendeleza Kilimo kupitia Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania - SAGCOT),* kwa lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa *ASDP,* ikijumuisha matumizi endelevu ya rasilimali ardhi na maji kwa ajili ya kuwezesha uwekezaji katika kilimo. Hata hivyo, bado uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji unategemea kwa kiasi kikubwa Sekta ya Umma ambayo peke yake haiwezi kukidhi mahitaji ya uwekezaji kutokana na majukumu mengi iliyonayo ikilinganishwa na rasilimali zilizopo.

Ili kufikia lengo la kumwagilia hekta milioni moja ifikapo mwaka 2015/2016, uanzishwaji wa chombo kitakachokuwa na uwezo kisheria kuangalia vyanzo vingine vya fedha ni muhimu. Suala hili limeainishwa kwa kina katika Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya mwaka 2010 *(The National Irrigation Policy, 2010).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti mbalimbali zilizofanywa katika Sekta Ndogo ya Umwagiliaji zimebaini changamoto nyingi zinazoikabili sekta hiyo. Baadhi ya changamoto hizo zimeainishwa kwa kina katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 na Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya mwaka 2010, ambazo ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Ukosefu wa utaratibu madhubuti wa umilikishwaji wa skimu za umwagiliaji maji kwa wakulima unaosababisha wakulima wanaomilikishwa skimu hizo kutokuwa na mipango madhubuti ya kuziendeleza;

(b) Matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za ardhi na maji yanayosababisha uharibifu wa mazingira hususan, kutolindwa kwa vyanzo vya maji, upotevu wa virutubisho katika ardhi, matumizi ya maji yasiyohakikisha upatikanaji wa maji kwa watu walioko upande wa chini ya skimu *(downstream).* Hivyo, kuogezeka kwa migogoro katika skimu za umwagiliaji na kukosekana kwa tija katika kilimo;

(c) Kutokuwepo kwa utaratibu wa kutunza na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa na Serikali hususan pale inapokabidhiwa kwa wakulima.

Serikali inawekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, lakini ushiriki mdogo wa wakulima na sekta binafsi kwenye mipango ya uwekezaji katika ujenzi, umesababisha uendelezaji wa skimu zinazojengwa ikiwemo ugharimiaji wa wataalamu wa kuwafundisha wakulima, ulinzi wa miundombinu na ukarabati wake, kwa kiasi kikubwa umebakia Serikalini badala ya watumiaji wa skimu husika;

(d) Ushiriki mdogo wa Halmashauri za Wilaya katika kusimamia na kuendeleza skimu za umwagiliaji ziilizoko katika maeneo yao;

(e) Kukosekana kwa mfumo wa kisheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, ambayo sehemu nyingi hapa nchini imekuwa ikitumika kwa ajili ya matumizi mengine yakiwemo ya makazi. Hii inatishia kupungua kwa eneo linaloainishwa katika mipango yetu ya Taifa kuwa linafaa kwa ajili ya kilimo;

(f) Kutoendelezwa, kutelekezwa na hujuma dhidi ya miundombinu ya umwagiliaji. Kwa kiasi kikubwa jambo hili limechangiwa na tatizo miongoni mwa Wananchi kushindwa kutambua na kutekeleza kikamilifu wajibu wao katika kumiliki na kuchangia ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji inayojengwa kwa fedha nyingi za Serikali;

(g) Kukosekana kwa mfumo wa kitaasisi wa kuratibu usimamizi na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji mathalani, baada ya mabadiliko katika Sera za Uchumi, baadhi ya Taasisi za Umma zilizokuwa zinajihusisha katika

kilimo cha umwagiliaji kama *NAFCO* na *SUDECO* zilikoma na za binafsi zilizochukua nafasi zake zimeshindwa kutoa msukumo unaostahili katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, mfumo uliopo sasa katika sekta haujaweka misingi madhubuti ya kitaasisi wa utaratibu wa usimamizi na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba, idadi ya Watanzania inaongezeka na kilimo cha kutegemea mvua kinaendelea kukosa uwezo wa kutosheleza mahitaji ya nchi ya chakula na kuongeza kipato, ipo haja ya kuanza kunufaika kwa ufanisi zaidi na uwezo mkubwa wa rasilimali za umwagiliaji maji uliopo. Aidha, juhudi hizo zizingatie sera za nchi zilizopo, ambapo wakulima watahusika katika uanzishwaji, umilikishwaji na uendelezaji wa skimu za kilimo cha umwagiliaji na Serikali itahusika katika usimamizi; na katika hali ambapo viwango vya maji kutoka katika vyanzo mbalimbali vinaanza kushuka kutokana na matumizi ya maji yasiyo endelevu na yasiyozingatia hifadhi ya mazingira, pamoja na tishio kubwa la athari za mabadiliko ya tabia nchi, ipo haja ya Serikali kuendelea kuhusika katika kutoa utaalamu wa uandaaji, utekelezaji na uboreshaji wa skimu za umwagiliaji na pia uendeshaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada: Katika mfumo tulionao wa sera za uchumi huria, Serikali inajitoa kwa kiasi kikubwa katika shughuli za uzalishaji na kujihusisha zaidi na kazi za usimamizi na uratibu. Hivyo, ni muhimu ukawekwa utaratibu unaotambuliwa kisheria, utakaowezesha kutatua changamoto za umwagiliaji.

Madhumuni ya Muswada uliopo mbele ya Bunge lako ni kutunga Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 *(The National Irrigation Act, 2013),* ambayo inalenga kutekeleza Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010, ambayo inalenga pamoja na mambo mengine, kutatua changamoto zilizopo za usimamizi na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kwa kuweka mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi na uratibu. Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza hapa Bungeni tarehe 28 Juni, 2013, umepitiwa na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na kuridhiwa kwa ajili ya kujadiliwa hapa Bungeni kwa kuzingatia Kanuni na taratibu za Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na masuala mengine, Muswada wa Sheria inayopendekezwa unaanzisha Tume ya Taifa ya Umwaagiliaji, ambayo itakuwa chombo cha usimamizi wa sheria na kuainisha mamlaka na majukumu yake. Aidha, sheria itaainisha mfumo mzima wa kisheria utakaolinda na kuvutia sekta binafsi kushiriki kikamilifu kwenye uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji na kuweka utaratibu wa kutambua, kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Sheria inayopendekezwa pia itaweka utaratibu wa kujengwa kwa miundombinu bora ya umwagiliaji inayojumuisha mifumo ya umwagiliaji, inayotumia teknolojia za kisasa zenye ufanisi katika matumizi ya maji, ikiwemo teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone *(Drip Irrigation)* na muundo mahususi wa kitaasisi wa kuendeleza Sekta ya Umwagiliaji kulingana na ongezeko la mahitaji ya sasa ya

sekta. Sheria itaweka utaratibu wa jinsi ya kuomba, kuidhinisha na kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

Sheria itaweka sharti la kusajili wamwagiliaji *(Irrigators)* wote na vilevile utaratibu wa kisheria wa uchangiaji wa gharama za uendelezaji Miradi ya Umwagiliaji na kuainisha mgawanyo wa majukumu ya usimamizi, uendeshaji na ukarabati wa skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kutungwa kwa Sheria ya Umwagiliaji ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuongezeka kwa mchango wa umwagiliaji katika uzalishaji na kuimarisha usalama wa chakula na lishe;

(a) Kuongezeka kwa pato la mkulima na Taifa kwa ujumla;

(c) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na utoaji wa huduma za umwagiliaji;

(d) Kuongezeka kwa fursa za ajira na kipato kwa vijana kutokana na vivutio katika kilimo cha umwagiliaji na hivyo kupunguza wimbi la vijana kukimbilia mijini;

(e) Kuongezeka kwa miundombinu ya umwagiliaji yenye ubora itakayotumia teknolojia mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi yenye kustahimili athari za mabadiliko ya tabia nchi;

(f) Kupata teknolojia mpya za kilimo cha umwagiliaji kutokana na shughuli za utafiti wa kilimo cha umwagiliaji; na

(g) Kuwepo kwa skimu za umwagiliaji zenye kutumia rasilimali maji na ardhi kwa ufanisi na kuzingatia hifadhi ya mazingira na watumiaji wengine wa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na kubainisha mamlaka, majukumu yake na vyazo vya mapato ya kuendesha shughuli za Tume;

(b) Kuweka utaratibu wa umilikishaji wa miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa na Serikali kwa vikundi vya wakulima, watu binafsi, Vyama vya Wamwagiliaji au Makampuni na utaratibu utakaowezesha sekta binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu mikubwa ya umwagiliaji na kuitoa au kuikodisha kwa wakulima, Vyama vya Wamwagiliaji, Kampuni binafsi na kadhalika;

(c) Kuainisha majukumu ya Waziri mwenye dhamana ya umwagiliaji na kuweka mfumo mzima wa kisheria utakaolinda na kuvutia sekta binafsi kushiriki kikamilifu kwenye uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji;

(d) Kuainisha wajibu wa wadau katika Sekta ya Umwagiliaji ikiwa ni pamoja na Tume ya Taifa ya Umwagiiaji, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji,

Idara za Umwagiliaji za Wilaya, Kamati za Usimamizi wa Skimu za Umwagiliaji pamoja na Wamwagiliaji;

(e) Kuainisha na kusajili Vyama vya Wamwagiliaji *(Irrigators Organisations)* na majukumu ya wamiliki wa skimu za umwagiliaji; Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumegawa kitabu kinachoonesha *Irrigators Organisations;*

(f) Kuainisha uratibu wa kusimamia, kudhibiti, kuendeleza na kulinda ardhi ya kilimo inayofaa kwa umwagiliaji. Jambo hili ni muhimu ili nchi isije kuwa na uhaba wa ardhi inayofaa kwa kilimo endelevu na hivyo kukumbwa na uhaba wa chakula;

(g) Kuweka taratibu shirikishi za kisheria za usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji;

(h) Kuweka utaratibu wa kuomba, kuidhinisha na kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(i) Kuanzisha na kuweka utaratibu wa kisheria wa kuusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji *(Irrigation Development Fund)* na majukumu ya wadau katika kuchangia na kusimamia Mfuko huo;

(j) Kuweka utaratibu wa kupata fedha kwa njia ya mikopo na misaada kutoka katika taasisi za fedha kwa ajili ya kuendeleza umwagiliaji;

(k) Kuweka na kusimamia utaratibu wa usimamizi na utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji katika ngazi ya Mkoa na Wilaya;

(l) Kuweka utaratibu wa uteuzi wa Wakaguzi wa Umwagiliaji *(Irrigation Inspectors)* na mamlaka na wigo wa utekelezaji wa majukumu yao; na

(m) Kuweka jukwaa la wadau la kujadili masuala ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kumi kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inaainisha Jina la Sheria pamoja na tafsiri ya maneno yalivyotumika katika Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa lengo la kuratibu, kuendeleza na kusimamia Sekta ya Umwagiliaji. Kadhalika, sehemu hii imeainisha Muundo wa Tume, Kamati za Tume, Mamlaka ya Tume, uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Tume na Mamlaka ya Tume ya kuajiri au kuteua Watumishi wa Tume.

Maeneo mengine muhimu katika sehemu hii yanajumuisha Ibara za 11 - 13 ambazo zinapendekeza kuundwa kwa Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa chini ya Tume. Wajibu na majukumu ya Idara za Umwagiliaji za Wilaya chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Ibara ya 14 na 15

zinapendekeza uwepo, uteuzi na majukumu ya Wakaguzi wa Umwagiliaji *(Irrigation Inspectors).*

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kuweka masharti yanayohusu utambuaji wa maeneo ya umwagiliaji na ugawaji wa makundi ya ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

Katika sehemu hii, Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi, amepewa mamlaka ya kutangaza maeneo maalum ya umwagiliaji. Mamlaka hayo yatatekelezwa baada ya mshauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Kilimo, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Maji na Waziri mwenye dhamana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ninaomba nirudie sehemu hiyo. Katika sehemu hii, Waziri mwenye dhamana na masuala ya Ardhi, amepewa mamlaka ya kutangaza maeneo maalum ya umwagiliaji. Mamlaka hayo yatatekelezwa baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Kilimo, Waziri mwenye dhamana ya masuala Maji na Waziri mwenye dhamana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Masharti mengine muhimu katika sehemu hii ni pamoja na Ibara ya 17 ambayo inampa Mheshimiwa Rais, mamlaka ya kutwaa ardhi kwa madhumuni ya umwagiliaji na Ibara ya 18 ambayo inahusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kuweka masharti yanayohusu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Masuala muhimu katika sehemu hii ni pamoja

na Ibara ya 20 inayoainisha watu na taasisi zinazoweza kufanya shughuli za ujenzi pamoja na utaratibu wa kupata kibali cha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; Ibara ya 24 inahusu fidia kutokana na uharibifu ambao mtu yeyote anaweza kuupata kutokana na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; na Ibara ya 25 inatoa mamlaka kwa Tume kukasimu jukumu la ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, vyama vya umwagiliaji au chombo kingine.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kuweka masharti yanayohusiana na Skimu za Umwagiliaji na Wamwagiliaji. Kwa misingi hiyo, masharti yanayohusiana na mgawanyo wa skimu za umwagiliaji na makundi ya Wamwagiliaji yameainishwa.

Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu usimamizi wa Skimu za Umwagiliaji. Katika sehemu hii inapendekezwa kwamba, Skimu za Umwagiliaji zisimamiwe na Tume; Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma na Binafsi na Wakulima au Vyama vya Wamwagiliaji. Kadhalika, inapendekezwa katika sehemu hii kuweka masharti yanayohusu uanzishwaji wa vyama vya wamwagiliaji, majukumu ya vyama vya wamwagiliaji, ugawaji na usajili wa maeneo ya umwagiliaji ndani ya skimu, uendeshaji na utunzaji wa skimu za umwagiliaji, utaratibu wa ukusanyaji wa ada za huduma za umwagiliaji, wajibu na umiliki wa ardhi kuhusiana na shughuli zinazoweza kuathiri shughuli za umwagiliaji, uhamishaji wa maji ya umwagiliaji baina ya mabonde, udhibiti wa usafiri ndani ya mifereji na vivuko

visisvyopangwa, vitendo vinavyokatazwa na usimamizi na tathmini ya utendaji wa skimu za umwagiliaji.

Sehemu ya Saba ya Muswada inaweka masharti kuhusu uhifadhi wa mazingira na afya. Kadhalika, inapendekezwa katika sehemu hii kuweka masharti yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira na uendelezaji wa tafiti za umwagiliaji.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza kuweka masharti kuhusu masuala ya fedha. Maeneo muhimu katika sehemu hii ni pamoja na Ibara ya 53 ambayo inapendekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji kwa lengo la kuendeleza na kuimarisha Sekta ya Umwagiliaji; Ibara ya 56 inahusu usimamizi wa mfuko; na Ibara ya 61 inatoa mamlaka kwa Tume kukopa na kuwekeza fedha za Tume kwa kadiri itakavyoona inafaa kwa maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inapendekeza kuweka masharti kuhusu makosa na adhabu mbalimbali kwa watu wanaokiuka sheria inayopendekezwa. Makosa yanayopendekezwa chini ya sehemu hii ni pamoja na kuharibu mifumo ya umwagiliaji na miundombinu ya umwagiliaji; kuzuia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; kumzuia afisa yeyote wa umma asitekeleze mamlaka yake halali chini ya sheria inayopendekezwa; na kuingilia au kubadilisha mkondo wa maji kwenye miundombinu ya umwagiliaji.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inahusu masharti ya jumla. Sehemu hii inaweka masharti yanayotoa kwa Wajumbe na Watumishi wa Tume na Kamati, wajibu wa kutunza siri katika utekelezaji wa majukumu yao chini ya Sheria inayopendekezwa. Sehemu hii pia inaweka masharti kuhusiana na mikutano ya wadau, mamlaka ya Waziri kuandaa kanuni na masharti ya mpito kutoka Ofisi za Kanda za Umwagiliaji kuelekea uanzishwaji wa Ofisi za Umwagiliaji za Mikoa chini ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, ninapenda kupitia kwako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kuujadili Muswada huu na kuupitisha kwa hatua mbili, yaani Kusomwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu. Ni imani yangu kwamba, kwa kutambua umuhimu wake katika kuleta matokeo makubwa ya haraka kwenye kilimo, Waheshimwa Wabunge wenzangu wataridhia Muswada huu na marekebisho yote yaliyopendekezwa kwenye Jedwali la Marekebisho ili hatimaye kuupitisha na uwe Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na

Ushirika, Engineer Chiza. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua Muswada ulio mbele yetu; anakuja Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Prof. Peter Msolla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yanayohusu Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2013 *(The National Irrigation 2013).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 na 16 Agosti mwaka huu, Kamati yangu ilipata fursa ya kuupitia Muswada huu na kuweza kutoa maoni yake ambayo yanalenga kuiboresha sheria itakayotungwa. Aidha, tarehe 13 na 14 Agosti, 2013 Kamati ilipata nafasi ya kukutana na Wadau wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 *(The National Irrigation Act, 2013)* ili Bunge lako Tukufu liupitie na hatimaye kuwa sheria baada ya kupitia hatua zake zote. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaona kwamba, Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu,

umechelewa sana kuletwa Bungeni ikizingatiwa mambo yafuatayo:-

(i) Tanzania ni nchi ya kilimo na takribani asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kwa uchumi na maisha yao kwa ujumla.

(ii) Tanzania ina eneo kubwa takribani hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo lakini eneo linalolimwa ni asilimia 24 tu. Aidha, kuna hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na ambazo zimegawanyika kiuwezo wa uzalishaji kama ifuatavyo: Maeneo yenye uwezo mkubwa wa umwagiliaji, yaani *high potential irrigation area* ni hekta milioni 2.3; maeneo yenye uwezo wa kati wa umwagiliaji *(medium potential irrigation area)* ni hekta milioni 4.8; maeneo yenye uwezo mdogo wa umwagiliaji *(low potential irrigation area)* ni hekta milioni 22.3. Hata hivyo, eneo linalotumiwa kwa kilimo cha umwagiliaji licha ya fursa hii ya kipekee ni hekta 452,392 tu, sawa na asilimia 1.53 ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

(iii) Kilimo chetu, kwa muda mrefu kimekuwa kikitegemea mvua ambazo kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi hasa katika miaka ya hivi karibuni, mvua zimekuwa hazitabiriki na hivyo kufanya kilimo kutokuwa na tija. Hivyo, kuletwa kwa Muswada huu ni kutekeleza azma ya KILIMO KWANZA hususan nguzo ya 3.1.4 inayosema; "kuanzisha Wakala wa Taifa wa Umwagiliaji *(National Irrigation Agency – NIA)* unaojitegemea chini ya Wizara ya Kilimo."

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudia kutunga Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 (*The National Irrigation Act*, *2013),* ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inayojitegemea *(The Establishment of the National Irrigation Commission)* na kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo na kuondoa changamoto zilizojitokeza kwenye Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaafiki kuwa, Bunge lako Tukufu katika kikao hiki sasa lijadili na kupitisha Muswada huu wenye lengo la kuanzisha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo hayo ya utangulizi, Kamati inatoa maoni ya jumla kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Sheria hii isimamiwe kwa umakini kwa lengo la kumlinda mkulima wa kilimo cha umwagiliaji ili anufaike zaidi.

(ii) Wakati wa utekelezaji wa sheria hii hasa katika kutenga maeneo ya umwagiliaji, Wananchi wa eneo husika washirikishwe kikamilifu ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Miradi ya Umwagiliaji.

(iii) Katika utekelezaji wa malengo ya sheria hii, ushirikiano unahitajika kati ya Tume, Wizara zote

zinazohusika, mikoa na Halmashauri ambako Miradi inatekelezwa ili iwe na tija na iwe endelevu.

(iv) Pamoja na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Sheria hii, Serikali iweke utaratibu mzuri ili wakulima wadogo wasiathirike.

(v) Serikali ihakikishe kuwa kanuni za kutekeleza sheria hii zinaandaliwa mapema iwezekanavyo kwani kumekuwa na mazoea ya kuchelewesha kanuni za kutekeleza sheria zinazopitishwa na Bunge.

(vi) Ili kilimo cha umwagiliaji kiendelee kuwepo lazima kuwepo na mikakati endelevu na kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

(vii) Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji kinalenga kuleta tija, Serikali iweke mkakati wa kujenga maghala na kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao yatakayozalishwa.

(viii) Usimamizi wa kutosha unahitajika ili maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya umwagiliaji yatumike kulima mazao yaliyokusudiwa.

(ix) Serikali ihakikishe wataalam na watendaji wa kilimo hususan kilimo cha umwagiliaji wanajikita zaidi kwenye utendaji badala ya kukaa maofisini.

(x) Serikali iendelee kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kama inavyooanishwa

> kwenye KILIMO KWANZA, Nguzo ya 2.1.4 inayosema; "Kuongeza bajeti ya umwagiliaji kufikia hekta zisizopungua milioni saba ifikapo mwaka 2015."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia sehemu na vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kurekebisha maneno, sentensi, kuondoa baadhi ya vifungu, kuweka vifungu vipya na Jedwali la Marekebisho liletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Baadhi ya maeneo yaliyoainishwa na Kamati ni kama yalivyooneshwa kwenye ukurasa wa nne mpaka wa kumi wa Taarifa hii.

Sehemu ya I, Kifungu cha 2 katika tafsiri ya neno *Commission* herufi 'a' iliyopo kati ya maeneo *Comission* na *established* liondolewe na badala yake neno *as* litumike. Katika tafsiri ya *drainage works* maneno *sub-oil drain* yaondolewe na badala yake maneno *sub-soil drainage* yatumike.

Katika tafsiri ya neno *irrigation area* baada ya neno *Minister* yaongezwe maneno *of Land.*

Katika tafsiri ya neno *irrigation inspector* maneno ya pembeni ya Muswada *(marginal note)* yaondolewe.

Katika tafsiri ya neno *irrigation service fees* neno *operational* lirekebishwe ili lisomeke *operation.*

Sehemu ya II, Kifungu cha 3(3)(d) neno *"do"* lirekebishwe na kusomeka *"doing"*.

Kifungu cha 3(8) Kamati inashauri kuwa kifungu chote kiondolewe na badala yake kisomeke "(8) *In nominating the members of commission, a regard shall be made to the gender, professionalism and competence in the irrigation and drainage issues."*

Kifungu cha 5(2)(b) neno *"the"* lililopo kati ya *"represent" na "government"* liondolewe.

Kifungu cha 5(2)(g) neno *"the"* lililopo kati ya *"in"* na *"irrigation"* liondolewe.

Kifungu cha 5(2)(n), liongezeke neno *"to"* baada ya neno *"and"*, pia neno *"overseeing"* lirekebishwe na lisomeke *"oversee".*

Kifungu cha 6(2), Kamati inashauri neno *"the"* lililopo kati ya maneno *"functions"* na *"terms"* liondolewe na alama ya mkato iwe kati ya maneno hayo.

Kifungu cha 7(1), yaongezeke maneno *"in the absence of"* baada ya neno *"chairman".*

Kifungu cha 8(3) Kamati inashauri maneno *in the absence of* baada ya neno *chairman.*

Kifungu cha 8(3) Kamati inashauri maneno *"officer by title or name"* yafutwe na badala yake maneno *"Principal Officer of the Commission"* yatumike.

Kifungu cha 8(4) neno *"function* lisomeke *"functions".*

Kifungu cha 9 neno *"efficient"* lisomeke *"efficiently".*

Kifungu cha 10(3) Kamati inashauri neno *"services"* lisomeke *"service".*

Kifungu cha 11(2)(b) Kamati inashauri neno *"irrigation"* lililopo baada ya maneno *"identification of"* liondoke.

Kifungu cha 11(2)(f) Kamati inashauri neno *"formulation"* liondolewe na badala yake neno *"formation"* litumike.

Kifungu cha 11(2)(i) Kamati inashauri neno *"rain"* liondolewe na badala yake neno *"surface"* litumike.

Kamati inashauri vipengele vifuatavyo viongezwe baada ya kifungu cha 11(2)(p):-

*" (q) be a liaison office between the Commission and the District Authorities on the implementation and enforcement of this Act;*

*(r) facilitate the promotion, development, fostering and upholding of local Government Authorities in realization of goals and targets of those local government authorities in relation to irrigation development;*

*(s) provide advice to the Commission as regards to the implementation of this Act including area to be declared as irrigation areas within their jurisdiction;*

*(t) facilitate the designation of the District irrigation offices in their areas to foster irrigation development and management and;*

*(u) perform such other functions as may be entrusted to him by the Commission for the better implementation if this Act and regulations made thereunder. "*

Kifungu cha 12(1), Kamati inashauri kifungu hiki kifutwe.

Kifungu cha 13(4)(g) Kamati inashauri neno *"association"* lililopo baada ya neno *"irrigators"* lifutwe na badala yake neno *"organization"* litumike.

Kifungu cha 13(5) Kamati inashauri maneno *"and the Commission"* yaongezwe baada ya maneno *"irrigation manager".*

Kamati inashauri nyongeza ifuatayo baada ya kifungu cha 13(5) isomeke:-

*"(6) in perfoming its functions under this Act, the District lrrigation Engineer shall be responsible to the Commission.*

*(7) every Local Government Authority shall facilitate the establishment and operation of the District lrrigation Office and to ensure that all resources located to such*

*officer are effectively utilized so as to achieve the objective of this Act".*

Sehemu ya IV, Kifungu cha 21(2), Kamati inashauri maneno *"other than the Commission"* yaliyopo kati ya neno *"area"* na *"shall"* mstari wa pili yahamie katika mstari wa kwanza baada ya neno *"person".*

Kifungu cha 21(3), Kamati inashauri kuongeza viambatanisho kwenye maombi yanayohusu kifungu na kuongeza kipengele kifuatacho ambacho kitakuwa "(g) *detailed feasibility study report"* na maneno yaliyo katika kipengele (g) yatakuwa katika kipengele (h).

Sehemu ya VI, Kifungu cha 29(2), Kamati inapendekeza maneno *"for the management of irrigation schemes"* yaliyo katika kipengele (a) *and management of the irrigation schemes* yaliyo katika kipengele (c) na *for proper management of the irrigation schemes* yaliyo katika kipengele (d) yaondolewe.

Kifungu cha 30(1) herufi 's' iondolewe katika neno *"disputes".*

Kifungu cha 39(2) namba 1 iliyopo baada ya neno *subsection* iwekewe mabano.

Kifungu cha 40(1) Kamati inashauri neno *and* lililopo kati ya maneno *"prescribe"* na *"irrigation"* liondolewe.

Kifungu cha 41(1), Kamati inashauri maneno *"as"* yanayoonekana katika kipengele (a) na (b) yaondolewe.

Kifungu cha 41(2), Kamati inashauri kuondoa neno *he* lililopo kati ya maneno *"owners"* na *"shall"* liondolewe na badala yake maneno *"the inspector"* yatumike.

Kifungu cha 42(1), Kamati inashauri maneno *"rats or other vermin"* yaondolewe na badala yake neno *"pests"* litumike.

Kifungu cha 42(5), Kamati inashauri maneno *irrigation inspector* yaliyopo kati ya maneno *"the"* na *"requires"* katika mstari wa kwanza yaondolewe na badala yake neno *"Commission"* litumike.

Kifungu cha 46(1)(a), Kamati inashauri neno *"land"* lililopo katika mstari wa kwanza kati ya maneno *"irrigation"* na *"for"* na neno *"agriculture"* lililopo katika mstari wa pili kati ya maneno *"irrigated"* na *"and"* yaondolewe na badala yake neno *"area"* litumike.

Kifungu cha 46(2)(c), Kamati inashauri neno *"to"* lililopo kati ya neno *"not"* na *"block"* liondolewe.

Kifungu cha 46(3), Kamati inashauri maneno *"and not exceeding five million shillings"* yaondolewe ili kuipa mahakama kutoa adhabu kulingana na ukubwa wa hasara iliyosababishwa.

Kifungu cha 47(4), Kamati inashauri maneno *director general”* yaliyopo kati ya maneno *“the”* na *“within”* katika mstari wa pili yaondolewe na badala yake neno *“minister”* litumike.

Sehemu ya VII, Kifungu cha 51(2), Kamati inashauri maneno *“washes articles in or otherwise”* yaliyopo kati ya maneno *“who”* na *“polute”* yaondolewe.

Sehemu ya VIII, Kifungu cha 53(2), Kamati inashauri maneno *“shall consist of”* yaondolewe na maneno *“resource of”* yawekwe mwanzoni mwa kifungu hicho.

Kifungu cha 55, Kamati inashauri kifungu hiki kiondolewe ili kumwondolea Waziri mzigo wa kuipa Tume fedha kwa kuwa itakuwa na vyanzo vyake vya mapato.

Kifungu cha 56(4), Kamati inashauri maneno yaliyopo katika mstari wa tatu yanayoanzia na neno *and liable on* … yaondolewe.

Sehemu ya IX, Kifungu cha 63(1)(i), Kamati inashauri neno *“years”* liongezwe kati ya maneno *“three”* na *or “both”.*

Jedwali, Ibara ya 1, Kamati inashauri neno *number* lililopo kati ya maneno *“their* na *“a vice chairman”* liondolewe na badala yake neno *“member”* litumike.

Ibara ya 3(1), Kamati inashauri kifungu hiki kirekebishwe na kusomeka *"the commission shall meet three times per year".*

Ibara ya 3(2), Kamati inashauri maneno *"in his absence"* yaongezwe kati ya maneno *"or"* na *"the vice chairman"* yaliyopo katika mstari wa pili.

Ibara ya 5, Kamati inashauri neno *"rot"* lililopo kati ya maneno *"shall"* na *"have"* liondolewe na badala yake neno *"not"* litumike.

Ibara ya 6, Kamati inashauri katika mstari wa kwanza maneno *"including the Chairman"* liongezwe kati ya maneno *"interest"* na *"direct".* Pia katika mstari wa nane wa ibara hii maneno *"Chairman or Vice Chairman"* yaliyopo kwenye mstari wa tano yaondolewe na badala yake neno *"meeting"* litumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine ni kama yatakavyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa, baada ya Muswada huu kuwa Sheria, Serikali itaweka utaratibu mzuri kwenye kanuni ya kuunda Tume na Kamati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kuwa, Muswada huu umebeba maoni mengi ya wadau na bila shaka utakapokuwa Sheria kamili, mabadiliko ya kweli

yataonekana katika Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitumie nafasi hii, kumshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika - Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Naibu Waziri - Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Katibu Mkuu - Ndugu Sophia Kaduma na Naibu Katibu Mkuu - Eng. Mbogo Futakamba, Wataalam wote wa Wizara pamoja na Wataalam wengine, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu. Aidha, nawashukuru wadau wote walioshiriki kutoa maoni yaliyosaidia kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Said Juma Nkumba - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mheshimiwa Namelok Edward Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdulsalaam Seleman Amer, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dkt. Lucy Sawere Nkya, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Lolesia Masele Bukwimba, Mheshimiwa Mch. Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Sylvestry F. Koka,

Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Sadifa Khamis, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na mimi mwenyewe Mheshimiwa Prof. Peter Msolla -Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati; Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Angelina Sanga, Mwanasheria - Ndugu Maria Mdulugu pamoja na Ndugu Sophia Vumbi - Msaidizi wa Kamati, kwa kuihudumia Kamati na kuhakikisha kwamba, taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na hapa namtambua Mheshimiwa Rose Kamili. Mheshimiwa Rose Kamili tafadhali!

**MHE. ROSE K. SUKUM - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeleta Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 *(The National Irrigation 2013),* kwa dhana kuu ya kutungwa kwa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013, ambayo pamoja na mambo

mengine, inalenga kuondoa changamoto zilizokuwepo kwenye Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji. Changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa mfumo wa kisheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji; kutoendelezwa, kutokutekelezwa na kuhujumiwa kwa miundombinu ya umwagiliaji; udhaifu wa mfumo wa kitaasisi usiokidhi kasi ya kuendelea kupanuka kwa shughuli za umwagiliaji na uelewa mdogo wa Wananchi unaopelekea kushindwa kutambua na kutekeleza kikamilifu wajibu wao katika kumiliki na kuchangia ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji inayojengwa kwa fedha nyingi za Serikali. Aidha, Sheria inalenga kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo itakuwa na jukumu la kuendeleza na kuendesha na kusimamia kilimo cha umwagiliaji na mifumo ya umwagiliaji na kuainisha masuala mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inaonesha kuwa wakulima wadogo walikuwa na umwagiliaji wa asili. Skimu za asili na mashamba makubwa ya umwagiliaji yaliendelea kuanzishwa kabla na baada ya nchi yetu kupata uhuru. Serikali ya Kikoloni ya Tanganyika ilianzisha mashamba ya miwa na viwanda vya sukari, ikiwa ni pamoja na *TPC*, Kilombero, Mtibwa na Kagera. Katika miaka 1950, mashamba mengi ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo yalianzishwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini ilichukua sura mpya tangu kuanza kutekelezwa kwa programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme – ASDP).*

Halmashauri za Wilaya ndiyo watendaji wakuu wa kazi za uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans – DADPs).* Asilimia 75 ya bajeti ya programu inaelekezwa katika kutekeleza maendeleo ya umwagiliaji ngazi ya Taifa na ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kisheria wa uangalizi wa ardhi na maji katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unafananisha rasilimali hizo kuwa ni mali za umma. Hivyo basi, Serikali ndiyo mamlaka pekee yenye dhamana ya kuangalia na kukidhi matumizi yake. Kwa mfano, utunzaji wa rasilimali za maji kama zilivyoainishwa katika Sheria ya *The Water Utilization Control and Regulation Act No. 42* ya mwaka 1974 na marekebisho yake kwa Sheria ya Marekebisho Na. 10 ya 1981. Aidha, Sheria hiyo ya Marekebisho yake ilifutwa na Sheria mpya ya *Water Resource Management Act No. 11* ya mwaka 2009, iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano hapo tarehe 28 Aprili, 2009 na kuanza kutumika rasmi kwa Waraka wa Serikali *(GN)* wa tarehe 1 Agosti, 2009, Namba 235, uliochapishwa tarehe 10 Julai, 2009. Sambamba na hilo ni kwamba, Sheria hii inatambua kuwa rasilimali yote ya maji katika nchi iko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan – NIMP),* mwaka 2002, ulibainisha kuwa, jumla ya hekta milioni 29.4 hapa nchini zinaweza kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, kati ya hizo hekta milioni 2.3 zina uwezo mkubwa wa kuendelezwa, hekta milioni 4.8 zina uwezo wa

kati wa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji na hekta milioni 22.3 zinao uwezo mdogo wa kuendelezwa. Takwimu za Serikali zinaonesha kuwa hekta 81,302 zimeendelezwa kufikia Juni, 2011 na kufanya eneo la jumla lililoendelezwa kuwa hekta 345,690 kati ya eneo lote linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira ya mwaka 2004 inahitaji kilimo cha umwagiliaji kufanyika sambamba na kutekeleza majukumu maalum ya kuhifadhi ardhi, rasilimali maji ya juu na chini ya ardhi na jamii. Sera ya ardhi haitoi ulinzi kisheria wa kutosha kwa ajili ya ardhi inayotumika kwa umwagiliaji na wala hakuna sera ya ugatuaji madaraka *(decentralization policy),* ambayo inajenga uwezo wa kitaasisi na kuziongezea nguvu mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuanzisha na kutekeleza mipango yenye tija kwa ajili ya maendeleo endelevu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hiyo hapo juu inapata nguvu kutokana na kauli ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa kwenye Kamati tarehe 13 Agosti, 2013 kwamba; "Mfumo uliopo haufafanui kwa kina ni jinsi gani Serikali za Mitaa ambazo ndizo zilizo karibu na Wananchi, zitashiriki katika Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji ikiwemo kuhusika katika usimamizi wa skimu zinazojengwa katika maeneo yao." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kwa ujumla wake unaonesha kuwa, badala ya kugatua madaraka kwa Serikali za Mitaa, unachukua hata madaraka kidogo

yaliyokuwepo hapo mwanzo. Hii inaonekana ngazi zote za uwajibikaji haziwajibiki kwa Mkurugenzi wa Halmashauri na badala yake zitawajibika kwa wateule wa Tume. Mfano ni kifungu cha 13(5).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwendelezo huo wa upokaji wa madaraka ya Serikali za Mitaa, kifungu cha 13(6) kinaeleza kuwa, katika utendaji wa majukumu yake, uwajibikaji wa masuala ya kitaalam, Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya ni kwa Tume na kifungu cha 13(7) kinazilazimisha Halmashauri za Wilaya kusaidia uanzishwaji wa Ofisi za Umwagiliaji za Wilaya kwa kutoa rasilimali zote zinazohitajika na pale pale uwajibikaji wa Watendaji wake Wakuu uwe ngazi zaidi ya Mkurugenzi. Hii ina maana kuwa, sheria hii inanyang'anya Halmashauri husika mamlaka za usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetumia rasilimali fedha, watu na muda mwingi kwa ajili ya maboresho ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reform Programme)* ya ugatuaji wa madaraka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze ni kwa nini inashindwa kuheshimu sera hii ya ugatuaji wa madaraka?

*Wetland areas suitable for irrigation* mtaisoma iko hapo chati yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo tajwa hapo juu tayari yanasimamiwa na mamlaka zilizopo kisheria. Mfano wa kwanza ni Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, Ofisi ya Maji Bonde la Rufiji inayosimamia matumizi ya

maji katika Bonde la Rufiji. Bonde hili maana yake ni eneo lote ambalo mwelekeo wa maji yake huingia Mto Rufiji na hatimaye Bahari ya Hindi. Bonde hilo lina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 177,420 na lina mito mikuu minne ambayo ni *Great Ruaha Mkuu* wenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 82,970, Kilombero wenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 39,990. Mto mwingine ni Luwegu wenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 26,300 na Mto Rufiji wenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 22,160.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde hilo lina Bodi yake ambayo ina Wajumbe kumi ambapo Afisa Maji wa Bonde ndiye Katibu wa Bodi hiyo. Bodi ina Ofisi ya Bonde la Rufiji iliyoanzishwa Septemba, 1993, kwa mujibu wa Sheria ya Maji Na. 42 ya mwaka 1974 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1981 na 1991. Aidha, kuna Sheria Na. 5 ya mwaka 1975, Sura ya 138, inayoitwa "*The Rufiji Basin Development Authority*" iliyoundwa na Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji. Pamoja na mambo mengine, Mamlaka ina jukumu la kuwezesha na kukuza shughuli za kilimo katika eneo la Bonde hilo. Kwa maana rahisi ni kwamba, shughuli za umwagiliaji haziwezi kuachwa pembeni katika muktadha wa kukuza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili ni Bonde la Ziwa Rukwa lililoanzishwa Desemba mwaka 2003 na Wajumbe wa Bodi ya Maji waliteuliwa mwezi Mei mwaka 2004. Kuanzia wakati huo, utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji uliendeshwa kwa kuhusisha Wajumbe wa Bodi kama ilivyoelekezwa katika Sheria

Namba 42 ya mwaka 1974. Ofisi ya Bonde ni chombo cha kutekeleza Sera ya Maji katika usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Mabonde haya ni usimamizi wa rasilimali za maji, uchunguzi na uchimbaji wa maji chini ya ardhi, vilevile kuweka mipango na kufanya utafiti, usimamizi wa Sheria na utunzaji wa mazingira ya vyanzo vya maji ambapo unahusisha kutoa vibali na hati za kutumia maji, kusimamia matumizi, kanuni na taratibu za kutumia maji, kusajili vyama vya watumia maji, kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji na kuratibu masuala ya mazingira ya vyanzo vya maji ndani ya bonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5(1) cha Muswada kinasema kuwa; "Tume itakuwa na majukumu ya kuratibu, kuendeleza na kusimamia maendeleo ya Sekta ya Umwagiliaji."

Mheshimiwa Naibu Spika, maandishi ya Serikali yanaonesha kuwa, kufikia mwaka 2002, Wizara ya Kilimo iliamua kukipandisha hadhi Kitengo cha Umwagiliaji kuwa Wakala (*National Irrigation Agency - NIA*) au Idara inayojitegemea na ndipo ilipokubalika na kuitwa Idara ya Umwagiliaji na huduma za Ufundi na mwaka 2008 Idara hiyo mpya ikahamishiwa rasmi kwenye Wizara mpya ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwamba, Serikali inazidi kuunda taasisi ambazo zinazidisha matumizi kwa walipa kodi tu, kwani

Sheria hii ingeweza kusimamiwa na Wizara chini ya Idara ya Umwagiliaji na huduma za ufundi na marekebisho kama yangehitajika yangeweza kufanyika. Tatizo ambalo tunaliona litaendelea kuwepo ni upatikanaji wa fedha za uwekezaji na uendelezaji wa rasilimali watu katika sekta hii. Hivyo basi, siyo kweli kwamba, Tume inayokusudiwa kuanzishwa itaweza kuondoa matatizo hayo ya msingi bali ni kuongeza ukiritimba tu. Hivyo basi, badala ya kutengeneza mfumo mpya wa utawala ingekuwa ni bora kuimarisha ule uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa hoja hiyo hapo juu ni vifungu vya 8, 9, 10, 11, 12 na 14. Vifungu hivi vyote vinatengeneza nafasi mpya wakati nafasi zinazotengenezwa zinaweza kuwepo katika mfumo wa sasa wa utendaji wa Serikali kwa kutumia Taasisi na Idara zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kilimo cha umwagiliaji, kumekuwepo na changamoto nyingi, nazo ni:-

- Uwekezaji mdogo katika uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji kutokana na ufinyu wa bajeti;
- Ushiriki mdogo wa Sekta Binafsi katika uwekezaji na kutoa huduma za kitaalam;
- Matumizi kidogo ya teknolojia zinazotumia maji kwa ufanisi na maji chini ya ardhi;
- Matumizi kidogo ya teknolojia za kuvuna maji;
- Uchache wa mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambayo yangeweza kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

- Uhaba wa wataalam na vitendea kazi katika ngazi zote hasa katika ngazi ya Halmashauri; na
- Usimamizi hafifu katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kuwa, muundo wa shughuli za umwagiliaji tayari upo na tayari taasisi na Idara za Serikali zinazojihusisha na shughuli hizo zipo na zinaendelea kufanya kazi. Changamoto zipo na zimeendelea kuwepo kwa kipindi chote hicho; hoja ya msingi ni Muswada huu wa Sheria pamoja na mambo mengine siyo kuunda Chombo kipya kingine ambacho kwa kiwango kikubwa ni kutumia rasilimali chache tulizonazo badala ya kuimarisha mamlaka za mabonde na Idara ya Umwagiliaji ili ziweze kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ni kuwa, Wakulima wa Tanzania wanakabiliwa na matatizo makubwa ya uzalishaji duni ambao unatokana na kutegemea mvua za msimu ambazo zinakuwa hazina uhakika mara nyingi. Umwagiliaji wa mashamba ndiyo suluhisho la uhakika katika kukifanya kilimo chetu kuwa na tija na kuondokana na umasikini wa kipato na kuwa na uhakika wa chakula. Aidha, Sera inasema wazi kuwa, uwezo mdogo wa wakulima kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha mfumo wa asili wa umwagiliaji ni tatizo na pia Serikali kuwa na uwezo mdogo katika kuwekeza katika umwagiliaji sambamba na uwekezaji binafsi katika umwagiliaji kuwa mdogo. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa,

tatizo siyo mfumo wa kiutendaji bali ni rasilimali zisizotosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa Tume inayoanzishwa na Muswada huu wa Sheria inaanzisha mfumo mkubwa na unaohitaji rasilimali kubwa kuuendesha. Kifungu cha 11 cha Muswada kinachoanzisha Ofisi za Umwagiliaji za Mkoa ni ukiritimba mkubwa kwani Ofisi za Mkoa siyo za utekelezaji kama ilivyo kwa Wakuu wa Mikoa. Kifungu cha 11(2)(c) kinachosema kuwa mojawapo ya majukumu ya Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji ni kuandaa upembuzi yakinifu wa Miradi ya Umwagiliaji, usanifu wa kina na nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anatoa maelezo ya Muswada, alisema kuwa, kwa sasa Wizara ipo katika maandalizi ya sehemu ya pili ya programu ya maendeleo ya kilimo *(ASDP-II).* Dhana ya Miradi inayofadhiliwa na programu hiyo ni kwa wanufaikaji wa miradi kuibua Miradi yao wenyewe na kuchangia katika Miradi hiyo asilimia fulani ili umiliki wa Mradi husika uwe kwa wanufaikaji. Hivyo basi, kwa kuwa Miradi ya Umwagiliaji ipo kwenye maeneo ya Waheshimiwa Wabunge ni bora Waziri alieleze Bunge; fedha za Miradi hiyo zikishatolewa na *DADPs* pamoja na michango ya wanufaikaji wa Miradi zinapelekwa kwa Tume au inakuwaje; kwani kifungu tajwa hapo juu kinaonesha kuwa Ofisi ya Mkoa ya Umwagiliaji ndiyo itakayotayarisha nyaraka za zabuni na hivyo ndiyo watakuwa wasimamizi wa Miradi hiyo ya Wananchi?

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi; Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri inasimama upande gani katika hili kwani fedha za *DADPs* ndiye mwenye dhamana na fedha hizo. Je, Ofisi hiyo ya Umwagiliaji ya Mkoa itakuwa na Kamati ya Zabuni?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11(2)(i) kinasema kuwa, Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji zitakuwa na jukumu la kuandaa mipango ya matumizi ya maji yaliyo chini ya ardhi na maji ya juu ya ardhi kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji. Sheria hii inasimamiwa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Wakati Sheria ya Utunzaji wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009, Kifungu cha 15 kinachohusu uwepo wa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji na majukumu yake kwenye kifungu kidogo cha 15(4), nanukuu; *"There shall be appointed such officers who shall have duty to ensure efficient, effective and sustainable economical management and supervision of water resources in accordance with the provision of this act".* Mwisho wa kunukuu.

Kifungu hicho kinasimamiwa na Waziri wa Maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi; ni kifungu cha Sheria ipi kati ya hizo ambazo zinasimamiwa na Mawaziri wawili tofauti kitakachokuwa na nguvu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11(3) kinasema kuwa, Injinia wa Umwagiliaji wa Mkoa atateuliwa kutoka miongoni mwa Watumishi Waandamizi wa Umma wenye uzoefu, sifa na uwezo katika maendeleo ya umwagiliaji. Kifungu hiki wadau walikiona na kuitaka Serikali ikirekebishe

kwani kinawanyima watu wenye uwezo na uzoefu katika tasnia nzima ya umwagiliaji ambao hawako kwenye ajira rasmi ya Serikali na kuwakumbatia watumishi waliomo kwenye ajira ya Serikali. Aidha, kifungu hiki hakitoi nafasi kupata uzoefu wa utendaji wa aina nyingine na badala yake kinaendeleza utendaji wa mazoea na ni cha kibaguzi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iondoe kifungu hiki kutokana na sababu tajwa hapo juu kwamba kuna watu wengine kwenye sekta binafsi wanaweza ku-*fit* kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mfumo huu mpya wa uundwaji wa Tume unaingilia na kuukwaza mfumo wa maboresho ya Serikali za Mitaa na unakinzana na *Local Government Reform Programme* inayosema uundwaji wa Idara za kiutendaji ndani ya Halmashauri ni jukumu la Baraza la Madiwani na si Waziri mwenye Jukumu la Serikali za Mitaa. Mfano wa hilo ni kifungu cha 13(1) kinachoanzisha ndani ya Halmashauri ya Wilaya, Idara ya Umwagiliaji bila ya Baraza la Madiwani kuhusishwa. Kifungu hiki kinazilazimisha hata Halmashauri zisizohitaji Idara hiyo ya Umwagiliaji kama vile Halmashauri ya Nyamagana, Halmashauri ya Bukoba Mjini, Ilala, Musoma Mjini na maeneo mengine, kulazimishwa kwamba wao pia waunde Idara hiyo. Ukweli ni kwamba, uanzishwaji wa Idara katika Halmashauri ni jukumu la Baraza na Idara zinatofautiana kati ya Halmashauri na Halmashauri kutegemeana na mahitaji na mazingira ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 14 cha Muswada kinahusu uteuzi wa Wakaguzi wa Umwagiliaji.

Kambi ya Upinzani inapingana na dhana nzima ya uteuzi wa watendaji na badala yake inashauri kuwepo na ushindani wa nafasi hizo na atakayeshinda apewe nafasi hiyo. Hoja hii inatokana na ukweli kwamba, Tume kwa dhana ya uwepo wake inatakiwa iwe huru ikiwemo uwezo wa kuajiri watumishi wake; hivyo, Sheria ikishawekwa kifungu cha kusema ichukue watendaji waliokuwepo katika Idara ya Umwagiliaji pasipo kuangalia umakini na ubora wa mtumishi ni dhahiri uwezekano wa kuhamisha utendaji wa mazoea kuja kwenye Tume ni mkubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15(1) kinachohusu mamlaka za Mkaguzi wa Umwagiliaji, badala ya kuonesha kuwa kinatoa msaada kwa wenye skimu ili ziendane na maagizo, badala yake kifungu hicho kinaonesha mamlaka kutishia mmiliki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa, Sheria inatakiwa iwe yenye kuweka mahusiano baina ya watekelezaji wa Sheria hiyo na wanaotakiwa kuisimamia. Tukumbuke kuwa, skimu nyingi ni za Wananchi hivyo sheria za kuwavizia ni kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 47 kinachohusu wajibu wa mmiliki wa ardhi kuhusu usalama wa miundombinu ya umwagiliaji, kati ya miundombinu iliyotajwa ni tanki na tanki linaweza kuwa la sementi au plastiki. Hali kadhalika, umwagiliaji ni wa aina nyingi na hivyo basi miundombinu ya umwagiliaji inatofautiana gharama zake kulingana na chanzo cha maji. Kifungu cha 47(3) kinachosema pale mmiliki wa miundombinu anaposhindwa kutimiza ushauri uliotolewa na Mkaguzi na

kupelekea Mkaguzi kuchukua jukumu la ukarabati wa miundombinu na gharama alizotumia kuzirejesha kwa mmiliki. Sheria hii haisemi mmiliki akishindwa kurejesha gharama ni nini kitatokea kwa mmiliki, badala yake Kifungu cha 47(4) kinampa mmiliki nafasi ya kukata rufaa kwa Waziri dhidi ya uamuzi wa Mkaguzi. Hii inamaanisha kwamba, hata mkaguzi wa mambo ya Serikali akiona barabara imeharibika akatengeneze halafu Halmashauri ilipe; tukiangalie hiki kifungu kwa undani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kifungu cha 11(2)(c) cha Muswada kinasema kuwa, moja ya majukumu ya Ofisi ya Umwagiliaji ya Mkoa ni kuandaa nyaraka za zabuni. Maana yake ni kwamba ujenzi au ukarabati wa miundombinu unafanywa ka njia ya zabuni, sasa Mkaguzi atafanya ukarabati kwa kutumia fedha gani na za kutoka wapi? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge juu ya utata huu kwani hapa ni mazingira ya matumizi mabaya ya rasilimali chache za Wananchi zilizopo. Rejea Kifungu cha 15 kinachohusu mamlaka ya mkaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulioletwa na Serikali kwa lengo la kupata Baraka za Bunge ili kuwa na Sheria, mbali na uundwaji wa Tume, hakuna kifungu chochote kinachotoa suluhisho kwa mkulima mdogo jinsi gani atapata unafuu wa kutumia miundombinu ya umwagiliaji na kuondokana na mtindo wa kutegemea mvua za msimu. Ukiangalia sehemu ya nne ya Muswada inahusu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, hasa kifungu cha 21 kinachohusu maombi kwa ajili ya ujenzi wa

miundombinu ya umwagiliaji; masharti ni mengi na makubwa, ambayo kwa mkulima wa kawaida ni aina nyingine ya ukiritimba inayomtoa nje ya maendeleo na hivyo kuwapa nafasi wale wenye fedha na hatimaye wakulima waishio maeneo yenye fursa za umwagiliaji kushindwa kunufaika na maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufafanuzi huo wa kazi za Mabonde, Kifungu cha 23(2) cha Muswada kinasema kuwa; "Mtu yeyote hataruhusiwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji au kuzuia mtiririko wa maji katika mfereji wa maji bila ridhaa ya Tume au Mamlaka yeyote iliyokasimiwa."

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni kwamba, kama mtu amekwishapewa kibali cha matumizi ya maji kutoka kwenye mamlaka husika ni kwa nini tena azuiliwe kuyatumia kwa kadiri anavyohitaji yeye? Kama ni miundombinu ya umwagiliaji au matumizi ya ufugaji wa samaki hilo linakuwa ni juu ya mwenye kibali cha matumizi ya maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kifungu hiki kinamnyima haki ya msingi aliyepatiwa kibali cha matumizi ya maji na hivyo kifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 66(1) kinachohusu utunzaji siri, naomba kununukuu; "Kila Mjumbe wa Kamati ya Tume na kila mtu aliyeajiriwa chini ya Sheria hii hatatoa kwa mtu yeyote, isipokuwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii au pale atakapotakiwa kufanya hivyo chini ya Sheria iliyoandikwa, taarifa yoyote ambayo atatakiwa katika kutekeleza majukumu yake kuhusiana na masuala ya fedha au taarifa za kibiashara za mtu."

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema umwagiliaji si biashara ya kuzuia kubadilishana uzoefu baina ya wamwagiliaji katika maeneo mbalimbali kwani lengo ni kukidhi matumizi bora ya maji na miundombinu ya umwagiliaji. Je, kama usiri ukitawala ni kwa vipi ubadilishanaji wa uzoefu katika tasnia hiyo utafanyika kama wenye taarifa sahihi watazifanya kwa ni siri? Tukumbuke kuwa, biashara hii siyo ya ugunduzi wa bidhaa na kushindania soko. Maji ambayo ndiyo rasilimali na bidhaa inatakiwa itumiwe kiuendelevu ili watumiaji wengi wapate. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukifuta kifungu hiki kwani hakitaleta tija katika tasnia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwamba, Wananchi wa Hanang' na Mkoa mzima wa Manyara, wana vikundi vidogo vidogo vya umwagiliaji, lakini tatizo kubwa ni uwezo mdogo wa vikundi hivyo. Hivyo basi, Mheshimiwa Waziri awaeleze Muswada huu wa Sheria unawasaidiaje kutatua tatizo hilo la uwezo mdogo wa ujenzi wa miundombinu bora na endelevu kwa kuwa tumebarikiwa kuwa na mabonde mengi na yenye rutuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru sana Wananchi wa Hanang', kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya Kibunge. Ahsante sana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rose Kamili, kusema ukweli amechambua Sheria sana na kama Hotuba

zote za Upinzani zingekuwa hivi, lingekuwa jambo la maana sana. Kwa kweli ameichambua Sheria kifungu kwa kifungu, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri, atazingatia maoni ambayo yametolewa na kuona namna gani Sheria inakuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Sasa dakika zetu zilizobakia siyo nyingi, ingekuwa ile enzi ya dakika kumi, kumi, tungepata wachangiaji wawili, lakini sasa ni dakika kumi na tano, tutaona hali inavyoenda, basi angalau tupate hata mchangiaji mmoja katika waliopo. Naomba nimwite Mheshimiwa David Silinde awe mchangiaji wetu wa kwanza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kujadili Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo tunahitaji kuipitisha siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inataka tuanzishe Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ukisoma malengo unaweza kuyaona ni mambo mazuri sana; lakini nchi yetu imepitia mambo mengi na mpaka sasa kama Taifa tumekuwa na mifumo ya umwagiliaji mingi tu katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzisha Tume, kuanzisha tu tulihitaji tupewe sababu kwa nini Tume inaanzishwa. Ukipitia mantiki ya kuanzisha Tume ya Umwagiliaji tafsiri yake ni kwamba, Idara na Vitengo vya Umwagiliaji vilivyopo chini ya Wizara ya Kilimo vyote vimeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuanzisha Tume, lakini kama hakuna fedha, hakuna wataalam, hakuna teknolojia kwa maana ya vitendea kazi, ni kazi bure tunarudia yale yale. Kwa sababu ukipitia vitengo vya umwagiliaji vilivyotangulia, ukipitia mipango na programu zote za kilimo zinazohusu umwagiliaji katika Taifa letu, zote utakuta masuala haya yameshindwa kwa sababu tumekosa fedha, tumekosa wataalam na tumekosa vifaa kwa maana ya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatengeneza Tume lakini mwisho wa siku majibu na matokeo yake yatabaki kuwa yale yale. Katika Tume ambayo tulitarajia kuizindua na katika vifungu vingi ambavyo tunatarajia kuvipitia, tumejaribu kuona kwamba, Tume inataka tuwe na Mkaguzi wa Umwagiliaji wa Kanda au wa Taifa, ambaye atasimamia shughuli zote za umwagiliaji katika maeneo yetu. Lakini ni kweli tutakuwa na Mkaguzi na Mkaguzi huyo atakuwa na jukumu la kupitia Miradi yote ya Umwagiliaji katika Taifa katika maeneo husika ambayo yanahusika na masuala ya umwagiliaji. Ukiangalia kwa undani amepewa mamlaka kwamba, atakwenda kukagua na mara atakapokagua akiona huo mradi haujatekelezwa na yale maagizo aliyopewa yule mtu hajayatekeleza, basi Tume yenyewe kwa maana ya Mkaguzi, atakuwa na mamlaka ya kujenga na kutengeneza upya ule mfumo wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kitu tunasema hakiwezekani kwa sababu tunataka tujue huo Wakala wa Ukaguzi, fedha hizi za kujenga hii miradi ya kushirikiana na

Mkaguzi atazitoa wapi. Kama ni hivyo basi tunataka hiyo sheria isiwe hiyo iende hata kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na yeye kama miradi ya ujenzi imeshindikana basi akishakagua Serikali za Mitaa ama Halmashauri zimeshindwa, apeleke hela ajenge barabara ili kazi ifanyike, lakini sasa unaangalia unakuta kuna mambo mengi yanayokinzana katika Muswada mzima wa hii sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia vilevile Kifungu cha 22 utakuta Tume inapewa madaraka ya kujitwalia ardhi kwa kutangaza kwenye gazeti tu kupitia Kifungu cha 22 cha Sheria iliyoko pale. Sasa haiwezekani Tume ikapewa mamlaka ya kupewa ardhi bila ya kushirikisha Wananchi eti inatangaza kwa sababu mtu ameshinda, kwa sababu unaposhindwa kuwashirikisha Wananchi maana tayari tunajenga migogoro ya ardhi kama inavyoendelea hivi sasa. Wizara inatakiwa ituambie ni namna gani itatoa maana haiwezi kutangaza gazetini Mwananchi anashirikishwaje au mwekezaji anashirikishwaje kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, Kifungu cha 4 kinaonesha kwamba, Tume itakuwa inaweza kuwekeza itakavyoona inafaa, aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi ama vinginevyo. Sasa tupewe maelekezo, inafuata sheria zipi, sheria za mzabuni ama sheria za kwake zenyewe ama sheria nyinginezo ambazo hazieleweki? Tujue ni sheria gani itakayowapa mamlaka ya wao wenyewe kuwekeza ili tujue ni namna gani tutaweza kuwasaidia, kwa sababu tusiweke tu sheria bila ya kuwa na mantiki ya namna gani tunaweza kulisaidia hili Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitia vilevile kifungu namba 66(1), kifungu hiki kinataka kuwepo na utunzaji wa siri wa taarifa hususan za fedha na biashara za wahusika ambao wanahusika na masuala ya umwagiliaji. Sasa kila siku tunalalamika, miongoni mwa mambo yanayosababisha ufisadi nchi hii ni pamoja na usiri hususan katika masuala ya fedha. Fedha haihitaji usiri, fedha tunahitaji tuweke wazi ili tujue namna gani tunaweza kuwakosoa; sasa kama tutaendelea kuwa na usiri na sheria ikapitisha kwamba itakuwa na usiri kama ilivyokuwa kwenye Katiba, Katiba inataka tuwe na uwazi tunakwenda kwenye baadhi ya Halmashauri na Madiwani wanapendekeza turudi kwenye usiri, usiri si ndiyo huo ambao unasababisha mambo yote haya! Sisi wenyewe hatukubaliani na Kifungu cha 66(1) na tuweke wazi kabisa kwamba, hata Waziri anapokuja katika majumuisho juu ya hii sheria, apitie upya na kuhakikisha kwamba patakuwepo na uwazi hususan kwenye masuala ya fedha na biashara zote zinazohusu masuala ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote nizungumze vilevile na masuala ya ujumla. Jimboni kwangu kumekuwa na Miradi ya Umwagiliaji ambayo tangu mwaka 2009 nimezungumza sana hapa Bungeni; kuna umwagiliaji Mradi wa *Ihembe Irrigation Scheme* iko katika Kata ya Kapere Momba. Vilevile kulikuwepo na Mradi wa Umwagiliaji wa Nyamingongo upo katika Kata ya Sibiti Makao Makuu Mpya ya Wilaya yetu ya Momba. Miradi ile tangu mwaka 2009 mpaka leo bado haijakamilika. Leo unakuja na sheria ambayo mimi siielewi na wakandarasi tukiwaambia

tunaomba mmalizie hii kazi, jibu wanalotoa wanakwambia Mheshimiwa Mbunge haiwezekani kwa sababu Serikali haijatupa fedha. Sasa na leo tunaunda Tume ambayo haina fedha kwa sababu watumishi wake ukiangalia mapitio yote hata sifa za watu watakaoteuliwa watatokana na mfumo uliopo. Sasa kama wapo walewale walioshindwa kazi ile ile inategemea wataleta majibu tofauti. Sasa hayo ndiyo mambo ambayo siku zote tumekuwa tukiyakosoa. Sasa tuambieni mifumo ya umwagiliaji iliyoko sasa kama niliyoitaja katika Jimbo langu la Momba itakamilikaje na mwenendo wa kutengeneza Tume kwa wakati unaokuja, maana tutakuwa ni watu walewale kila siku. Tume, Idara, sijui nini; hatuwezi kuendelea kwa sababu inawezekana sisi kama Bunge tukaishauri Serikali badala ya kutengeneza Tume ikaboresha mfumo ambao upo sasa hivi ili tuweze kwenda kule ambako tunahitaji tufikie hayo malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka na hizi kaulimbiu; "Kilimo sijui ni siasa", "Kilimo na Kujitegemea", "Kilimo cha Kufa na Kupona", "KILIMO KWANZA" ambavyo havitekelezeki. Tuwe na mifano na mtuambie ni nchi gani imewahi kuendelea kwa kuwekeza kwenye kilimo. Mtuambie moja tu ambayo inategemea kitu kimoja bila ku-*shift* kwamba tujue kilimo cha umwagiliaji kitaposaidia kwenye ukuaji wa viwanda, lazima mtoe mantiki, kwa sababu hamna Taifa duniani ambalo limetegemea kilimo tu peke yake likaendelea, ila kunakuwepo na viwanda hususan vidogo vidogo ambavyo vinachangia katika masuala ya kilimo ndiyo vinakua. Nadhani tunaweza tukawekeza katika sekta za viwanda vidogo vidogo hususan tukaongeza ajira ili Wananchi waweze kufikia

malengo ambayo tunahitaji. Sasa twende tukizingatia katika kilimo ambacho hatuhusiani na umwagiliaji kitakuwa kwenye Idara gani na kitasimamiwa na nani. Sheria inasema kutakuwa na Afisa Umwagiliaji hususan wa Wilaya, kutakuwa na Afisa Kilimo wa Wilaya, kutakuwa na Mhandisi wa Maji wa Wilaya, *it is too contradicting.* Sasa kilimo kisichokua, kinachotegemea msimu wa mvua hususan kama kule kwetu Momba, kitakuwa chini ya nani na nani atakayekisaidia ili kiweze kufikia malengo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tupate majibu. Vilevile kabla hatujakwenda kwenye kilimo ambacho kinahusu umwagiliaji, tuelezwe tunawahakikishiaje wakulima wetu soko la uhakika la mazao watakayolima, tunawahakikishiaje pembejeo kwa maana ya mbolea za ruzuku, kwa maana ya madawa, pamoja na mbegu? Tunawahakikishiaje maana tunaweza kutengeneza mifumo ambayo haina kitu? Mimi kama mimi kama ingekuwa ni hoja yangu ningeliunga mkono na ningelitaka Bunge, bora tupitishe Tume itakayosimamia masuala ya maji, Watanzania wote wapate maji safi na salama, tutengeneze mifumo ya maji nchi nzima halafu tuje awamu ya pili ya kilimo; hilo linawezekana. Tukienda katika mfumo huu, haki ya Mungu tutarudi tena hapa miaka mitano *story* ni zile zile, miaka mitatu inayokuja bado tutabaki na kitu kile kile, kwa sababu watu wanaoongoza ni wale wale, tunawajua uwezo wao, tunaufahamu na tunajua kabisa kwamba hizi ni *story* na hawawezi kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuambiwe kwamba, bado kilimo hiki tunachoendelea nacho msimu

huu, sasa tunakwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji, asilimia 80 ya Wakulima wa Tanzania bado wanatumia majembe ya mikono hatutumii matrekta kama yalivyo. Kwa hiyo, tunategemea kilimo cha umwagiliaji kitakuja na matrekta; tuelezane ikiwa tu mikopo ya matrekta machache ambayo yalikuwa yametolewa na SUMA JKT katika kipindi kilichopita wamepata watu wachache na matreka yenyewe mpaka sasa hivi hata haieleweki historia yake sijui yalifia wapi! Kwa hiyo, tunataka tuoanishe, lazima Wizara itupe ufafanuzi wa kutosha; Sheria imejaribu sana kuainisha mambo mengi, lakini mambo mengi yanakinzana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sasa tuweke vizuri ili tuweze kujua ni mambo gani tutawasaidia Watanzania wetu. Kwa hiyo, tusijadili tu kilimo cha umwagiliaji wakati asilimia 90 ya Watanzania wanategemea kilimo cha msimu wa mvua bado wako chini na ni wakulima wa kilimo cha kawaida cha majembe ya mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, niseme tu kwamba, tunahitaji majibu kabla na baadaye nitatoa hoja kama itashindikana tuiondoe kabisa hoja ili tuweze kujadil. Tuwape muda Wizara wakajipange waje na hoja kwa sababu imekaa tu kiholela, hata ukiangalia kama kuna watu fulani wana-*push* ili waje kupata fedha za umwagiliaji na miradi ambayo haijakamilika. Baada ya kusema maneno hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Silinde. Mheshimiwa Leticia Nyerere; kuna dakika kumi zinakufaa?

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, siwezi kuchangia bila ya kumpongeza Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mwanamke ambaye nimejifunza mengi kutoka kwake. *She is our role model*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Muswada. Pamoja na kwamba, Muswada huu umechelewa, lakini endapo sheria itatekelezwa ipasavyo, kwa kweli Taifa letu litakuwa limejikomboa. Nasema hivyo kwa sababu Serikali yetu imekuwa na matatizo ya chakula kila mwaka. Watanzania tumekuwa na tatizo la njaa kila mwaka na Serikali yetu imekuwa ikilazimika kuwa ombaomba kutafuta chakula kwa wafadhili, lakini endapo sheria hii itapitishwa, nina uhakika matatizo haya yataondoka kabisa na nchi yetu itajenga heshima yake na kuachana na tabia ya ombaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ku-*introduce irrigation system* peke yake bila ya kuwa na *coordination* haiwezi ku-*solve* matatizo yetu Watanzania. Wizara ya Kilimo itaweka msisitizo katika zoezi la kilimo cha umwagiliaji, lakini kama hai-*coordinate* na Tume au Wizara ya Ardhi au Mazingira, kwa kweli zoezi hili litakuwa gumu sana. Unaweza ukahamasisha kilimo cha umwagiliaji lakini ukaambiwa umwagiliaji kandokando ya mto ni uharibifu wa mazingira kama hamtafanya *coordination* au unahamasisha kilimo cha umwagiliaji au KILIMO KWANZA bila ya ku-*coordinate* na Wizara ya Ardhi, unaanza kuhamasisha KILIMO KWANZA kumbe hakuna ardhi. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na *coordination* katika utendaji wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu ni muhimu sana katika *irrigation system* na hoja hii alii-*support* mwanangu, Naibu Waziri Malima, kwa kusema kwamba, Wananchi wa Kwimba wanafanya umwagiliaji wa kienyeji. Kwa hiyo, ni kweli kabisa naungana naye, wanahitaji miundombinu; na ningependa kupendekeza zoezi la kwanza lianzie Kwimba na Mheshimiwa Malima, mwanangu, ndiyo aongoze hilo zoezi kufuatilia na kuhakikisha kuwa, Wananchi wa Kwimba, wanawekewa miundombinu inayofaa ili waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia miundombinu ya kisasa na hatimaye kuwa na ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, si suala la Kwimba tu, suala la njaa limekuwa ni la Tanzania nzima na endapo tungelibaini hilo kama Taifa, tusingekuwa na matatizo ya njaa ambayo yanatukumba kila mwaka. Nashangaa Serikali ilikuwa wapi, ukizingatia kwamba kiuchumi ukitaka ku-*improve* uchumi wa nchi, wekeza kwa Wananchi walio wengi. Sisi Wananchi walio wengi ni wakulima, lakini tulishindwa kulielewa hilo kwamba ili tuwakomboe Watanzania kiuchumi, tulitakiwa tuwekeze kwenye maeneo ya wakulima. Hata hivyo, nashukuru kwamba, Serikali imeliona hilo pamoja na kwamba *it is too late,* lakini ni matumaini yangu kwamba, sheria hii itakapotungwa itawasaidia na kuwanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mjadala leo jioni wa Muswada huu wa Sheria ya Umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii, kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 kamili jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka tulifikia hatua ya majadiliano na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wale walioomba kuchangia ndio wanafika. Kwa hiyo, nitatazama, walioko hapa ndio ambao nitawapa nafasi na wengine watafuatia kadri tunavyoendelea.

Naomba tuanze na Mheshimiwa Jitu Soni na wanaofuata nitawataja baadaye. Mheshimiwa Jitu Soni, dakika kumi na tano.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kuja na Muswada huu ingawa umechelewa sana, ulitakiwa uwepo kwa muda mrefu. Ninaamini kwamba Muswada huu ndiyo utakuwa moja katika sehemu ambazo tutamkomboa mkulima wa kawaida na pia kuongeza tija katika sekta hii ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Kwanza kabisa, tukizingatia Idara hii ya Umwagiliaji ilikuwa inatupwatupwa; mara ilikuwa Wizara ya Kilimo kama Idara ndogo na baadaye ikapelekwa Wizara ya Maji, ikawa ina-*hang,* lakini baada ya hii Sheria kupitishwa itakuwa inatambulika rasmi na itakuwa ina Tume ambayo itaisimamia masuala yote ya umwagiliaji. Hata kama itahama kwenye Wizara katika siku za usoni, lakini Tume bado itaendelea kufanya kazi, na kuboresha umwagiliaji ndani ya nchi hii.

Lengo na nia ya Sheria hii ni kuhakikisha kuwa kuanzia ngazi ya chini kabisa kwa wale wamwagiliaji *(irrigators)* hadi kufikia ngazi ya Taifa wote wanakuwa wanaratibiwa, na yale mambo yote muhimu kwa upande wa umwagiliaji yanafanyiwa kazi.

Pia naipongeza Serikali kwa kuunda Tume hii ambayo ina watu kutoka kila Wizara muhimu katika Sekta hii ya Umwagiliaji na Kilimo. Kwa hiyo, kutakuwa na *coordination* baina ya Wizara zote husika na wawakilishi kutoka kwa wale wamwagiliaji *(irrigators)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kuanzisha *Reginal Managers,* wale ndiyo itakuwa kazi yao kubwa. Mimi napongeza kwasababu, kwa mfano kwetu Babati tulishindwa kupata miradi mikubwa ya umwagiliaji kwa sababu hatukuwa na wataalamu wa ngazi ya Mkoa. Labda Mkoa ulikuwa hauoni umuhimu wa kuwa nao. Hivyo hivyo katika Wilaya, hawa wataalamu wa umwagiliaji utakuta ana *desk* dogo tu, yuko chini ya Mkuu wa Idara ya Kilimo, wakati ule ikiwa ni Kilimo na Mifugo. Sasa hivi yeye

atahusika moja kwa moja na hapa Sheria imependekeza awe Mkuu wa Idara ndani ya kila Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maeneo yale ya Mjini ambapo wenzetu wengine wanachangia kuwa hawatakiwi, ni muhimu sana. Kila Halmashauri hata zile za Mjini, kwa kuwa umwagiliaji hata mjini upo, na umwagiliaji siyo ule wa kutumia mito mikubwa na mashamba makubwa, unaweza ukawa na eneo dogo, hata *green house* ndani ya Miji ukamwagilia na ukapata manufaa makubwa na kuweza kuzalisha kutokana na eneo dogo kwa tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muhimu kuliko yote, Muswada huu utasaidia pia namna ya kupata uwezo wa Kisheria. Tume hiyo inaweza kuingia mikataba mbalimbali, na namna ya kuboresha na kuhakikisha kuwa wanawasaidia wale *irrigators,* yaani wale wakulima wa kilimo cha umwagiliaji namna wanavyoweza kupata misaada mbalimbali ya kiufundi, yaani *technical support,* lakini pia na kuwaunganisha katika *institutions* ili waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo mwanzoni niliona wenzangu wanachangia kwamba itapokonya madaraka ya Halmashauri siyo kweli! Kazi ya *Reginal Manager* ambaye ni mtaalamu, yaani engineer wa umwagiliaji, kazi yake itakuwa ni kumshauri yule mtaalamu ambaye tumependekeza kwamba kila Wilaya iwe na Mkuu wa Idara kwa upande wa umwagiliaji kumshauri katika mambo mbalimbali, kuangalia maeneo mapya ya umwagiliaji, fursa

mbalimbali za umwagiliaji zilizopo na *technical support* yote, lakini pia kuwasaidia.

Wengine walihoji kwamba atakuwa na Bodi ya Tenda; yeye atakuwa anasaidia kuandaa *documents* za tenda ili zisikosewe ili zile kazi za tenda zinapofanyika ziwe kwa viwango vinavyotakiwa kitaalamu na upande wa *engineering.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Sheria hii imeletwa na nitaomba Wabunge wote tuiunge mkono na tutaona manufaa yake. Kutakuwa na manufaa makubwa na itairuhusu pia kama ilivyo *Tanroads* katika ujenzi, watakuwa na *National Irrigations Agency* ambao wao wataangalia fursa mbalimbali. Leo hii tuna 1.5% tu ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji, linalotumika. Lakini sasa itakuwa ni jukumu la hiyo Tume kuhakikisha kuwa maeneo yote ambayo fursa zipo, waangalie namna ya kuziboresha, kuishauri Serikali, kumshauri Waziri na Serikali na kutushauri sisi Wabunge ili tuweze kupitisha bajeti na pia kuangalia namna ya kutafuta fursa mbalimbali ili haya maeneo yaongozeke angalau ndani ya miaka hii miwili, mpaka mwaka 2015 tuweze kufikia hata hiyo 25% ya hilo eneo ambalo tunaweza kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna maeneo mbalimbali ambapo katika Sheria ukiangalia tafsiri ya Kiswahili bado hapo ningeomba Serikali iangalie namna ya kuboresha kwa sababu kwenye tafsiri ndiyo mahali ambapo panaleta mgongano.

Ukisoma kwa Kiingereza imekaa vizuri, lakini ukisoma kwa Kiswahili, ndiyo maana wachangiaji wengine walioanza kuchangia walikuwa wanachangia kwa kutokuelewa vizuri, kwasababu tafsiri ile haijakaa vizuri. Kuna maeneo mbalimbali ambapo Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Msolla imepitia na mimi ni Mjumbe katika Kamati hiyo, tumepitia maeneo yote, asilimia kubwa tunaamini kwamba hii Sheria imekaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine ambayo tutapata tukishapitisha Sheria hii ni ile *coordination* baina ya Wizara mbalimbali.

Leo hii ingekuwa bado ipo chini ya Wizara ya Kilimo, watakapotaka mawasiliano na Wizara ya Maji au Vyuo mbalimbali ambavyo vinafundisha mambo ya umwagiliaji, bado ingekuwa ni ngumu kuwakutanisha wote kwa pamoja bila kuwa na chombo cha Kisheria. Hii itaweza kuwakutanisha na tutakuwa na maoni mbalimbali ya kitaalamu ambapo Sheria hii itakuwa inaweza kufanya kazi vizuri na pia itawasaidia wakulima ambao wanatumia umwagiliaji kuwaunganisha na kuhakikisha kwamba wanasajiliwa kisheria, maeneo yao yanajulikana, lakini pia waweze kufundishwa namna ya kutumia maji yaliyopo waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hiyo pia sheria hii italinda maeneo mbalimbali ya umwagiliaji ambayo leo yamegeuzwa kuwa makazi, yamegeuzwa kuwa maeneo ya viwanda, na mengine kuwa maeneo ya hifadhi mbalimbali. Hii Sheria italinda haya maeneo lakini pia

ningeshawishi Wabunge wenzangu wote kuwa, tujitahidi kuiomba Serikali na kuishinikiza ilete haraka Sheria ya Kulinda Ardhi za Kilimo.

Leo maeneo mengi ya kilimo yamegeuzwa kuwa maeneo ya makazi na viwanda. Yale tunaweza tukayafanya katika maeneo ambayo hayafai kwa kilimo au umwagiliji na tukifanya hivyo, huko mbele ya safari tutakuwa na uhakika wa kupata chakula cha kujitosheleza.

Fursa zilizopo Tanzania, sisi tunaweza kuwa moja katika nchi ambazo zinajitosheleza kwa chakula cha kila aina, lakini mbali na hilo, pia tukaweza kupeleka chakula katika nchi za Afrika na duniani kote, na tutakuwa na ziada . Hilo linaweza likanyanyua uchumi wetu, lakini kama tutakuwa tunazalisha vizuri, basi fursa nyingine kama viwanda vya kusindika mazao yetu, viwanda na ajira vitaendelea kuongezeka. Lakini kama hatuna ziada ya chakula, hata hivyo viwanda vitakosa malighafi.

Kwa mfano, leo asilimia kubwa ya ngano tunayokula inatoka nje ya nchi na asilimia kubwa ya sukari na nini, vinatoka nje ya nchi. Haya yote tutaweza kuondokana nayo kama hii Sheria itakuwa imepitishwa. Kama sheria hii itasimamiwa vizuri, nina uhakika uzalishaji utaongezeka maradufu na mkulima atanufaika moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima akinufaika ambaye ni 80% ya Watanzania, uchumi wa nchi pia utabadilika na yale maeneo yote ambayo yanafaa kwa umwagiliaji yatakuwa yanaendelea kuboreshwa. La muhimu, naomba

kuikumbusha Serikali kwamba mbali na hii Sheria kupitishwa, Kanuni zije mara moja. Kanuni zake ziendelee kuandaliwa ili Sheria itakapopitishwa, Kanuni pia ziwe tayari ili ziweze kufanya kazi mara moja ili wote tuendelee kunufaika. Kanuni zisisubiri muda mrefu baada ya hii Sheria kupitishwa kama ilivyo katika maeneo mengine.

Hapo hapo, katika mambo mbalimbali, yule mtaalamu ambaye tumesema kwamba waajiri, wale *Reginal Managers,* tuangalie sifa zake. Sifa ziendane na masuala ya umwagiliaji, awe ni mtaalamu kweli kweli. Lakini pia awezeshwe vizuri, tuhakikishe kuwa yule ambaye tunapendekeza kwenye ngazi ya Wilaya, yule mtaalamu wa umwagiliaji na yeye pia ofisi yake iwezeshwe ili aweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa hiyo ninaamini kuwa Sheria hii ikipita tutakuwa tuna mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninaomba Wabunge wenzangu wote tuipitishe ili tunufaike katika Sekta ya Kilimo na Umwagiliaji. Ahsanteni sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hoja iko mbele ya Bunge lako Tukufu, Muswada wa Sheria unaozungumzia Sheria ya

Umwagiliaji wa mwaka 2013; kama walivyotangulia Wabunge wengine kusema, kwamba ni kweli hii Sheria imechelewa kufika, ilikuwa mara baada ya Serikali kuanza mpango wake wa Kilimo Kwanza, tulitarajia hii Sheria ingekuwepo mapema ili iende sambamba na hii Sera ya Kilimo Kwanza. Lakini nasema bado hatujachelewa, bado tunao muda wa kutosha kuweza kufanya vizuri katika eneo hili. Kwani inaonekana kabisa kwamba kilimo chetu kwa muda mrefu kilikuwa kinategemea mvua zaidi, lakini tumeona tumekwama katika eneo la kilimo kwa kukosa uwezo wa kuweza kuhifadhi maji katika kuendeleza kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *litres* kwa *litres* zinamwagika kwenda katika Bahari ya Hindi ambazo zingesaidia kulima wakati wote wa masika na wakati wa kiangazi. Lakini kutegemea mvua tu kumetufanya sisi hata wakulima wetu sasa wakate tamaa na kuona kilimo hakina tija na kutafuta njia nyingine za kujipatia mapato. Zaidi ya 80% ya Watanzania huwa wanajishughulisha na kilimo huko vijijini, lakini tulishindwa kuwatengenezea mazingira mazuri ili kilimo hicho kiweze kuwaletea tija na maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linategemea zaidi kilimo. Kama tunavyosema Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa hili, lakini kusema ukweli ilifika mahali mtu hatamani tena kuwa mkulima. Lakini ni vyema pia Sheria hii isijikite tu kwa wakulima wakubwa, ifikirie kuwa ni vyema Sheria hii irudi kwa wakulima wadogo, kwani tunategemea hii sekta ya wakulima wadogo wadogo ndiyo inayowapatia tija Watanzania na kuongeza kipato katika Taifa letu. Kwa hiyo,

ni vyema tujielekeze zaidi kwa wakulima wadogo wadogo ambao wanaweza kusaidia kukuza uchumi wa maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nizungumzie suala la uharibifu wa mazingira. Maji ambayo tutafanyia *irrigation* yanategemea vyanzo vyetu vya maji katika maeneo mengi ya nchi yetu, lakini hali halisi tuliyonayo hivi sasa, vyanzo vingi vimeharibika. Vimeharibika kwa sababu ya tabia nchi, lakini pia tabia nchi nayo inasababishwa na utaratibu wetu wa kutumia vibaya rasilimali ya maji tuliyokuwa nayo. Mathalan kule kwetu katika Mikoa ya Kusini, baada ya kuona maeneo ya Kaskazini yote yameharibika na kuwa jangwa, Serikali ikatoa maamuzi kuwa wafugaji wote wahamishie mifugo yao katika Mikoa ya Lindi na Mtwara; nako tulikuwa tunajivunia kuwa maeneo ya Kusini ni maeneo yenye ardhi nzuri, yenye rutuba, kwasababu tulikuwa tunapata mvua katika kipindi chote cha mwaka. Lakini hali inavyokuja, sasa tunatarajia na sisi kukabiliwa na jangwa katika maeneo hayo.

Hivyo, pamoja na umwagiliaji, ni lazima tuzingatie kwamba vyanzo vyetu vya maji ambavyo tutatumia katika *irrigation* bado viko salama? Hivyo Sheria hii nayo ije ikizingatia hilo kuwa pamoja na kuhitaji umwagiliaji, lakini pia suala zima la uhifadhi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu nayo pia yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kama tulivyosema katika Mikoa yetu ya Lindi na Mtwara wafugaji wengi kutoka Ihefu kule Mbeya na maeneo mengine ya Kaskazini yamekuja

katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, leo vyanzo vingi vya maji katika maeneo yale vinaharibika, na tulitegemea kwamba Wizara ya Mifugo ingekuja na Sera maalum kwa Wafugaji wapya ambao wanahamia katika maeneo yale wafuge katika utaratibu wa kisasa utakaotunza na kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kizazi kijacho, lakini imekuwa ni kinyume, kiasi kwamba tunakatishwa tamaa na tunakuwa na hofu.

Sasa huenda hata katika maeneo ambako tunasema ni maeneo mazuri, huenda pia kukawa na hali ambayo inaweza kufanya lile tegemeo la Watanzania kuwa kuna eneo ambalo limebakia kwa ajili ya kilimo bora na ufugaji nalo pia likaharibika. Hicho ni kitu cha kuzingatia, pia suala la vyanzo vya maji nalo pia ni muhimu kuzingatia ili tuone hali gani ya kimaendeleo katika maeneo ya maendeleo.

Lingine ninapenda kuzungumzia suala la *SAGCOT.* Inaonekana kwamba mpango huu utajikita katika mpango mzima wa *SAGCOT,* lakini kule tulikuwa na mpango wa *Southern Corridor* ilikuwa inaitwa *Mtwara Corridor* katika maeneo matano, sita ambayo yalikuwa yanashughulikiwa; ni pamoja na maeneo ya kilimo katika sekta ya kilimo. Kulikuwa na miundombinu, lakini pia kulikuwa na eneo la kilimo.

Katika mabonde ya Kitere kule Mtwara, maeneo ya Lukuledi, Rufiji, ni maeneo ambayo tayari hayajaonesha kwamba tayari Serikali ina nia thabiti ya kutaka kuyafanya maeneo yale ndiyo maeneo ya *irrigation* area kwa ajili ya

maendeleo ya Mikoa ya Kusini maeneo ambayo yanaonekana yako nyuma kimaendeleo sisi tulistaajabu.

Kwa nini kama eneo lile tayari ni zuri lina mabonde mazuri ya kutosha, kwa nini huu mpango wa *SAGCOT* bado haujaja katika maeneo ya Lindi na Mtwara? Hivyo Sheria hii iangalie uwezekano wa maeneo yote ambayo yanafikika kwa ajili ya kilimo, kilimo cha *irrigation* basi kizingatie maeneo ambayo tayari ni mazuri kama yale mabonde ambayo yaliainishwa katika mpango mzima wa Mtwara *Corridor* ambayo sidhani kama Mheshimiwa Waziri anajua kama ipo au vipi.

Lingine ni suala la Kilimo Kwanza. Kama nilivyosema hapo mwanzo kuwa Kilimo Kwanza kingezingatia pia *irrigation* ambayo ingekuwa ipo katika maeneo mbalimbali, lakini ni miradi ya *irrigation* ambayo ipo mingi ambayo tayari inaonekana kuwa ilitolewa pesa, miradi ile haina *value for money,* miradi yote inaonekana kuwa haipo, mabilioni ya pesa yalitumika leo na mradi mmoja kule kwangu Lindi katika eneo la Gongo. Ninapozungumzia suala la umwagiliaji siyo suala la kipindi kifupi cha msimu cha kutegemea mvua, umwagiliaji tunahitaji kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini miradi mingi ya umwagiliaji inahusisha wakati ule tu wa msimu wa mvua. Mvua ikiisha, basi hata ile *irrigation* ambayo tunatarajia inakuwa haipo. Kuna maeneo ya Makangaga kule, kuna maeneo ya Kitere ambako Serikali ili *invest amount* kubwa ya fedha kwa ajili ya miradi ile, lakini miradi ile bado

haioneshi kwamba inaweza kuleta tija pamoja na pesa nyingi za Watanzania kutumika katika kuikamilisha ile miradi.

Ni lazima tuwe na Sheria ambazo zitaonyesha kuwa kama mradi ni kwenda katika eneo na haujaleta mafanikio yoyote: Je, Sheria inasemaje? Tutafanyaje katika eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naishauri hii *commission* ambayo tayari inaundwa izingatie kupitia miradi yote ya awali, miradi ambayo ipo, inaonekana kwamba miradi hiyo tayari haioneshi tija kwa Watanzania, inaonekana kwamba hata hiyo mipya ambayo itakuja kwa utaratibu huu, bado haiwezi kutuletea tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie kanuni. Tuna uzoefu hapa tunapitisha Miswada inakuwa sheria baadaye, sheria zile zinachukua mpaka miaka mitano hadi sita, mpaka Bunge linamalizika lakini bado Kanuni zitacheleweshwa kuletwa. Hivyo kuwepo kwa sheria ni jambo lingine lakini pia kuwepo kwa kanuni katika maana ya tayari kuanza kwa utekelezaji wa sheria ile, nalo pia ni suala lingine.

Hivyo, naishauri Wizara iharakishe haraka iwezekanavyo suala zima la kutengeneza kanuni ili iende sambamba na sheria ambayo tunaianzisha ili Bunge hili tutakapomaliza sisi kama Wabunge tuone fahari sasa, tuieleze nchi kwamba katika Bunge hili la Kumi liwe ni Bunge ambalo lilitengeneza sheria ya *irrigation*, ikatengeneza kanuni na tayari ipo katika *function.* Wananchi wanafurahia

matunda ya Bunge lao katika utekelezaji wa sheria hii ambayo tumeitengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Barwany. Kama nilivyosema sasa anafuatia Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa David Kafulila atafuatia.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Wanaokatiza katiza mbele ya Mheshimiwa Cecilia nawaomba wazingatie kanuni.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika sheria hii ya Taifa ya Umwagiliaji. Kwanza naunga mkono hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba ninapinga Muswada huu wa Sheria kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika madhumuni na sababu ya kuanzisha sheria hii, Waziri ameeleza hapa katika kitabu naomba kunukuu, kwamba “sheria hii inalenga kuondoa changamoto zilizojitokeza katika Sekta ya Kilimo cha Umwagiliaji.” Changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa mfumo wa sheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji,

changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa mfumo wa sheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, panapokuwepo na changamoto yoyote katika jambo lolote, sheria siyo suluhisho la kuondoa hizo changamoto.

Mimi nilifikiri ni vyema uongeze fedha, uongeze rasilimali watu katika chombo kilichokuwepo katika umwagiliaji kuliko kuanzisha Tume hii ya Umwagiliaji ambayo itatumia fedha. Itahitaji fedha kuajiri, itahitaji fedha kuendesha shughuli zake, itahitaji fedha nyingi tu za kukamilisha mfumo huu, lakini kwanini Waziri hakuona umuhimu wa kuongeza fedha katika hiyo nia iliyopo sasa hivi ambayo *structure* yake ipo katika *Local Government*?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kunukuu changamoto nyingine, anasema: "kutekelezwa na kuhujumiwa kwa miundombinu ya umwagiliaji." Kama miundombinu ya umwagiliaji imehujumiwa, hivi suluhisho ni sheria au suluhisho ni kuwa na watu ambao watasimamia kuwa na rasilimali watu wa kutosha wa kuzimamia miundombinu, kushirikiana na mamlaka ya Serikali za Mitaa kuimarisha miundombinu hii? Kuwa na fedha pale ambapo uharibifu unatokea katika miundombinu kuweza kuimarisha miundombinu hii. Je, Wizara imeona suluhisho ni sheria tu au suluhisho ni vitu vingine? Hiyo ni sababu ambayo naendelea kuupinga Muswada huu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine imeonesha ni udhaifu wa mfumo wa Kitaasisi usiokidhi kasi ya kuendelea kupanuka kwa shughuli za umwagiliaji. Kama kuna udhaifu katika mfumo huu ule uliopo umejitathmini, kuna tathmini iliyofanyika kuhusu hiyo nia? *National Irrigation Agency* imefanyia tathmini kujua upungufu wake ni upi? Imetengewa fedha za kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti, mara kwa mara wanatuambia kasungura kadogo, fedha hakuna. Leo mmepata wapi fedha ya kuanzisha hiki chombo ambacho kitahitaji fedha?

Kwanini fedha za kuanzisha hiki chombo isiende kwenye hiyo nia, ikaimarishwa, ikajengewa watumishi wakaongezwa, wakaajiri watu kwenye *Local Government* ambao watakwenda kuwa Maafisa Umwagiliaji kwenye Kata na Vijiji kushirikiana na *Local Government* ili kuondoa hizi changamoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini anaendelea kwamba changamoto nyingine ni uelewa mdogo wa wananchi unaopelekea kushindwa kutambua na kutekeleza kikamilifu wajibu wao katika kumiliki na kuchangia ukarabati wa miundombinu. Kama uelewa wa wananchi ni mdogo: Je, suluhisho ni kuwa na sheria au suluhisho ni kutoa elimu kwa wananchi kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa iliyopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema kwamba madhumuni na sababu ya kuanzisha sheria hii, naona bado siyo muafaka, tungeendelea kuimarisha

vyombo vilivyopo, kuimarisha mpaka kwenye *Local Government* zetu kuona kwamba ni namna gani inaleta ufanisi unaotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tu katika Muswada huu Kifungu cha Tisa inaeleza suala la uteuzi wa Wakurugenzi; uteuzi huo unasema kutakuwa na Wakurugenzi mbalimbali, lakini hata haija-*specify* kwamba ni Wakurugenzi wangapi? Ikiamua kuajiri Wakurugenzi 20, wote watahitaji ma-VX, ni gharama; wote wanahitaji mishahara, ni gharama; ndiyo maana nasema Muswada huu ni bora tungeendelea tusiwe na hiki chombo tuendelee kuwa na hiyo nia na kuimarisha inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naendelea kuelezea kwenye kifungu cha 13 Idara za Umwagiliaji za Wilaya, inaeleza jinsi ambavyo huyu Mhandisi wa Wilaya atafanya kazi, lakini haijaonesha pia namna gani moja kwa moja Serikali za Mitaa inashirikishwa. Kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani imeelezea kwamba Serikali inaelekeza ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kupeleka kwa Serikali za Mitaa ambako kuna wananchi. Lakini tukija kwenye vitendo, siyo uhalisia.

Kule ndiyo kuna wananchi, leo unakitenga hiki chombo kisihusiane moja kwa moja na Halmashauri zetu za Wilaya na kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa, inaelezea namna gani Mabaraza ya Madiwani ndiyo yenye nguvu na yenye mamlaka katika Halmashauri husika katika masuala yote. Sasa Baraza la Madiwani hapa halionekani, ndiyo hao hao wanatakiwa wasimamie fedha, lakini hata namna

ambavyo fedha zitakuja kama *Accounting Officer* wa Halmashauri ni Wakurugenzi wetu: Je, hizi fedha za kuanzisha hizi chombo zinapitia wapi? Inapitia kwenye hicho chombo, inajitegemea na Wakurugenzi wa Halmashauri umewaacha wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bado tunaona kwamba siyo wakati muafaka kuleta hii sheria, mpaka ile nia ingeweza kutathminiwa, ingeweza kuboreshwa, ingetengewa fedha za kutosha, ingeweza kujitegemea na kuwa na rasilimali watu wa kutosha mpaka kwenye vijiji vyetu wafanye kazi inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kifungu cha 14 inaeleza uteuzi wa Wakaguzi wa Umwagiliaji, kwamba Tume itaweza kuteua wakaguzi wa umwagiliaji. Ukija kwenye tafsiri ya Muswada, kazi za Mkaguzi wa Umwagiliaji ni kukagua kazi zote zilizofanywa, sasa Mkurugenzi ndiyo atakayeteua hao Wakaguzi wa Umwagilaji; hapo hapo inasema kwamba atawajibika kwa Mkurugenzi. Uwazi uko wapi? Uwajibikaji utakuwa wapi? Mimi nikuteue uje unikague kazi yangu ninayoifanya, hakutakuwa na uwajibikaji. Huu ni baadhi ya upungufu uliopo katika kipengele hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda sehemu ya tatu, Kifungu cha 17 inaeleza suala la Tangazo la maeneo ya mgawanyo wa ardhi. Tumeshuhudia nchi hii ina matatizo kibao ya ardhi, kila mahali ni kelele za ardhi. Katika kifungu cha 18 inaelezea suala la Waziri mwenye dhamana ya ardhi kwa kushirikiana na Waziri husika kwa maana ya Kilimo

na Umwagiliaji watamshauri Rais kutumia Sheria Na. 4 ya mwaka 1999 ya ardhi ya ku-*revoke* maeneo yale ambayo wanaweza kuona kwamba yanafaa katika umwagiliaji. Lakini tumeona matatizo haya ya ku-*revoke* kuna *double standard* nyingi sana, sasa leo mnaona kwamba hiki kitu ni kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunapinga kwamba Muswada huu siyo wakati muafaka, tuone kwamba tunaimarisha, tunaondoa migogoro ya ardhi iliyopo, hata baadaye tukija kusema suala la kutaka maeneo kwa ajili ya umwagiliaji tuwe kwanza salama katika suala zima la kuondoa migogoro ya ardhi ndipo tuweze kuleta hiki kitu kipya cha ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Muswada huu pia haujazungumzia suala lolote la utunzaji wa vyanzo vya maji. Unaweza ukawa na miundombinu ya maji wakati huna maji? Ni lazima kuwepo na mkakati wa kuona ni namna gani unatunza vyanzo vya maji vilivyopo. Huwezi ukategemea maji ya mvua kila siku na mvua yenyewe haitabiriki. Kwa hiyo, katika Muswada huu hawajaonesha hilo suala la utunzaji wa vyanzo vya maji unasimamiwa vipi, ukoje, ni namna gani vinaweza kulindwa visiingiliwe na wananchi, visiharibiwe. Kwa hiyo, huu ni baadhi ya upungufu uliopo katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani. Tunaona kwamba siyo wakati muafaka sasa, bado tuimarishe ile nia tuliyonayo, Wakala wa Umwagiliaji katika

Wizara husika, iimarishwe, ipatiwe fedha, iongezewe rasilimali watu mpaka kwenye Serikali za Mitaa tuone ufanisi wake ndiyo baadaye tuanze kuona ufanisi wake ukoje? Ni mzuri au siyo mzuri? Ndiyo tufikirie vyombo vingine vya kuanzisha, kuliko kuanzisha vyombo ambavyo vitaendelea kutugharimu fedha, tutaendelea kuona kwamba hatupati ufanisi lakini tunaona tu dhana na suluhisho ni kuwa na sheria; ni kuwa na vyombo kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa David Kafulila atafuatiwa na Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafsi ya kuchangia Muswada huu ambao unahusu Umwagiliaji, katika nchi ambayo ina fursa nyingi kabisa kuliko nchi nyingi katika dunia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ninakushukuru kwa sababu mara kadhaa nimepata kuzungumza hapa ndani ya Bunge kuelezea ni kwa namna gani ambavyo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu Taifa ambalo katika hali ya kawaida tusingezungumza masuala ya kuagiza sukari nje, tusingezungumza masuala ya kuagiza mchele nje, tusingezungumza njaa wala tusingekuwa na Serikali ambayo inakwenda kuweka mageti kwenye mipaka kuzuia chakula kisiende nje ya nchi, na badala yake tungekuwa na Serikali ambayo inawafanya wananchi wazalishe zaidi ili kusudi badala ya kulipa posho za Polisi kuweka mageti

kwenye mipaka tungekuwa tunauza mazao yale tunapata pesa za kigeni, tunajenga uchumi, tunakuza maisha ya wakulima.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakushukuru kwa sababu hiyo. Sote tunafahamu kwamba dunia ya leo hauwezi ukazungumza kilimo kwa kutegemea kilimo cha majaliwa ya mvua. Njia pekee ya kujenga kilimo cha uhakika ni lazima muwe na kilimo chenye miundombinu ya kutosha ya umwangiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii imekuja leo, lakini bahati mbaya sana wakati inakuja leo hatujaelezwa ni kwa kiasi gani *structure* iliyokuwepo awali, *agency* iliyokuwepo awali ni kwa kiasi gani ilikuwa haiwezi kutimiza majukumu yake? Leo Tanzania tuna takribani hekta 29,400,000 ambazo zinafaa kwa umwagiliaji. Miaka 50 tangu tupate uhuru maeneo ya umwagiliaji, *scheme* za umwagiliaji ambazo zimetengenezwa nchi nzima ni 360,000. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni kwamba ili tutitimize ujenzi wa *scheme* za umwagiliaji kwa maeneo yote ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia katika nchi hii nzuri, kwa Chama hiki, itakihitaji miaka 3,625 kukamilisha maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili siyo jambo la kuchukulia kwamba ni jambo la kawaida, haiwezekani! Tunahitaji tupate tathmini ya kwanza, kwamba kwa miaka

hii 50 kilimo cha umwagiliaji ni kwanini kilishindikana? Sababu siyo sheria! Kuna zaidi ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza na watu wa *Legal and Human Rights Society* wanasema kwamba tathmini waliyoifanya wao utendaji wa sheria au usimamizi wa sheria mpaka sasa tupo takribani asilimia 37, yaani kwamba sheria tunazo nyingi lakini usimamizi wake! Kwa hiyo, hizi sheria zinakuwepo lakini hazifanyi kazi kwa sababu *system* ime-*paralyze*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kuangalia upya kwamba kikwazo ni zaidi ya sheria. Leo hii tunaunda hii Tume ambayo ndani yake itakuwepo Ofisi ya *AG*, lakini najiuliza mantiki ya kawaida tunasema hii Tume itakuwa huru kwa ajili ya kukopa, kukopwa, na kushtaki na kushtakiwa. Tujiulize swali la kawaida, ikitokea sasa hii Tume inatakiwa iishtaki Serikali na *AG* ni sehemu ya Tume unaishtaki vipi? Kwa hiyo, unatengeneza Tume ambayo unasema kwamba unaipa uhuru lakini wakati huo huo atakayekuwa msumbufu namba moja atakuwa Serikali, na Serikali hii itakuwa inashindikana kushitakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kwamba sioni mantiki ya kuwa na *AG.* Sisemi Werema, maana anaweza akawepo leo, kesho asiwepo yeye, lakini *AG* kwenye *structure* ile sioni mantiki ya yeye kuwemo mle.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza umwagiliaji unazungumza pia vyanzo vya maji ambavyo kimsingi ndiyo

mafuta ya kuendesha umwagiliaji. Ni bahati nzuri kwamba Tanzania imejaliwa sana.

Nilikuwa nasoma takwimu za maji duniani, dunia nzima maji yanayofaa kwa umwagiliaji ni takribani kilomita za ujazo milioni 35. Tanzania peke yake kwa maana ya Ziwa Tanganyika achilia mbali ziwa Victoria, achilia mbali mito mingine, ziwa Tanganyika peke yake ambalo lipo kule Kigoma lina kilomita za ujazo 5,800,000. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba asilimia 17 ya *fresh water* yote duniani ipo ziwa Tanganyika, ipo ndani ya Tanzania lakini bado miaka 50 tunazungumza kilimo cha umwagiliaji kimeshindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza ardhi ya umwagiliaji ipo hekta milioni 29 na tumeshindwa kuzitumia; maji kwa ajili ya kumwagilia Ziwa Tanganyika peke yake linaweza kumwagilia ardhi yote ya Tanzania. Tatizo ni nini? Ni kweli kwamba tatizo ni sheria? Hivi kweli Serikali imefanya *homework* ya kutosha ikagundua kwamba tatizo ni sheria? Mimi sidhani kama tatizo ni sheria! Bado tuna *inefficiency* ya kiwango cha juu sana, tuna udhaifu mkubwa, Serikali ina udhaifu mkubwa katika utendaji wake. Hii ndiyo *critical problem* ambayo iko pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunayoizungumza hapa, tunapitisha sheria, najua mtaipitisha kwa sababu ya wingi wa kura, lakini hata hii sheria yenye upungufu mkubwa, kanuni zake huenda zikachukua zaidi ya miaka mitano. Ushahidi upo, zipo Sheria zimepitishwa zina miaka mitatu, minne tulipitisha sheria hapa za *Telecom* kwamba ziwe

*registered DSE* ndani ya miaka mitatu. Mwaka wa tatu umekwisha mwezi wa Saba, mpaka leo hakuna Kanuni.

Kwa hiyo, haya ni mazaoea, bado Serikali inaendeshwa kwa mazoea. Kazi haifanyiki ya kutosha, ushahidi wa kwamba kazi haifanyiki ya kutosha ni kuangalia tu, huu Muswada umeletwa hapa, Muswada huu upo ndani ya Bunge tangu mwezi wa Sita wakati wa Bunge la Bajeti, lakini leo Serikali wakati inataka kuchangia inaleta *amendment* kurasa saba. Huu Muswada mnaandika upya au ni *amendment* hizi? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaleta *amendment page* saba Muswada ambao Serikali mnao tangu mwezi wa sita hamjaona! Leo Wizara ndiyo inaleta *amendment page* saba. Huyu Mbunge sasa ajiandae saa ngapi? Maana yake hizi *amendments* mmeleta wakati tumo ndani ya Bunge hili, *that is a challenge*. Hapa kuna tatizo la kimsingi, kwamba inawezekana tuna watendaji wengi ambao hawako *serious* na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati vijana wapo nje wanatafuta ajira wanatamani kuajiriwa, lakini bado kuna watu wengi ambao wamepewa ajira hawatimizi majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema tu kwamba katika Muswada huu, moja ya eneo ambalo ni muhimu mlizingatie kama Wizara, moja ni kwamba kanuni zitaje zitakuwa tayari ndani ya muda usiozidi miezi mitatu, ioneshwe kabisa ili kusudi tuweze kuwabana, sheria

isiposema kwamba kanuni zitakuwa tayari ndani ya muda gani? Upo uwezekano tukatunga sheria hapa, tukasubiria kanuni hata miaka mitano. Kwa hiyo, moja ya eneo ambalo ninapenda liongezwe humu ni hiyo kanuni, kwamba ndani ya muda gani kanuni ziwe tayari? Tukubaliane kwamba ndani ya miezi mitatu kanuni ziwe tayari ili kusudi sheria i-*operate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo ningependa kuyazungumzia kama nyongeza, Sheria hii inapaswa iwe *clear*, kwamba ni kwa namna gani tutakuwa na uhakika wa *finance* kwa sababu kwa kadiri ya ufahamu wangu tatizo kubwa la sheria hii au la *irrigation* ni kwa hakuna vyanzo ni kwamba Serikali haitengi fedha ya kutosha kwa ajili ya kuifanya miradi hii itekelezwe. *(Makofi)*

Sasa ni kwa kiasi gani Sheria hii inasema, ni kwa kiasi gani huu Muswada unaoletwa una-*address issue* ya kukosa fedha. Bado ipo kimya, bado ipo kimya na ninashangaa kwa nini Muswada unaoletwa unakuwa kimya kuhusu ni namna gani tutatatua tatizo la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha hiyo miradi na wakati miaka yote Mheshimiwa Waziri unatujibu kwamba tatizo la umwagiliaji ni fedha.

Tunazungumza hapa kwamba kutengeneza skimu moja *I mean* hekta moja kuitengenezea skimu *irrigation scheme* inagharimu kati ya dola elfu moja mia tano mpaka dola elfu tatu mia tano kutegemea na maeneo na kutegemea sekta zingine na kwamba siku zote hii ndiyo tatizo ambalo limefanya miaka hii ipite takribani nusu karne

huku tukipiga *mark time* kwenye kujenga ya umwagiliaji. Sasa ni kwa namna gani huu Muswada una- *address?* Wataalam wako ni kwa namna gani wanakusaidia Muswada ambao una-*address* hiyo kitu kwa *problem?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bado? Nilidhani muda umeniishia kumbe bado ninao. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba ni lazima hii Sheria ioneshe kwamba ni kwa namna gani tutatatua tatizo la upatikanaji wa rasilimali fedha, ni kwa namna gani tutakuwa na *assurance* kwamba rasilimali fedha haitakuwa mgogoro ili kusudi majibu yako yale ya kila kwa siku ya kwamba tatizo ni fedha, tatizo ni fedha tufikie mwisho kwa sababu hiyo *critical problem.* Lakini pia Sheria hii ionyeshe kwamba, kwa mfano, huduma kama ya maji, inaelezwa kiasi gani kwenye Sheria hii ili baadaye tusije kuingia kwenye mgogoro?

Mheshimiwa Naibu Spika, naisema hii kwa sababu kuna mambo mawili. Moja, ukitengeneza mradi mkubwa, kuna kitu wanaita *Environmental Impact Assessment* ambayo ni lazima ifanyike. Lakini pili, ni lazima vile vyanzo vya maji ambavyo vinatoa hiyo huduma ya maji kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji iwe *considered.* Nimetoa mfano

hapa, Ziwa Tanganyika linaweza lika-*service* miradi yote ya maji ndani ya nchi hii kama tuna Serikali ambayo ina uwezo, na kama iko *committed* kufanya kazi. Sasa *arrangement* zake ni kwa kiasi gani zinaonesha kwenye Sheria hii? Bado Sheria ipo kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasisitiza tena kwamba tunahitaji Sheria ambayo inaweza kuondoa utata katika maeneo haya ya kilimo cha umwagiliaji. Zaidi ya hapa tunafahamu kwamba tuna-*engage private sector* kwenye maeneo haya ya *irrigation:* Je, ni kwa kiasi gani sasa tutakuwa na uhakika kwamba hawa wawekezaji ambao tutawaingiza kwenye *irrigation* kama kweli wata-*operate?* Kweli watafanya kazi kulingana na mkataba? Wenzangu wengi wamezungumza kwamba leo hii, hii nchi imeshageuzwa kuwa ndiyo shamba la Bibi, anakuja mtu anachukua ardhi, akishapata hati zote kwa ajili ya kilimo hata umwagiliaji pengine, anaweza akaenda aka-*list* hata kwenye *Toronto Stock Market* au akaenda popote akatafutia mtaji, ule mtaji atautumia ama kwa biashara nyingine na akautumia ama chini ya kiwango au asiutumie kwenye malengo ambayo tulikuwa tumeyakusudia.

Sasa ni kwa namna gani uhusishaji wa sekta binafsi katika miradi hii ya umwagiliaji unakuwa unadhibitiwa kuhakikisha kwamba kile kiasi ambacho *private investor* atapewa kwa ajili ya *irrigation* kweli anapewa na anatekeleza kwa kadiri ambavyo amekubaliwa?

Tumesema hili kwa sababu ni *challenge,* na hii siyo ardhi pekee ya kilimo cha umwagiliaji, hata ardhi nyingine;

na siyo kwenye ardhi pekee, hata kwenye mafuta na *gas.* Wanakuja Wazungu hapa hata viatu hawana, wana-*sign* vitalu wanapata leseni za vitalu wanakwenda Toronto *Stock market* wanachukua fedha. Mtu amekuja na pesa kiduchu, anakuwa *billionear* kwa sababu sisi tunabaki tunashangaa tu. Watanzania tunashangaa tu! Wanatumia mali hizi hizi kupata mikopo mingi. Wanatumia mali hizi kukusanya mitaji, lakini hakuna *capital gain tax,* hakuna uhakika wa kuona kwamba huyu mtu huu mtaji aliupata kutokana na rasilimali yetu tunafaidikaje kwa mtaji huo? Hakuna!

Kwa hiyo, ni vitu ambavyo ilipaswa Wizara ivitafakari kwa kina. Wizara inapaswa itafakari ivione kabla, tusiwe na Serikali ambayo iko nyuma, inakuja baada ya matukio. Tuwe na Serikali ambayo ina-*oversee* ili kusudi matatizo ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu yasiweze kuendelea.

Mimi naamini kwamba lengo la kujenga misingi ya kilimo ni kuwasaidia wakulima maskini. Lakini ni kwa kiasi gani mkulima maskini atahakikishiwa uhakika wa kushiriki kwenye kilimo kwa uhakika katika mazingira ambapo tuna soko huria na *private sector* yenye nguvu bado haijawa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nakushukuru kwa mchango wako. Kama nilivyosema, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Joshua Nassari. Taarifa, Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nataka kumpa tu taarifa mdogo wangu Mheshimiwa Kafulila kuhusu Ziwa Tanganyika. Anazungumzia Ziwa Tanganyika kwamba litumiwe kwa *irrigation* likauke. Lile ziwa ni la nchi tano; Burundi, Rwanda, Congo, Zambia na Tanganyika. Ni watu wengi wanategemea uvuvi. Siyo kwa ajili ya *irrigation* peke yake. Ziwa likikauka, wananchi watapata taabu katika Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Kafulila ajue kwamba siyo kwa ajili ya *irrigation* peke yake, wananchi wanategemea uvuvi katika Ziwa Tanganyika. Nchi tano zinategemea Ziwa Tanganyika! Siyo Tanganyika peke yake. Ajue taarifa hiyo! *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo nzuri Mheshimiwa Keissy. Mheshimiwa Kafulila ameridhika na taarifa hiyo. Mheshimiwa Kafulila kwa dakika moja kwa kifupi sana tafadhali. *(Kicheko)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Keissy, ni kwamba katika Ziwa Tanganyika Mkoa wa Kigoma peke yake unamiliki asilimia 45 ya ziwa lote. Sijazungumza kwako Rukwa. Ukijumlisha na Rukwa, tuna sehemu kubwa zaidi ya Ziwa Tanganyika. Lakini pili, Mheshimiwa Keissy, lile ziwa lipo pale kwa ajili ya kujenga uchumi na haliko pale kwa ajili ya kazi nyingine*. Irrigation* ndiyo ufufuo wa uchumi wa nchi hii kuliko jambo lolote lile kuliko kazi ambazo wewe unazungumza. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, haelewi. Nchi ya Kongo ndiyo inamiliki asilimia 44, Tanganyika tunamiliki... *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari. Mheshimiwa Keissy kaa chini. Mheshimiwa Kessy! Mheshimiwa Nassari, tafadhali. *(Kicheko)*

**MHE. JOSHUA SAMWEL NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa maoni yangu kwa Muswada wa Sheria ya Umwagiliaji ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na kwamba tulibadilisha Kanuni, lakini naomba tu Bunge lako Tukufu na Watanzania wote wajue kwamba nimerudi, nimepona, niko safi na ili ning'ae vizuri, napaswa kufika kwenye moto. Nimepita kwenye moto, nang'aa vizuri kweli! Kwa hiyo, uwezo na ari imeongezeka kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuchangia, nasikitika kwamba katika dakika takribani tano au kumi kabla ya kuchangia nimepokea *schedule of amendment* ambayo imekuwa *moved* na Waziri husika. Mimi ninaamini kwamba Muswada unapokuja ndani ya Bunge, Serikali inakuwa imejiridhisha hata kama siyo kwa asimilia mia moja, angalau kwa asilimia 90 ama 95. Lakini mabadiliko yaliyokuja yapo hapa, ni takribani kurasa saba zilizojaa za lugha ya Kiingereza, lugha ya kisheria. Maana yake ni nini?

Ukiangalia maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwenye kitabu hiki kidogo ni karatasi zilizoandikwa zilizojaa 11. Maana yake maoni ya Kamati peke yake ilikuwa takribani karatasi tano kubwa, halafu mabadiliko yanaletwa na Waziri husika ambaye analeta Muswada ndani ya Bunge wenye kurasa saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijui kwamba nakwenda kuchangia kitu gani? Kwa sababu mimi nimesoma *Bill* na nakwenda kuzungumza kulingana na *Bill* na mabadiliko yanakuja ya kurasa saba. Sasa sijui kama ninachokwenda kuchangia kimeshabadilishwa kwenye *schedule of amendment* au lah! Lakini ni tatizo! Kwa hiyo, inahitaji muda kuipitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza habari ya umwagiliaji, habari ya kilimo, habari ya asilimia 80 ya Watanzania; tunazungumzia maisha ya watu, tunazungumzia chakula cha nchi hii, tunazungumzia uchumi wa Watanzania. Sasa nina wasiwasi kidogo, nafikiri hii peke yake inatosha kujenga hoja kwamba pengine Muswada urudi, Serikali ikajipange, ijitathmini upya halafu pengine uletwe tena baadaye ikiwa imejiridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia kuhusu Muswada wenyewe. Mwaka 1996 ulifanyika Mkutano Mkuu wa Kitaifa ambao ulikuwa na kauli mbiu ifuatayo: Ilikuwa inasema, *towards a shared vision for Local Government Tanzania* yaani kuelekea fungamani kuwa Serikali za Mitaa Tanzania na baada ya Mkutano huu ndipo hapo nafikiri kama Taifa tuliamua kuingia kwenye mfumo

ama kwenye sera ya ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ilikuwa ni hii; ili kwamba mamlaka yarudi kwa wananchi moja kwa moja, Halmashauri ziwe na mamlaka ya kufanya mambo yake kupitia wananchi wake. Sasa leo hii, imekuja *Bill* tunajadili Muswada, na ukiusoma kwa undani kuna mashaka na sintofahamu kubwa sana kwenye Halmashauri zetu. Kuna sitomfahamu kubwa ya wananchi kule vijijini tunakotokea na vile vile kwa wataalam wetu kwenye *Councils* kwa sababu ni kama vile Muswada huu unakwenda kupoka madaraka ya Halmashauri. Ni kama vile Muswada huu unakwenda kuizuia Halmashauri, ni kama vile Muswada huu unakwenda kupingana hata na ile sera ya ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kuja kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiusoma vizuri Muswada huu, nitakwenda haraka sana. Ukiangalia ile misingi ya maboresho ya Serikali za Mitaa maana yake halisi misingi yake ilikuwa, naomba kunukuu: "Moja, ilikuwa ni kuimarisha ushiriki wa moja kwa moja kwa jamii katika kuiendesha Serikali yao na kuchagua Madiwani.

Pili, ilikuwa ni kuweka huduma za jamii chini ya usimamizi wa jamii kupitia Halmashauri zao. Tatu, ilikuwa Halmashauri kuwa na nguvu za kisiasa na maamuzi juu ya mambo yote ndani ya maeneo yao.

Nne, ilikuwa ni kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa fedha. Tano, ilikuwa kujenga utawala unaowajibika kwa

jamii. Saba, ilikuwa kupunguza mwingiliano wa watendaji wa Serikali za Mitaa na kutoka kwa Wizara mama kwa maana ya Serikali Kuu. Lakini vile vile nane, ilikuwa ni kuweka mfumo mpya wa mahusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiusoma vizuri Muswada huu ni kama vile unakwenda kuvunja hii misingi; ni kama vile unakwenda kuchukua Mamlaka ya Serikali za Mitaa; ni kama vile hatuna sababu ya kuendelea kuwa na Halmashauri zetu; ni kama vile hakuna sababu ya kuendelea kuwa Madiwani; ni kama vile hakuna sababu ya kuendelea kuwa na Mbunge kwenye Halmashauri yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya Sera ya Maboresho ya Serikali za Mitaa kufanya Halmashauri ilikuwa ni kuzifanya Halmashauri hizi ziwe huru na zinazojitegemea. Lakini Muswada huu bado unatoa wasiwasi na kuna sintofahamu kubwa. Mimi leo nimezungumza na baadhi ya wataalam kwenye Halmashauri yangu, ni kwamba wana wasiwasi na wana hofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nchi hii siyo Sheria, tatizo la nchi hii siyo Miswada mingi kule kwenye Bunge, tatizo la nchi siyo kuwa na Sera na maandiko mazuri sana, tatizo la nchi hii siyo kutokuwa na semina nzuri tena elekezi zinatumia pesa nyingi; tatizo la nchi hii ni tatizo kubwa la kimfumo na tuna tatizo kubwa la kutokuwa na dhamira njema ya kuwatumikia watu wetu lakini vile vile ile *commitment haipo.* Kwa sababu gani?

Nitatoa mfano rahisi tu. Ndani ya Bunge hili kwa mfano, mwaka 2012 tumepitisha azimio hapa, baada ya hoja binafsi ya Mheshimiwa Halima Mdee kuhusu masuala ya ardhi kwa wananchi, kwamba ifikapo mwezi wa Nne mwaka huu Serikali ingeleta tathmini kwenye Bunge hili na kiasi cha ardhi ambacho kinamilikiwa na wageni na *status* zake.

Leo mwezi wa ngapi? Leo mwezi wa Nane tunaelekea mwisho wa mwaka hili azimio halijatekelezwa. Kwenye Bunge hili yameshapitishwa maazimio mengi. Nakumbuka mwaka 2011 hata kabla ya mimi kuwa Mbunge, wakati wa Bunge la Bajeti, Bunge lilipitisha Azimio la kuongeza kodi kwenye mafuta ya taa, lengo likiwa ile kodi izuie uchakachuaji wa mafuta ya *petrol*, lakini vile vile ile kodi iliyoongezwa itumike kwenda *REA* iwapelekee umeme wananchi ambao wana-*consume* yale mafuta ya taa. Lakini ni Shilingi ngapi zilipelekwa *REA* kwa ajili ya kuwapelekea wananchi umeme wa vijijini? Hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo siyo Sheria, tatizo siyo kutokuwa na maamuzi, tatizo siyo kutokuwa na Sera; tatizo lipo kwenye mfumo, tatizo lipo kwa viongozi wetu ambao hawana *commitment,* tatizo lipo kwa viongozi ambao hawana *passion*, tatizo lipo kwa watumishi wote ambao pengine hawajui ni wapi sisi kama Taifa tunaelekea?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa mfano, katika masuala ya umwagiliaji, Idara ipo. Ukizungumza nao wanakwambia tatizo kubwa ni fedha, tatizo kubwa ni

rasilimali kwa maana ya rasilimali watu, vifaa na vitu vingine kama hivyo. Sasa leo tunakwenda kuunda Kamisheni, tunakwenda kuunda Tume. Mimi nafikiri ni mipango mwingine wa kuendelea kupiga *deal* tu kama tulivyofanya kwenye Kilimo Kwanza. Kwamba tumewatangazia watu Kilimo Kwanza, tumepeleka pembejeo za ruzuku, *I mean* kwenye Halmashauri zetu Vijijini. Lakini leo unajaribu kwenda kwa wakulima, ni wakulima wangapi ambao wanafaidika na hizo pembejeo? Hakuna!

Juzi Kamati hii ya Bunge ya Kilimo imekuja kwenye Halmashauri yangu kwenye Jimbo langu, wamekuta madudu mengi sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao walikuja. Mwananchi anapewa risiti inaonesha amepokea pembejeo za aina tatu, lakini kimsingi anapewa moja, na anasainishwa risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo lipo. Nami nafikiri tu cha msingi cha kufanya hapa labda nitangaze tu nia baadaye kwa kutumia hizi Kanuni za Bunge Kanuni ile ya 87 (1), nitaomba kwamba Muswada huu urejeshwe kwenye Kamati ukapitiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii kuhusu Muswada huu, na siungi mkono kwa asilimia hata moja Muswada huu ambao umewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Waziri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Joshua Nassari. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani ajiandae. Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nami nichangie kuhusu huu Muswada wa umwagiliaji wa mwaka 2013. Nimeusoma huu Muswada kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Sasa nilipofika mwisho, nikaona kwamba sababu za kutengeneza huu Muswada kwenye madhumuni ya hii Sheria ni kwamba kuna matatizo ya kukosekana mfumo wa kisheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, nyinyi mmekaa huko mkafikiri, mkaona sasa mkileta Sheria hii ndiyo umwagiliaji utasonga mbele, ndiyo kilimo kitakua. Kwa hiyo, mmeona hii ndiyo *solution! (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ya kusikitisha sana.  Ukiona Serikali ambayo imeshindwa kuendesha shughuli za kilimo, kilimo kimekuwa hakikui, hakiongezeki, inabaki ni kutapatapa. Ukiona Serikali ambayo imekwama inashindwa kuendesha mambo yake wanabaki wanatapatapa kutengeneza mifumo, kwamba sijui tukifanya hivi labda mambo yatabadilika. Ndiyo maana kila siku matatizo yakitokea, wanakimbilia kuunda sijui *Presidential Delivery Beurau,* sijui Tume, sijui *Big Results Now*. Haya ni matatizo ya kutokuwa na *vision,* kutokuwa na *focus,*

kutokuwa na mtazamo! Ndiyo matokeo yake haya! *(Makofi/Kicheko)*

Hii Tume nimejaribu kuifuatilia, wanataka kuiga kama ule mfano wa *Tanroad.* Nikasema hawa watu, kama wanajua, basi badilisheni mfumo wa Serikali iwe kama ilivyokuwa zamani. Kama mnataka kuwa na Taasisi za Mikoa, Sekeretarieti za Mikoa, Wilaya; mmempa Waziri kazi kubwa hizo! Rudisheni, kila Waziri awe na kazi zake, kuanzia Wizarani mpaka chini. Lakini haya ambayo mnayafanya ni kutapatapa. Sasa hivi mnatapatapa! Mmesha-*paralyze* kuendesha mambo, mnatapatapa tu! Lakini hii siyo *solution***.** *(Kicheko/Makofi)*

Tuambieni! Tumeshajenga miradi ya umwagiliaji na mimi nimekuwa nashangaa sana nchi hii, miradi ya umwagiliaji siyo kujenga mfereji. Mimi kule kwangu Muhambwe huwa wanatenga fedha za umwagiliaji, tena fedha zile zinaibiwa. Watu wanatengeneza mifereji chini ya kiwango na Mheshimiwa Waziri wewe ni jirani yangu, unapafahamu Mgondogondo wametengeneza mradi, fedha zimeibiwa, hakuna mradi wa Shilingi milioni 600 wa pale Mgondogondo pale Kibondo wa namna ile. Unafahamu! Sasa badala ya kutafuta *solution* kwa nini hii miradi inatengenezwa vibaya, mmekuja na hii Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachosema mimi, ninachosisitiza kwenye suala hili la umwagiliaji, kwanza umwagiliaji siyo kutengeneza mifereji kama ambavyo mnafanya. Unakwenda unakuta kuna mto unapita, ndio wanavyotengeneza kwangu, sijui huko kwenu! Lakini hata

kwako Mheshimiwa Waziri huwa nakuja na wewe unafahamu. Mnatengeneza, mnajenga huku mnajenga na huku na katikati maji yanakuwa yanapita, ndiyo mnaita umwagiliaji. Hakuna pampu za kutoa maji huko, hakuna mashine za kuvuta, sasa ninyi umwagiliaji ndio kutengeneza hii mifereji? Sasa ndiyo mmekuja na hii Tume? Tume hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, umwagiliaji ni mambo mengi, pampu za kuvuta, mbolea za kuweka kwenye hayo mazao, na kadhalika, Mheshimiwa Waziri, pale kwetu Kibondo, mbolea imefika mwezi wa Kwanza mahindi yakiwa yamekua na wewe uliona. Badala ya kusimamia mbolea ifike kwa wakati, hata ukiunda hii Tume, hii Tume itasimamia mbolea ifike kwa wakati? Kama mbolea inafika baada ya mwaka, watu mahindi yamekomaa, ndio mnaleta mbolea inafika Kibondo, sasa hii Tume itasaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uendeshaji wa mambo siyo Tume. Hii ni kutapatapa tu! Kutapatapa katika hii, Wizara imeshawasumbua, huwezi kuendesha Wizara kwa namna hii. Mimi nimekuwa najiuliza, hivi Tume ni nini? Wizara kazi yake ni nini? Mtu anaweza asijue, hivi ni kwa nini tuunde Tume hapa? Kwa nini tuunde Kamati? Tofauti ya Kamati, tofauti ya Tume, tofauti ya kazi ya Wakala, kazi za Waziri ni zipi? Lazima ujue kwamba, aah, *okay,* tunaunda Tume kwa sababu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mmesema mifumo ya kisheria imeshindwa. Sasa hivi hao wamwagiliaji ambao mnasema hawa Maafisa Umwagiliaji ambao mnawa-

*create, qualifications* zao zitakuwa hizo hizo! Sawa na ma-*engineer* wa maji walioko kule, sawa na Idara za Kilimo zilizoko kule, lakini shida, mmeshindwa kusimamia! Mmeshindwa! *You have failed!* Ndiyo maana mnabaki mnatapatapa kuunda Tume, kuhangaika hivi; lakini kwa mchezo huu, kuendesha nchi kwa kubabaikababaika na watu hawa, *I am not sure,*hii ni namna tu ya kupoteza muda kabisa kwa sababu, mambo yako hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukija kwenye vifungu hapa, kifungu cha (4) kinasema, kwa kuzingatia masharti ya Sheria, hii Tume inaweza yenyewe au kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, kuwekeza kwenye maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtuambie, hawa watu mmewachukua kutoka Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanaweza kuwekeza kwenye kilimo kwa namna gani na wenyewe? Wanaanza na wenyewe kuwa na mashamba? Kwa utaratibu upi? Tena wao wakijisikia, nimesoma kwenye kifungu hapa, wao wenyewe ni wawekezaji kwa mujibu wa hii Sheria. Ni wawekezaji wakijisikia. Wana uwezo wao wenyewe kuchukua ardhi wanapoona inafaa, wao wenyewe na kusema sasa hii ardhi itakuwa kwa umwagiliaji. Maana yake wanaweza wakaenda mahali wakasema hii ardhi inafaa, *then* wakajigawia wao wenyewe, wakawekeza. Kwa utaratibu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TIC* inafanya nini? Watu wengine wa ardhi ambao tunafahamu, kama mtu yeyote anahitaji ardhi anapaswa aombe. Kama hawa watakuwa

wanashirikiana na watu binafsi, wanashirikiana na *TIC*, utaratibu ule ufuatwe. Hii ni *paralysation* kubwa! Huwezi ukasema Tume. Hapa kuna Mawaziri huwa wanajibu tukiwa Bungeni, hii Serikali haifanyi biashara. Sasa mbona mmerudisha tena Tume ikawekeze kwenye kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 5(ii)(a) kinasema, "itakuwa ni kuishauri Serikali katika kutekeleza na kuihusisha Sera ya Taifa ya Umwagiliaji." Sasa hii Tume kwanza ukiiangalia ni Tume ya Serikali kwa sababu wanaoiunda ni watu kutoka Idara za Serikali *then* inaishauri Serikali tena. Ndio hivi! Ndio Tume hii yenu hii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Kifungu cha 11 cha Sheria hii, kinazungumzia Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji. Mimi nimekuwa napata shida sana na hawa watu. Hii miradi mmesema mingi itakwenda kutekelezwa kwenye Halmashauri, *then* mnatengeneza Ofisi za Mikoa za Umwagiliaji. Za nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnataka muwe na chombo ambacho kitaanzia juu mpaka chini, fanyeni kama *TASAF,* japo na wenyewe sasa hivi wamechakachua wanaanzisha Ofisi za Mikoa, lakini ile *TASAF* Awamu ya Kwanza walikuwa na mifumo yao kutoka juu mpaka chini kwenye Halmashauri. Wakaanza ku-*perform* vizuri, baadaye mkabadilisha. Sasa mmeweka hapa katikati, mmeona *TANROAD* wanafanya vizuri; nilimsikia Waziri wa Maji anasema aah, na sisi tunafikiria kuanzisha *TANWATER.* Nanyi mmefikiria kuanzisha kitu cha *Irrigation* kwenye Mkoa, mkifikiri kwamba hicho kitu kitakuja kufanya kazi kama

*TANROAD* inavyofanya kazi. Kumbe kile kitu kinafanya kazi kwa sababu ya Waziri binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri binafsi wa Ujenzi siyo kwa sababu ya chombo kilivyo, hapana. Kwa hiyo, hata mkidanganyana huko Mawaziri eti kila mtu; kwenye elimu uanzishe sijui vya Mikoa, kwenye kilimo, kwenye nini, *no!* Ile ni kwa sababu ya Waziri binafsi! *Aggressiveness* ya kufuatilia, ukali wake; lakini siyo kwa sababu kwamba, *no!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii Sekretarieti hapa itapoteza muda, inapoteza *resources.* Mnatwambia Wizara ya Kilimo ni ndogo. Fedha, kila siku mnalalamika! Badala ya kuweka mipango ambayo inakuja kutumia hizo fedha kidogo, mnaongeza gharama kubwa kwenye kuanzisha vyombo, kwenye *operations,* badala ya kupeleka fedha ziende kuzalisha mmetengeneza kitu kingine hapa katikati. Huku ndiyo nakuita kutapatapa!

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna Idara za Umwagiliaji za Wilaya. Hizi Idara zinaanzishwa na Waziri wa Serikali za Mitaa kwa kushauriana na Waziri wa Umwagiliaji ambayo itaendeshwa na Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya. Sasa mlichogundua kule Halmashauri, tatizo ni nini mpaka mmeleta hii? Kwa sababu Idara ya maji ipo. Idara ya Maji tunafahamu kuna Idara za Maji, Mamlaka zipo, Idara za Kilimo zipo za kutosha na Wahandisi wapo. Mlichogundua twambieni ndugu zetu. Hii Idara ya Umwagiliaji inayoanzishwa itakuwa na kitu gani kipya sana, tofauti sana na Idara ya Kilimo, Ofisi ya Maji? Kitu gani kipya tukitegemee Watanzania wenzenu? Tuambieni!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chiza, wewe ni Mhandisi kabisa. Sasa tupe majibu. Wewe ni Mhandisi wa Umwagiliaji na kwako kuna umwagiliaji na kwangu na ninaona palepale, na *I have to look example face to face* kwamba, hapa ni kwa Mhandisi, *what is the difference?* Mimi ni Mwanasheria, sijui haya; mbona wanajenga chini ya kiwango? Sasa hii Tume: Je, itakusimamia na wewe? Maana sijaona? Au tunafanya nini hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20, mnasema kutakuwa na watu ambao wanasimamia Sheria hii. Mnasema kwa madhumuni ya Sheria hii, miundombinu ya umwagiliaji inaweza kutengenezwa katika eneo la umwagiliaji na wahusika wafuatao: Halmashauri za Wilaya, Mkulima binafsi, Vyama vya Umwagiliaji, Kampuni iliyosajiliwa. Hebu tufafanulieni ni kila kampuni? Kampuni imesajiliwa kuchimba mitaro, inamwagilia na yenyewe? Kampuni ya Ujenzi na yenyewe inaweza tu? Maana mmesema kampuni iliyosajiliwa popote, kampuni ya wafuga nyuki? Zote zinafanya umwagiliaji? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiki kifungu cha 22 cha Tume kutwaa ardhi, hiki ndiyo hakipo tena, mkifute kabisa. Tume haiwezi ikatwaa ardhi kwa kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali. Kama ni ardhi ya Kijiji, lazima Mkutano Mkuu wa Kijiji ushirikishwe. Halafu hata hii mifumo yenu, humu nimesoma vifungu kwamba Tume itakuwa inaweza kumshauri Rais, kwenda kuchukua ardhi kwa ajili ya... *(Makofi)*

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felix Mkosamali. Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Amina Mwidau, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengea Kamani.

Mheshimiwa Amina, hayupo badala yake Mheshimiwa Magdalena Sakaya, halafu Mheshimiwa Titus Mlengea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada huu wa umwagiliaji wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa Umwagiliaji wa Taifa umekuja umechelewa kwa kweli, tena sana. Kwa sababu, kwa muda mrefu Serikali imekuwa inakuja na *slogan,* "Kilimo Kwanza, Kilimo ni Uti wa Mgongo, Kilimo cha Kufa na Kupona", lakini hakijawahi kuwa na tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoangalia hali halisi ya sasa hivi na mabadiliko ya hali ya hewa ya dunia kwa ujumla, bado Watanzania wengi wanategemea mvua, bado wakulima wengi wanategemea kilimo cha jembe la mkono, bado kilimo kimekuwa hakina tija kwa sababu hatuwezi kuendelea kutegemea tena mvua ambazo hazitabiriki na hazinyeshi za kutosha.

Kwa hiyo, Muswada huu tunauchangia kwa maana ya kwamba, ikiwa utekwenda kutekelezwa kwa ufanisi kwa sababu, tatizo siyo kuja na Muswada, tatizo utakwenda kujibu matatizo ya Watanzania ya Kilimo? Tatizo, utakwenda kusimamiwa kikamilifu ili uweze kuwa na tija kwa Taifa? Kwa hiyo, Wabunge tunaleta michango yetu ili Serikali ihakikishe kwamba, inakwenda kutekeleza kwa ukamilifu wake iweze kuwa na tija kwenye kilimo cha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmojawapo wa Wajumbe wa Kamati ambayo ilikaa na Muswada huu kuujadili kwa muda. Tuliweza kutoa michango yetu mbalimbali na ushauri maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama ambavyo Wabunge wengine wamechangia, tulishauri kwamba wale Wataalamu wa Umwagiliaji kwenye Sekta mbalimbali kuanzia Taifa, kwenda kwenye Mikoa mpaka kwenye Wilaya, Sheria inasema kwamba, ni lazima awe *Public Service* kwa muda mrefu. Tukasema tufungue mwanya, yaani Sheria itoe uwazi zaidi. Wakipatikana watu ambao wako nje ya Serikali, lakini ni watu wenye uwezo mkubwa, watu ambao ni *credible,* watu ambao ni Wataalamu wazuri waweze kupata hizi fursa na tusiji-*concentrate* kwenye eneo la kwamba, ni lazima awe *Public Service,* matokeo yake tukapata watu ambao ni dhaifu ambao hawataweza kwenda kukidhi mahitaji ya Sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 13 cha Muswada huu, Idara ya Umwagiliaji ya Wilaya; Sheria

inaainisha kazi nyingi sana za Idara hii kwenye ngazi ya Wilaya, ikiwepo kuanzisha *scheme* za umwagiliaji, kuwezesha uwezeshwaji wa Vyama vya Umwagiliaji, kutoa mafunzo, kutoa miongozo na pia kusaidia wamwagiliaji kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi hapa nina mashaka sana kwa sababu, tatizo kubwa ambalo limekuwepo ni kwa wakulima kutokuwa na pesa. Wakulima wetu wengi ni wadogo wadogo ambao hawawezi kupata fedha ya kutosha kuwa na miundombinu ya umwagiliaji.

Leo tukisema kwamba tukaache kwenye Wilaya ambapo sasa hivi tu zipo Idara mbalimbali, Idara ya Kilimo, Idara ya Maji, Wataalamu wa Kilimo wanakaa kwenye Ofisi hawana fedha za kutoka. Kwa hiyo, tunahitaji zile Ofisi za Halmashauri za Umwagiliaji, ziwezeshwe vya kutosha. Tukisema kwamba, waachwe Halmashauri watafute pesa kwa ajili ya wamwagiliaji kwenye Halmashauri zetu, tunajidanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali, ihakikishe ni namna gani ya kutumia mifumo mbalimbali kuhakikisha kwamba, fedha zinakuwepo za kutosha kwenye ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya wakulima, waweze kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwenye ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili lisiachwe peke yake kwenye ngazi ya Halmashauri kwa sababu, Halmashauri zimekuwa zinatumia *OC* kwa ajili ya Idara zake mbalimbali. Leo nenda kwa Idara ya Kilimo, waambie *OC*

kwa mwaka mzima mnapokea kiasi gani? Ni kidogo sana! Hana kitendea kazi, amebaki kukaa Ofisini. Kwa hiyo, ofisi inabaki ni meza, kiti na Ofisa Kilimo pale. Leo tukitaka kuwa na ufanisi, hatuwezi kwenda mbali kwa mwendo ambao upo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye kipengele cha 51, maendeleo ya umwagiliaji ni lazima yaende sambamba na usimamizi wa maliasili, ikiwepo vyanzo vya maji kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi mazingira. Ningependa kupendekeza na ninaomba Serikali itilie maanani sana, tumekuwa na matatizo ya maeneo mengi ya kilimo kuchukuliwa bila kufanyiwa hata tathmini. Anakuja mwekezaji, anakuja na nguvu zote kuwekeza. Serikali inampa kilaini kabisa, matokeo yake hafanyi kazi aliyotarajiwa, anafanya anachokijua, labda ni kuvuna mbao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wapo waliokuja kwa majina kwamba wanaanzisha sijui kilimo cha mibono, mwingine anakuja anaanzisha sijui kilimo cha kufuga samaki, matokeo yake anaharibu ardhi bure na hatimizi haja ile ambayo amekujanayo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kabla ya eneo lolote kutwaliwa kwa ajili ya umwagiliaji au kujenga miundombinu ya umwagiliaji ni lazima lifanyiwe *Environmental Impact Assessment.*

Kwa kutumia Sheria ya Mazingira ambayo ipo sasa hivi, nina mashaka kama kweli tutakuwa na ufanisi mzuri kufanya *EIA,* kufanya tathmini ya mazingira kwenye maeneo haya, kwa sababu, Sheria inasema kwamba, mwekezaji ambaye anataka eneo ndiye anayelipa fedha kwa ajili ya kufanyiwa tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata mashaka kwa sababu tumekuwa na matatizo mengi. Mwekezaji anashinikiza kwamba, anavyotaka yeye alime lazima apate pale kwa sababu yeye ndiye anatoa hela kwa ajili ya kufanya tathmini.

Kwa hiyo, Serikali inakuwa haiwezi kumnyima kwa sababu, yeye ndio katoa pesa na tunavyojua, ni kwamba, kwenye ngoma anayelipa zeze ndiye anayechagua wimbo. Hii itakuja kuwa hivi, mwekezaji kwa kuwa amelipa hela ya tathmini lazima atachagua eneo hata kama halifai kwa umwagiliaji, hata kama ni eneo la hifadhi, atapewa kwa sababu, katoa hela ya tathmini.

Kwa hiyo, ni lazima Serikali ije na mfumo kwamba, zipatikane fedha za kufanya tathmini maeneo muhimu, ili kuhakikisha kwamba, maeneo ambayo hayafai kwa umwagiliaji au maeneo ambayo yana shughuli nyingine, yasibadilishwe matumizi kwa sababu tu mwekezaji katoa fedha na pia wanafanya *lobbing* mbalimbali. Tumepata matatizo kwenye maliasili, maeneo mazuri inajengwa hoteli, pasipostahili kuwepo hoteli, *simply* kwa sababu mwekezaji katoa fedha ya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha 52, Tume itafanya uratibu na kuendeleza utafiti wa umwagiliaji. Pamoja na kufanya utafiti na kuratibu utafiti kwenye umwagiliaji, ni kweli kabisa kwamba, bila kuwepo na utafiti hatuwezi kuwa na kilimo bora, hatuwezi kuwa na umwagiliaji wenye tija, wala hatuwezi kujenga miundombinu ambayo inaweza ikawa na tija. Ninachosisitiza hapa ni kwamba, tupate Watafiti ambao ni makini na ambao watakuja na majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua miradi ya vijiji 10 ya kila Wilaya ili-*fail* kwa sababu, Halmashauri walikwenda kuchukua Watafiti ambao hawajui jinsi ya kutafiti maji. Rasilimali zimetumika, wamechimba visima, hakuna maji yaliyotoka kwa sababu Watafiti hawakufanya kazi yao vizuri. Wamekwenda kuchukua Watafiti *fake* ambao hawaijui kazi, rasilimali za Watanzania zimepotea na bado mpaka tunavyoongea hawajawahi kuyaona maji.

Kwa hiyo, nina hofu na mashaka kwenye suala la umwagiliaji, tusipokuwa makini kwenye utafiti; tutafute watafiti wazuri. Watakuja wale ambao ni vihiyo, watafanya utafiti, tutajenga miundombinu ya maji kwa gharama kubwa za walipa kodi na bado hawataona maji kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba pia suala la utafiti, Tume yenyewe haiwezi kufanya kwa sababu ninavyoona Tume kwa *position* yake haina wataalam wa utafiti, lazima tu-*outsource,* tutafute watafiti ambao ni

wazuri tunao kwenye vyuo vikuu na maeneo mbalimbali kuweza kufanya kazi ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji. Kwa kweli Mfuko huu kwa maoni yangu na nilipoona kwenye Muswada ndiyo itakuwa roho ya umwagiliaji, bila fedha hatuwezi kuwa na umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu unatakiwa upate fedha ya kutosha. Kwa hiyo nataka kusema kuwa mfuko huu kwenye Sheria inasema itapata fedha za mvuko zitatokana na ada, tozo mbalimbali, mauzo ya vifaa, mitambo chakavu, fedha itakayoidhinishwa na Bunge; fedha hii haitatosha miaka yote tumekuwa tunapitisha fedha ya kilimo hapa kiduchu, haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu kwa kutegemea fedha ya kutengwa na Bunge, fedha ya tozo, fedha ya ada, kuuza mitambo chakavu ambayo hatujui iko wapi, bado siyo *source* ya kutosha ya kupata fedha kwa Mfuko huu. Ni lazima Serikali ije ituambie kwamba, wapi hasa itatoka fedha ya kutosha, ni chombo gani kitakachohakikisha kwamba Mfuko huu unakuwa *stable,* unakuwa imara, unakuwa na fedha ya kutosha ili pale ambapo mwananchi anahitaji fedha kwa ajili ya kazi ya umwagiliaji, iweze kupatikana na isije ikawa tena ni mtindo ule ule wa kilimo ambacho hakina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa Ofisi za umwagiliaji katika Halmashauri zetu za Manispaa. Ofisi siyo

jengo, ofisi siyo meza, ofisi siyo kiti, Ofisi ni uwezeshwaji. Tunaomba sana lazima Ofisi hizi za umwagiliaji ndani ya Wilaya ziwezeshwe vya kutosha. Leo ukienda pale Wilaya ya Urambo au Kaliua au Wilaya nyingine yoyote ile atakachokwambia Afisa wa pale wa Kilimo au Maji ni kwamba, niko Ofisini kwa sababu sina kitendea kazi cha kwenda hata kwenye *field.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na maafisa Ugani wanaokaa ofisini kama masekretari kwa sababu hawawezeshwi kwa vitendea kazi wala fedha ya kwenda kufanya kazi kwa ajili ya kusaidia wakulima. Kwa hiyo kwenye suala la umwagiliaji ni lazima Sheria hii ikatoe nguvu na ikatueleze sisi Wabunge fedha kwa ajili ya Halmashauri itatoka wapi, tusitegemee *OC,* Halmashauri tunazijua uwezo wake na Serikali inajua vizuri uwezo wa kila Halmashauri, hatuwezi kutegemea *OC* za Halmashauri zikaweke ofisi ambayo itafanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inaeleza kulinda na kutunza maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji. Imekuwa ni tatizo kwa maeneo mengi ya Tanzania kwamba, maeneo ambayo yanafaa kwa umwagiliaji au ambayo yangefaa kuendelezwa kwa ajili ya umwagiliaji, yanabadilishwa matumizi tena maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mifano hai; maeneo ambayo ni yana maji ya kutosha, yana ardhi yenye rutuba yanakwenda kujengwa *Hotel*. Maeneo ambayo yana ardhi ya kutosha, nzuri yenye rutuba, yana maji, yana mito jirani, yanakwenda kujengwa makazi. Mfano halisi ukienda

pale Burka Arusha, kila mmoja anafahamu ambaye amepita maeneo yale lilikuwa ni eneo lenye maji, eneo zuri ambalo lina chemchem za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo lile eneo limegawanywa makazi, nimepita pale nimekuta lina bikoni tayari ni makazi ya watu, wakati makazi ya watu yanaweza yakawa katika maeneo mengine yoyote na yale ya kilimo yakaendelea kubaki kuwa ni ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda pale Morogoro kwa wale waliosoma Sokoine *University,* tulikuwa na eneo la bustani zuri pale la mkoa ambalo lilikuwa linalima machungwa na mbogamboga, mbogamboga nzuri zote za Mkoa wa Morogoro zilikuwa zinatoka pale, leo wakubwa wamechukua lile eneo wamejenga *Hotel* nzuri. Kwa hiyo, siyo eneo la kilimo tena, pale kuna Nashera *Hotel* leo kwa sababu tu kwamba, tumeshindwa kudhibiti na kuyatunza maeneo yanayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji, pamoja na sekta binafsi, mashirika na taasisi mbalimbali ni lazima wahakikishe wameshirikishwa vizuri kwenye sheria hii. Tunafahamu kabisa wenye mashamba makubwa ni wawekezaji, kama mashamba ya mpunga, mpaka hapa Dodoma mashamba ya zabibu, mengi ni mashirika na taasisi za dini, watu binafsi, mashamba ya miwa maeneo mbalimbali Mtibwa, Kilombero na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwenye Sheria hii lazima washirikishwe kikamilifu kwa sababu wao ndiyo

wataweza kutoa *challenge,* pia wanaweza kutoa mchango na kwenye suala la Mfuko wa Umwagiliaji, wao tukiwatumia vizuri wanaweza sana kutoa fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie suala la mgawanyo wa rasilimali ya maji. Inapokuja sasa ni suala la mashamba makubwa ya wawekezaji na suala la mashamba madogo ya wananchi mmoja mmoja wadogo wadogo, Serikali lazima isimamie ihakikishe kuna uwiano wa kutosha kwenye mgawanyo wa maji maeneo ambayo kuna wawekezaji wakubwa na wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili litaondoa tatizo la migogoro ya mara kwa mara, litaondoa pia tatizo la kutokuwepo na maelewano kati ya wakulima wadogo wadogo na wawekezaji wakubwa wakubwa. Mimi nimeshuhudia mgogoro wa Mtibwa, wakulima wadogo wadogo wa Mtibwa wana kilio cha muda mrefu, mkulima mkubwa yule wa Kiwanda cha Mtibwa anakwenda kuziba eneo lote kwenye maji, anabeba maji yote anapeleka kwake, wakulima wadogo wadogo kule nyuma wanakuwa hawana maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Mheshimiwa Titus Mlengeya Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi. Mheshimiwa Titus Kamani!

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Umwagiliaji. Kwanza nianze kupongeza Serikali kwa hatua ya kuleta Muswada huu kwa maana kwamba, Watanzania ambao ni 80% wanategemea kilimo. Kwa hiyo, Muswada huu unagusa jamii kubwa ya wananchi wa Taifa hili, lakini vile vile kuna changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo sasa yanabadilisha hii misimu ya mvua na hivyo kile kilimo cha kawaida kinakuwa kigumu sana na hakina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake tumekuwa tunapata njaa ya mara kwa mara katika Taifa letu na hasa mikoa ile ya Kanda ya Magharibi ambako natoka, kwa kweli ni tatizo kubwa sana na niseme sasa Muswada huu umefika kwa kweli umechelewa, lakini tunaipongeza Serikali kwa kuuleta. Mkulima wa Mkoa wa Simiyu, Geita, Mwanza na Shinyanga atashangaa sana Mbunge anayepinga kwamba Muswada huu usiletwe leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna utumwa mbaya kama utumwa wa njaa na wananchi wa Simiyu, Geita, Mwanza na Shinyanga wamekuwa wakitegemea chakula kutoka Mikoa ya Kusini ambayo ina hali nzuri ya mvua, kwa hiyo, wamekuwa wakilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona wanaopinga huu Muswada, wote wanatoka kwenye mikoa ya neema, lakini mtu anayetoka kwenye Mikoa ya shida hawezi akaupinga Muswada huu. Muswada kuletewa *amendment* nyingi si

ina maana umekuwa *democratic* zaidi, ina maana Watanzania wengi zaidi wameuchangia, wametoa maoni.

Kwa hiyo, ni kitu kizuri na naipongeza Serikali kwamba imeweza kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na ni sahihi. Muswada ambao unategemewa na Watanzania 80% kwa nini usichangiwe vya kutosha, kwa hiyo nawapongeza sana waliochangia na naishukuru Serikali imepokea mapendekezo hayo na imeweza kuyaleta.

Mheshimiwa naomba karatasi yangu hapo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kwanza Serikali kwa kuleta huu mpango wa matokeo makubwa sasa *Big Result Now,* kilimo kina mchango mkubwa sana katika matokeo hayo na kwa hiyo kwa kuleta Muswada huu ni jambo jema na tunategemea kwamba nchi yetu itaweza kupata mabadiliko ya haraka ya kiuchumi kwa sababu ya kuleta mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina utajiri mkubwa sana wa maji, mabonde, maziwa na kwa hiyo, kwa kuletwa Muswada huu na ndani ya Muswada huu kuna kuundwa ile Tume ya Umwagiliaji, sasa Tume hii ni muhimu kwa sababu itarahisisha maamuzi ya matumizi ya maji, maamuzi ambayo kwa kawaida yalikuwa yanapita kwenye Wizara ambayo ni Wizara kubwa sasa yatafanywa na Tume na kupunguza urasimu. Kwa hiyo, hili jambo ni jema sana na ningependa tulipongeze na tuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Sheria hii inaeleza hata kuundwa kwa Idara za Umwagiliaji kwenye ngazi ya Wilaya ambazo hazikuwepo, kabla ya hapa kulikuwa na ofisi za umwagiliaji wa kanda, zinasimamia mikoa kadhaa, sasa inakwenda mpaka Wilayani. Sasa, hivi tunataka Watanzania wasogelewe zaidi na huduma vipi? Tunakataa huduma hii kwenda ngazi ya Wilaya kwa kweli inashangaza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi na kwa Jimbo langu binafsi, naona kwa kweli Muswada huu utakuwa na manufaa makubwa. Wilaya yetu ya Busega ina mwambao wa takribani kilomita 120 za Ziwa Victoria, lakini hazitumiki kwa sababu ya urasimu wa maamuzi katika Wizara kubwa na rasilimali chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapopelekwa maamuzi katika ngazi ya Wilaya naamini sasa shida za msingi katika ngazi ya Wilaya zitaangaliwa. Tuna mabonde ya mto duma, tuna mabonde makubwa ya Busega, Mkula na Nyaruhande, yote haya sasa yanaweza kuangaliwa kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo napongeza sana kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile nijiridhishe dhamira ya Serikali, kama kweli ni ya dhati kuhakikisha kwamba tunabadilika kutoka hekta 450, 392 hadi 7,000,000 ambazo wameziweka kama Waziri alivyowasilisha. Hili ni lengo kubwa na zuri na hakika linaweza likalibadilisha Taifa letu kutoka utegemezi wa chakula na kwenda kuwa mzalishaji wa chakula, hata

kulisha nchi nyingi za maziwa makuu ambazo ni soko kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi kuna Mfuko ule wa Umwagiliaji, sijaona dhahiri ni wapi rasilimali za Mfuko huu zitatoka. Kama zitategemea Serikali peke yake, nina wasiwasi kama Mfuko huu utakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uzoefu wa taasisi nyingine za Serikali ambazo zimefanya vizuri, bahati nzuri ni Serikali hiyo hiyo, *TANROADS, EWURA* ambao wameshajiwekea misingi mizuri na taasisi hizi zinafanya kazi nzuri wote tunashuhudia. Kwa hiyo, nategemea kwamba na hii Tume ya Umwagiliaji iwe vile vile na vyanzo vingine vingi ambavyo vitakuwa vya uhakika kuhakikisha kwamba, sekta hii ya tasnia ya umwagiliaji inafanyika kwa umakini na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea Ofisi ya umwagiliaji ya Kanda ya Mwanza, kwa kweli haionekani kama ni ofisi ya kanda. Iko duni kwa maana ya Watendaji, vitendea kazi yaani hata ofisi ukiingalia tu unaona kwa kweli imechoka. Nategemea sasa kwa kuwa na hii Tume rasilimali za kutosha zitaelekezwa ili kuhakikisha kwamba Tume hii inafanya kazi vizuri na umwagiliaji unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala la teknolojia, ziko teknolojia nyingi ambazo zinawezesha kilimo cha umwagiliaji. Hizi inabidi ziangaliwe kutegemea na mazingira ya maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa, maziwa yote makuu, kuna maji ya kutosha na kuna

mabonde, kunawezekana kabisa kuweka mifumo ya kuvuta maji na kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mabonde ya mito, kuna maeneo ambayo ni makame na tambarare ambako kutahitajika labda mabwawa au maji ya ardhini, kuna maeneo utahitaji nguvu ya upepo lakini sasa hivi kuna *drip irrigation* ili kuweza kuhifadhi matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea nchi ya Zimbabwe ambayo kwa eneo kubwa ni kame na inapata mvua kwa msimu mchache sana, lakini Zimbabwe ilikuwa inafanya vizuri katika masuala ya kilimo, inazalisha matunda, lakini vile vile mifugo na nafaka vizuri sana. Sasa ningetegemea kwamba, kwa kuanzisha Tume iwe na wataalam wajielekeze na kuangalia kubainisha maeneo kuyafanyia *mapping* na kutambua mifumo halisi kutokana na maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa sababu kule kwangu Busega sasa kuna ujenzi wa lile bwawa zuri, kubwa la Lutubiga ambalo linawekewa miundombinu ya umwagiliaji. Naomba shughuli hii isimamiwe vizuri na ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha vile vile tasnia hii ya umwagiliaji, kuna suala la wataalam. Bahati mbaya naona katika nchi yetu bado wataalam wa umwagiliaji ni wachache, inaundwa Tume hii wakati kuna uhaba mkubwa wa wataalam na kuna chuo kimoja tu kinachozalisha wataalam wa umwagiliaji kwa maana ya

wataalam wa kati, wale mafundi mchundo ambacho ni Chuo cha Maji cha Rwegarulila pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, udahili wake uko karibu wanafunzi 100 kwa mwaka, tunazo zaidi ya Halmashauri 150 katika nchi yetu, ina maana kwamba, kama ukiwagawanya wale wanaozalishwa kila mwaka, hawawezi kuenea katika Halmashauri zote, lakini Wilaya hizo zina maeneo makubwa, kwa hiyo na kazi ya umwagiliaji ni kubwa. Sasa kwa udahili huo, naomba Serikali ijielekeze vile vile katika Chuo hiki kuhakikisha kwamba, wanazalishwa wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna Wahandisi wanaozalishwa katika Chuo cha Kilimo cha Sokoine, hawa nao bado ni wachache kwa sababu ni chini ya hamsini kwa mwaka. Sasa inabidi udahili uongezeke vya kutosha ili kuhakikisha kwamba, tunayafikia maeneo yanayohitajika kwa kilimo cha umwagiliaji kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo mliyojiwekea ni katika miaka miwili kufikia hekta milioni saba mtazifikiaje kama wataalam ni wachache namna hii naomba hili mjielekeze na mlitekeleze kwa juhudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili matumizi ya umwagiliaji yaweze kufanikiwa lazima iende sambamba na Wagani wa kilimo wale Maafisa Mazao wafike kule, kwa sababu hii miundombinu itawekwa kwa gharama kubwa, lakini kama ulimaji utakuwa ule ule wa kizamani, hawatumii nafasi, hawatumii mbolea, hawatumii madawa haitakuwa

na tija. Kwa hiyo, ni muhimu sana na Wagani wa kilimo waelekezwe kuhakikisha kwamba, mifumo hii inayowekwa kwa gharama kubwa inakuwa ya tija na manufaa katika Taifa letu na kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ninayoiona katika suala hili la kilimo cha umwagiliaji ni kwamba, Tume hii iko Wizara ya Kilimo, lakini maji na vyanzo vyake vinasimamiwa na Wizara ya Maji sijui namna gani Wizara na Tume hii imejipanga kuhakikisha kwamba, hakuna mgongano wa mawazo, hakuna mgongano wa utekelezaji kati ya Wizara ya Maji na Wizara hii ya Kilimo na hiyo Tume yake ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine muhimu katika kufanikisha shughuli hii, kwa miaka ya karibuni tumekuwa tukishuhudia migongano mikubwa kati ya wakulima na wafugaji na mpaka sasa Serikali haijatoa majibu sahihi na ya uhakika ya namna gani migongano hii inaondolewa, lakini jibu la uhakika la kuondoa migongano hii ni kutenganisha maeneo, kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili suala naomba kama halijaangaliwa na halijashughulikiwa kisheria na hakuna ushirikiano wa dhahiri kati ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Maji, Wizara inayosimamia TAMISEMI, hakuna ushirikiano wa dhahiri kushughulikia hii migogoro kwa sababu kila Wizara inatetea upande wake lakini ndani ya Serikali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limeleta matatizo makubwa, migongano mikubwa, hasara kubwa kwa wafugaji, hasara kubwa kwa wakulima na imepelekea hata kupoteza maisha ya watu. Sasa nashauri Wizara na Serikali yote kwa ujumla iangalie namna ya kuweka kipaumbele katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi ili miundombinu ya umwagiliaji itakayowekwa isije ikaharibiwa na mifugo na kwa sababu ukishaweka ardhi katika mfumo wa umwagiliaji ina maana itatumika kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima kuwe na mfumo sahihi wa kuhakikisha kwamba mifugo ina maeneo yake ambayo itatumia ili tuweze kuwa na mifugo mizuri, lakini vile vile maeneo ya makazi yasiweze kuingilia maeneo haya kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Muswada huu ni muhimu, naamini kabisa kama siyo ushabiki tu ni Muswada wa muhimu sana kwa nchi yetu, ni aibu kama Taifa kuendelea kuombaomba chakula au kutegemea chakula kutoka nje wakati tukiwa na hazina kubwa hii ya ardhi na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa ambayo yana ukame wa asili kama Sudan yanajitosheleza kwa chakula kwa sababu ya umwagiliaji, sasa tunapofanya ushabiki katika suala hili kwa kweli siyo sahihi. Tuiunge mkono hoja hii na tuhakikishe kwamba Tume hii inaanzishwa na inaanza kazi mara moja kama walivyopendekeza wenzangu na kanuni zije mara moja zipitishwe ili kazi hii ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Titus Kamani. Mheshimiwa Modestus Kilufi atafuatiwa na Mheshimiwa Mustapha Akunaay. Mheshimiwa Modestus Kilufi!

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Kwa niaba ya wananchi wa Mbarali, tunaishukuru sana Serikali kwa kuja na Sheria hii ambayo sasa itafanya wakulima wa Mbarali na Watanzania kwa ujumla waweze kujiona kwamba Serikali haijawatupa, iko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani wakulima katika nchi hii walikuwa wameachwa peke yao, zilikuwepo Idara za Umwagiliaji katika ngazi za Wilaya na Kanda katika maeneo mbalimbali kwa maana ya kuunganisha Mikoa, lakini bado kulikuwa hakuna msukumo kamili thabiti wa kuhakikisha kwamba kilimo kinatiliwa mkazo kama ambavyo sasa sheria inakuja. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba, kwa kufanya hivi sasa Serikali imewakumbuka wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii kwa asilimia kubwa Watanzania wanategemea kilimo na ndiyo ajira kubwa pekee kwa Watanzania ambayo inategemewa na walio wengi na wanaendesha maisha kwa kutegemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha sasa kinataka umakini, hii Tume inayoundwa kupitia sheria hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba, sasa kilimo kinakwenda na kasi mpya na ari mpya kama ambavyo tulianzisha ile *slogan* ya Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza kilianzishwa bila kuwa na mpangilio wa namna gani kitasimamiwa. Lakini kupitia sheria hii sasa naamini kabisa kwamba kilimo kitasimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali sana pamoja na Kamati ya Kilimo kwa kupitisha mpango huu na kuleta sheria hii ili tuweze kupitisha Wabunge kwa pamoja na naomba kwa kauli moja wote tupitishe sheria hii ili Watanzania waweze kufaidika. Naamini hata wanaopinga, wanapinga ili mjadala uwe mzuri, lakini hawapingi kwa maana ya kwamba Sheria hii haifai hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wanafanya hivyo ili mjadala huu uweze kuwa mzuri na utakapotoka utoke ukiwa na sura nzuri kwa maana ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbarali sisi ni wa kwanza kwa kuwa na skimu nyingi za umwagiliaji katika nchi hii. Sasa hivi tunavyozungumza tuna skimu zaidi ya 84 zinazofanya kazi, naamini hakuna wilaya ambayo ina skimu zaidi ya hizo ninazozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na Watanzania wengine waje wajifunze Mbarali, wana Mbarali hawangoji kuanzishiwa *schemes* na Serikali, wana Mbarali wamejipanga wenyewe na ndiyo maana tuna skimu nyingi,

wana Mbarali sasa wanachopigania ni hali ya hewa ambayo inawaumiza, wanalima vizuri sana, lakini hali ya hewa imekuwa siyo nzuri sana, siyo rafiki kwa wakulima, wamekuwa wakilima kwa nguvu nyingi sana na kwa kutumia gharama nyingi lakini hali ya hewa siyo rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokuwa rafiki kwa hali ya hewa hakumaanishi kwamba tuache kulima, maana yake ni kwamba, tutumie akili zaidi. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba na ninyi huko mliko kama wakulima wa maeneo yenu hawajajua vizuri kilimo cha umwagiliaji, waje Mbarali wajifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji sasa kinataka tutumie akili zaidi, tunahitaji tuwe na mabwawa ya umwagiliaji, kwa sababu hata kama mvua zitakuwa ni chache, lakini huwa zinanyesha, maji yanapita yanakwenda. Kama tutayatunza maji kwa vyovyote vile maeneo mengi katika nchi hii yatawezekana kuwa na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba, kama Serikali kupitia Tume hii inayoundwa, itasimamia na kuhakikisha kwamba mabonde yote yanayofaa kwa kilimo yanatengenezewa mabwawa, sehemu zile ambazo hakuna mito, nina hakika maeneo mengi katika nchi hii yataimarika kwa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mfumo mpya wa kilimo cha matone, yaani kwa kutumia matone, kwa maana ya kutumia maji kidogo kwa eneo kubwa. Kilimo hiki kweli ni

kizuri, mimi nimekiona, pale Kapunga mwekezaji amejaribu kuonesha mfano, lakini kile kilimo ni ghali sana, ile mitambo ya kuweza kumwagilia kwa matone, sidhani kama Watanzania wengi watamudu, hawawezi, twende na mfumo pekee ambao Watanzania wataumudu, ambao ni wa kuwaboresha miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kabisa kwamba, maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo hapa Tanzania yalikuwa hayajapata namna gani yanaweza yakasimamiwa. Nichukulie Mbarali, Mbarali tumebahatika kuwa na bonde nzuri sana ambalo linafaa kwa kilimo na inawezekana ndiyo sababu ya kuwa na skimu nyingi za umwagiliaji. Naamini katika nchi hii kama alivyosema msemaji aliyepita, kwa mfano Kanda ya Ziwa na maeneo mengine ambayo kilimo hiki bado hakijawa kikubwa, wakifika Mbarali wataona jinsi gani wakulima wale wanavyohangaika kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Tutakuja bwana.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, waje wajifunze waone jinsi gani wale wananchi wametafuta namna gani wafunge makorongo, watengeneze mifereji kuelekeza kwenye mbuga zinazofaa kwa umwagiliaji, waje waone namna gani wale Watanzania wanavyohangaika. Sasa hivi ninavyozungumza tuna skimu ya Mwendamtitu, ambayo wananchi wale sasa hivi Serikali pamoja na kuahidi kuwachimbia ule mfereji, lakini wao wenyewe wameunda Tume zao, wanachimba,

wenyewe wametafuta mashine wamekodi, wanaendelea na Serikali inawafuata nyuma lakini na wenyewe wanaendelea kuchimba mifereji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitaweza kumudu kutengeneza skimu zote katika nchi hii ,ni lazima ushirikishwaji uanzie kwenye vijiji, wakulima waungane na Serikali. Kwa kufanya hivyo, hata hiyo mitaji tunayozungumzia watapata wapi, mitaji ni pamoja na wakulima wetu wenyewe washirikishwe ili wajue ile mifereji ni mali yao. Waone kwamba ile mifereji si ya Serikali na kwa kufanya hivyo hata utunzaji wa mifereji hii utakuwa ni rahisi na miundombinu ya maji itatunzwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna matatizo kati ya Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji; kwa mfano, kumekuwa na hawa watu wa mabonde, wamekuwa wakikinzana sana na wakulima wanapotaka kuanzisha kilimo cha umwagiliaji. Utasikia hapa haiwezekani, unajua maji haya, sasa unakuta kuna kukinzana na hawa wakulima walikuwa hawana msemaji, lakini kwa sasa naamini kabisa wakulima wamepata mtu wa kuwasemea, wamepata chombo ambacho kitashughulika kuboresha miundombinu, ambacho kitashughulika hata kutafuta masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Tume hii ikaundwa tukapitisha sheria hapa, wakulima wakazalisha mazao mengi halafu ikashindwa kushughulikia masoko, siamini hivyo. Kwa hiyo, naamini kwa kupitisha sheria hii tutapata chombo madhubuti ambacho kitasaidia sasa

hata kutafuta masoko kwa ajili ya mazao ambayo wakulima sasa hivi wanahangaika, hawana kwa kuuzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba tunayo maziwa ambayo maji yanayofaa kwa umwagiliaji, tunahitaji kutumia maeneo mengine *water pumps* kubwa ambazo zinaweza zikamwagilia hata hekta 50 na zaidi ambazo zikiletwa Tanzania zinaweza zikasaidia kuokoa maeneo yale ambayo tayari kilimo cha umwagiliaji hawana. Kwa mfano Ziwa Tanganyika, inawezekana likawa chini sana usiweze kutengeneza mfereji kwa maana ya umwagiliaji, lakini kwa kutumia *water pumps*, ikawezekana kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge naomba tuunge mkono, tupitishe Sheria hii ili kusudi Tume hii sasa iweze kushirikiana na wakulima. Ingekuwa ni vizuri sana hata upande wa wafugaji, nao wakatengenezewa kitu kama hiki. Ili kusudi adha ya wafugaji kupata shida na mifugo kuonekana kama hawana mwenyewe, ikaondoka. Kwa hiyo, naomba hata upande wa mifugo vile vile wafugaji hawa waangaliwe na wenyewe waundiwe chombo ambacho kitawasimamia kwani sasa hivi hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafugaji hawa wakienda huku wanaonekana hawafai, wanafukuzwa, walipelekwa Mtwara na kwenyewe tena wanaonekana na kule hawafai, waende wapi hawa Watanzania? Wanakwenda huku wanafukuzwa, wanakwenda huku wanafukuzwa badala ya kuwaundia chombo muhimu ambacho kitawasimamia. Kwa hiyo, nimefurahi sana kuona kwamba sasa wakulima watapata neema hii, chombo hiki ndugu

zangu Waheshimiwa Wabunge tukipitishe ili wakulima wapate msimamizi sasa, kilimo kitakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hata nchi zilizoendelea, hazikuwaachia wakulima peke yao, hazikuwaachia watu peke yao wahangaike, Serikali lazima iweke mkono wake ndipo mambo yanaweza yakaenda. Tume hii itasaidia kupata mitaji kutoka sehemu mbalimbali kwa wafadhili mbalimbali ili kuwaunga mkono Watanzania kuboresha skimu zao, inawezekana. Wakulima peke yao hawawezi, lakini kwa kushirikiana na Serikali na wataalam mbalimbali ambao wamekuwa kila mwaka wanahitimu lakini hawajui cha kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao hawa Mabwana Shamba mpaka tunafika mahali tunawalaumu kwamba hawafanyi kazi, watafanyaje kazi mfumo hauwaruhusu, hakuna anayewasimamia, lakini kupitia Tume hii na hakika Mabwana Shamba wetu ambao tunawalaumu kwamba hawafanyi kazi sasa watafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa hata Idara za Umwagiliaji, ngazi ya Wilaya, sasa zitafanya kazi kwa sababu kuna chombo kinachofuatilia. Naunga mkono kwa asilimia mia moja, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tupinge, lakini mwisho tukubaliane, Sheria hii tuipitishe kwa manufaa yetu na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mifano, lakini siwezi kutolea mifano nje ya Mbarali ninakotoka, nina maeneo ambayo tulikuwa tunahangaika sasa hivi ni namna gani

tutaanzisha skimu nyingine. Tuna maeneo kama Iyala, tuna eneo kubwa sana, tuna maeneo ya Mpunga Mmoja, sasa hivi tumemalizia kujenga bwawa kubwa pale Igulusi, linahitaji kuimarishwa miundombinu, lakini pekee wale wakulima walikuwa hawawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna pale Madibira, tunataka kujenga bwawa kubwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji ambacho tutalima na wakati wa kiangazi kwa kumwagilia, lakini peke yao walikuwa hawawezi na msukumo mwingine ulikuwa haupo. Sasa kwa kupitia Tume hii naamini kabisa kwamba, vyote vitawezekana, hii sheria ipitishwe ili wana Mbarali waendelee kuneemeka na Taifa hili liweze kupiga hatua kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema sana juu ya barabara inayotoka Igawa kwenda Ubaruku kwa maana ya shida ambayo wakulima wa Mbarali wanapata kwa ajili ya kusafirisha mazao yao. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Waziri wa barabara waje waone magodauni yalivyojaa mipunga kule Mbarali, sioni sababu kwa nini barabara ile haitengenezwi. Waje waone mpunga ambao umejaa Madibira, waone mpunga ambao unapelekwa Mafinga, unatoka Madibira lakini barabara zake ni mbovu, sijajua kwa nini. Kwa kweli nilikuwa naomba... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Modestus Kilufi.

**MHE. MODESTUS A. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Modestus Kilufi. Kabla hatujaendelea naona Waheshimiwa Wabunge wanatoka toka nje na nini, nataka kuwahakikishia tu kwamba, mpaka sasa *Coastal Union* moja na Yanga moja na Simba moja, Oljoro sifuri. Mheshimiwa Mustapha Akunaay endelea.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Jambo la kwanza, napenda kuarifu kwamba, tunazungumza hapa si kwa ajili ya ushabiki, tunazungumza hapa tukiwa tuna hoja na kwanza, naunga mkono hoja ya Upinzani mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba, kuna Wizara ya Kilimo ina *instrument* ya Wizara na imeelezwa kazi zake ambazo sasa hivi siwezi kuzisoma kwa sababu ya muda niliopewa, lakini inatosha kusema kwamba katika Muswada huu kifungu cha (3) inaeleza kwamba, Tume hii inaanzishwa kufanya kazi kwa kifupi sana, ni kusimamia kazi ya umwagiliaji ambayo sasa hivi inafanya umwagiliaji nchi nzima, katika sehemu ambazo kuna mabonde ya umwagiliaji au kuna skimu. Sasa kitu ambacho hakipo ni rasilimali watu na fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Serikali ingetaka kuboresha umwagiliaji, ingeboresha rasilimali watu, wataalam tulionao na kuongeza fedha, lakini kuunda Tume ni kuongeza *liability* zaidi, kuwafanya wananchi walipe kodi zaidi ili wapate pesa za kuwamudu watu hao. Nina imani kwamba Tume hii itakuwa na waajiriwa si chini ya mia kwa nchi nzima, maana nimeona kazi zake katika kifungu cha (5) itakuwa mpaka inawasiliana na nchi za nje, itakwenda kuhudhuria mikutano ya nchi ya nje, kwa ujumla itakuwa kama inachukua sehemu kubwa ya kazi, itahitaji maofisi na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tukiongezewa pesa katika miradi sasa hivi inayoendelea hapa nchini, kwa mfano, katika Jimbo la Mbulu, sisi tuna skimu tatu, tuna miradi miwili ya umwagiliaji ya malambo. Sasa hivi tukipewa pesa wala hatuhitaji wataalam wengine, tutamwagilia maji na tutapata mazao bila kuomba chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilivyosoma mpaka vifungu vingine kama kifungu cha 40 kitawataka watu binafsi baadaye wakiwekeza, wananchi wawe wanatozwa ada ya kufanya umwagiliaji. Sasa hivi kama Serikali ikitupa pesa katika bajeti, umwagiliaji ni bure, maji yanatoka chini. Nchi hii ina maji na ardhi ya kutosha, sasa ukianza kuweka Tume kama hizi, naona haina sababu yoyote. Kama kuna mtu wa nje anaishauri Serikali kwamba tuweke Tume, ametushauri vibaya au kama kuna watu ndani ya Wizara wanataka kufanya miradi, maana yake sasa hivi nchi hii kila mahali kuna watu wana kichaka, kama wanataka kufungua kichaka, sielewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie kwamba, katika *objectives* za sheria hii mojawapo ni kwamba Watanzania hawana elimu ya umwagiliaji, sasa wakiweka Tume ndiyo watakuwa na elimu, badala ya kuwaelimisha watu ambao hawana elimu sasa hivi? Mbona tumefanya miradi hii ya umwagiliaji kwa muda mrefu, laiti kama tungekuwa na pesa hata tusingejua kama hatuna umwagiliaji, uzoefu wetu sasa hivi tulionao, ni elimu ya kutosha, hicho ni kisingizio cha kutaka hii sheria ipite.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatupingi umwagiliaji ufanywe, tusieleweke vibaya, tunataka umwagiliaji na tunauhitaji sana, lakini hatujafikia kwenye Tume, kwanza iboreshwe Wizara ya Kilimo, ipewe fedha zaidi, idara ile inayoshughulika na umwagiliaji iboreshwe, ikikua zaidi ikifikia kiwango cha kuwa na Tume, tunaiachia Tume. Sisi tunaelewa maana ya Tume ni *Agency* au ni *Commission*, lakini sasa hivi sisi hatuna fedha, tunaanzisha Tume, itataka hela zaidi, hatuoni Mtanzania ameshakuwa *tasked* zaidi ya anavyoweza kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukindelea na kifungu cha 13, kinazungumzia juu ya *Irrigation Officers* wa Wilaya. Pale kuna Wizara karibu nne ambazo zinahusika; kuna Wizara ya Kilimo, kuna Wizara ya Ardhi, kuna Wizara ya Maji, mpaka kuna Wizara ya Fedha kwa sababu ya kutozwa hiyo ada. Hiki kitu ni mtambuka, sasa tunahitaji Halmashauri za Wilaya zihusike katika Wilaya kwa sababu zina madaraka ya kutosha na wataalam inao wa kutosha, Tume hii itakuwa inaondoa madaraka ambayo sisi tumepewa kisheria. Hii

inakwenda kinyume na sera kwanza ya kilimo, ukiangalia sera ya kilimo hamna ugatuaji wa madaraka kutoka chini kwenda juu, badala yake ni juu kwenda chini.

Pili, *irrigation policy* ya nchi inataka ifanywe na wenyeji wenyewe, haitaki tena wawekezaji. Sasa unataka tena kuwaweka wawekezaji, wawekezaji wawepo katika sekta zingine siyo katika sekta hii ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiweka hii katika sekta hii ya *irrigation,* ina maana sasa utawaleta kama wasemaji waliotangulia walivyosema, utaleta wawekezaji kutoka nje, watachukua pesa hapa hapa kwenye mabenki, baadaye watazi-*list* katika *stock market* halafu waweze kuuza kwa sababu ni mikataba ya Kimataifa, kwa hiyo, wananchi wetu watakosa maji yao wenyewe kwa sababu ni ya kutozwa na bado wataondolewa katika maeneo ambayo Rais atatamka kwamba, maeneo haya yanafaa kwa ajili ya *irrigation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mustapha Akunay. Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe. Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma!

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza

kabisa naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleweke kuwa mimi ni mmoja wapo wa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo. Napenda kusema kuwa *amendments* ambazo tumeletewa hapa mezani zimetolewa na kuandaliwa na Kamati na sana sana ni ufafanuzi na tafsiri ya maneno na mengine toa hiki kwa *number* au maneno tu, lakini hazijabadilisha maana yoyote ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ieleweke kuwa umwagiliaji ulikuwepo, umwagiliaji wa mifereji iliyotengenezwa na umwagiliaji wa asili, lakini ieleweke kuwa, haikuwepo Sheria ya kusimamia umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuletwa kwa sheria hii kunaboresha sana mambo ya umwagiliaji. Naishukuru sana...

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, namwona Mheshimiwa Machali amesimama!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(8) kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Mbunge ambaye umemtaarifu aweze kunisikiliza. Anatueleza kwamba, hizi *amendments* zimefanywa na Kamati, *amendments* hizi zimefanywa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa niaba ya Wizara, na siyo Kamati.

Kwa hiyo, napenda tu kwamba pengine kumpatia taaarifa hiyo ili kusudi aweze kueleza vitu ambavyo wote tunaviona kwamba vimeandikwa mahali hapa, basi naomba aipokee taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, endelea.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakataa, kwa sababu Kamati ndiyo iliyokaa. Aliyeandika ni Waziri, lakini Kamati ndiyo iliyokaa na ndivyo nilivyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuleta Sheria hii na naomba sana, Waheshimiwa Wabunge, tuone kuwa ni muhimu sana huu Muswada, tuweze kuujadili na kuupitisha. Naamini kuwa Wabunge wote walio humu ndani na Watanzania wote, kila mmoja anafahamu maana ya umwagiliaji na faida ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Mikoa yetu mingi kutokana na tabia nchi ilikuwa na matatizo ya ukame na upungufu wa mvua. Mikoa mingi hata wale ambao wamekataa, lakini naona kuwa hawatakataa watakubali, kwani Mikoa mingi ilikuwa na njaa. Mikoa mingi ilipata matatizo na iliomba chakula cha njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na kilimo cha umwagiliaji hatutakuwa na njaa, kilimo cha umwagiliaji

*perse* ni kuvuna na kulima na kuvuna. Kwa hiyo, maana yake chakula kitakuwepo *throughout the year*, mwaka mzima tutakuwa na chakula. Kwa hiyo, naomba sana tukubaliane tuweze kujadili na kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mkombozi wa mwananchi na mkombozi wa Mtanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kwa mara nyingine namwona Mheshimiwa Barwany!

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa msemaji ambaye anaendelea kuzungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatuna chakula cha njaa. Nilikuwa nampa taarifa hii tu!

**NAIBU SPIKA:** Unaweza ukarudia, Mheshimiwa sidhani kama Waheshimiwa Wabunge wamekuelewa! (*Kicheko*)

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Hatuna chakula cha njaa, chakula ni chakula tu! (*Kicheko*)

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naikataa, inaeleweka kuwa ni chakula cha msaada, lakini unatibu njaa, ukiomba chakula cha msaada maana yake una njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba hizo dakika zangu wanazoharibu uziangalie. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kuwa sheria hii itakuwa ni mkombozi wa mwananchi, mkombozi wa kila mmoja hata aliye humu ndani, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe umeshuhudia Wabunge mbalimbali wanaomba chakula cha msaada kwa sababu mikoa yao ina njaa. Kilimo cha umwagiliaji, ni kilimo ambacho kinamkomboa mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ambacho tunalima sasa hivi cha kutegemea mvua, siyo kilimo cha uhakika. Kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba na nasihi kuwa huu Muswada ujadiliwe na Wabunge wote na uweze kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani 80% ya Watanzania wanaishi vijijini na hawa Watanzania wanategemea kilimo. Hiki kilimo ili kiwe kilimo cha uhakika na tuweze kupata chakula cha kutosha, lazima kiwe kilimo cha umwagiliaji. Hasa tunapokwenda kwenye mambo ya *big results now (BRN)*, pamoja na Kilimo Kwanza, ni vizuri tutumie kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuunda Tume ambayo itasimamia mambo ya umwagiliaji. Hii Tume ni muhimu sana na imeweza kujumuisha wataalam wengi na hao wataalam ni wadau wa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, hii Tume itaweza kusimamia na kuweka sawasawa mambo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoona ni kuwa, hapa kuna *Engineer* wa Mkoa na *Engineer* wa Wilaya, *Engineer* wa Wilaya ataweza kushirikiana na *Engineer* wa Mkoa ambapo hawa wote watakuwa *answerable* kwenye Tume. *Engineer* huyu wa Wilaya akifanya vizuri chini ya Tume ataweza kuzalisha mazao kwa wingi na kwenye Halmashauri tutaweza kupata chakula cha kutosha na pia tutaweza kupata mapato ya kutosha kutokana na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na chakula hiki na kilimo cha umwagiliaji, Mkulima ataweza kupata chakula cha kutosha na ataweza kupata pato la kutosha kwenye familia yake na ataweza kupata lishe kwenye familia na tutaweza kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuweze kujadili huu Muswada na tuweze kuupitisha. Umwagiliaji narudia kusema kuwa, naomba sheria iendelee kuangalia wakulima wadogo wadogo na wenyewe waweze kufaidi wakati watapokuwa wanagawa maeneo hasa kwa mashirika mbalimbali, basi na wakulima wadogo wadogo waweze kufaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kugawa maeneo haya na wakulima wa maeneo hayo pamoja na Halmashauri, inabidi washirikishwe kikamilifu ili kupunguza migogoro ambayo mara kwa mara huwa inajitokeza kwa upande wa ardhi. Ili kumnufaisha mkulima, narudia kusema kuwa, sheria hii iweze kupitishwa na wananchi waweze kunufaika na kilimo hiki cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kilimo cha umwagiliaji inabidi tutunze vyanzo vya maji, kwa sababu tunafahamu kuwa kama vyanzo vya maji havitatunzwa, kilimo cha umwagiliaji hakiwezi kwenda vizuri. Huu Muswada tumeuchambua na kila mmoja anauelewa na kila mmoja anajua maana ya kilimo cha umwagiliaji. Huu Muswada unaeleweka, masahihisho na kujadili ni kitu cha kawaida; tujadili, tusahihishe, lakini mwisho wa yote huu Muswada uweze kupitishwa kwa faida ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kuwa, wataalam watakaowekwa huko mikoani, japokuwa hatuna wataalam wengi, lakini nafurahi kusema kuwa mwanzoni tulikuwa na wataalam wa Kanda. Sasa hivi hiyo kada ya wataalam wa Kanda hawatakuwepo, sasa hivi huduma zitakuwa karibu kwani zitakuwa mikoani na zitakuja kwenye Wilaya. Maana yake ni kwamba, huduma zinazidi kuwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiitumia vizuri na kuisimamia vizuri hii sheria, naamini kilimo cha umwagiliaji ambacho kilikuwa hakina tija sasa hivi kitakuwa na tija na watu wataweza kukifurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kila mmoja ajielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Sasa hivi tunakuja na teknolojia mpya ambayo tayari imeshaletwa na baadhi wanaitumia ambayo ni kilimo cha umwagiliaji wa matone. Kilimo cha umwagiliaji wa matone ni kilimo kizuri ambacho

kinatumia maji machache, lakini hayo maji yanafika *straight to the roots of the plant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kila mmoja aunge mkono hii sheria, kwani hii sheria ni nzuri sana, tuijadili na tuweze kuipitisha na iweze kupitia kwenye hatua mbalimbali na mwisho wa yote iweze kuwa sheria ya kumnufaisha mwananchi ambaye anategemea sasa hivi kilimo cha mvua. Kama tutasimamia vizuri, asilimia kubwa itaweza kutegemea kilimo cha umwagiliaji.

Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana, kila mmoja anapenda umwagiliaji, hata anayebisha anapenda umwagiliaji, hakuna ambaye hapendi umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba tuungane tuwe kitu kimoja, tuweze kupitisha Muswada huu, hatimaye uweze kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nafikiri kila mmoja amenisikia. Ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kwa mchango wako mzuri sana, ni kweli kabisa kila Mbunge hapa anapenda umwagiliaji. Sasa Mheshimiwa Munde Tambwe atafuatiwa na Peter Serukamba na dakika zitakazobaki atatumia Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Mheshimiwa Munde Tambwe!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nikupongeze kwa kutupa taarifa

kwamba Simba imeshinda goli moja, ukizingatia kuwa kule Tabora ninakotoka kuna Rais wa Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia moja kwa moja kwenye Muswada. Kwanza kabisa nianze kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu hapa Bungeni wa Sheria ya Kuunda Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Mimi binafsi nadhani Serikali ilichelewa kuleta Muswada huu, kwa sababu Muswada huu una *impact* kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia mabadiliko ya tabia nchi, ni lazima tujielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mtu anaposema sheria hii haifai, simwelewi, kwa sababu bila kilimo cha umwagiliaji hatuwezi kufika, tukizingatia ratiba za mvua zimebadilika. Kama umezoea kulima mwezi wa Tisa utalima mwezi wa Kumi na Mbili na ukilima mwezi wa Kumi na Mbili mwezi wa tatu hakuna mvua. Kwa hiyo, ni lazima tujielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Naipongeza sana Serikali kwa kuja na Sheria hii hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko ya njaa yamekuwa mengi, hata kule Tabora kwetu tuliwahi kuwa na malalamiko, lakini naipongeza Serikali ilitusaidia. Kutokana na tatizo hili ni lazima tujielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashawishi sana Wabunge wenzangu kupitisha sheria hii, bila sheria hii hatutakuwa na wawekezaji, hakuna mwekezaji

atakayekuja kuwekeza bila kuwa na sheria. Ni lazima tuwe na sheria ndiyo tupate wawekezaji na napinga kusema kwamba, kusiwe na wawekezaji wa suala la umwagiliaji, ni lazima tuwe na uwekezaji ndipo nchi yetu iweze kuendelea na kuongeza fursa za ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi zimekuwa zikifanikiwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. *Egypt* imefanikiwa sana, *South Africa* imefanikiwa sana, Sudan imefanikiwa sana, pamoja na nchi nyingi tofauti tofauti, kwa sababu ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naamini na sisi Tanzania tukianzisha kilimo cha umwagiliaji, tutafanikiwa kwa kiwango kikubwa sana na kwa hili Tume imejibu malalamiko ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya umwagiliaji yalikuwa katika kanda tu, kulikuwa hakuna Mkoani wala Wilayani, lakini kwa Tume hii tutapata umwagiliaji mpaka kwenye Wilaya zetu na mpaka kwenye Halmashauri zetu. Naipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatoe wasiwasi Wabunge wanaosema Tume hii haina maana, ina maana kubwa sana. Kulikuwa na urasimu mkubwa sana kwenye suala zima la umwagiliaji, lakini sasa Serikali imekusanya vitu vyote kwa pamoja. Imekusanya Wizara ya Kilimo, Ardhi, Maji, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TAMISEMI, Mifugo na Uvuvi. Imekusanya pia wawakilishi kutoka kwenye *irrigation* na wao wameingia humo ndani. Kwa hiyo, kitu hiki kimekusanya vyombo vingi na vimekuwa kitu kimoja, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani ilikuwa mtu akitaka kufuatilia mambo ya umwagiliaji lazima aende kilimo, unaambiwa kutoka Wizara ya Kilimo uende Wizara ya Maji, uende TAMISEMI, Wizara ya Ardhi ukaangalie masuala ya ardhi. Mtu alikuwa anachoka na anakata tamaa, lakini sasa hivi Serikali yetu imeturahisishia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa maana imeliona hilo mapema. Kwa Tume hii, sheria hii ni nzuri sana, lakini Serikali sasa lazima iwe na fedha, hatuwezi kuunda Tume hii bila kuwa na fedha. Kwa mfano, nitoe kule kwetu Tabora, tulipata bwawa la Inara, tukatengewa fedha, zile fedha zikahamishwa, zikaenda sijui wapi mpaka leo zile fedha hazijaja. Kwa hiyo, hii sheria ni nzuri, lakini tuwe na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani umwagiliaji ulikuwa kwenye Kanda, lakini kwa Muswada huu sasa, niwatoe wasiwasi Wabunge, tutakuwa na Mkuu wa Idara ya *Irrigation* kwenye Halmashauri zetu. Tutakuwa na mafungu ya umwagiliaji kwenye Halmashauri zetu. Zamani tulikuwa na Mkuu wa Idara wa Kilimo, kwa hiyo tulikuwa hatuna Mkuu wa Idara ya *Irrigation* kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kila Halmashauri itakuwa na fedha za umwagiliaji. Hivyo, Madiwani watakaa, watatengeneza *scheme* za umwagiliaji na naamini tutapata *impact* kubwa ya kilimo kama alivyosema Mheshiiwa Waziri kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini sana hilo suala litawezekana. Niwatoe wasiwasi Wabunge, hili suala ni zuri sana, tutakuwa na Afisa *Irrigation* wa Mkoa ambaye ni *Engineer*, atasimamia Wilaya zote na yeye ndiye atakuwa Mkuu wa Idara ya *Irrigation* kwenye Wilaya. Tunataka nini tena Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba tupitishe sheria hii, kwani sheria hii ni nzuri sana na ndiyo maana nasema tuache ushabiki. Mtu anayepinga sheria hii ni ushabiki tu, kwa sababu sheria hii inakwenda moja kwa moja kwa Mtanzania. Ukikipeleka kitu kwenye Halmashauri umekipeleka kwa wapiga kura wetu, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali yetu imekuwa na mipango mizuri mingi mara kwa mara na mipango mingine mizuri huwa haitekelezeki. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, huu mpango ni mzuri sana na una *impact* na kwamba mpango huu umetoa urasimu kwa Watanzania. Tunaiomba sana Serikali, mpango huu ufanikiwe kama ulivyoletwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tabia ya kuandaa mipango mizuri, lakini mipango hiyo inafika njiani inakufa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwa mpango huu ambao utakwenda kumkomboa mnyonge wa chini kwa kutengeneza *scheme* za umwagiliaji, tunaomba mpango huu usife, mpango uje hapa Bungeni tuone unafanya kazi. Tunaomba idara hizo za *Irrigation* zitengewe mafungu ya

fedha kwa sababu Idara hizo zinakwenda kuwakomboa Watanzania kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ni kilimo kizuri sana, sisi kule Igunga nadhani safari hii tumeongoza kwa kilimo cha mpunga kwa sababu ya *Irrigation*. Naamini Watanzania wote na Halmashauri zetu zote zikiwa na Wakuu wa Idara zikapelekewa fedha za *Irrigation,* naamini tutakombolewa sana na tutaacha kuipigia Serikali kelele njaa njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali imekuja na mpango huu mzuri, tuuunge mkono, kwani hatutaweza kila siku kuja hapa Bungeni kuomba chakula, kwa sababu tunalima kilimo cha mvua. Hata hivyo, tukilima kilimo cha umwagiliaji hatutakuwa na haja ya kuja kupiga kelele ya njaa, tutafanya kazi nyingine za maendeleo na kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema haya machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Munde Tabwe. Sasa Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Ole-Sendeka atakuwa mchangiaji wa mwisho.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna hekta milioni arobaini na nne zinazofaa kwa kilimo, lakini kama nchi tunalima *only* asilimia ishirini na nne ya hizo hekta milioni 44. Pia, tuna hekta milioni 29.4 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Tujiulize ngapi sasa tunazilima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza kuzichambua hizi hekta tulizonazo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, wataalam wenyewe wanasema, hekta milioni 2.3 ndiyo wanaita *high potential irrigation area;* hekta milioni 4.8 ni *medium potential,* lakini hekta milioni 22.3 ni zile *low potential irrigation area*, lakini eneo la hekta 452,392 tu, ndilo ambalo linalimwa kwa kilimo cha umwagiliaji ambao ni asilimia 1.53. Nimeamua kuanza kwa kusema haya, ili nioneshe umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, kama nchi tumechelewa sana. Haiwezekani nchi ambayo tuna hekta milioni 29.3, tunazo-*irrigate* peke yake ni hekta 452,000, haiingii akilini hata kidogo. Mimi nashukuru Mheshimwa Waziri ameleta Sheria hii, kama ameleta Sheria hii sasa, ningeomba yafuatayo Serikali iyafanye:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ni jambo muhimu sana katika jambo lolote. Ukitaka kuleta maendeleo ya namna yoyote, lazima uwe na *legal framework* ambayo ina *clarity.* Lazima Sheria yetu hata mtu anayekuja, anataka kuwekeza kwenye chochote, cha kwanza anachoangalia ni Sheria iliyopo. Ukitaka kuleta Wawekezaji kwenye sekta

yoyote, jambo la kwanza ambalo wataangalia ni Sheria iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kweli kama nchi tumekwenda nje kuleta Wawekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji, hakuna ambaye angekuja kwa sababu Sheria haikuwepo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niwaombe wenzangu Waheshimiwa Wabunge, kuleta Sheria kwanza ni ukombozi kwenye kilimo cha umwagiliaji. Maana tulikuwa tunajiendea tu, kama Mungu anatusaidia, ndiyo maana tulikuwa tunasema leo tunaleta kilimo kwanza, kilimo cha uti wa mgongo, lakini bado hatukuweza kutumia *potential* tuliyonayo kwenye umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema, hili la kuanza na Sheria, angalau linaleta ahueni, kwamba sasa unaweza ukamwambia mtu njoo Tanzania uwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji, akija cha kwanza atauliza Sheria yako ya Umwagiliaji iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akishasoma Sheria yako ya umwagiliaji, ambayo kuna *clarity*, huyu mnaweza mkaanza kuongea. Ni matumaini yangu sasa hii *Commission* moja ya kazi ya kwanza wanayofanya, waende kutengeneza *Land Bank,* waende kutengeneza Benki ya Ardhi, tujue ni maeneo gani yanafaa kiukweli kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, isije ikawa, tumeanzisha Tume, tumeweka *bureaucracy*, ikaja kuondoa *bureaucracy* ya Wizara ya Kilimo, ikahamia kwenye Tume, hapo mtakuwa hamjatusaidia. Kwa hiyo, niomba, Mheshimiwa Waziri, tunatunga Sheria hii, aende haraka atunge Kanuni, lakini akishaweka watu ofisini, kazi ya kwanza wafanye utambuzi wa maeneo yote ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *data* zipo, *area* gani ni *high potential, medium potential* na *low potential,* angalau tuanze na zile *high potential,*ambazo ni karibia hekta milioni 2.3. Tukiweza ku-*irrigate* maeneo hayo, hayo tu ya 2. 3, naamini tutaweza kuwa na chakula cha kutosha nchini, na tutaweza kuuza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niiombe Serikali, tumeleta Sheria nzuri sana, tunaanzisha Tume kwa ajili ya suala hili la umwagiliaji, lakini kama Serikali hatutakuwa tayari kuweka fedha kwenye bajeti, bado Tume hii haitafanya kazi tunayoitarajia. Haiwezekani tukaendelea kwenye kilimo cha umwagiliaji bila kuwekeza. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata bahati, ukienda *Egypt*, ni vile tu leo imeharibika kwa sababu za kisiasa, ukaona mashamba makubwa ya *irrigation* na mashamba yenyewe siyo makubwa kama ya Tanzania, lakini yanalisha nchi ile na wanaweza kuuza nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Ethiopia, utaona. Ukienda *South Africa*, unapotoka Mbabane unakwenda *all*

*the way to Durban*, unakutana na mashamba makubwa ambayo yako *irrigated*. Maana yake ni nini, ukiwa na chakula kingi, utaweza ku-*carve inflation,* utaweza kupata fedha za kigeni, lakini na watu wako na utulivu ndani ya nchi utakuwa mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda India, hakuna muujiza, ni kilimo cha umwagiliaji na wenzangu wamesema, katika mabadiliko haya ya hali ya hewa duniani, unahitaji sasa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, niombe, wako wanaosema, rafiki zangu wa Upinzani, nimewasikiliza kwa makini sana, wanakubali umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, lakini wanapinga uwepo wa Sheria, hii ni *contradiction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuibana vizuri Serikali, kwa sababu kwenye Sheria hii wameeleza mambo mengi sana watakavyotekeleza kilimo cha umwagiliaji, maana yake hii Sheria, tukikutana mwaka kesho, tutamuuliza Waziri wa Kilimo, umefanya nini kwenye maeneo haya. Sasa kama tunasema tunaona umuhimu wa umwagiliaji na Mungu ametujalia, Tanzania tuna maji mengi sana, lakini ajabu, maji yote yanakwenda baharini, yanakwenda kwenye maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa unatoka Dar es Salaam, unakuja mpaka hapa tu Dodoma, usiende mbali, utakuta mabonde mazuri ambayo tungefanya *irrigation* yangelisha nchi hii. Unapotoka Dar es Salaam unakwenda Mtwara, ukiangalia ile *Basin* ya Rufiji, unatoa machozi, unasema hivi sisi tuna tatizo gani? Nadhani leo Waziri

amekuja na mwarobaini, sasa niombe Serikali iweke fedha za kutosha kuhakikisha tunatekeleza haya tuliyokubaliana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kusema hayo, niseme kwamba, kazi nyingine tuliyonayo kubwa mbele yetu, ni Watendaji. Tunaleta Sheria nzuri sana, naamini hapo nyuma, kwa sababu ambazo wote tunazijua, tulichelewa kidogo kwenye kusomesha ma-*engineers* wa *irrigation*, wapo lakini siyo wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Sheria hii, ina tu-*demand* tuwe na *workforce* kubwa katika *area* hii ya umwagiliaji. Tulifanya hivyo kule nyuma, baadaye wakawa hawana kazi, wengine wakaanza kufanya shughuli zingine, kuna *slow* kwa sababu hatuna *workforce* nzuri. Kwa hiyo, ni vizuri sasa Serikali tunapoanza kuja na hii nguvu mpya ya kutaka kufanya kazi ya kilimo hasa cha umwagiliaji, tusisahau *area* ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale *University* yetu ya Sokoine, sasa lazima *Department* ya *Irrigation* iboreshwe kweli kweli. Tupate *Engineers* wazuri wa *irrigation*, lakini tusiishie kuwapeleka Sokoine, tuwapeleke Vyuo Vikuu ambavyo vimebobea katika suala la *irrigation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Egypt, Cairo *University* wamefanya, wana *Department* nzuri sana, Bangalore *University* wana *Department* nzuri sana katika *irrigation*. Tuwapeleke watoto wetu wakajifunze Uhandisi huu, kwa sababu sasa, hata ukiangalia hapa unaona kuna

*hierarchy* kubwa kuanzia Tume mpaka kwenye Halmashauri, lakini nenda kwenye Halmashauri zetu *Engineers* wa *irrigation* ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia hapa ni kutaka hadi kwenye Halmashauri tuwe na *Engineers* ambao wamesoma mambo ya umwagiliaji. Kwa hiyo, ni lazima tuwekeze vya kutosha kwenye elimu, hili hatuwezi kuliepuka. Niombe Serikali sasa wakati tunayafanya yote haya, yatusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida nyingine ya Tume hii, inakuja sasa kuondoa matatizo yaliyokuwepo kimfumo, ukienda pale Wizarani, kwa kweli suala la *irrigation* lilikuwa halipewi kipaumbele cha kutosha, ukienda Mikoani, *irrigation* kulikuwa hakuna watu, unaambiwa watu wote wako kwenye Kanda. Ukienda kwenye Kanda, pale Tabora kwa Kigoma, unakuta watu wawili, watatu, hawawezi kufanya kazi za Mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo mazuri sana. Ukija leo Kigoma, Bonde la Ruiche, lenyewe peke yake tukiwekeza vizuri, tuna hakika tutalima mara tatu kwa mwaka na kwa sababu hiyo, kama tutalima mpunga, tutaweza kuwapa chakula watu wote kwenye ile Kanda yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe sana, Sheria ni nzuri, naiunga mkono, lakini naona changamoto ya kwanza ni fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, ni kubadili tabia ya kufanya kazi, *we must change our mindsets*, lazima tubadilike sasa, ili tuweze kwenda na matakwa ya Karne ya 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii, naomba Mheshimiwa Waziri haya niliyoyasema ayafanyie kazi, ili tuweze kuitekeleza azma hii ya kufanya mapinduzi katika kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo, ni Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kushiriki na Wabunge wenzangu kwa kuchangia Muswada huu muhimu, kwa maslahi ya Watanzania na kwa mustakabali mwema wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, nchi yetu ina mabonde mazuri yanayofaa kwa umwagiliaji, lakini ni ukweli pia kwamba kwa kadri ninavyokumbuka na wote tunakubaliana, hatujafanya maendeleo katika mabonde hayo kiasi cha kuweza kufanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na ambacho kinaweza kumtoa mkulima wa chini kutoka katika umaskini uliotopea na kumpeleka katika hali ya neema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lengo la Serikali yetu ni kushughulikia ustawi wa watu wetu. Kama kumbukumbu zangu ni sahihi, maana yake Watanzania kwa zaidi ya asilimia 70 mpaka sasa bado wanategemea kilimo, lakini mchango wao kwenye pato la Taifa ni wastani nadhani wa asilimia labda 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wao huo ni mdogo sana na hii inatokana na sisi kutokuwekeza kwa kiasi cha kutosha kwenye sekta ya kilimo. Kwa hiyo, uamuzi uliofanywa leo na Serikali kuleta Muswada huu mpya wa Sheria, una manufaa makubwa kwa ustawi wa watu wetu na kichwa chenyewe au Muswada wenyewe wa Sheria una jina jema sana na linalovutia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inasema huu ni Muswada wa Sheria inayoweka masharti kwa ajili ya kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Maendeleo, Uendeshaji, Utunzaji wa Mifumo ya Umwagiliaji kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Mkakati wa Maendeleo ya Umwagiliaji na kwa ajili ya mambo mengine yanayohusu maudhui ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kunukuu jinsi ambavyo Muswada huu ulivyo mtamu kwa maelezo yake, lakini ulivyo pia mtamu iwapo Serikali itaamua kutekeleza kama kichwa cha Muswada wenyewe kinavyoeleza, jina la Muswada linavyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashaka yangu yalipo ni pale ambapo kifungu cha 18 cha Muswada huu kinakinzana kidogo na utaratibu tuliouzoea wa umiliki wa ardhi. Kama mnavyojua nchi yetu huweka dhamana ya ardhi katika ugawaji kwenye ngazi za Vijiji, kwenye mikutano mikuu ya Vijiji, baada ya mapendekezo ya Halmashauri za Vijiji, lakini ukienda kwenye kifungu cha 18 cha Muswada huu, kinasema, pale ambapo, naomba kununukuu kwa ruhusa yako:-

"Pale ambapo ni lazima kwa lengo la kufanikisha madhumuni ya Sheria hii, Waziri anaweza, baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Ardhi na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, kumshauri Rais kwa kuzingatia Sheria ya Utwaaji wa Ardhi, kutwaa ardhi yoyote kwa lengo la kuendeleza kilimo cha umwagiliaji".

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo mashaka yangu yalipo, kwamba kifungu hiki kikitumika vibaya, kinaweza kupokonya mamlaka ya mikutano mikuu ya Vijiji, katika mabonde ambayo wananchi wamekuwa wakiyalima kwa kilimo chao hicho hicho kidogo na hatimaye kuwafanya wananchi kuwa wakimbizi kwenye ardhi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri sana Mheshimiwa Waziri aliangalie eneo hili, hakuna sababu ya ninyi kutwaa ardhi hii. Ardhi ya mabonde haya yanayofaa kwa umwagiliaji ibaki chini ya Vijiji vinavyohusika, kazi ya Serikali iwe ni kuboresha miundombinu katika ardhi inayomilikiwa na Vijiji vyenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishakutwaa ardhi hii najiuliza ni nani atakuwa anagawa ardhi hiyo, baada ya kwamba umelipa fidia, kama siyo kutengeneza utaratibu mwingine ambao ardhi hiyo inaweza kuwa mikononi mwa chombo kingine na kuwapokonya wananchi ardhi ambayo ni ya kwao ambayo wamekuwa wakiitumia ajili ya kilimo na kwa ajili ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili ni jambo la kuangalia, si hili tu pia katika suala zima la uhifadhi wa mazingira. Kwa sababu tumeshuhudia baadhi ya watu wanaofanya *environmental impact assessment*, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja na wakati huo huo unakuta kabisa kwamba vyeti vinatolea katika mazingira ambayo yanatia mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyejua kwamba kuna eneo linalopakana na Hifadhi ya Taifa ya Saadan, ambalo limetengwa leo na limetolewa cheti cha *environmental impact assessment* kutoka *NEMC* na kutoka Wizara inayohusika ambayo imetolewa sasa kwa Kampuni moja ya *Eco-Energy*, lakini shamba hilo la Miwa, linapakana na Hifadhi ya Taifa. Maana yake upande huu wa Mto, linakuwa ni shamba la miwa, upande wa pili wa Mto, ni Hifadhi ya Taifa ambayo tembo wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni nani atakayewapeleka semina tembo waliomo kwenye Hifadhi ya Saadan ili wasivuke huo Mto na kuingia katika hilo shamba la miwa kuweza kula kama wanavyofanya katika maeneo mengine, lakini wakati huo vyeti vimeshatolewa na watu wanasema,

kwa mujibu wa ripoti, kwa mujibu wa ushauri wa wataalam wetu, hilo nalo ni jambo jema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema, ni vizuri tukaangalia sana Sheria hii, isije ikaondoa mamlaka kutoka kwenye Vijiji vyetu, ikapeleka mamlaka kwa watu ambao hawajui mahitaji halisi ya wananchi wetu. Nasema kama Sheria ikiboreshwa, vifungu kama hicho cha 18 kikarekebishwa, kifungu cha 17 kikarekebishwa na kuhakikisha kwamba ardhi inabaki mikononi mwa wananchi, siwezi kuwa na tatizo kabisa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo lazima nifike mahali pa kutahadharisha, ni kwamba uendeshaji wa Serikali sasa hivi ni gharama kubwa sana. Ukiangalia *Agencies* zinazoanzishwa katika Serikali hii, kwa majina tofauti, hii ya leo inaitwa Tume, lakini ukienda maeneo mengine unaambiwa ni Wakala, kazi ambayo ilikuwa inafanywa na Idara katika Wizara sasa inageuka tena, ukiangalia fedha zinazotengwa kwa ajili ya mishahara ya hizo *Agencies* au hizo Wakala, inakuwa ni mzigo mwingine tena kwa mlipa kodi, kiasi kwamba fedha za kupeleka kwenye miradi ya maendeleo inakosekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuogopa tena kwamba, kwa Tume hii msipoitumia vizuri pia, inaweza kuwa ni kichaka kingine cha kuongeza ukubwa wa matumizi ya Serikali, wakati huo huo mkihakikisha kwamba hakuna fedha zinazokwenda kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine watu wanapiga kelele na kusema kuhusu wingi wa Wizara. Nataka niwaambieni, wingi wa Wizara siyo idadi ya Mawaziri na Makatibu Wakuu. Wingi wa Wizara hivi leo baada ya kufutwa kwa Mashirika ya Umma, ni kuanzishwa kwa Wakala mbalimbali ambazo zinawapeleka watu wenye sifa mbalimbali, ndiyo wana sifa za kuweza kuajiriwa, lakini wanakwenda kupatiwa mishahara minono na kuwafanya wakubwa walioko kwenye *Agencies* hizo kuwa na mishahara isiyolingana hata na Watendaji Wakuu wa Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukija kuangalia baadaye gharama zilizoko kwenye Tume na kwenye Wakala hizo zinazoundwa, utakuta kwamba mzigo mkubwa wa fedha ambazo zingepaswa kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo, sasa inalazimika kupelekwa kwenye uendeshaji wa Taasisi hizi zinazoanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine napata mashaka, kwamba baadhi ya Wakala hizi zinazoanzishwa na Serikali, wakati mwingine Wizara zinaanzisha kwa ajili ya kuweka mtandao wa maswahiba na marafiki wa baadhi ya watu. Maana kazi hizo hizo zingeweza kufanyika chini ya Idara hizo hizo na wataalam hao hao, hawatoki Mbinguni, ni hao hao mlionao, kiasi kazi mnayofanya ni kubadilisha majina ya vyeo na wakati mwingine kuwapa mishahara minono zaidi na kuacha wengine kwa kweli wakipigwa jua pale Wizarani na kuona kwamba wengine wamekwenda kwenye maeneo ya neema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kutahadharisha juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hiki kitu kinachoitwa Benki ya Ardhi. Mara nyingi sana ukiongea na watu kama wa *TIC* na wakati mwingine viongozi wetu wa Kitaifa wanapokutana na baadhi ya Wawekezaji, wanasema kuna ardhi tele ya kuwekeza Tanzania, ninajiuliza ardhi hii inapatikana wapi? Maana kila kukicha ni ugomvi kati ya Wafugaji na Wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wewe leo Mheshimiwa Job Ndugai ukiamka, nenda leo hapo tafuta ardhi ambayo unataka ulime, hutaipata kwanza ardhi hiyo. Kama ardhi hiyo ingekuwa ni kubwa kiasi hicho, kama hiyo inayodaiwa leo Pwani kwamba inatolewa kwa Kampuni ya *Eco-Energy,* hivi wale Wamasai wanaopigwa pale na wale Wasukuma wanaopigwa wale wafugaji kutokana na ugomvi kati ya wakulima na wafugaji. Hivi Mwekezaji ni lazima awe mweupe au ni lazima atoke Ulaya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ardhi hiyo siioni. Kwangu sinayo ardhi, nina kilometa za mraba 20,000, lakini hadi leo ardhi yote ile inatumika na watu hawa karibu 200,000, kwa ajili ya ufugaji wao na maisha yao na mifugo yao. Leo mkikaribisha Wawekezaji kupita kiasi kwa kisingizio cha kuwekeza kutoka nje, sioni kama hapa tunainua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu ni kwamba, Serikali ichukue hatua za makusudi, itengeneze

miundombinu ya umwagiaji, iwakabidhi Watanzania, siyo wawekezaji kutoka nje. Mkiendelea kukabidhi ardhi kwa Wawekezaji kutoka nje, mtaleta ya Zimbabwe. Maana leo ugomvi ulioko Zimbabwe, ardhi iliyo nzuri kwa ajili ya kilimo, iliyotolewa kwa Walowezi wachache na kuwaacha wananchi wa Zimbabwe wakiwa kwenye ardhi kame na ambayo hawawezi kujipatia riziki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kusema, kama ardhi hii itatwaliwa na kuwekwa chini ya Tume inayoundwa na kuondolewa kwenye mikono ya Viongozi wa Vijiji na Serikali za Vijiji na Mikutano Mikuu ya Vijiji, hiyo nayo itakuwa ni utumwa mwingine wa kuwanyima Watanzania uhuru wa kutumia ardhi yao na mamlaka waliyo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kusema, kwa kweli siwezi kupinga hoja hii, najua ina maslahi makubwa, wananchi wangu wa Msitu wa Tembo wanasubiri kuona miundombinu yao ya umwagiliaji ikiboreshwa. Wananchi wa Kiriwani halikadhalika, tuna maeneo mengine ya umwagiliaji pale Ngage, Lobosiret, Ruvuremiti, Vunge, Kambi ya Chokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maeneo kwa hakika ambayo leo miundombinu ingeboreshwa, wale wananchi wangeweza kuondokana na umaskini walio nao hivi sasa. Tusingeendelea tena kwa Mheshimiwa Chiza, tusingehangaika tena kwenda kwa Mheshimiwa Lukuvi kuomba chakula kwa ajili ya watu wasiokuwa na chakula, iwapo kama yale mabonde yataweza kuboreshwa, lakini kuweka miundombinu ile ni gharama kubwa.

Ningependa Serikali iamue kama ilivyoahidi, baada ya kufanya upembuzi yakinifu katika baadhi ya maeneo niliyoyataja, kutenga fedha sasa kwa ajili ya miundombinu hiyo, lakini siyo kwa kukaribisha Mwekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwa Wilaya kama ya kwangu ya Simanjiro wala hatuhitaji yeyote, ni afadhali ardhi hiyo ibaki tuilime, tuendelee kulima lima na kumwagilia kwa kiasi tunachoweza, kuliko ardhi ije itwaliwe, halafu ikabidhiwe mamlaka nyingine na hatimaye ikabidhiwe kwa wageni kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale vifungu hivyo vitakaporekebishwa na kuhakikisha kwamba Sheria ya Ardhi ya Vijiji inatumika na Sheria ya Ardhi itatawala na kutambuliwa vizuri kwenye Muswada huu, nitaunga mkono hoja hii, lakini kama ilivyo hivi sasa ambapo naona kuna mkinzano kati ya maelezo yaliyoko kwenye tafsiri ya Kiswahili na yaliyoko kwenye tafsiri ya Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndipo ningependa kupata *clarity* au kupata ufafanuzi vizuri zaidi kama mamlaka ya Mikutano Mikuu ya Vijiji inapaswa kutambuliwa kwa mujibu wa Sheria, lakini suala la kutwaa ardhi, sitaunga mkono kabisa kifungu chochote kinachopelekea kutwaa ardhi ya wananchi kwa mamlaka aliyopewa Rais. Kwa sababu kufanya hivyo ni kuwapora wananchi ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, nakushukuru sana. Umekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo. Tutaendelea na uchangiaji kesho asubuhi na kesho jioni tutaendelea na hatua zingine zote zilizobaki.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii, kwa shughuli zilizopangwa leo, zimekamilika. Kwa hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 29 Agosti, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*